# UKWELI

**Kitabu iki kimeandikwa na mpenzi wa Mungu :**
**SALEH KALONDA BIN RAMAZANI**

Mimi Saleh Kalonda Bin Ramazani "nimezaliwa katika kijiji Kadingila / miabe, mtaa wa Nonda, tarafa la Kasongo, jimbo la Maniema, Katika jamuuri ya kidemocrasia ya Kongo,

Baba ni Ramazani, na mama ni Zamuda .

Ni meowa na kuzaa watoto watatu.

Nilifunuliwa na Mungu katika mwaka wa elfu moja mia kenda makumi kenda na ine, Mungu aliniita na kunituma na ujumbe huu.

**Kitabu iki kina milango saba : USILIMU, ENZI TUKUFU, NURU TAKATIFU, CHEM CHEM, NJIYA YA MUNGU, UZIMA, KAULI TUKUFU**

**Apa tunatangaza kwanza milango sita, kuna baki moja :KAULI TUKUFU**

## UTANGULIZI

Ametakasika mwenyezi Mungu M'bora wa kuumba ambae kanijaza Nguvu ya kuandika kitabu hiki kitukufu.

Maana ni yeye Mwenyewe Muumba aliye nifunulia na kunituma na ukweli wake huu ku watu ili wapate kua yakini na uzima wake.

Kukosa yakini kuna fanya mutu adidimie katika ukafiri na katika unafiki moyoni mwake.

Basi ndugu , someni kitabu hiki na nia safi ili upate kua yakini na Mola wa ulimwengu;upate kurithi bustani ya neema.

Wenu shahidi wa Mungu Saleh KALONDA bin Ramazani.

## MULANGO WA KWANZA: USILIMU

### 1. UFUNGUZI

1. Ametakasika Mwenyenzi Mungu, m'bora wa kuumba

2. Mlezi wa viumbe aliye na uzima, wa pekee anaye stawi arshini

3. Mola mshindi awezaye yote na ajuaye yote

4. Ni wewe mkamilifu tunaye kuomba msamaha wa zambi zetu

5. Na ni wewe Mkarimu unaye tosheleza maitaji ya waja wako

6. Utupatie zawadi ya kiroho, na utubarikie na utuokoe

7. Utukaribize mbinguni baada ya kufa kwetu (Amin!!!).

### 2. KIYAMA

1. Ametakasika Mwenyenzi Mungu, Mufalme aletaye ujumbe ku watu ili kusadikisha uzima wake.
2. Atakaye amini kwamba Mungu peke yake ndiye mwenye uzima,na ku amini ujumbe wake wote ndio musilimu.
3. Watu wengi hawakubali ya kama ukamilifu upo, bali wamekubali tu upungufu ambae ndio hali yao pia, wameshindwa kuzingatia njee ya kambi lao.
4. Mwenyenzi Mungu ndio muumbaji wa Anga na ukiwa, aliye tangulia kabla ya ulimwengu na walimwengu.
5. Bwana wa mabwana aliye na utasi juu ya kila falme, anaye rehemu na anaye kirimu
6. Hakuna aliye huru kama yeye, mustaarabu wa milele, asiye fikiwa na asicho kitaka, hajaanake na hasira wala hajaanake na cheko.
7. Mkamilifu asiye najisika na upungufu wowote, hakuna upatikanaji njee ya idhini yake, na ndiyo maana hakuna cha kum'buguzi.
8. Ni muweza wa kila jambo, mtendaji wa jumla ya matendo, anaye umba na anaye uwa.
9. Kiumbe hakiwezi kumuongezea wala kumupunguzia chochote, Enzi yake humiliki Mbingu, Hadeze na Dunia, uwezo wa kuenea.
10. Arshi yake sio chombo wala umbo, lakini ni utukufu usiyo kurubiwa.
11. Uwezo wa Mungu hauna mipaka, lakini wenye kuenea namna ya kukamilika pasipo upungufu wowote.

12. Haifae kumuwekea Mungu mipaka katika utendaji wake. Yeye ndio Mfalme Mkamilifu, Muweza yote, anaye hukumu vyote bila kuhukumiwa na yeyote.
13. Wamekufuru wanao sema : << uumbaji umekomea hapa,Mungu hata umbaka tena chochote >>.
14. Na wamekufuru wanao sema : << uyu ndio mtume wa mwisho,Mungu hata tumaka tena (mtume) mwengine >>
15. Ogopeni Mungu kikweli, wala usipokee andiko takatifu kwa uziwi na upofu, usifikie kukufuru bila kufahamu.
16. Kauli tukufu hutoweka katika lugha za watu, amemfunulia kila Mtume katika lugha yake ili apate kusikia.
17. Mungu hana lugha maalumu bali lugha zote ni zake, ndiye aliye tokeza yote kwa jumla.
18. Kutenda kwake ni tafautu na utendaji wa viumbe, ndio maana kweli yake hukadiriwa katika mifano.
19. Mungu sio mfano wa kiumbe wala uzaifu wa kuishi (ao kufikiri) hamkurubie kamwe.
20. Mwenyenzi Mungu ni muujiza, hakuna kilicho mfanana, ukamilifu wake ni hali ya upekee, mamlaka ya milele.
21. Muumba wako hayuko mbinguni wala hadezeni wala duniani, lakini yeye hustawi Enzini.
22. Enzi imepatikana juu sana kupita mbingu.

23. Amestawi katika dhati yake mwenyewe hali ya kua yote katika yote, mwenyi kuenea.
24. Sema : Usilimu ni usalama wa nafsi katika mapenzi ya Mungu,yaani ndio dini ya Mungu Mwenyenzi.
25. Kusilimu ndio kuingia katika dini ya Mungu, na anaye silimu ndio musilimu.
26. Kuamini kwamba Mungu Mwenyenzi yupo mzima, na ndiye Muumbaji,na ndiye muabudiwa,hakuna mwengine kama yeye.
27. Na pia kuamini Mitume yake yote, yaani kutumikisha maneno ya mitume yake yote kwa jumla.
28. Ndio kuingia katika dini, yaani kusilimu, kadiri ya kusalamisha nafsi katika mapenzi ya Mungu.
29. Mitume huamrishana mema na kukatazana mabaya na huwabashirieni habari ya kiyama,wala hawahitilafiane kwa lolote
30. Ni amri kwa wasilimu wote kufanya ibada, hakika imani pasipo ibada ni bure kabisa.
31. Kila tendo njema linalo fanyika sababu ya kupata radhi ya Mungu ni miongoni mwa ibada.
32. Na usifanye ibada yoyote ispokua ajili ya kupata radhi ya Mungu.
33. Tendo njema lolote linalo fanyika kinyume na tumaini ya kupata thawabu kwa Mungu sio miongoni mwa ibada ya Mungu.

34. Sala na dua (ombi) ni mambo mbili tafauti kabisa,laiti mungeli musikiya Nabii mtukufu Muhamadi.
35. Ibada kubwa zaidi ya yote ni Sala.
36. Kumuimidi Mungu na kufunga sala, kusujudu na kutoa shaada na kutakiana amani,katika kipindi maalumu ndio kusali.
37. Utakapo funga sala, soma sura za ufunguzi zote ili sala yako ikubalike
38. Na utakapo sujudu, umtukuze Mola wako na kumuomba, hakika yeye ndie anaye jibu maombi ya watu.
39. kufanya safari ya kwenda maala pa takatifu ajili ya kutimiza ibada mbalimbali kwa yule aliye na uwezo ni miongoni mwa ibada kubwa ya hija.
40. maala pa takatifu duniani ni miskiti takatifu na milima takatifu na miji takatifu.
41. Ni kawaida kusali na unyenyekevu, hali ya kuogopa Mungu:muskitini ao mlimani ao nyumbani ama popote utakapo kua.
42. Hapana kufanya upuuzi wowote katika sala: usipige mziki wala usicheze katika sala.
43. Sala ndio ibada kubwa sana yenyi kuleta nguvu ya ushindi na nuru ndani ya musilimu, pia na saumu na dhikiri.
44. Umsujudie Mola wako asubui na jioni na usiku, na umtukuze mchana.

45. Hakika maneno mazuri ambae humtukuza Mungu huzidisha umri wa mutu anaye ya tamka.
46. Na atakaye jidai kua roho tupu na ili hali iko na mwili, yaani angali na ishi duniani, kiisha akavunja alama ya dini, atanyimwa fadhila ya mbinguni.
47. Ni bora kutumikisha mwili katika kuijenga roho, kuliko kutumikisha roho katika kuujenga mwili.
48. Maadamu mutu angali na ishi duniani, inamubidi kutumikisha mwili na roho, maana ndiyo umbo lake timamu
49. Matendo ya mwili wake ya ongozwe na roho takatifu katika kuitimiliza ibada.
50. Mungu ni Mfalme wa ajabu anaye stahili kuhimidiwa usiku na mchana.
51. Ni yeye anaye tawala peke yake ulimwenguni pote bila wa kumkombola, Mfalme wa milele.
52. Mkuu aliye huru kufanya anayo penda bila kiziwizi, ambae huukumu yanayo tendeka ulimwenguni.
53. Amejaa mamlaka yote, Mtukufu kuliko wote anaye miliki walimwengu wote.
54. Msikiaji na mpokeaji wa maombi ya viumbe, Mjuzi wa hesabu ya walimwengu.

55. Watu hawafahamu daraja yake, ndio maana wame mlinganisha na viumbe, wakimuwekea wapinzani kwa midomo yao.
56. Hakuna kiumbe cha kumgombeza Mwenyenzi Mungu, vyote kwa jumla ni chini ya uwezo wake.
57. Vyote hufuata kanuni yake mshindi, maana hutokana na idhni yake tukufu.
58. Shetani sio mpinzani wa Mungu, lakini mpinzani wa Malaïka.
59. Yule ni simamizi la ubaya na uyu ni simamizi la uzuri, Mfano wa kinyume chake, na ndio maana hupingana.
60. Mungu aliye tafauti na umbo hizi, hagusike na lolote katika shuruli zao.
61. Mola Mkarimu ni m'bora wa mahakimu, humlipa kila mmoja wao sawasawa na matendo yake.
62. Mungu angelipenda Shetani asijumuike kama asingeli muumba.
63. Na kama ali muumba sio makosa, upungufu asilia ulibidi upatikanaji wa namna hiyo kufanyika.
64. Ni mfano wa kapi iliyo anguka wakati wa uchoraji.
65. Kadiri mchoraji anavyo kusanya makapi yote baada ya kazi na kuyatupa, ndivyo Muumba atakavyo kusanya (ma) Shetani na wote waliomfuata na kuwatupa Hadezeni (motoni).

66. Hawata kuwa miongoni mwa wanao ishi, wala hawatakua miongoni mwa wafu ,bali wa takosekana ulimwenguni,itakua kwao kama ilivyo kua kabla ya kuumbwa kwao.
67. Ndipo wale watakao rithi watakua salama ndani ya bustani, maana mustaki wao amekwisha ondolewa
68. Shetani hana maisha ya milele, bali yeye ni mwenyi umri mfupi sana, hasira imewaka ndani mwake sababu anafahamu kwamba kiyama ni karibu.
69. Mungu ni m'bora wa kukadiria, anaye miliki wakati, ambae kawawekea wakaaji wa dunia siku ya mwisho.
70. Siku hiyo Mungu atamtuma Yesu Masiya ili asawanishe ardhi sawasawa, hakuta bakia bonde wala kisuguu.
71. Waovu wata angaika na kulia na kujilaumu, na waaminifu ndio watashangilia neema ya Mola wao.
72. Hakika ahadi ya Mungu itatimia, hakuta chelewa hata nukta moja.
73. Jitayarisheni vizuri, Enyi wasilimu,ili mupate kurithi bustani ya neema siku ya mwisho.
74. Makafiri wanauliza wakisema : itatimia lini ahadi hii? si leo,tangu kuumbwa kwa Adamu mpaka ujio wa Yesu Masiya manabii walitabiri neno hili lakini hakikutokea.
75. Yesu Masiya pia alitabiri neno hili akisema: Kiyama ni karibu, hakikutokea mpaka ujio wa Muhamadi.

76. Na Nabii Muhamadi pia alitabiri neno hili akisema:<< Hakika kiyama ni karibu >> ,hakikutokea mpaka ujio wa Ahmadi.
77. Naye Ahmadi pia alitabiri kuhusu kiyama, hakikutokea mpaka leo, kitatokea wakati gani?
78. Sema: "Hakika kiyama ni karibu sana", ma nabii na mitume walio pita mbele yangu walisema kweli kabisa.
79. Dunia ni umbo dhalili, haiwezi kudumu milele ajili ya uzaifu wa mwili.
80. Wakaaji wake ambae huvaa miili huzoroteka na ujinga pamoja na wakaaji wa Hadeze.
81. Siku moja mbinguni ni muda wa miaka elfu duniani.
82. Tangu Yesu Masia kwenda mbinguni mpaka ujio wa Muhamadi,haikuenea hata siku moja mbinguni.
83. Na tangu Muhamadi kwenda mbinguni mpaka ujio wa Kalonda ni muda wa siku moja na nusu mbinguni.
84. Na tangu mwanzo wa Dunia mpaka leo hii ni muda wa masiku chache mbinguni.
85. Mutu mwenyi akili asijali muda ulio pita kabla yake, wala muda utakao kuja baada yake, lakini ni vema kwake kutumia vizuri umri wake katika njia ya Mungu ili apate kurithi bustani ya neema hiyo siku ya mwisho.

86. Watu wa Dunia wamezani kama wamedumu na ili hali hawajadumu, hayo husababishwa na uzaifu wa mwili.
87. Amani ya Mungu kwa wasilimu wote.

## 3. PAPU KWA PAPU

1. Ametakasika Mwenyezi Mungu, M'juzi wa kuumba,alie na uwezo kamili,ambae hutegemewa na kila kitu.
2. Upatikanaji wote umetoka kwake,ni yeye anaye weza yasiyo wezekana kwao viumbe,anaye tenda maajabu bila mfano wake.
3. Anapo fanya miujiza ndipo watu hutetemeka hali ya kuogopa punde kidogo wanasahau.
4. Mungu ni Mshindi anaye jaa mamlaka ambae hupatikana kimuujiza bila msaada wa yeyote.
5. Alitangulia kadiri ya kuenea bila mwanzo wala mwisho, wa pekee aliye kamilifu.
6. Ni yeye anaye helekeza waja wake kwenyi kheri ya kila namna,na kuwahepusha na shari ya kila namna.
7. Muhimidiwa aliye na sifa kamilifu, wa milele juu ya mambo yote.
8. Lakini walio kufuru hawajali utukufu wake, wamemtolea maovu ya kila namna.
9. Wamejigamba ajili ya kupewa muda duniani, hawafahamu kwamba kutafikia muda ulio wekwa ambae haki itainuliwa.

10. Hayo ni kwa sababu hawa hazibiwe papu kwa papu pindi wanapo kosa, hukumu itafanyika siku ya mwisho baada ya maonyo yote.
11. Matukio yote hutoka kwake, hakuwezi kufanyika jambo kigeni katika ujuzi wake.
12. Hakuna kitakacho badiri mpango wake,maana vyote ni chini ya uwezo wake
13. Kauli tukufu ndio mpango wake usio badirika, haita pita bure mpaka itimie.
14. Heri mutu anaye tekeleza kwa makini kauli ya Mwenyezi Mungu.
15. Mungu ndio mkweli wa ahadi ambae kauli yake hutimiliza idhni yake.
16. Ametangulia katika fahamu ya vyote isiyo badirika, haiongezeke wala kupunguka ajili ya kuenea.
17. Vipi itaongezeka ambae imekwisha jaa kabisa! hakuna kuongezeka wala kupunguka katika jambo lenye kukamilika.
18. Ni bora zaidi kutii amri ya Mungu kuliko kugeuzageuza maneno kwa kiburi, hakika Mola wenu anajua sana mradi wa kila jambo.
19. Usijilinganishe na Mola wako kwa lolote wala usishakie anayo ya sema, kwani hauna fahamu ya kumkosoa yeye ajuaye yote.
20. Ogopeni sana Mungu, mamlaka isiyo na kipimo, Mlezi wa viumbe aliye pasipo yeyote.

21. Mumiliki wa anga na ukiwa atawalaye katika ulimwengu bila mfano wake.
22. Mbingu, hadeze na Dunia hufuata hukumu yake,wala hakuna umbo njee ya kawaida yake.
23. Muumbaji, atokezaye kwa rafla bila kutumika kazi na bila shauri na yeyote,Mjuzi aliye juu.
24. Atakaye toa shaada na kuishi katika woga wa Mungu, Ataingizwa mbinguni na kuishi milele.
25. Amegundua baba wa siri aliye kwa siri, anaye fanya siri kwa siri.
26. Mola Mshindi atanguliaye namna ya kuenea katika tendo kua, kwake hakuna kuanza wala kukoma Mfalme mwenyi kukamilika.
27. Mkongwe zaidi ya wote, wa maajabu anaye patikana juu ya wakati,ambae humiliki muda wote bila kipimo.
28. Yeye ni tafauti na viumbe vipatikanavyo ndani ya wakati na chini ya wakati, kadiri ya umri fulani.
29. Enzi yake ndiyo inayo mkamilisha bila upungufu wowote,milki ya ushindi ambae huzidia kila kitu
30. Anakua yote katika yote, Mkuu wa majeshi, ambaye ukubwa wa milki yake humfanya awe huru kuliko wote, hupatikana kile anacho idhinia,Bingwa asiye buguziwa.
31. Msifiwa wa ajabu, Mola wa karne na karne, tumaini la walimwengu.

32. Baba wa salama aliye salama, Mtangulizi na Mtakatifu, anaye rehemu viumbe vyote kwa jumla.
33. Enyi walio silimu! Tumieni urakibuni matendo yenu na ogopeni Mungu ukweli wa kuogopa ili mupate kuokolewa.
34. Afazali watu wa kuzingizie bila wewe kuwamo, ijapokua wakuzarau usibabaike, hakika wao ndio wenye hasara.
35. Mungu alikupatia akili kua kifaa cha maisha, jinsi ya ukaguzi baina ya mema na mabaya.
36. Kama haufahamu mradi wa hukumu yake fulani, helewa kwamba Mola wako anajua zaidi.
37. Hakika sheria ya Mungu haikuja ila kwa wenyi akili, ambae hujichagulia njia wenyewe.
38. Watu wengi wamesilimu ajili ya hanasa ya dunia, wala hawana tumaini ya wokovu.
39. Na wakisali masiku chache tu wanachoka na kuacha na kugeuka, wanapupia kumshirikisha Mola wa walimwengu.
40. Hawa ndio wenyi hasara hiyo siku ya maamuzi, mambo yao yote ni ya kidunia, hawana akiba yoyote mbinguni.
41. Ni bora kusilimu ajili ya kupata radhi ya Mola wako, ukitarajia wokovu siku ya mwisho, na pia kuonesha shukrani kwa yule aliye kuumba.

42. Wasiwasi ni ya Shetani, heri kua na subira, usiache sala na maombi na wema,hakika Mola wenu hutosheleza kila nafsi inayo muhitaji.
43. Kadiri unavyo kula kila siku ili kuujenga mwili wako, ndivyo unavyo pashwa kusali kila siku ili kuijenga roho yako.
44. Usiharakishe jambo ambae Mungu ameikawisha, wala usikawishe jambo ambae Mungu ameisha harakisha.
45. Na usifunue kile Mungu amekifunika, wala usifunike kile Mungu amekifunua.
46. Tulia baada ya kuomba, usitafute kujibiwa pale pale, wasiwasi ni alama ya tamaa ya maisha ya dunia, pia ni alama ya imani haba.
47. Lau kama Mungu angelikua na jibu dua ya watu papu kwa papu, bila shaka taratibu hii ya maisha isingeli kuwako, wala dunia aingeli patikana.
48. Mutu angeli omba utimilifu wa nafsi yake, kama ingeli takika ageuzwe roho takatifu papu kwa papu.
49. Na kama angeli omba uharibifu wa nafsi, ingeli takika ageuzwe muzimu palepale.
50. Umutu ungeli futika mbele ya wakati na pia mipango iliyo pangiliwa muda mbalimbali isingeli timilizwa.
51. Maombi ya mwanadamu haipatikane katika ukamilifu, lakini katika upungufu.

52. Dua nyingi za watu huruka mipaka, hazistahili kujibiwa papu kwa papu, isije kuleta muvrugo katika kawaida la umbiko.
53. Kama watu elfu moja wangeli omba ufalme wa dunia yote kila mutu, ingeli takika kufanyike ma dunia elfu, ili kila yule ajibiwe papu kwa papu, kadiri ya hitaji yake.
54. Watu wote hawakuzaliwa siku moja bali siku mbalimbali, makarne na makarne, inabidi kaumu zote zipite mpaka siku ya mwisho.
55. Hakika Mwenyezi Mungu ni M'bora wa kukadiria, mwenye ujuzi.
56. Kila analo lifanya ni haki, hakuna kosa hata kidogo.
57. Je! utamkosoa Mjuzi aliye kuumba? ama ni kweli jembe itamuongoza mlimaji?
58. Ni vema kumsifu na kumshukuru Mungu kuliko kumlahumu, anajua msiyo ya fahamu.
59. Matendo ya watu yamelindwa huko juu,hiyo siku ya kiyama itakua ndio wakati wa mavuno,kila yule atavuna aliyo ya panda.
60. Mungu amewakadirishieni malipo kwa kuwapa sehemu duniani na sehemu kubwa kuwalindia mbinguni, ili muda ulio kadiriwa utimie.
61. Mungu peke yake ndio mzima, anaye stahili kuabudiwa, mwenyi kuenea katika tendo kua, wa milele aliye juu.
62. Viumbe hawana uzima, bali hunusu na vipande,wamepatikana bila kuenea katika tendo kua.

63. Yule anaye kosekana kiisha anapatikana, kiisha tena anakosekana, hayuko kabisa.
64. Ni mwenyi kuwako kikweli, yule asiye kosekana muda wowote, anaye enea katika tendo kua.
65. Hakika uzima ni utukufu wa ajabu, mamlaka yenyi ushindi kadiri ya kuenea.
66. Mungu ni Mkubwa sana, Mtukufu mwenyi uwezo zaidi ya kila kitu,Bingwa mkuu asiye shindwa na chochote,Mumilki aliye juu.
67. Tenda adili popote ulipo, ukitarajia kuleta amani duniani.
68. Siasa yako isiwe uchimbi wala uvamizi, lakini amani kwa watu wote.
69. Wala usifuraikie aibu ya mwenzako,wala usimnyanyase yeyote,lakini tizama wenziwe kwa upendo na furaha.
70. Wala usimtegee aliye amini usije ukamfanana Shetani.
71. Mungu ni mumoja na dini yake ni moja,hakuna dini ya Mussa wala ya Yesu,wala ya Muhamadi.
72. Ma nabii na mitume wote walipewa kazi ya kusilimusha watu,yaani kuwaingiza watu katika dini ya Mungu.
73. Lau kama watu wangeli fuata maubiri ya manabii na mitume wote vilivyo, hakungelikua mgawanyiko wowote kati yao.
74. Haya ni kwa sababu wamebagua miongoni mwa mitume.

75. Hakika yule asiye amini mitume wote hawezi kuingia mbinguni,kumpinga Mmoja tu ni kama kuwakanusha wote kwa jumla.
76. Amani ya Mungu kwa wasilimu wote.

## 4. UAMINIFU

1. Mungu ni jina lake yeye aliye umba viumbe vyote kwa jumla,Mshindi anaye jaa utukufu,ambae huthamanisha ulimwengu.
2. Hakuna mwengine anaye stahili kuitwa jina hili isipokuwa yeye peke yake, imemaanisha upekee wa ukamilifu.

3.Ni Muweza na Mjuzi wa mambo yote,anaye miliki ulimwengu.

4.Na atakaye mpachika mwanahewa ama muzilahewa jina hili,amebuni zambi kubwa,maana amenajisi utukufu wa Mfalme wa wafalme.

5.Hana umbo sababu hakuumbwa,sio mume wala muke,hutangulia mwenyewe tafauti na kila kitu .

6.Mungu ni Baba wa salama aliye Salama,mkuu ajaaye mamlaka,ambae tamko lake hutokeza ambacho hakikua,mfinyanzi wa umbo za walimwengu.

7.Hatendake kama watendavyo viumbe,mtukufu aliye na uwezo wa kuenea.

8.Kiumbe hutaabika na shuruli ya kila namna na hali yeye hashurulikie chochote,M'bora wa kuenea.

9.Na ndio maana Mola wa viumbe hana maisha lakini yeye ni Mzima,mwenyi uhuru.

10.Hana shida yoyote ajili ya kuenea,hakuna palipo wazi katika yeye ambae pangeli dai kujazwa,Mkamilifu aliye juu.

11.Milki kamilifu inayo hukumu yote yanayo tendeka,wa pekee kadiri ya Muujiza wa mahajabu.

12.Mufalme wa wafalme na Bwana wa mabwana,anaye jua yote bila kusahau,na kuweza yote bila kushindwa,mtukufu aliye juu.

13.Yeye ndio tumaini la walimwengu na kimbilio la wasilimu.

14.Ombeni yote unayo hitaji,utapewa ,msaada wake hukufikia kadiri ya unyenyekevu wako.

15.Yeyote anaye ishi pasipo kuzingatia uzima wa Mungu ni kipofu,hana akili ambae ndio macho ionayo.

16.Uwezo wote ni wake Mwenyezi aliye na mamlaka ,mtukufu atendaye kwa idhni bila kazi yoyote.

17.Hakuna aliye na sifa mfano wake maana pekee huzidia kila kitu.

18.Milki yake ni kubwa zaidi,ambae husababisha miujiza pindi anapo tenda,m'bora wa kuumba.

19.Mtukuzeni Mungu aliye na ushindi,Mola wa jumla ya viumbe,atakasikaye na azidiaye.

20.Mila nzuri katika imani,inaleta usalama wa nafsi yako milele na milele.

21.Matendo ya musilimu ni tafauti na ya makafiri,maana wameachana njia katika safari zao.

22.Na ndio maana watafika maala mbalimbali;aliye amini ataingia mbinguni na aliye kufuru ataingizwa hadezeni

23.Musilimu ametenda adili popote,ni m'nyenyekevu tena mpole wa moyo.

24.Ni mtenda salama,mfano muzuri wa kuiga ,tafauti na muovu anaye leta wasiwasi katika jamii la watu.

25.Muaminifu ni mwenyi yakini kwamba Mungu anamuona popote alipo na amehifadhi yote anayo ya tenda kwa siri ao kwa wazi.

26.Mwenyi utaalamu,anaye pokea watukufu wa mbinguni maishani mwake.

27.Ametambua haki yake na ya wengine pia,mwenyi kumiliki tamaa ya nafsi yake.

28.Yeye sio mkali wala hana kiburi,ametumia uadilifu hali ya kua moyo wake umejaa woga wa Mungu.

29.Ametenda urakibuni daima;akawa mwanamuke humtii mume wake,na akawa mwanaume humpenda muke wake,kila yule hutosheka na mwenzake.

30.Husaidia wasio jiweza na hufikiria maendeleo ya jamii la watu.

31.Moyoni mwake hana kiburi wala fitna,chuki wala tamaa mbaya.

32.Humsujudia Mola wake asubui,jioni na usiku,pia humtukuza mchana,heri mutu anaye soma kitabu hiki usiku na mchana.

33.Nongo haina fasi moyoni mwake,amesema kweli wakati wote ijapokua katika hatari

34.Kwake ni afazali kujishusha kuliko kijipandisha, hana hila wala majivuno.

35.Yeye sio muuwaji wala mzinifu,sio mwizi wala mvamizi,hadanganyake wala hasengenyake.

36.Ni mwepesi wa kusamehe pindi wanapo mkosae,na pia huomba masamaha anapo kosea,hana mima wala naziri na yeyote.

37.Hazingiziake yeyote ijapokua yeye huzingiziwa kila mara na watu wa dunia.

38.Hana chonganisho wala wasiwasi moyoni mwake,mpole anaye tenda haki.

39.Amewapenda sana walio amini na amewasikitikia sana walio kufuru,wala hazarau yeyote.

40.Anapo tazama wenzake hufuraika moyoni,mutu mwema anaye patanisha walio gombana,wala hafuraikiake magumu ya mwenzake.

41.Wala yeye sio mshirikina wala mnafiki,sio mwongo wala mwivu.

42.Muvumilivu tena mpenda cheko,anaye tumika kadiri ya nguvu yake ili apate kuishi,hana uvivu wala kangami.

43.Hakika hii ndio mila ya musilimu mwenyi imani anaye tumainia Mungu maishani mwake.

44.Kusilimu na nia safi ni neema,wala hakiri uzima wa Mungu isipokua kwa ukarimu wake mwenyenzi.

45.Shika ulicho pewa ewe uliye amini, hakika zawadi ya kiroho ndio pato na ngao.

46.Utakatifu ni wake Mungu,M'shindi aliye huru, mtawala anaye zidia,m'bora wa kuenea.

47.Kwa nini hustarehe duniani walio kufuru na ili hali huwafanyia hila waaminifu?

48.Sema: makafiri wamepewa muda mchache duniani kufatana na kawaida la umbiko ili dunia isiondolewe kabla ya wakati.

49.Kuifanya dunia isipatikane na uovu wowote isingeli kua ila mbingu takatifu.

50.Na kuifanya dunia isipatikane na wema wowote isingelikua ila Hadeze.

51.Kwa dunia kupatikana ilibidi umbiko ya namna hii kupatikana,maana dunia ni changachanga ya uzuri na ubaya.

52.Ni maunganio ya anga na ukiwa,maisha ya humo ni kwa wanahelewa haramu wote .

53.Utafauti wa maisha yao utatokea siku ya malipo,kila yule atavuna aliyo ya panda.

54.Aliye kufuru duniani ataangamia na aliye amini duniani ataokolewa.

55.Starehe ya makafiri ni ya muda,umbo dhalili kuliko umbo zingine zote .

56.Matamshi yao haina buguza yoyote huko juu,na vivihivyo matendo yao,bali hubuguzi nafsi zao wenyewe.

57.Wao ni mfano wa makapi,hujumuika sababu mchoraji angali na chora,wataogotwa na kutupwa motoni.

58.Ujumbe wake ndio ufundi wake ambae huchora nafsi ya wanaadamu:wanao upokea ndio vyombo halisi na wanao ukataa ndio makapi inayo anguka.

59.Uchoraji wa pumzi unaendelea mpaka siku ya kiyama,ndipo Mungu atakapo tenganisha adili na batili.

60.Mungu ni muweza wa vyote na mjuzi wa vyote atanguliaye mwenyewe bila msaada wa yeyote,mtukufu asiye fanana na yeyote ajili ya kuenea.

61.Atakavyo hufanyika kwa rafla,mlezi wa viumbe anaye miliki ufalme wote,mshindi aliye juu.

62.Mungu ni taa ya ulimwengu,ameangazia viumbe kwa utukufu wa dhati yake.

63.Nuru yake hutokea ndani mwake,imetua mbinguni na kuzagaa kama mwangaza wa taa kwenyi kilauri.

64.Heri mutu anaye fikiwa na nuru,pumzi yake imetakasika,amefanana mwangaza usio fifia wala kuzimika utokao Enzini.

65.Amepata maisha ya milele sababu ya kuamini ujumbe utokao kwa Mungu,kiongozi pekee wa jumla ya viumbe.

66.Watu wengi hawaamini ajili ya kiburi na chuki,wame chukia neema aliyo pewa mchaguliwa wake.

67.Na yule ambae Mola wake amemtukuza, hakuna atakaye weza humzalalisha.

68.Na yule ambae Mola wake amemzalalisha ,hakuna atakaye mtukuza.

69.Anaye jazwa na nuru hupata uhai na anaye fikiwa na giza hupatwa na mauti.

70.Fanyeni ibada kwa wingi,wala usitoshe tumaini ya kutoshelezwa na Mungu peke yake.

71.Mola wako atakujaza roho kadiri ya msaidizi,hakuna kitakacho angamiza nafsi yako.

72.Mungu ni muweza yote,mwokozi, wa miujiza,anaye jumuisha pasipo kujumuika,shina la vilivyomo ulimwenguni.

73.Ni bora kumtukuza usiku na mchana,mtatuzi wa shida zote,akadiriaye na asaidiaye.

74.Mwenyezi ametosheleza kua mlinzi,tegemeo na kimbilio la watu.

75.Anaye penda kuishi salama milele ashike maagizo ya Mola wake Mlezi wa viumbe.

76.Amani imetawala mbingumi ajili ya uzuri, na mateso imetawala hadezeni ajili ya ubaya .

77.Amani ya Mungu kwa wasilimu wote.

## 5 . MATIBABU

1.Ametakasika Mwenyezi Mungu,M'bora wa kuumba,mamlaka itokezayo kuujaza ulimwengu

2.Mola wa ulimwengu wote,Mumiliki anaye patikanisha na anaye kosekanisha

3.Walio kufuru wamesema hakuna maisha ingine kinyume na hii ya duniani!

4.Sema: Maisha ya dunia sio ila alama mfano wa kifebe,maisha ya kweli ni hiyo ya mbinguni

5.Kinacho fanya mwili udumu ni pumzi,vikatengana tu,mwili huaribika kwa haraka

6.Na pumzi inakua na nguvu zaidi ilipo peke yake bila kuchangikana na mwili.

7.Aliye wa dunia hazingatie isipokua mwili peke yake,mfano wa kipofu,hawezi kuzingatia roho.

8.Mtenda mema ni pumzi timilifu ambae hukomazwa na jaza la mbingunil,ndio maana huishi milele.

9.Tafauti na makafiri wanao kufa mara ya pili ,kuharibika kwa mwili duniani ,napia kuharibika kwa pumzi hadezeni.

10.Na yule ambae hukosewa mwili na hukosewa pia pumzi hayuko bali hukosekana ulimwenguni.

11.Waovu watakufa mara ya pili baada ya kutaabika muda mrefu na maumivu ya wakati wa kubomoka kwa pumzi zao hadezeni.

12.Hawata kua hai wala hawata kua mauti,humo sio  ila maala pakubomolea umbo,ndio maana hawata ishi milele humo bali watakosekana baadaye.

13.Mola wenu ni mwenyi uwezo wa kubomoa mjengo kihewa kama alivyo na uwezo wa kuujenga,hakuna kigumu kwake,mumiliki aliye juu.

14.Hadeze ni kambi mbaya sana na ndio maana haidumu kama mbingu.

15.Ma nabii na mitume ambae wamekwisha ihama dunia,wamekwisha ionja raha ya bustani.

16.Kwao hakuna maamzi ni watakatifu walio chagua urakibu kama njia.

17.Wamegeuzwa nuru ya taa isiyo zimika,neno na nguvu yake kadiri ya roho takatifu.

18.Ujuzi ni wake Mwenyezi Mungu,mwalimu wa walimwengu,anaye funulia watu mambo ya siri.

19.Ndiye anaye fundisha watu kugundua,wala hakuna anaye unda pasipo msaada wake,m'bora wa wanao ruzuku.

20.Kupatikana kwenu na kutenda kwenu ni katika makadirio yake,mtukufu aliye huru kutenda yote anayo ridhia.

21.Makafiri hujigamba kwa maovu wanayo ifanya, hawafahamu ya kwamba muda wao ni mufupi.

22.Hakika  waovu watalia muda wote mpaka mwisho,wala cheko haitapatikana kwao humo hadezeni .

23.Hadeze hupoteza umbo kama vile moto upotezavyo kuni.

24.Maisha ya humo ni fupi sana,ni  muda wa kubomoka kwa umbo lote na ndio maana hupatwa na maumivu kali.

25.Afazali kurefusha umri wako kwa kutenda adili,ukitembea urakibuni kwa imani na amani.

26.Nini kitakacho kudanganyeni katika maisha ya dunia na hata mufikie kupotea?

27.Vyote ni vya bure kabisa hakuna cha kudumu starehe ya milele hupatikana mbinguni.

28.Tetea namna ya kustiri umbo lako milele,ukipata kufuzu kwa mazao ya zamiri yako.

29.Hakika matumizi ya neno la Mungu ni matibabu ya nafsi.

30.Mungu ametosheleza kua mlinzi,mfariji na m'bora wa wanao rithi.

31. Mwenyi ukamilifu,anaye miliki na anaye kadiria,tegemeo la walimwengu.

32.Mola wa miujiza anaye fanya maajabu,wa pekee asiye lingana wala kufanyika,Mjuzi aliye juu.

33.Mfalme wa vyote anaye jaa uwezo wa vyote,mtukufu atanguliaye kadiri ya kuenea.

34.Mwingi wa rehema na mlinzi mwema,anae letea watu usalama kuwalinda  na shari ya Shetani.

35.Kila hatua ya mutu huviziwa na Shetani,amemtegea ili amuangushe katika imani.

36.Atakae fuata maubiri na akazoea kusoma kitabu kitukufu hiki kila siku kiasi cha nguvu yake,Mungu atamjaza nguvu ya ushindi.

37.Anae soma aya zake katika mpango maalumu na kuitumia maishani mwake kadiri ya silaha na ngao,ndio shujaa katika mapambano.

38.Mwenyenzi amelea wote kwa usawa,akiwagawia neema mbali mbali kwa ukarimu wa jaza lake.

39.Usimlaumu Mola wako ijapokua umefikiwa na madhara ya aina yote,lakini zidisha ibada,ukisoma aya zake kwa wingi,na kuomba masamaha na wokovu.

40.Mungu pekee ndio aliye huru,afikiwake na asicho kitaka,anaye zidia walimwengu wote.

41.Ni zambi kubwa kabisa kuchanganya nuru na giza,mara hutumia uchawi na mara hutumia ibada.

42.Na wanao tumia vitabu vya ushirikina,ambae kualika majeshi ya zimuni,na kuwafananishia mizimu na roho,wakisema:kuna mizimu nzuri na mbaya,wamepotea.

43.Hakuna mizimu (Majini) nzuri,umbo hizi zingelikua na mila nzuri zisingeli jumuika hadezeni bali mbinguni.

44.Sala ambae hupangiliwa na mizimu,ikisaliwa na mutu,hukurubiwa na jeshi la zimuni,na fadhila yake hukomea zimuni.

45.Mizimu inayo majina mengine katika lugha zingine,usidanganyike ajili ya lugha.

46.Atakaye unga urafiki na mizimu,ameangamiza nafsi yake.

47.Ni vema kuunga urafiki na watakatifu wa mbinguni,ukikurubiana nao kwa njia ya ibada.

48.Hakika kuwasiliana na Malaïka na roho kunaleta furaha ya milele

49.Umbo za kihewa zinazo mteremukia mutu bila kualikwa,na kumuelekeza kwenye dini ya Mungu ni miongoni mwa roho ndogo ndogo ya barazani mwa mbingu.

50.Mushirikina hujivuna anapo tumia jeshi lake,anazani kupata kumbi kupatikana,na amezani kajaa nguvu kumbi kazoroteka.

51.Mungu amemkirimu muaminifu kwa namna ya ajabu,kumruzuku na kumkinga na hatari ya kila namna.

52.Tosheka na ulinzi wa Mola wako,usitafute walinzi wengine kinyume naye,hakuna mwengine kama yeye.

53.Kama dunia ili kunyanyasa,lakini mbingu imekutukuza,umepewa kila unacho hitaji na kufanyiwa wema wa kila namna ajili ya uadilifu wako

54.Mungu ni mkubwa anaye fanya makubwa,akiinuka katika daraja isiyo fananishwa,mwenyi ushindi.

55.Atakaye mpenda sana hunusuru nafsi yake na atakaye mkataa huangamiza nafsi yake.

56.Ni upumbafu kumkataa Mola wako aliye kuumba na ili hali ndio hifadhio ya nafsi yako,hakuna chemchem ingine ya maisha badala yake.

57.Hakika aliye silimu hatendi ila kwa hekima,anaogopa kuruka mipaka aliyo wekewa na Mola wake.

58.Ametakasika Mwenyezi Mungu,mlezi wa viumbe,anaye tarajiwa na wote katika mambo yote,M'bora wa kukadiria.

59.Usiku ni wake na mchana ni wake,mpanaji mkuu anaye zawadia kila umbo,mkuu na mshindi anaye tawala milele.

60.Hapana kuzembea katika imani,Shetani na jeshi lake wanayo desturi ya kiviziana katika uzembe.

61.Na yule aliye dondoka,atakapo tubu,atazingatia wakati roho atakapo mrudilia

62.Roho na Malaika hawarogewake wala kuuwawa, bali huchuguwa hatua na nafsi iliyo dondoka,na kumrudilia tena atakapo tubu.

63.Muaminifu anaye sali sana na kutumia aya za kitabu hiki kama dhikri,atahepushwa na uchawi wa aina yote.

64.Tegemea kwa Mungu aliye uzima,muweza yote aliye chemchem ya maisha,hakuna mwengine kama yeye ambae angaliweza kusimamia jumla ya viumbe.

65.Ametukuzika Mwenyenzi aliye juu,bila yeye kusingeli patikana chochote,m'bora wa kuumba.

66.Mshangiliwa aliye na sifa kamilifu, wa ajabu anaye enea namna ya kujaa katika tendo kua tafauti na uzaifu wa kuishi,mzima.

67.Hana baba wala mama,bibi wala bwana,wala uzaifu wa kujumuika haumkurubie kamwe,wa pekee anaye stawi arshini,hakuna msaada njee ya mapenzi yake,mlinzi mwema anaye fariji viumbe.

68.M'bora wa kuumba anaye umba ginsi ya kuendelesha umbiko,mtukufu anaye helekeza fikara yao kwenyi ugunduzi wapate kutumia faida ya umbiko.

69.Mungu hakuumba chochote kwa bure hapana,bali matayarisho makubwa ajili ya maisha yao.

70.Watafiti wangeli amini vilivyo,kama wangeli funuliwa zaidi,lakini mwingi wa rehema huwafahamisha bila kujali upuuzi wao.

71.Mwenyezi Mungu ni mwema sana na zaidi,amezawadia watu neema ya kila namna.

72.Mchoraji wa pumzi ya wanaadamu,Mjuzi anaye geuza mutu kua roho,M'bora wa kuumba.

73.Kusilimu kwa mutu ndio mwanzo wa uchoraji wa pumzi yake,ndio maana waovu huanguka kadiri ya makapi kandokando yake.

74.Kuona kama nuru na giza haviambatane,ndio maana waovu humshambulia aliye amini wa kianzia na masingizio na kumalizia na ushambulizi mkali.

75.Hakika wao ndio makapi inaye anguka wakati pumzi yake inapo fanyika roho takatifu.

76.Musilimu atakapo jaribiwa,ajiandae kuvumilia na kusamehe,apate kukomaza umbo lake la sasa la kiroho.

77.Yeye ni mfano wa mboleo ya uzuri,nafsi ya mbinguni inayo pamba matunda mazuri.

78.Basi jihazarini,Enyi wanaadamu,musije kuanguka kadiri ya makapi pembeni ya wachamungu.

79.Utakatifu ni wake Mwenyezi Mungu,mlinzi mwema,anaye okoa kutokana na vitimbi vya Shetani.

80.Amani ya Mungu kwa wasilimu wote.

## 6.MAKAO

1.Ametakasika Mwenyezi Mungu aliye uzima ,milki kamilifu itanguliayo kadiri ya kuenea, fahamu ya vyote itokezayo ambacho hakikua, kiongozi wa jumla ya viumbe.

2.Amepana maisha ya milele kwenyi viumbe halisi ambae hutii sheria yake.

3.Kila maisha iko na kawaida yake,iliye muimu kutimilizwa na umbo lake.

4.Ole kwao makafiri ambae hukataa mwongozo utokao kwa Mola wao,wametumikisha matamanivu ya nafsi zao.

5.Neno la Mungu ndio kawaida ya maisha ya mutu,atakaye ishi kinyume na kawaida yake hupotezo umbo lake.

6.Tukuzeni Mola wenu,Mshindi awezaye yote,Mola wa mashariki na magharibi,chemchem ya nuru ulimwenguni.

7.Mlinzi wa viumbe anaye ziwilia watu shari ya kila namna,na kuwafungulia Heri kwa wingi,na kuwafutia giza kwa nuru yake,na kuwafanyia mapito ardhini na angani,Mola wa nyakati zote,mfariji wa milele.

8.Hakuna Mola mwengine kama yeye,wa pekee anaye ruhusu kipatikane ao kikosekane ulimwenguni.

9.Muanzishaji wa vilivyomo angani, na vilivyomo ukiwani,m'bora wa kuumba.

10.Tatizo hizingira maisha ya watu ajili ya kupinga sheria ya Mungu,hakika Mwenyenzi ndio mtatuzi wa mashida,Mkarimu aliye juu.

11.Teteeni namna ya kufika mbinguni mupate utimilifu,mutaishi bila kufikiwa na kifo,wala hamtafikiwa na msiyo ya taka,bali furaha ya milele.

12.Kuweni na upendo na fanyeni dhikri kwa wingi ,mukirudilia aya zake kwa kuisoma kiasi cha nguvu yenu,na kumtapa hakika ya kadiri yake.

13.Namna ya kuonesha shukrani kwa Mola wako kufatana na uwingi wa rehema zake.

14.Na ndio namna ya kupakiza nguvu ya ushindi ndani ya nafsi yako.

15.Dhikri ni ibada kubwa,mfano wa funguo ya kheri,maana anapo tukuzwa Mungu ndipo Shetani hulia.

16.Na kulia kwa Shetani ndio alama ya mafanikio ya mutu,kwani inapofanyika dhikri hushuka rehema ya Mungu kwa wingi.

17.Na anapo kataa mutu kumtukuza Mungu ndipo Shetani hucheka.

18.Na kucheka kwa Shetani ndio alama ya hasara kwa mutu,kwani laana humfikia anaye kataa kumtukuza Mwenyenzi.

19.Kesheni katika ibada mujichugulie jaza la nuru litokalo mbinguni.

20.Malaïka na roho huporomoka taratibu,kufuata sifa ya Mwenyenzi,wakileta fadhila nyingi kwa waja wake.

21.Mlinzi ni Mungu, muhifadhi wa milele,anaye nusuru shaidi wake na shari ya kila namna.

22.Makafiri wameimizwa na Shetani ili washambulie haki,hawata weza kumuangamiza ambae Mungu kamuokoa.

23.Nuru ya wachamungu huangamiza giza iliyemo ndani mwao makafiri.

24.Hakika nuru na giza haviambatane kamwe ,maana uyu ni kinyume cha yule.

25.Bila shaka waaminifu hufikiwa na vitimbi vya kila namna ambae hujaribu kuangusha haki.

26.Yule atakaye vumilia na kubakia imara bila kugeuka,pumzi yake itageuzwa roho takatifu na kupata neema ya kuishi milele.

27.Mola wenu ni mwepesi wa kuhisabu katika kheri kuliko shari,mpenzi wa watu.

28.Watu wengi wamepotea ajili ya ushirikina,wamejaana na jeshi la zimuni bila woga ajili ya kuipenda sana dunia.

29.Na wanao silimu pasipo kutubu wamepotea,maana wao ni wanafiki,wanazidi kutumikisha jeshi la zimuni,wamejiwekea kiziwizi baina yao na nuru ya Muumbaji wao.

30.Magumu ya dunia isiwapotezeni,enyi wanaadamu,hiyo ni mtihani, kuweni yakini kwamba itakwisha na baadaye furaha ya milele.

31.Katika wema wake mshindi,hubadiri machungu kua furaha ,maana yeye ni Baba wa salama aliye Salama

32.Hakuna mfano wake popote,maana kilicho njee ya dhati yake ni tafauti naye,ijapokua neno lake sio yeye.

33.Mwenyenzi hagusanake na chochote,maana yeye ni Mkamilifu ,kugusana ao kuchagikana na kitu zaifu ao pungufu ni kuzaufika ao kupungukiwa.

34.Na ijapokuwa umbo fulani hufanya miujiza,haina uzima,maana uzima ndio ukamilifu.  Ingeli kua na uzima isingeli jumuika duniani wala hadezeni wala mbinguni,bali ingeli stawi enzini.

35.Mungu hawezi kujumuika katika umbiko bila hiyo kufutika,maana Enzi yake hufuta upungufu wote kando kando yake,hakuna ginsi ya kukurubia dhati yake.

36.Kama unaona yeyote ama chochote duniani ao hadezeni ao mbinguni,tambua ya kama ni mwana hewa ao muzila hewa.

37.Hapana kumfananisha yeyote na Mwenyenzi,hakika Mola wenu ni tafauti kabisa na viumbe.

38.Kuonekana na umbo fulani ni kua kiumbe fulani.

39.Na kulazimisha Mungu aonekane na umbo fulani ni kulazimisha Mungu awe kiumbe fulani.

40.Eti hakustahili kupatikana muumbaji isipokua viumbe pekee yake?

41.Kama ndivyo kitajitokezaje kiumbe ambae ni zaifu pasipo muumbaji?

42.Haiwezekane kuonana uso kwa uso na Mwenyezi aliye muuijiza wa maajabu,ambae hana uso wala umbo.

43.Enzi iko mbali sana na dunia;vilivyomo duniani tu hauvizingatie vyote,wala vilivyomo hadezeni na pia vilivyomo mbinguni na ili hali ndio vilivyo pamoja  nawe angani na ukiwani.

44.Hakuna kujumuika wala kufanana katika umungu na ndio maana katika viumbe vyote hakuna mfano wake.

45.Ni wapekee anaye tawala ulimwenguni bila mshirika,angeli fanana na fulani hasingeli kamilika;bali angeli kosewa uwezo wa kutangulia kadiri ya kuenea.

46.Mungu ni Mfalme anae inukia kila kitu,viumbe vyote ni chini ya uwezo wake katika  mambo yote.

47.Kila mutu ashike imani hii ya kumpwekesha Mwenyenzi peke yake,hakuna anaye fanana naye.

48.Kila kilicho njee ya dhati yake ni miongoni mwa viumbe,ijapokua nuru yake sio sawa naye

49.Vitu vyote ni katika upungufu,hakuna anaye fanana naye,maana ukamilifu uliye umungu ni katika upekee.

50.Shuudieni umoja wa Mungu,enyi watu,hakika Mola wenu amewapenda sana wanaotoa shaada.

51.Na anaye shaidilia umoja wa Mungu,akakubali ujumbe wake wote,yeye ndie anaye silimu.

52.Mungu alitangulia katika mamlaka yake mwenyewe,anaye miliki kila kitu, Bwana wa ma bwana.

53.Ni kheri kumtegemea peke yake,katika magumu na furaha,vyote ni vyake yeye muweza wa vyote.

54.Sio zambi kutunzwa utakapo gonjwa,lakini usifanye shirki.

55.Sio zambi kuuliza usicho fahamu,ni vema kuchuma elimu katika neno la Mungu,upate kuridhika usiwe mnafiki.

56.Sio zambi kulipisha kisasi kwa yule anaye chupa mipaka,lakini ni bora zaidi kuvumilia na kusamehe.

57.Sio zambi kuowa,lakini uowe mwanamuke ao wanawake,njee ya undugu wa damu.

58. Sio zambi kuolewa,lakini uolewe na mume njee ya undugu wako wa damu.

59.Alaaniwe yule anaye owa mwanaume mwenzake,na alaaniwe yule atakaye olewa na mwanaume mwenzake.

60.Na alaaniwe yule anaye owa mwanamuke mwenzake,na alaaniwe yule atakae olewa na mwanamuke mwenzake.

61.Na walaaniwe muke na mume wanao zini njee ya ndoa zao.

62.Watoto ndani ya ndoa ni wa bwana na bibi na hupewa haki ya kuwarithi.

63.Muzinifu hastahili kupewa isipokuwa azabu ya kifo,hakika madhalimu hunyimwa fadhila zote.

64. Maisha haiendelee pasipo sheria ya Mungu,tumieni uadilifu popote mtakapo kua,na ogopeni Mungu,wala msiruke mipaka.

65.Mupendane wote kwa jumla,hakika upendo ndio jambo kubwa katika imani,imehepusha mutu kutenda mazambi mengi.

66.Utukufu ni wake Mwenyenzi Mungu,anaye chipua maisha ya kila aina,Mwalimu wa jumla ya wapumuao.

67.Mola mwenyi uwezo wa ajabu,mamlaka ya kudiriki vyote kwa jumla,M'bora wa kuumba.

68.Mufalme anaye tawala vitu vyote bila mshirika,wa pekee anaye angazia kila umati,taa ya ulimwengu.

69.Ma Nabii na Mitume ndio vipenzi vyake ambae hutangaza kweli yake kwa kauli na matendo.

70.Maneno wanao kuja nayo sio yao,lakini ya Mola wao aliye watuma

71.Na yule atakaye fitinisha baina ya Mjumbe na watu wake ili wasimuamini aliye tumwa,ni mfano wa pumbafu anaye jiandaa vita na Mola wake.

72.Mola wenu ni mwingi wa huruma,hata waacheni mayatima bila kiongozi.

73.Mungu ametukuzika namna yote,amehepukana na upungufu sababu ya kukamilika kwake,hapungue wala haongezeke,mwenyi kuenea bila kasoro.

74.Yeye ni yote katika yote zaidi ya yote,Bingwa mshindi anaye tenda bila kufanya kazi.

75.Mungu wa miujiza anaye miliki ulimwengu,muabudiwa anaye sikia na anaye jibu maombi ya watu.

76.Ametangulia katika uwezo na katika ujuzi hali ya kua muweza wa vyote na mjuzi wa yote.

77.Mjuzi anaye tabiri kuzaliwa kwa mujumbe wake kabla ya ndoa ya mababu wa huyo.

78.Anajua yalio pita yote,ya sasa na yote yatakayo kuja baadaye.

79.Yeye ndio mwanzo wa vyote,chemchem ya upatikaji na maisha .

80.Kila kilicho na mwanzo kipo na mwisho,kilicho muanzisha kinaweza kumukomesha.

81.Sema:Mwenyezi habadirishake makao kama vile kiumbe,kwake hakuna kuhama,wala kushurulika maana yeye ni mwenyi kukamilika.

82.Yule asiye kua na mwanzo ndie asiye kua na mwisho sababu ya kutangulia kadiri ya kuenea,maana yeye ni mkamilifu.

83.Amestawi milele katika Enzi tukufu,Milki isiyo gusana na chochote cha umbalimbali naye.

84.Mamlaka yake ni kubwa zaidi,hupoteza kwa rafla upungufu wote kandokando yake.

85.Mtukufu aliye pasipo yeyote,wa pekee kadiri ya mwanzo wa vyote,Mjengaji wa makao ya wote anaye pangiza viumbe.

86.Fasi yenye Mungu iko ndipo alipokua na ndipo atakapo kua milele na milele.

87.Amani ya Mungu iwe juu ya wasilimu wote.

## 7. DAWA

1.Utakatifu ni wake Mwenyezi Mungu,muhifafhi wa milele anaye meremeta zaidi ya mwangaza.

2.Mumiliki wa falme zote,asiye kurubiwa na yeyote ku vyovyote ulimwenguni.

3.Anga na ukiwa hutii amri yake,wala hakuna umbo njee ya kawaida yake.

4.Mtukufu wa kauli ajaaye mamlaka kadiri ya uwezo wa vyote.

5.Hutokeza ambacho hakikua popote,amekua yote katika kutenda ,na yote katika kufahamu,Bwana wa ulimwengu.

6.Mtakatifu wa ajabu anaye jaa huruma,ambae husamehe zambi zao wanao tubu.

7.Mungu mkubwa anaye tenda kwa haki,ambae ajabu ya tendo lake hufanyika kadiri ya fumbo mbele ya viumbe.

8.Nuru juu ya nuru,tumaini na kimbilio,mwenyi kujieneza kadiri ya ukamilifu.

9.Mola wa pekee anaye jumuisha walimwengu kwa idhni yake.

10.Mamlaka yote imetoka kwake,ni yeye anaye podoa wasilimu na rangi yake takatifu.

11.Mlezi wa viumbe aliye na upendo,ambae kawawekeeni wasaidizi katika maisha yenu.

12. Ameumba mbingu angani na dunia katika maunganio ya anga na ukiwa,kadiri ya mpango maalumu.

13.Mungu mjuzi aliye Enzini,muujiza wa maajabu ulimwenguni.

14.Watu wamenajisi utukufu wake katika masemi yao,maana lugha zao hazitimize hakika ya hali yake.

15.Hakika ujuzi ni tafauti kabisa na fikara,kila atendalo mwenyi ujuzi huzidia kabisa kutenda kwao wenyi fikara

16.Ni mshindi juu ya kila kitu,Mola wa ulimwengu wote,Mfalme anaye stahili kuhimidiwa.

17.Amejaa uwezo usio na kipimo,ambae humiliki vyote ulimwenguni

18.Mushinda-kushinda anaye tawala viumbe vyote kwa jumla,uwezo wa kuenea.

19.Hakika,ushindi ni wake Mwenyezi,M'bora wa mahakimu afanyaye mambo yote kwa haki.

20.Hazulumiwe yeyote miongoni mwa viumbe vyake,kila yule amefanikiwa na rehema zake kadiri ya kipaji chake.

21.Umbo zote hutoshelezwa naye,kwake hakuna upendelevu,ujuzi wake umetimiliza umbiko katika kawaida yake.

22.Usilaumu lolote,lakini kuwezi yakini kwamba mfinyanzi wenu amejua sana na zaidi.

23.Umbiko ni mfano wa fumbo ambae hufumbilika na yule anaye funuliwa na Mungu.

24.Ugunduzi wote wa mutu kuhusu vifaa vya nafsi yake,katika maisha yake,unatoka kwa Mungu.

25.Maisha njee ya nuru haiendelee,lakini hukoma kadiri ya kupotea.

26.Komboa nafsi yako kwa kutumia neno la Mungu,maana hutatua shida zote maishani.

27.Hakika neno la Mungu ni dawa ya kila magonjwa.

28.Watu wangeli fahamu faida ya kisomo kitukufu namna ya dhikri,kama wangeli kua nasoma kauli tukufu ya kitabu hiki mara na mara kila siku.

29.Kauli tukufu ni mamlaka ,kutokezwa kwayo ni ajabu ya kupatikana kwa rafla ambacho hakikuwa.

30.Mungu hujitukuza sana katika neno lake: atakaye itumia atajazwa nguvu ya ushindi,wala nafsi yake haita vamiwa,lakini itaishi salama milele.

31.Atakaye itumia katika kawaida yake,atafanyika umbo mpya ya mbinguni.

32.Laiti mungeli musikia Yesu Masia,mtukufu wa daraja aliye mfano wa kauli tukufu.

33.Nuru kubwa yenyi nguvu mbinguni kadiri ya roho takatifu,wokovu wa watu.

34.Ametakasika Mwenyezi Mungu,mneemeshaji anaye tukuza nafsi ya musilimu.

25.Mola wa majeshi yote,anaye simamisha imara ufalme wa kipenzi chake.

36.Na kuvunja jeuri ya makafiri,na kulainisha kilicho kigumu.

37.Ni wewe unaye nusuru mutu aliye katika hatari,ukimsimamisha aliye anguka.

38.Vikwazo vya maisha yake,hutoweka kama vile giza hufukuzwa na nuru.

39.Mumgu ni ponyo ya kila nafsi,msaada na wokovu wa watu.

40.Amemupa ushindi mutumishi wake,na kuwazalalisha watesi wake.

41.Utulinde kutokana na zulma,fitna pia na masingizio ya watu wa Dunia.

42.Sisi hatuna tegemeo ingine kinyume nawe.

43.Na kweli umetutosheleza katika maitaji yetu.

44.Mungu mkuu anaye lipisha kisasi,ambae humpiga aliye kusudia kutupiga, na humnyanyasa aliye kusudia kutu nyanyasa.

45.Mtukufu aliye na ushindi juu ya kila kitu,anaye rehemu na anaye kirimu.

46.Uzima wake hauzingatiwe isipokua na wenyi akili.

47.Ni muujiza mkubwa sana usio lingana na chochote,jambo ambae hizidia fikara ya viumbe,iletayo msangao,ajabu ya utukufu wake.

48.Mtangulizi pasipo msaada wa yeyote, atawalaye katika ulimwengu, uwezo wa kuenea.

49.Bingwa aliye na milki kuu,anaye fanya jambo bila shuruli yoyote,ambae idhini yake kutenda.

50.Bwana wa mabwana aliye chemchem ya uwezo na fahamu,atakasikaye na ashindaye.

## 8. MUMILKI

1.Ametakasika Mwenyezi Mungu,mumilki,anaye pinduwa mipango ya maadui.

2.Mlinzi mwema anaye semelea walio onelewa na kuwapanguza machozi wanao lia.

3.Mumilki anaye jazikisha palipo wazi,na kunyoosha kilicho kunjama,na kuunganisha kilicho vunjika .

4.Hakuna kufaulu inje ya msaada wake,mtefuzi wa kila zamiri,anaye ona yote na anaye sikia yote.

5.Mola wa manabii na mitume wote,chemchem ya upatikanaji na maisha,kiongozi pekee wa jumla ya viumbe.

6.Hakuna bwana asiye muita Mungu bwana ,wala asiye tetemeka mbele yake,mufalme wa wafalme wote anaye jaa milki kamilifu,mwenyeji wa ulimwengu.

7.Alikua,yuko na atakua,mwenyi kuenea;hakuna mwengine kama yeye, wa milele aliye juu.

## 9. IMANI TIMAMU

1.Usalama wa nafsi katika mapenzi ya Mungu ndio usilimu,dini ya Mungu kwa watu wote.

2.Mtume anaye fundisha dini kinyume na hii,ni wa uwongo.

3.Kama unamtaja mtume uyu katika shaada yako na yule anamtaja mtume mwengine katika shaada yake,nyinyi wote ndio wasilimu.

4.Ispokuwa yule atakaye shaidilia  Mungu mwengine kinyume na Mwenyenzi Mungu,ndiye kafiri aliye njee ya usilimu.

5.Usilimu sio kwa yule anaye mtaka nabii ao mtume fulani,lakini kwa yule anaye muamini Mungu na mitume wake wote.

6.Sio kwamba usilimu ni kwa yule anaye muamini Muhamadi peke yake,wala sio kwa yule anaye  muamini Yesu Masiya peke yake.

7.Kama mutu anasali kwa kumuhimidi Mungu na kufunga sala na kusoma sura ya ufunguzi kulingana na shaada yake,na kusujudu pia na kutoa shaada katika kipindi maalumu,bila shaka mutu uyu ni musilimu.

8.Atakaye mtaja Muhamadi katika shaada yake,itakubaliwa na Mwenyenzi lau kama moyoni mwake ame waamini pia ma Nabii na Mitume wengine wote.

9.Na atakaye mtaja Yesu Masia katika shaada yake,itapokelewa na Mungu lau kama moyoni mwake amewaamini ma Nabii na Mitume wengine wote.

10.Na anaye amini mitume wote,ameamini pia vitabu vyao vyote,haiwezekane kuamini mtume ambae haukubali maneno yake.

11.Kitabu cha Mtume wa Mungu ni kile kinacho andikwa kwa njia ya ufunuo,sio kinacho andikwa kwa njia ya utafiti.

12.Katika utafiti munamo hitilafu,maana ni Kazi ya kibinaadamu" yenyi upungufu.

13.Anaye amini kitabu hiki kitukufu cha "ukweli",ni lazima kwake aamini pia Qur'ani na Injili na Zaburi na Taurati.

14.Na anaye amini Qur'ani ni lazima kwake kuamini kitabu hiki cha "Ukweli" na Injili,Zaburi na Taurati

15.Na vivihivyo kwa yule anaye amini Injili,Zaburi na Taurati,ni amri kwake kuamini kitabu hiki cha "Ukweli" na pia Qur'ani.

16.Sio muaminifu yule anaye amini sehemu na kukataa sehemu ya kauli tukufu.

17.Na ndio maana haifai kuchanganya utafiti na ufunuo.

18.Amani ya Mungu kwa wasilimu wote.

## 10. AL-KARIM

1.Utukufu ni wake Mwenyenzi Mungu anaye funulia watu ili wapate kusadiki uzima wake

2.Watu hawawezi kumzingatia bila kufunuliwa,maana fikara yao ni yenyi kuzaufishwa na mwili

3.Utukufu wa mutu unatokana na nuru ya Mungu: anaye funuliwa ndio mtukufu na asiye funuliwa ndie mdhalili

4.Mungu alimutukuza Muhamadi kwa kumjaza nuru ya zamana ambae humulika duniani na mbinguni

5.Popote alipo kua duniani palionekana pamejaa nuru kubwa kadiri ya umbo ya zamanani.

6.Alipewa kazi kubwa ya kufundisha usilimu,

7.Hakika asiye amini kwamba Qur'ani ni Al-Karim,hataingia mbinguni;asema roho wa Mungu

## 11. UTAALAMU

1.Ametakasika Mwenyenzi Mungu atanguliaye kadiri ya kuenea,juu ya maala pa juu

2.Uzima wake ni mbalimbali na kila kitu, ukafikiria kuhusu umungu,usizani kama kuna mfano wake,hakuna kitu cha kilinganisha na ukamilifu.

3.Usilazimishe kumuona Mungu na hiyo macho ya mwili wako isiyo zingatia ila miili peke yake

4.Hauta muona kimwili yeye asiye kua na mwili,tena asiye jumuika angani wala ukiwani

5.Ukalazimisha Muumba akuonekanie ama ajumuike pamoja nawe,ni kwamba umelazimisha ageuke kiumbe,jambo lisilo wezekana

6.Umutu na mambo yake yote ni katika upungufu, hali kama hii haichuguane hata kidogo na mwenyi uzima

7.Kumbi usimtazame Mola wako kimwili,lakini umtazame kiroho ili upate kuzingatia uzima wake

## 12. ALAMA YA DINI

1.Enyi walio silimu! fanyeni ibada katika usawa,usifanye upuuzi katika kazi ya Mungu,wala usijifanyie lolote pasipo mwongozo wa Mungu wala usifute kitambulisho cha Dini

2.Na anaye jidai kusali kiroho pasipo kudhihirisha Sala yake kimwili ni miongoni mwao wafutao alama za dini ya Mungu.

3.Umbo la mutu ni timilifu katika changachanga ya mwili na pumzi

4.Mutu angelikua pumzi peke yake,asingeli jumuika duniani,lakini mbinguni (ao hadezeni).

5.Nyenyekea uzima wa Mungu kimwili na kiroho,ili upate kutimilika

6.Kutumikisha mwili wako katika sheria ya Mungu ndio kuamini Mungu

7.Mwili wako ukatenda zambi,roho yako pia huchafuka,usijidai kua roho tupu na ili hali upo na mwili,yaani ukingali duniani

## 13.. SAUMU

1.Enyi walio amini! Mumelazimishwa kufunga saumu kwa kufuata jukumu lake.

2.Saumu inayo sehemu mbili,kulingana na umbo lako:sehemu ya kimwili na ya kiroho.

3.Kutokula wala kunywa tangu asubui mpaka mangaribi,ndio kufunga kimwili.Na kutotumia kiungo chako hata kimoja kwa kutenda zambi,ndio kufunga kiroho.

4.Kimwili utafunga muda fulani na kufungula muda fulani,lakini kiroho utafunga bila kufungula mpaka mwisho wa umri wako.

5.Yule atakaye funga kimwili-tu bila kiroho ni miongoni mwa wanafiki;na vivihivyo kwa yule atakaye jidai kufunga kiroho-tu bila kimwili ni mnafiki.

6.Na kama hali yako haistahili:kama vile afya,safari,jela,umri... basi usifunge kimwili.

7.Usitumikishe roho ajili ya kuujenga mwili peke yake,ni bora zaidi kutumikisha mwili wako katika kuijenga roho yako,ili upate kurithi bustani ya neema mbinguni.

## 14. SIJIDA

1.Ametakasika Mwenyezi Mungu,wa pekee anaye stahili kusujudiwa.

2. Lengo ya kuumbwa kwa mwanaadamu ni kumuabudu Mungu.

3. Na kilicho muimu katika tendo kuabudu ni sijida.

4. Hakuna sala pasipo sijida na haistahili kwa mwengine ispokua kwa muumba peke yake.

5. Sijida ndio tendo kubwa la unyenyekevu,linalo leta utafauti kati ya sala na dua(maombi),ambae humaanisha kuabudu.

6. Kuona kama sala ndio ibada kubwa zaidi,ndio maana matendo haya makubwa, sijida na shaada, hupatikana ndani mwake.

7 .Kuinama kadiri ya kupeleka uso mpaka chini,katika unyenyekevu,ndio kufanya sijida ,

8.kujishusha mbele ya Mungu kwa utiifu na heshima.

9. Asiye msujudia Mungu sio mnyenyekevu wala hana sala.

## 15. UPEKEE

.1.Ametakasika Mwenyenzi Mungu Mjuzi atendaye makuu ambae milki yake hustaajabisha

2.Upekee wa dhati yake humfanya azingatiwe na wenyi akili peke yake

3.Wasio kua na akili hawawezi kugundua uzima wake ajili ya uzaifu wa fikara yao.

4.Mwenyenzi ni Mkamilifu,amepatikana kadiri ya kuenea bila mwanzo wala mwisho.

5.Uwezo wake wa ajabu unamfanya kua katika upekee,hachuguane na yeyote wala hachangie fasi na yeyote.

6.Amestawi kikamilifu kadiri ya mwanzo wa vyote,chemchem ya upatikanaji na maisha.

7.Alikua,yuko na atakua,Mufalme wa milele.

## 16.UFUNUO

1.Mwenyezi Mungu amefunulia waaminifu katika njia mbalimbali,zaidi sana katika ndoto.

2.Nuru imezidiana kufatana na daraja ya watumishi.

3.Ma Nabii na Mitume ni wenyi nuru kubwa,ndio maana ufunuo wao ni bayana.

4.Ufunuo wote sio unabii wala utume,unaweza kufuniliwa na ili hali wewe sio nabii wala mtume.

5.Usijidai utume ajili ya kufunuliwa,mpaka Mungu akutume ku watu na ujumbe wake.

6.Hakuna mjumbe pasipo ujumbe.

7.Na usiwe kama aliye gizani:kutofunuliwa hata kidogo ni alama ya imani haba.

## 17. UCHUPAJI

1.Ametakasika Mwenyenzi Mungu,kiongozi mkamilifu,anaye endelesha ulimwengu kadiri ya idhni yake

2.Mwenyi sifa kamilifu,anaye fanya yote tafauti na wote

3.Sifa ya viumbe ni pungufu ajili ya kutokamilika

4.Usimtukuze yeyote kwa sifa isiyo kua yake,ijapokua Nabii,usije kaangamia ajili ya kuchupa mipaka

5.Uzuri wa jambo ni kati kwa kati,usizidishe wala usipunguze

6.Wengi wamefikia kuabudu Nabii ajili ya kumsifu kwa kuchupa mipaka

7.Mungu peke yake ndie anaye stahili kusifiwa sifa ya aina yote,kwani yeye ni mkamilifu,mwenyi uwezo wa vyote.

## 18. SHAADA

1.Hakuna Mola mwengine apasaye kuabudiwa ila Mwenyezi Mungu peke yake,na hakika Yesu Masiya ni Mtume aliye tumwa naye.

2.Hii ndio Shaada ya musilimu anaye tumia nuru ya Mungu katika dhati tukufu ya Yesu Masiya.

3.Hakuna Mola mwengine apasaye kuabudiwa ila Mwenyezi Mungu peke yake,na hakika Muhamadi ni Mtume aliye tumwa naye.

4.Hii ndio shaada ya musilimu anaye tumia nuru ya Mungu katika dhati tukufu ya muhamadi.

5. Kukiri kwa yakini kwamba Mungu peke yake ndio mwenyi uzima,na kushaidilia ya kwamba hakuna mwengine kama yeye ,na pia kuamini mitume wote,ndio kutoa shaada.

6. Anaye mtaja Yesu Masiya katika shaada yake pamoja na yule anaye mtaja Muhamadi katika shaada yake wao wote ndio wasilimu.

7. Atakaye bagua miongoni mwa mitume ndie kafiri asiye amini kauli ya Mungu; hakika shaada ndio tendo la msingi wa imani.

8. Kumtaja Nabii ao Mtume fulani katika sehemu ya pili ya shaada yako sio kuwakanusha wengine,hakika kuamini mitume wote ndio imani ya kweli.

9. Ni bora sana kumtaja mtume wa zama zako ao mitume wakuu ,katika sehemu ya pili ya shaada yako.

10. Hakika shaada ndio msingi wa imani,ambae huleta utafauti baina ya musilimu na kafiri.

11. Hakuna imani pasipo shaada ya mungu.

12. Yeyote asiye toa shaada sio muaminifu lakini kafiri.

19 . HALI

1.Ametakasika Mwenyenzi Mungu,Mzima,anaye stawi katika utukufu usio kurubiwa na yeyote

2.Hali yake ni tafauti na viumbe vyote,na ndio maana makao yake ni tafauti na kambi za wengine wote

3.Yeye hana pumzi wala mwili,ndio maana hapatikane angani wala ukiwani

4.Lau kama angelikua na hali ya viumbe,bila shaka angeli jumuika pamoja na viumbe

5.Kutojumuika pamoja na viumbe sio kukosekana ulimwenguni,kambi lenu sio ulimwengu wote

6.Hali yake ni tukufu ajabu inamfanya atengane na vitu vidhalili milele na milele

7.Amepatikana Enzini maala pa upekee,ukamilifu hauchangane na upungufu kamwe.

## 20. UCHIMBI

1.Ametakasika kabisa yule aliye Enzini,Mfalme anaye hukumu vilivyomo angani na ukiwani

2.Mamlaka itokezayo kuujaza ulimwengu,mtendaji wa jumla ya matendo

3.Mbingu na dunia hufuata hukumu yake,kiongozi wa mwili na roho,anaye miliki falme zote

4.Mamlaka yote imetoka kwake ;amempandisha amtakaye na amemshusha amtakaye

5.Uchimbi ni haramu kwa musilimu;usimgombanishe kiongozi wako wala jerani yako bila sababu,lakini umuombee ili Mwenyenzi amfanye kua muadilifu

6.Wala usipiganishe dini ya Mungu ajili ya kuimarisha mila ya ukafiri

7.Mwenyenzi ndie wa kutegemea katika yote,maana vyote hutokea kwake,ni yeye peke yake aliye na uwezo juu ya kila kitu

## 21. USWAHABA

1.Neno la Mungu ndio nuru inayo angazia watu duniani

2.Mungu amemteremshia nuru amtakaye na kumupa kazi ya kiroho

3.Kuona kama amemupatia mutu kama wao,wengi huchukia na humzarau aliye tumwa

4.Ni aibu kwao kumfuata mutu kama wao,ambae wamemzidia utukufu wa kidunia

5.Kumuamini mtume na kumfuata katika uhai wake ni neema,na ndio maana ni wenyi daraja mbinguni maswahaba wa mitume

6.Watu hujiunga upesi kwao watetezi wa mambo ya kidunia ajili ya hanasa ya dunia

7.Hawana yakini na uzima wa Mola wao ajili ya upofu,hawazingatie inje ya dunia.

## 22. USINGIZI

1.Uzima ni.wake Mwenyenzi Mungu,wa pekee anaye kamilika ulimwenguni

2.Asiye kubali uzima wa Mungu ni kwamba bado kuamuka katika usingizi

3.Watu wengi wameamini kwa midomo-tu,lakini moyoni hawana yakini na ukamilifu wake

4.Ni kwa sababu hawatumie njia yake ndio maana hawazingatie utendaji wake

5.Mungu ndio msimamizi wa maisha,mwenyi mamlaka ya ajabu ambae idhni yake hutenda bila kutumika kazi

6.Mola wa miujiza afanyaye maajabu,Mjuzi anaye hifadhi yote yanayo tendeka kila fasi na kila wakati, M'bora wa kuenea

7.Hakuna Mola mwengine kama yeye,mumiliki,aliye tayari kutokeza mapya kila wakati pahali pote,wa pekee aliye na ushindi.

## 23. DINI MOJA

1.Usilimu ni usalama wa nafsi katika mapenzi ya Mungu .

2.Na ndio dini ya Mungu tangu mwanzo mpaka mwisho wa dunia.

3.Hata mababu zenu (wazee wenu) walikua wasilimu miongoni mwao kulikua wachaguliwa ambae Mungu kawafunulia na kawajaza roho kwa namna mbalimbali.

4.Maneno walio pokea haikuandikwa yote,lakini kayahifadhi vifuani kadiri ya kanuni yao.

5.Shetani akawa shawishi ili waingize shirki katika ibada yao,kama ilivyo desturi yake kwa kila umati.

6.Mwenyenzi alionesha mapenzi yake kwa kila kabila na kila umati,akiwajaalia nuru kulingana na fikara yao wakati wao.

7.Walio silimu miongoni mwa mababu zenu walikuwa na mila nzuri sana,ya upendo kati yao na unyenyekevu kwa Mwenyezi Mungu.

## 24. TUNDA LA SHETANI

1.Ole wao wanafiki wanao jiundia wenyewe ma kundi ya kidini ajili ya anasa ya dunia

2.Hawana dini ispokua hufichamia katika neno la Mungu na ilihali hawana imani.

3.Wengi ni wanasiasa wanao tumia jina dini,ili  wafaulu katika mambo yao

4.Na wengine ni wachawi ambae hutumia jina dini katika vikundi vyao ili wawadanganye watu

5.Na wengine hutumia neno la Mungu kama viashara ili watajirike kwa pesa na vifaa vya kimwili

6.Wanafiki kama hawa ndio wanao kataa kabisa kusilimu katika kweli na haki,maana wao  ni «  Tunda la Shetani «

7.Ispokuwa wanao tafuta kweli njia ya Mungu ndio wanao silimu na kutubu.

# 25. KIPINDI

1.Na utakapo nuwiya kusali ni lazima huelekeza akili yako yote kwa Mungu,kumuhimidi na kufunga Sala

2.Katika kisomo chako anzia na sura ya ufunguzi kulingana na shaada yako

3.Atakaye tumia dhati tukufu ya Muhamadi ,ni lazima kurukuu na kusujudu, (kulingana na kipindi anacho sali).

4.Na atakaye tumia dhati tukufu ya Yesu Masiya ni lazima kusujudu bila kurukuu,(kulingana na kipindi anacho sali).

5.Imamu mbele na wengine wote nyuma yake katika masahafa ,juu ya misala ao mfano wa hayo ;

6.Hakika mnao mfano bora kwake Muhamadi,na Yesu Masiya pamoja na mitume wengine wote

7.Watu wasio fahamu kusali ni wale wasio amini mitume wote,wanampinga mwalimu wa sala,ndio maana wanabakilia -tu katika maombi peke yake

## 26. KIVULI CHA MTUME

1.Ametakasika Mwenyenzi Mungu anaye fadhilisha mutu kwa kumkutanisha na neema

2.Mutu anaye jazwa roho takatifu ni nuruni na matendo yake ni yenyi kubarikiwa

3.Ameongozwa katika yote ,mwenyi hekima timamu ambae huujenga sawasawa umutu wake

4.Hafikiriake mabaya wala kuyakurubia,miguu yake urakibuni maisha yote

5.Amewanukulu ma Nabii na Mitume katika hoja na tendo,wala hatumikishe matamanivu ya nafsi yake bila kuyalinganisha na kauli tukufu

6.Mutu atakaye iga mila ya Mitume atakua kama kivuli cha Mtume,mwenyi kujazwa roho takatifu

7.Mungu peke yake ndio anaye stahili kupelekewa shukrani,Msamehevu na Mrehemevu,hakuna mwengine kama yeye.

27.UTANGULIZI

1.Wengine hawa muamini Mola wao katika yakini sababu hawaonane naye kama wanavyo onana wao kwa wao

2.Na ili hali wao ni katika upungufu mfano wa vifebe,hawastahili hata kidogo kukurubiana na ukamilifu

3.Enzi yake ni milki kamilifu inayo waka bila mfano wake ambae hufuta  kwa rafla upungufu wa aina yote kando kando yake

4.Na ndio maana hakuna umbo yenyi kukurubiana na Mwenyenzi katika makao wala katika fahamu wala katika uwezo

5.Tendo kutangulia ni jambo ndogo sana kwa yule aliye kamilika,ndio kawaida yake sababu ni muweza yote,anaye enea kadiri ya uzima

6.Kutangulia ni  tendo lisilo wezekana  kamwe kwa yule mpungufu sababu hukosewa milki kamilifu,ndio maana yeye huanza maana ni hununsu na kipande.

7.Shangilieni uzima wa Mola wenu aliye Enzini,Mshindi,awezaye yote na ajuaye yote

## 28. TASWIRA

1.Ametakasika Mwenyenzi Mungu,m'bora wa kuumba aliye umba mbingu saba na ardhi saba.

2.Na baina ya mbingu na ardhi akaumba Hadeze na dunia,kadiri ya maunganio.

3. Dunia juu ya ardhi na hadezeni chini ya mbingu.

4. Aliye na mwili mzito unao changikana na pumzi mwepesi,hudhihirika duniani.

5. Na aliye na pumzi nzito inayo changikana na mwili mwepesi ,hudhihirika hadezeni.

6. Ndio maana husemekana hadeze hupatikana angani na dunia hupatikana ukiwani.

7. Huzingatiwa  na watu viumbe vinao husika na maisha yao,na havizingatiwe na watu viumbe visio husika na maisha yao.

## 29. MASHAKA

1.Ushindi ni wake Mwenyenzi Mungu,anaye tokeza anga na ukiwa pamoja na vilivyomo

2.Hakuna mwengine aliye na ujuzi kama yeye na ndio maana haifae kushakia lolote katika ujumbe wake

3.Kushakia neno litokalo kwa Mungu ni alama ya uchache wa imani na alama ya kiburi

4.Kama kweli upo yakini na ujuzi wake,haustahili kushakia utendaji wake,hauna budi ya kumkosoa Mjuzi

5.heri yule aliye amini maneno ya Mtume bila kushakia lolote analo sema wala analo tenda,maana ni mwenyi yakini kwamba ameongozwa na roho wa Mungu

6.Kushakia asemalo Mtume ni kushakia kauli ya yule aliye mtuma,jambo ambalo humaanisha uchache wa imani

7.Mutu sio chochote katika fahamu wala lolote katika uwezo mbele ya yule aliye muumba

## 30. ALIKO LA JESHI

1.Roho takatifu ndio zawadi wanao pewa walio amini,inateremuka tokea juu mbinguni kwa amri ya Mungu Mwenyezi

2.Kwa kupokea zawadi hii kwanza ni kusilimu na kutubu na kujitolea sana katika ibada

3.Kusali kila siku asubuhi na jioni,na usiku;hakika kumtukuza Mungu kwa wingi usiku humkurubisha mutu na watakatifu wa mbinguni

4.Ni bora zaidi kupangilia mwenyewe kisomo na dhikri ya kila siku,pia na sala ya suna

5.Utakapo zoea kuifanya ibada uliopangilia kila mara,itakua kama anaye alika jeshi la mbinguni.

6.Roho ya Mungu itakukurubia na mwenyewe utazingatia upatikanaji wake ndani mwako bayana ama katika ndoto

7.Malaïka na roho huporomoka kwa wingi maala inapo somewa kauli ya kitabu hiki kitukufu.

## 31. ASIYE FANANA

1.Utukufu ni wake Mwenyenzi Mungu,Muhifadhi wa milele,anaye mililki vyote pahali pote muda wote

2.Mjuzi anaye elimisha wanahewa,na kuhukumu yote yanayo tendeka angani na ukiwani bila msaidizi

3.Busara chache ya kibinaadamu hufanya mutu ajilinganishe na Mola wake

4.Mara hulazimisha kujumuika naye na mara hutaka kuhojiona naye kama kiumbe chenzake

5.Mola wako ni Mtukufu wa hali ya juu sana,na wewe ni kitu dhalili sana,hamlingane ku vyovyote kamwe

6.Kumlazimisha atende kadiri mtendavyo nyinyi ni kumlazimisha aishi kama nyinyi,na ili hali uzima sio maisha

7.Mungu ni mwenyi kuenea,anapo tenda sio ila katika yote,kila yule ameishi kwa msaada wake Mwenyenzi.

## 32. HATUA

1.Ametakasika Mwenyenzi Mungu,Mfalme mkamilifu,anaye simamia viumbe vyote kwa hekima ya ajabu

2.Mwalimu wa walimwengu,anaye angazia watu kwa njia mbalimbali,M'bora wa viongozi

3.Hatua kubwa ya tafsiri ya kweli yake ni katika unabii na utume,yaani hupatikana kwa njia ya Malaïka na roho.

4.Na hatua ndogo ya ulabudishaji ni katika uhasidu na urozi maana hupatikana kwa njia ya Shetani na muzimu

5.Aliye katika njia ya Shetani na muzimu ni gizani na ndio maana hazingatie kweli ya Mungu

6.Na yule aliye katika njia ya Malaïka na roho ndio aliye nuruni,na ndio maana ameamini kweli ya Mungu ajili ya kuzingatia

7.Mungu Mwenyenzi ndio mwenyi uzima,ni amri kwa kila mutu kumuamini na kumuabudu.

## 33. UMUNGU

1.Ametakasika kabisa yeye anaye stawi arshini kadiri ya kuenea

2.Umungu ni utukufu wa ajabu,Milki kamilifu isiyo punguka wala kuongezeka ajili ya kuenea

3.Yeye ni yote katika kajua na yote katika kutenda, wa miujiza aliye na ushindi

4.Ufalme wake ni wa milele ajili ya kutangulia,Mola wa mashariki na magharibi,kiongozi wa jumla ya viumbe.

5.Mungu wetu aliye Mungu wenu na Mungu wao,wala hakuna asiye milikiwa naye

6.Muhimidiwa na wote,anaye inukia wote ,aliye huru katika yote juu ya maala pa juu ulimwenguni

7.Mola wa pekee aliye na Enzi tukufu dhatini mwake kadiri ya uzima,M'bora wa kuenea.

## 34. KUKOSA SHUKRANI

1.Mungu ndio tumaini ya watu wenyi akili,wametambua mamlaka yake ambae humiliki kila kitu

2.Imani ndio humaanisha akili ya mutu,kukiri uzima wa Mungu ni neema

3.Kafiri hana akili wala shukrani,amepuuza neema ya Mola wake na kusema:sioni anacho nifanyia

4.Kila ulicho nacho ni neema kutoka kwa Mungu,wala haungeli patikana bila yeye kutangulia

5.Kafiri amempelekea adui yake shukrani na sifa ,akisema:shirki yangu ndio inayo ni saidia

6.Amekosa shukrani ajili ya uziwi na upofu,hana macho ya kuona wala masikio ya kusikia

7.Hakika mishirikina hawana amani katika maisha ya leo wala ya kesho,wamejitwiga mizigo ambae hawata weza kuibeba.

## 35. NGUVU YA MAOMBI

1.Mungu ni mwenyi fahamu ya yote,Mjuzi,anaye jua ambae kiumbe hakihelewe;lakini kama yeye anajua ya mbele ya wakati,ni kweli na wewe unajua kama yeye?

2.Na kama hauna ujuzi kama yeye,kwa nini kupinga amri ya Mola wako ajuaye yote?

3.Kama ali amrisha watu kumuomba,anajua faida ya maombi katika maisha ya wanadaamu

4.Maombi ya waaminifu inayo nguvu ya kubadiri ile ambae ilikua imeandaliwa kwa mutu

5.Aliye wa kuangamia,ajili ya maombi anaweza kuokolewa;na pia aliye kua wa kuokolewa,anaweza kuangamia sababu ya kutofanya maombi.

6.Ibada ndio funguo ya kila la kheri na uovu ndio funguo ya kila la shari

7.Wala usijingikiwe kwa sababu Mungu anajua yote na ili hali wewe haujui kama yeye wala usijiamulie mwenyewe mbele ya wakati na ili hali haufahamu ya mbele ya wakati.

## 36. ARSHI

1.Ametakasika Mwenyenzi Mungu,m'bora wa kuumba anaye stawi arshini

2.Amezidia vyote wala hakuna mfano wake popote ulimwennguni

3.Amewaleteeni ujumbe wake kwa namna ya mifano ili wapate kuzingatia

4.Kiti cha Enzi ambae ndio arshi yake Mwenyenzi ,sio mfano wa viti vyenu vya kuikalia,lakini utukufu ao ufalme wa milele

5.Hakika sifa ya Mungu ni miongoni mwa tafsiri ya umungu

6.Ufalme wa milele ao utukufu wa ajabu usio najisika ndio hali yake Mwenyenzi

7.Kuona kama hakuna mwengine ajumuikaye Enzini,ndio maana hakuna wanaenzi isipokua Mwenyenzi peke yake.

## 37. NABII WA UWONGO

1.Dini inayo anzishwa na Nabii ao mtume wa uwongo ni ya uwongo pia na wanao shiriki pamoja naye wamepotea

2.Na maubiri yake sio ila udanganyifu mtupu,maana mwalimu wake ni Shetani

3.Kupiga ramli ama kuaguza sio kutabiri maono ,wala miujuza yake isi kudanganye hata Shetani pia huyafanya

4.Kilicho muimu ni maneno,kwani ndio ujumbe:kauli tukufu ni ukweli usio na shaka

5.Chunguzeni kauli yake na matendo yake na pia kumuomba Mungu akuoneshe undani wake

6.Nabii asiye kua na ujumbe wala haamini Mitume wote wala haamini vitabu vyote ni wa uwongo

7.Na pia nabii anaye muita Nabii wa Mungu Yesu Masiya kua ndio mungu wake ni nabii (ao mtume)wa uwongo.

## 38. KIBLA

1.Ametakasika Mwenyenzi Mungu aliye umba kila kitu,wala hakuna kisicho kua chake.

2.Amestawi Enzini kadiri ya kuenea,pande zote ni zake,hakuna kwa kumfichamia.

3.Ni lazima kuhelekea kibla wakati wa Sala; ambae ni katika sehemu mbili: ya kimwili na ya kiroho.

4.Kimwili ni kuhelekeza uso wako maala patakatifu,kwenyi muskiti mtakatifu ao mlima mtakatifu.

5.Atakaye tumia dhati tukufu ya Muhamadi,hujihelekeza kwenyi muskiti mtakatifu wa Maka.

6.Na atakaye tumia dhati tukufu ya Yesu Masiya hujihelekeza kwenyi muskiti mtukufu wa Yeruzalema.

7.Na atakaye tumia dhati tukufu ya Mussa,hujihelekeza kwenyi mlima Sinaï.

8.Na atakaye tumia dhati tukufu ya (Shaidi wa Mungu) Kalonda,hujihelekeza kwenyi Muskiti mtakatifu wa kadingila(ao mlima karombwe).

9.Ki roho,kuhelekeza akili yako yote kwa Mungu namna ya kumtegemea yeye peke yake,ndio kuhelekea kibla.

10.Kama haufahamu upande wa kibla ,usikose kusali kimwili,Mola wako ni tayari popote.

11.Na kama muskiti huelekea kibla na ili hali wewe hutumia dhati tukufu ya mwengine,usikose kusali humo,pande zote ni zake.

12.Amani ya Mungu kwa wasilimu wote.

## 39. UTUKUFU

1.Enzi ni utukufu wa ajabu usio najisika,milki kamilifu kadiri ya uwezo wa vyote na ujuzi wa vyote

2.Ilitangulia kimuujiza kadiri ya kuenea bila mwanzo wala mwisho namna ya kukamilika

3.Utukufu wake huu ni wenyi kustaajabisha ajili ya kuzidia,ushindi katika yote,milele na milele

4.Ni mwenyi uhuru ajili ya kuenea,Mufalme anaye tawala ulimwenguni.

5.Pahala alipo hakuna mwengine,wa pekee aliye juu.

6.Kila kilicho njee ya dhati yake ni kipungufu,maana hutengana na ukamilifu

7.Na ndio maana vyote vilivyomo angani na vyote vilivyomo ukiwani ni vitu dhalili sana mbele yake,hakuna mfano wake.

## 40.KITABU KITUKUFU

1.Kauli  ya Mungu ni kweli na haki ambae ndani mwake hamna shaka

2.Kama kauli yake imeandikwa katika kitabu,bila shaka kitabu kile ni kitukufu,maana ni nakala ya ufunuo

3 Na ndio maana ni amri kwa watu wote kuamini vitabu vyake ambae kawa teremshia Mitume wake

4.Hapana kuamini sehemu na kukataa sehemu ya maandiko matakatifu: kama si kimwili kumbi ni kiroho

5.Ugumu ni kwamba neno lake huletewa kadiri ya kusema kwao viumbe ili wapate kufahamu

6.Ndio maana kunapatikana neno iliye waziwazi na ambae ni katika mifano

7.Kauli tukufu yote sio mifano wala kauli tukufu yote sio waziwazi,na ndio maana haiwahusu isipokua wenyi akili.

## 41. KWELI MOJA

1.Dini iliyo kuja na manabii wote ni Usilimu,hakuna Nabii aliye tumwa na dini ingine kinyume na hii

2.Usitafautishe dini ajili ya lugha zenu wala ajili ya uwingi wa mitume yake

3.Usilimu ndio dini aliye kuja nayo nabii Mussa,Yesu Masiya na nabii Muhamadi,na pia mitume wengine wote

4.Wote walipewa kazi ya kusilimusha watu wa dunia ambae walikua bado kujisalimisha katika mapenzi ya Mungu Mwenyenzi

5.Kuona kama mafundisho yao ni kweli moja isiyo pingana ambae huambatana sawasawa,ndio maana wote ni katika kundi moja yenyi kushuudia kweli moja

6.Ukweli ni mmoja,utafauti wa madini unatokana na uchache wa imani pia na uchache wa elimu,na pia vishawishi

7.Basi ondokeni gizani na ingieni wote nuruni,mukijaana na imani ya Mungu Mwenyenzi

## 42. MACHO

1.Uzima wa Mungu ni utukufu wa ajabu,fikara ya viumbe haizingatie ajili ya uzaifu wake

2.Hali yake hustaajabisha kadiri ya muujiza,wa pekee bila mfanano

3. Fikara ya kiumbe ndio macho inayo zingatiaka ndani yake,kisicho kua na fikara hakiwezi kuzingatia chochote

4.Na utimilifu kifikara ndio utaalamu ambae ni akili,macho izingatiaye kimwili na kiroho

5.Akili huzingatia kile ambae kiungo cha mwili kiitwacho jicho hakiwezi kuzingatia

6.Ndio maana akili humzingatia Mwenyenzi Mungu ambae macho ya kimwili haiwezi kumzingatia

7.Mutu asiye amini Mungu ni mfano wa kipofu,amekosewa akili ambae ndio macho ionaye kiroho

## 43. KIWE NA KINAKUWA

1.Mungu asingeli kuwako kama vyote visingeli kuwako,lakini kuona kama Mungu Mwenyenzi yupo,ndio maana ulimwengu na walimwengu hupatikana

2.Mwenyenzi ni mwenyi milki kamilifu yenyi uwezo wa kuumba

3.Mamlaka kubwa ajabu ambae huweza kufanya kila kitu bila kutumika kazi.

4.Akapenda kutokeza jambo hawezi kutumika,lakini hutoa amri: << kiwe na mara kina kuwa kadiri ya idhini yake >>

5.Ni kwa sababu alitangulia katika mamlaka yake mwenyewe, namna ya kuenea bila upungufu wowote

6.Hali kama hiyo ndio uzima kadiri ya ukamilifu,ndani mwake hakuna upungufu wowote,Muweza na Mjuzi wa vyote.

7.Ukamilifu wake ndio uliofanya atangulie kadiri ya kuenea na ndio maana amepatikana na mamlaka kubwa kadiri ya uwezo wa vyote,chemchem ya upatikanaji na maisha.

## 44. HAKIMU

1.Ametakasika Mwenyenzi Mungu,bwana wa mabwana,Mtukufu wa ajabu sana,mwenyi mamlaka ya juu sana

2.Ni amri kuheshimu sheria ya Mfalme wa ulimwengu ambae atahukumu vyote wala hakuna atakaye weza kuhepuka hukumu yake.

3.Haifae kwenda kinyume na kauli yake sababu hakuna wa kukusemelea utakapo hukumiwa naye.

4.Mungu ndio muweza wa vyote anaye fanya yote kadiri apendavyo, mwenyi uhuru na ushindi.

5.Kauli yake imejaa nguvu ya ushindi,atakaye itumia duniani atageuzwa roho takatifu atakapo ihama dunia.

6.Ujuzi wa Mola wenu umemfanya ainuke sana zaidi ya wote, wala hakuna mwengine mfano wake.

7.Yeye ndio chemchem ya utukufu,jihelekezeni kwake,mupate kijitekulia utukufu wa kila namna.

## 45. BWANA WA ULIMWENGU

1.Ametakasika Mwenyenzi Mungu, anaye jua yote wakati wote pasipo kisinzia wala kulala

2.Ukamilifu wake umemfanya astirike katika yoye, mbali na vitenguzi vyote,milele na milele.

3.Amejua yote na ameweza kufanya yote,namna ya kuenea katika yote kinyume na upungufu wote.

4.Mwenyi mamlaka na uhuru,mtawala wa vyote katika yote,wakati wote pahali pote ulimwenguni.

5.Ameumba,amekadiria na amelea,mkamilifu anaye jitosheleza na anaye tosheleza viumbe vyote,mshindi aliye na uzima.

6.Mungu ndio Bwana wa ulimwengu,Mufalme wa milele, anaye pindukia,anaye tangulia.

7.Hakuna mwengine kama yeye ,wa miujiza aliye juu.

## 46. SAUTI YA MUNGU

1.Ametakasika Mwenyenzi Mungu, m'bora wa kuumba, aliye umba tabaka la anga na tabaka la ukiwa

2.Mamlaka yote imetoka kwake,ni yeye atanguliaye kadiri ya kuenea bila mwanzo wala mwisho

3.Hasemake kama wasemavyo viumbe, kwani hana kiungo chochote dhatini mwake

4.Sauti yake hutukia kwa rafla kadiri ya idhini yake, katika jina lake,mwenyi uhuru na ushindi

5.Kauli yake ni yenyi mamlaka ya utendaji wa vyote, kusikia sauti yake ni kufanyika upya kiroho

6.Mjuzi wa kusema anaye agiza yanayo tokea,sauti ya maajabu inayo tokeza,toka sifuru, umbo za kila aina

7.Hakuna Mola mwengine anaye stahili kuabudiwa ispokua Mwenyenzi peke yake, Mjuzi na muweza aliye na uzima.

## 47. UDHU

1.Ametakasika Mwenyenzi Mungu Mtukufu asiye na doa,anaye kosoa bila kasoro.

2.Ni yeye anaye amuru kuchuma udhu kwa kila aliye silimu, wala asisali yeyote katika najisi.

3.Udhu ni yenyi sehemu mbili,kadiri ya umbile ya mwanaadamu: kimwili na kiroho.

4.Kadiri maji inavyo safisha mwili,ndivyo neno linavyo safisha roho.

5.Ndio maana hutumia maji ili kusafisha viungo vitano vya utambuzi,kimwili.

6.Na pia hutumia neno la Mungu ili kusafisha roho ndani ya mutu .

7. Heri mutu anaye takasa mwili na roho,maana ametakasa nafsi yake yote.

8. Atakaye kataa kuchuma udhu kimwili na akazingizia kuchuma udhu kiroho ,ni miongoni mwa wanafiki.

9. Na atakaye kataa kuchuma udhu kiroho na akazingizia kuchuma kimwili ni miongoni mwa wanafiki.

10. Ni amri kwa wasilimu wote kuchuma udhu kimwili na kiroho,maana ndio utimilifu wa umbo lao.

11. Kitenguzi cha udhu kimwili ni najisi,na kitenguzi cha udhu kiroho ni zambi.

12. Chakula halali inayo ingia ndani ya mutu haiweze kumchafua,lakini Choo ambae hutoka ndani yake ndio humchafua.

13. Iliingia ndani mwake kadiri ya utimilifu,lakini imetoka ndani mwake kadiri ya uaribifu.

14. Roho yako isifanane na mwili wako,ambae huingiza halali kwa njia ya juu,lakini baada ya kazi ndani mwake , huitoshea katika njia ya chini kadiri ya kinyume chake hali ya kua haramu.

15. Neno la mungu ambae ndio nuru,liingie ndani mwako kupitia akili yako,baada ya kazi yake ambae ni kufuta giza,itokezwe na akili yako kadiri ilivyo ingizwa,hali ya kua utimilifu.

## 48. NGAO

1.Ametakasika Mwenyenzi Mungu, muhifadhi wa milele, anaye jengea waja wake ngao

2.Muja wa Mwenyenzi ni yule anaye tumainia Mungu zaidi ya yote na pia huogopa kutenda zambi

3.Ametoshelezwa na roho takatifu ambae humsaidia kwa idhni ya Mungu; wala hatumiake kafara ya wakaaji wa Hadeze kua ukingo

4.Shetani amewaimiza sana wafuasi wake ili wa washambulie wachamungu,kuwategea mitego mbalimbali

5.Ulinzi wa Mungu ndio wenyi nguvu na ushindi, ngao ya miujiza,ambae huwakinga na mizinga ya maadui

6.Kauli tukufu ya kitabu hiki inapo tamkwa kila mara huleta nguvu ya ushindi ndani mwake anaye ya tamka

7.Hakika Sala na dhikri ,saumu na wema, hujengea mutu Ngao,hawezi kuangamizwa na chochote

## 49. BIDII

1.Mungu Mwenyenzi ali muamba mwanaadamu ajili ya kumuabudu na ndio maana ibada ni jambo muimu maishani mwake

2.Hapana kuacha wala kupumzika masiku kadhaa bila kumsujudia Mola wako

3.Ni amri kumuabudu kila siku, maishani mwako, mpaka mwisho wa umri wako

4.Wala usijingikiwe moyoni mwoko ajili ya ibada yako ya zamani kwamba imetosha; wala usivunjike moyo ajili ya kutojibiwa papu kwa papu

5.Mwenyenzi hawezi kukuzulumu, kuweni yakini kwamba kila utendalo huhesabika na atakulipa kwalo

6.Usitafute sana malipo duniani ,lakini tetea kwa bidii malipo ya mbinguni ambae hudumu milele

7.Imani ni katika tumaini ya maisha ya mbinguni,asiyekua na tumaini hana imani

## 50. MILKI KAMILIFU

1.Milki kamilifu ndio Enzi ambae ni uzima kadiri ya umungu

2.Mwenyi kua na milki kamilifu dhatini mwake ndio Mungu Mwenyenzi

3.Yeye ndio mwenyi uwezo wa kuumba,namna ya kutokeza ambae hakikua

4.Hayo ni kwa sababu ukamilifu ni ndani mwake,ndio maana huweza yote

5.Hali yake ni muujiza na matendo yake ni maajabu,wa pekee aliye juu

6.Hakosekanake muda wowote wala hatanguliwake na yeyote ku vyovyote,mwenyi kuenea

7.Hakika Mwenyenzi ndio mwenyi uhuru peke yake, hakuna mwengine kama yeye.

## 51. CHAKULA YA ROHO

1.Mungu amempenda sana anaye pupia kutubu pindi anapo dondoka

2.Mwanaadamu ni mpungufu ,anaweza kudanganyika ajili ya uzaifu asilia

3.Maisha ya dunia ni jambo dhalili, haina utimilifu ajili ya uzaifu wa mwili

4.Utimilifu kimaisha hupatikana mbinguni, kambi tukufu yenyi kujaa nuru ya taa isiyo zimika

5.Anaye tumia urakibu ndio mzaliwa wa sehemu ya kwanza ya bahazi la juu angani

6.Na atumiaye uatidu ndio maskini tena mnyonge, anaye viringita gizani ,umbo la hadezeni.

7.Tumieni neno la Mungu kadiri ya chakula ya roho, ili mupate kuishi salama milele na milele

## 52. MKAMILIFU

1.Enyi watu wa dunia! ni lazima kwenu kumuabudu Mungu Mwenyenzi aliye umba mbingu ,hadeze na dunia bila kutaabika na kazi yoyote

2.Viumbe havikujitokeza vyenyewe sababu hukosewa uwezo wa vyote; ilibidi kupatikane mwenyi milki kamilifu ambae peke yake huweza yote ili awatokeze wote toka sifuru.

3.Vyote ambae mumeviona na ambae hamuvione vimetoka kwake , pasipo uzima wake hakungeli umbwa chochote.

4.Mungu hafanane na viumbe kwani yeye ni Mkamilifu na viumbe vyote ni vipungufu.

5.Mkamilifu hastahili kuanza wala kukoma,hawezi kuchoka wala kushindwa,kusahau wala kujifunza...

6.Yeye ni muweza wa yote tena Mjuzi wa yote,na ndio maana ame kamilika hali ya kua na uzima .

7.Hakuna mwengine aliye na uzima isipokua Mwenyenzi peke yake

## 53. SALA

1.Enyi walio silimu! mumelazimishwa kusali kila siku ,asubui na mangaribi ,na pia kumtukuza mola wenu usiku na mchana.

2. Sala imeleta nguvu ya Mungu na pia humkurubisha mutu na mola wake .

3. Ni tendo bora kabisa mbele ya muumba,alama ya unyenyekevu na shukrani,ambae humpandisha mutu daraja ya kiroho.

4. Kufuta mabaya kwa mema ndio mradi wa kufunga sala.

5. Kisomo cha sura ya ufunguzi ni miongoni mwa funguo ya milango ya mbingu.

6. Kuitika uito wake na kunyenyekea dhati yake,na kukiri uzima wake kwa yakini ,ndio humaanisha kurukuu,kusujudu na kutoa shaada.

7. Kuchuma udhu na kuhelekea kibla na kusali ni kielelezo cha uchamungu,kadiri ya nakala ya maisha ya mbinguni.

8. Atakaye kataa kusali kimwili na akazingizia kusali kiroho tu ,ni miongoni mwa wanafiki.

9. Na atakaye kataa kusali kiroho na akazingizia kusali kimwili tu,ni miongoni mwa wanafiki.

10. Ni muswalina wa kweli yule anaye sali kama kawaida kimwili na kiroho na ndio mpenzi wa Mungu.

11.Usijidai kua roho tupu na ilihali uko na mwili,wala usijidai kua mwili mtupu na ilihali uko na pumzi.

12. Jihadharini na elimu kiakilia musije mukafuta alama za dini ya Mungu.

## 54. SHUJAA

1.Ametakasika Mwenyenzi Mungu,mtangulizi aliye kamilika tafauti na woote,mwenyi mamlaka ya milele

2.Mbingu,hadeze na dunia hupatikana kadiri ya mapenzi yake,wala hakuna upatikanaji inje ya idhni yake.

3.Shujaa mkamilifu anaye zidia kila kitu,mufalme anaye hukumu bila mipaka

4.Anaye stawi maala penyi utukufu wa ajabu,ambae kiumbe hakiwezi kukurubia

5.Wa miujiza anaye badiri majira ulimwenguni na ili hali mwenyewe habadirikake.

6.Musifuni yeye aliye mzima,chemchem ya fahamu ulimwenguni,anaye tumainiwa na wote katika mambo yote.

7.Mtukufu anaye miliki ufalme wa ulimwengu bila msaidizi wala muchoko,muweza wa kila jambo.

## 55. JAMBO MUIMU

1.Mwenyenzi Mungu ni baba wa wote,amelea viumbe vyote katika usawa,kiongozi mwema.

2.Ukapenda kupata msaada wake,utaupata bila shaka,lau kama utaamini na kutenda salama kama inavyo andikwa katika vitabu vyake

3.Tembea urakibuni namna ya kuingia nuruni,wala usitumie uatidu kamwe usije ukaingia gizani

4.Nuruni munamo kheri nyingi ajili ya kupatikana katika mapenzi ya Mungu,wala maisha haina ukomo

5.Ibada ndio << Jambo muimu >> ku watu wote wenyi akili, wala usitumie uchawi kamwe maishani mwako.

6.Inaleta bahati ya kufikia wokovu wa roho yako.

7.Na uchawi ndio unaleta mikoshi maishani,namna ya kuangamiza nafsi kuingia hadezeni

## 56. JINA YA KITABU

1. Ewe.Kalonda! ni mimi Mungu wako,nimekupasha ya kama hawata kukamata wala hawata kusuluhu kadiri wanavyo kusudia

2.Amka, na uvuke ngambo ya mtoni,nenda zako; maana makafiri wanakaribia;

3 .Kuona kama wao wamekutizama kwenyi T.V. sisi tumekupatia redio: yote wa takao zungumuza juu yako utakua na sikia.

4.Inafaa kupata buku kabambi ya kuandika manemo yote pamoja

5.Jina la kitabu hiki kitukufu ni << UKWELI >>

6.Na inatakika kujenga Muskiti wetu maala petu, ambae watu watakua na salia wale watakao kuja kwetu.

7.Hii ni kauli tukufu kutoka kwa Mola wenu aliye Enzini,hakuna shaka ndani yake.

## 57. FAIDA

1.Utakatifu ni wake Mwenyenzi aliye huru juu na chini, wa pekee asiye lingana na yeyote

2.M'bora wa kukadiria anaye tokeza kila umbo na faida yake kubwa,wala hakuna umbo isiyo kua na mafaa

3.Kile kisicho kua na faida katika maisha ya uyu kinayo faida kubwa katika maisha ya yule.

4.Ni kwa sababu kila kile kilifanyika na Mjuzi aliye  na busara kamilifu

5.Haifai kulaumu chochote wala lolote ambae Mwenyenzi kalifanya,hafanyi ispokua yanayo stahili kabisa, lakini wanaadamu hawafahamu

6.Lau kama wangeli fahamu faida ya kuumbwa kwa kila umbo, bila shaka wangeli muogopa Mungu na kumsifu na kumshukuru

7.Na ijapokua uchafu ambae hutokea ndani ya kiumbe, na ijapokua kuumbwa kwa Shetani ambae ni simamizi la ubaya; maana dunia isingelipatikana pasipo ubaya na uzuri kupatikana

## 58. KAWAIDA

1.Ametakasika Mwenyenzi Mungu Mjuzi wa kuumba ,anaye kadiria kila mwanahewa fikara ya sawa na maisha yake

2.Fikara yao huwatosheleza katika utetezi wao,kulingana na umbo zao

3.Na ndio maana maitaji yao ni tafauti ajili ya utafauti wa umbile zao,kila yule  hufanya shuruli ya namna yake

4.Mumgu peke yake ndio anaye jua mradi wa kuumbwa kwa kila kiumbe

5.Hakupendelea yeyote pasipo haki,bali vyote hufanyika katika kawaida la umbiko

6.Atakaye kanusha ujumbe huu sio ila kafiri mkuu, wala hawata nusurika wale wanao husudu, wata rundikwa hadezeni sababu ya kuipinga haki

7.Heri mutu anaye amini kweli hii ambae hupata yakini ya uzima wa Mungu,na kufunika mabaya kwa mema,miguu urakibuni siku zote.

## 59. ChUKI

1.Ametakasika sana na zaidi yule aliye umba mbingu na dunia kwa kauli yake tukufu

2.Mjuzi wa kukadiria ,anaye jaalia waja wake neema ya kila namna

3.Atakaye vizia kunyanganya ao kuvruga neema aliye pewa mwenziwe,ukomo wake ni hadezeni

4.Mushirikina aliye na elimu ya Nyota anaye zingizia kutabiri ni sawa na wafumu wengine wote.

5.Wao wote wametumia wakaaji wa zimuni,ndio maana wanayo kazi moja ya kurogana.

6.Utazani ameombeana kumbi amerogana,na utazani muaminifu kumbi muovu mkuu.

7.Chuki imejaa moyoni mwake,wala hawatakie wenziwe amani kamwe.

## 60. TAMAA YA DUNIA

1.Nani aliye pumbafu kuliko yule anaye taabikia maisha ya dunia peke yake?

2.Utamuona ametamania kila kitu, hashukuru wala hatosheke

3.Mizimu anayo sharikiana nayo humzidishia wasiwasi ili kuivruga zamiri yake

4.Ni kwa sababu amekaribiza wakaaji wa hadeze ndani mwake ndio maana amechafuka

5.Ame helekezwa upande ambae mwenyewe kautarajia.

6.Atakaye kataa neno la Mungu ajili ya kuipenda sana dunia, amepotea mbali na njia.

7.Tumaini ya Mungu peke yake moyoni ndio matumizi ya njia iliyo nyooka.

## 61. NIA

1.Shukrani ,sifa na heshima kumustahili Mwenyenzi Mungu peke yake,mlinzi mwema

2.Atakaye  penda kuona utukufu wa Mungu maishani mwake basi afanye "Nia"

3.Hatua ya kumtegemea na kumtumikia Mungu maisha yako yote

4.Na kua na desturi ya kuamuka usiku kwa kufanya ibada.

5.Kumtukuza katika kisomo na dhikri kwa wingi pia na maombi katika mpango maalumu

6.Mola wa ulimwengu atajitukuza kwake na kumupatia zawadi ya kiroho

7.Na bila shaka atazingatia bayana utukufu wa Muumbaji wake; hakuna mwengine aliye na uwezo kama yeye.

## 62. MWENYE KITI

1.Ametakasika Mwenyenzi Mungu bingwa (Mshindi) aliye huru kufanya yote anayo penda katika ulimwengu

2.Ni yeye anaye miliki falme zote,utupu wa Enzi,kinyume na uzaifu wa aina zote

3.Anacho kishika kujaa nguvu ,na anacho kiacha  kukosa nguvu

4.Yeye ndio yote katika yote,mwenyi kiti,anaye simamia jumla Ya viumbe

5.Mkaguzi wa mambo yote, anaye endelesha na anaye komesha maisha ya viumbe

6.Ameinuka juu zaidi ya kila kitu ,wa pekee anaye stahili kuabudiwa

7.Bwana wa mabwana ,mwenyi uwezo wa kuenea, wa miujiza aliye juu.

63. NUSRA

1.Ametakasika Mwenyenzi Mungu muweza na mujuzi anaye kamilika peke yake ulimwenguni

2.Mganga mkuu,anaye ponya kila magonjwa kwa kauli yake tukufu

3.Neno la Mungu ndio dawa kubwa,yenyi kutibu malari ya mwili na ya roho

4.Umungu ndio nusra ya walimwengu mamlaka ya ajabu  inayo okoa na shari  ya kila namna

5.Kamanda wa majeshi anaye irikisha warozi kwa kauli yake tukufu

6.Kisomo kitukufu na dhikri ni miongoni mwa silaha za nuru  ambae hutekeleza falme za giza

7.Someni kwa wingi aya za kitabu hiki cha "UKWELI", ili mupate kupokea zawadi ya kiroho.

## 64. MTATUZI

1.Ametakasika Mwenyenzi Mungu Mshindi aliye na utasi juu ya yote,anaye tokeza na anaye angaza

2.Uzima wake husababisha upatikanaji wa viumbe vyote, na kuvilinda

3.Ni yeye aondoaye dhiki, atatuaye utata wa kila aina angani na ukiwani

4.Ombeni msaada kwake yeye aliye na uwezo wa vyote ,magumu ya aina yote hukomeshwa naye kwa idhni bila kutaabika na kazi yeyote

5.Mlinzi mwema anaye tarajiwa na wote, tajiri wa vyote, anaye tosheleza katika shida zote, mwingi wa rehema na mwingi wa ukarimu

6. Heri mutu anaye mtegemea Mwenyenzi peke yake bila kumchanganya na chochote

7.Hakuna mwengine apasaye kuabudiwa kwa haki kama yeye,mwokozi aliye juu

## 65. TAA ISIYO ZIMIKA

1.Mwenyenzi ametakasika sana na zaidi , amestawi mbali na uchafu wa aina yote;

2.Enzi yake ni tafauti na kila kitu, uwezo wa kuenea

3.Hakuna kunajisika kwake aliye kamilika; mamlaka ya milele pasipo mabadiriko yoyote

4.Mwenyenzi ni kiongozi mwenyi busara kamilifu, anaye jua yasiyo fahamika na yeyote

5.M'bora wa kukadiria anaye fanya yote katika usawa , hakuna kisicho kua sawa miongoni mwa alivyo viumba

6.Watu hawamzingatie Muumba wao ajili ya kuzorota kwa pumzi yao mwilini

7.Mungu ndio Bwana wa mabwana,taa ya ulimwengu inayo angazia bila kufifia wala kuzimika milele na milele

## 66. KIFO

1.Ametakasika sana Mwenyenzi Mungu M'barikiaji,anaye tawala maala pote ulimwenguni

2.Mbingu na dunia hushangilia jina lake, wa milele mwenyi sifa kamilifu

3.Hasahau chochote wala hashindwe na chochote wala hakuna wa kumzidia kwa lolote

4.M'badirishaji wa majira,anaye geuza umbo ya mwanaadamu baada ya kufa kwake

5.Kifo cha mutu sio mwisho wa maisha ya mutu,angani lakini ukiwani,maana ni mtengano wa mwili na pumzi

6.Pumzi ya mutu hufanyika roho urakibuni ama muzimu uatiduni,na mwili wake ndio hukoma baada ya kifo

7.Na hiyo siku ya kiyama ndio ukomo wa Shetani na mizimu,isipokua malaïka na roho ndio watakao kua hai

8.Kuzila neno la Mungu ndio kufa kiroho;maana pumzi yako sio kitoto cha roho,bali kitoto cha muzimu.

9.Tumieni neno la Mungu katika kawaida yake ili mupate kurithi ufalme wa mbinguni

## 67. UFUFU KO

1.Sema : kufufua wafu ni jambo raisi sana kwa Mungu Mwenyenzi, atakapo idhinia itafanyika kwa rafla kadiri ya idhni (mapenzi)yake

2.Kutokeza toka sifuru ndio jambo kubwa ajabu lakini karudishia kitu hali yake ya zamani sio jambo ngumu zaidi ya kuumba

3.Kwa nini makafiri wamefanya ubishi kuhusu habari ya ufufuko? aliye na uwezo wa kuumba atashindwaje kukiamusha tena alicho kilaza?

4.Hiyo siku ya kiyama kila nasfi itaonja mauti,ispokua dhati yake tu ndio itakayo bakia, maana Mwenyenzi peke yake ndio mkamilifu

5.Na punde kidogo,ndipo atakapo fufua wote ili kutenganisha adili na batili.

6.Uwezo wa Mungu ni wa ajabu sana,wala yeye hatumikake kazi kwa kutenda jambo

7.Atakavyo hutukia kwa rafla kadiri ya idhini yake,m'bora wa kuumba

8.Mutu anaye didimia katika zambi,akaamini na kutubu,tendo hili ni ufufuko kiroho

9.Amezaliwa upya maana alikua amekwisha fariki kiroho,mfano wa mauti inayo puliziwa pumzi ya uhai.

## 68. KAWAIDA YA NENO

1.Mwenyi uzima ni mmoja na dini yake ni moja,wala hakutaanza dini mupya njee ya Usilimu maana hakuta tokea Mungu mwengine

2.Na yule atakaye silimu kiisha akajipatia dini ingine ambae hutoka njee ya kauli tukufu yeye sio ila munafiki

3.Amedanganya kusilimu na ili hali hana imani.

4.Mwenyi imani hawezi kukataa mafundisho ya Mitume ya Mungu

5.Tumieni neno la Mungu maishani katika usawa,enyi walio silimu; hakika maisha pasipo neno la Mungu ni hasara kubwa

6.Ma Nabii na Mitume ndio wengi lakini dini ya Mungu sio nyingi bali moja tu.

7.Kuishi katika kawaida ya neno la Mungu ndio kuishi katika dini ya Mungu.

8.Kuchinja, kutokula haramu na kutovunja amri ya Mungu na kadhalika ni katika mwili na katika roho sio kimwili tu wala sio kiroho tu

9.Na vivihivyo pia kuhusu Hija, ibada hii inayo tafsiri yake kiroho, ni amri kwa watu wote kuitimiliza kimwili na kiroho pia: ndio kawaida ya neno la Mungu

## 69. DINI YA UWONGO

1.Ondokeni wote katika ma dini ya uwongo na njooni wote katika usilimu,dini ya kweli ya Mungu Mwenyenzi

2.Dini ya uwongo yote huletewa na mitume wa uwongo,ambae hujidai utume na ili hali hawakutumwa na Mungu

3.Watu hawa ndio waovu wakuu ambae wamekwisha chagua Hadeze(Jahanamu) kua makao yao ya milele

4.Wamepoteza watu wengi na uwongo wao ambae hupinga kweli ya Mungu:

5. Bahadhi miongoni mwao humpachika mtume wa Mungu daraja ya umungu, na wengine husema kuna wa Mungu wengi

6.Na wengine humkanusha Nabii aliye pewa Qur'ani, na wengine hukanusha mbingu na hadeze,na hukanusha siku ya Kiyama

7.Hakika ni muimu kuchunguza kauli yao na matendo yao pia ili mupate kugundua hakika ya roho zao.

## 70. JAMAA MOJA

1. Kuamini Mitume mbalimbali walio tumwa katika ma umati mbalimbali kusiwatenganishe,hakika wote walitumwa na Mumgu mmoja

2. Miongoni mwao hakuna aliye na dini yake, lakini wote ni katika dini moja ya Usilimu

3.Mungu hakuwapa Mitume ispokua kazi ya kusilimusha watu wa dunia, yaani kuwaingiza katika usilimu, dini ya Mungu Mwenyenzi

4.Atakaye kataa kusilimu ndio anaye kataa kujumuika katika dini ya Mungu

5.Jihadharini na manabii wa uwongo,ambao huwaondoa watu wa dunia katika njia na kuwapoteza mbali sana.

6.Mbinguni hakuna mtengano wowote lakini umoja,wamejaa upendo wa ajabu

7.Watu wote wanao muamini Mungu Mwenyenzi peke yake na Mitume wake wote ndio wandugu wa kiroho, jamaa moja la mbinguni.

## MULANGO WA PILI : ENZI TUKUFU

## SURA YA KWANZA

1. Hapo mwanzo kabla ya anga na ukiwa kupatikana, kulitangulia ‟enzi” tukufu.

2. Enzi hiyo ni milki kamilifu ambae huweza yote na hujua yote.
3. Ilitangulia yenyewe ulimwenguni bila kufanyika ajili ya kukamilika kwayo.
4. Ni mamlaka yenyi kuenea kiushindi, bila upungufu wowote.
5. Na utangulizi wa enzi kadiri ya ukamilifu ndio uzima ambae ni umungu.
6. Uzima huo, ambae ni umungu, ulikua enzini hali ya kua mwenyenzi Mungu.
7. Alitangulia mwenyewe mbele ya vyote hali ya kua yote katika yote, kadiri ya mwanzo wa vyote.
8. Hapakupatikana yeyote badala ya mwenyenzi Mungu, ajili ya upekee wa milki yake kamilifu.
9. Alikua ametawala peke yake kabla ya ulimwengu na walimwengu, katika mamlaka yake mwenyewe.
10. Mwenyi kukamilika namna ya kujieneza katika yote bila msaada wa yeyote.
11. Enzi ni taa ya ulimwengu, kadiri ya chemchem ya mwangaza wa aina yote.
12. Na itanguliapo taa, kifuatacho ni nuru yake.
13. Na ndiyo maana, baada ya utangulizi wa enzi tukufu, kilicho fuata ni nuru yake.
14. Nuru ni sehemu ya utukufu wa taa, kadiri ya uvuli wake.

15. Enzi ni taa kadiri ya ujuzi, ni fahamu kuu ambae humiliki kila kitu, isiyo zaufika wala kushindwa na chochote, ajili ya kuenea.

16. Na sehemu ya utukufu wake inayo mtoka kadiri ya nuru yake ni hewa (anga) kadiri ya fikara.

17. Neno lake ndio nuru yake ambae kutoka ndani mwake; imepatikana kadiri ya mapenzi yake na huzingatiwa kadiri ya nguvu yake namna ya utokezaji.

18. Ulimwengu na walimwengu vilifanyika kwa njia ya mapenzi yake.

19. Mungu akitaka kitu Fulani kipatikane hukiruhusu «kiwe» na mara «hupatikana».

20. Ni kwamba kwa kitu kupatikana inatakita kipangiliwe (mbele) katika mapenzi ya Mungu.

21. Umbiko hufanyika kwa njia ya neno lake kadiri ya mapenzi yake.

22. Na katika mapenzi yake ndio katika roho yake ; kwamba aliye katika mapenzi ya Mungu ni roho takatifu ya Mungu.

23. Roho ya Mungu haipatikane katika uzima wake, lakini katika mapenzi yake.

24. Uzima wake ndio katangulia mapenzi yake ; kama vile taa itanguliavyo mwangaza.

25. Uzima ndio Enzi ambae ni dhati yake ; yaani ndio umungu.

26. Na mapenzi yake ndio nguvu yake kadiri ya roho yake ambae ni miongoni mwa nuru yake.

27. Roho yake sio dhati yake ; wala nguvu yake sio uwezo wake .

28. Uwezo wake ni mamlaka iliye dhatini mwake kadiri ya milki ya ushindi.
29. Mamlaka ya uwezo wake ndio katokeza nguvu yake kiutendaji.
30. Na nguvu yake ni miongoni mwa idhini yake kadiri ya tendo lake kiutokezaji.
31. Alipo kua akitawala peke yake kabla ya umbiko kufanyika, roho yake ilikua, mfano wa uvuli wake ; yenyi kufulumia katika neno lake hali ya kua mapenzi yake.
32. Roho na neno ni miongoni mwa nuru yake, na nuru yake sio Uzima wake.
33. Na ndio maana hakuna roho – Mungu wala Mungu roho, na pia hakuna neno-Mungu wala Mungu – neno, kwani dhati yake haiwezi kuchangana na uvuli wake.
34. Umungu ni ukamilifu, ndani mwake hamuna utafauti wowote wala mipaka wala viungo, ispokua upekee kadiri ya uzima.
35. Hakika Mungu mwenyenzi ni mumoja tu, mkamilifu katika sifa ya upekee, m’bora wa kutangulia.

**SURA YA PILI**

1. Mwenyenzi Mungu alitangulia ulimweguni kabla ya vyote kupatikana.
2. Alikua amestawi katika utukufu wake hali ya kua mwanzo wa vyote.

3. Lakini hakuona ya kama hali hiyo ya upekee pasipo vitu vingine ni kitu cha kushikamana nacho.
4. Ndipo alipo umba, kwa mapenzi yake, viumbe mbalimbali ili mamlaka yake itawale juu yao hali ya kua mufalme wa wote.
5. Akainua anga juu ya ukiwa, namna ya daraja katika umbiko.
6. Akaweka wanahewa_halisi juu ya wanahewa_haramu,na akaweka wanahewa-haramu juu ya wazilahewa, ili aitwe musimamizi wa wasimamizi, mtukufu wa daraja.
7. Uwingi wa viumbe vyake haukuunajisi kamwe utukufu wake huo wa ajabu, hakubadirika wala kutingizika, kupungua wala kuongezeka.
8. Ni yeye ndio hubadiri umbo zao kadiri apendavyo ; akiwafanyia mipaka katika umbo zao na katika maisha zao.
9. Na hudhihirisha uzaifu na upungufu wa kila umbo ili asalie peke yake katika ukamilifu.
10. Kadiri alivyo tangulia hali ya kua mwanzo wa vyote ndivyo atakavyo salia pekee hali ya kua mwisho wa vyote.
11. Wakati atakapo poza kila umbo, ili asalie mwenyi uzima hali ya kua yote katika yote kadiri ya mwanzo wa vyote.
12. M'bora wa kutangulia ambae huanzisha na hukomesha vyote kwa mamlaka yake mwenyewe.
13. Mwenyi kutawala kabla ya viumbe, juu ya viumbe, na baada ya viumbe, mufalme wa milele.

14. Mtukufu anaye timiza kwa idhini, mshangiliwa wa viumbe ajaaye heshima, mjuzi aliye juu.

15. Hutoa neno lake kadiri ya mapenzi yake mfano wa nuru yake ku watu, ili kuwanusuru na shari ya giza.

16. Mara ya kwanza hutoweka katika utaratibu, mfano wa mwana Kondoo, kipindi cha ujengaji.

17. Na mara ya pili hutoweka katika ushujaa, mfano wa mwana simba, kipindi cha ubamoaji.

18. Siku hiyo neno la mungu litasaga milima kuisawanisha ardhi, hakuta bakia bonde wala kisuguu:

19. Hakuta patikana mwengine mwenyi mamlaka ya kutenda badala ya Mungu mwenyenzi, ispokua yule atakaye ruhusiwa, itakua kama ilivyo kua kabla ya uumbaji.

20. Na baadaye ndipo atakapo chamusha tena umbo atakayo idhinia, mola mtukufu, mfinyanzi wa maisha.

21. Hakika Mungu mwenyenzi hufanya vile apendavyo kwenyi viumbe vyake, wala hakuna aliye huru mfano wake.

## SURA YA TATU

1. Ujuzi haustahili kuanza kwa namna yoyote ile ajili ya ukamilifu wake.

2. Kinacho anzaka ni kile kipungufu kisisho kamilika ; kile kisicho jiweza na kisicho weza, kisicho jijua na kisicho jua lolote.

3. Ukamilifu ni utukufu, namna ya kuenea katika yote kimilki na kibusara bila upungufu wowote.
4. Ni hali tukufu sana pasipo doa wala kasoro, mipaka wala uzaifu wowote katika yeye.
5. Hakuna maanzio wala makomeo wala kasoro, mipaka wala utafauti ndani mwake.
6. Hakika kuanza na kukoma ni uvuguvugu utokao katika uzaifu na upungufu.
7. Mungu hukamilika pasipo upungufu wowote ajili ya kupatikana na milki ya ushindi,ambae ni uwezo wa kuenea kadiri ya mamlaka.
8. Mtukufu wa ajabu ambae uwezo wake ni muujiza wa maajabu, ambae kiumbe hakiweze kuukagua.
9. Fikara haikagui ujuzi, bali ujuzi ndio ukaguao fikara pasipo shuruli yoyote ajili ya ushindi wa milki yake.
10. Hakika tendo sio chochote mbele ya mtendaji, hawafanani wala kulingana katika hali zao.
11. Lau kama fikara ingeli fahamu siri ya utukufu wa ujuzi kama ingeli zidia ujuzi ama kulingana.
12. Na kama fikara ingeli zidia ujuzi isingeli fanyika bali kutangulia. Na ujuzi usingeli tagulia bali kuanza.
13. Mtoni haumezi kamwe bahari, bali bahari ndio imezayo mtoni.
14. Hakika umungu ni siri kubwa sana isiyo kaguliwa na yeyote ulimwenguni.

15. Kama kungeli kua wa kufichua siri hiyo ya utukufu wa umungu hasingeli fanyika huyo bali kutangulia; na siri hiyo isingeli tangulia bali kufanyika.

16. Lakini kuona kama hakuna azidiaye utukufu wa umungu, ndio maana hakuna ajuaye siri ya utukufu wa Mungu mwenyezi.

17. Kungeli kuwako ajuaye siri ya umungu, kama angeli kuwako ajuaye namna ya kutangulia kwake, ambae humfanana.

18. Na kama kungeli kuwako wa kumfanana, (wao wote) wasingeli tangulia hali ya kukamilika.

19. Maana ukamilifu haustahili kulingana wala kufanana na chochote, wala upungufu wa uwingi haumgusi kamwe.

20. Hakika kutangulia kwake ndio kukamilika kwake, hakuna mwegine aliye na hali tukufu kama hiyo.

21. Na baadhi miongoni mwa watu, baada ya kushindwa kukagua siri ya utangulizi, hulazimisha kila kitu kianze namna Fulani.

22. Na ilihali haiwezekane kiumbe kipatikane pasipo muumbaji kutangulia.

23. Ni kwamba ya faa kupatikane mmoja asiye kua zaifu ambae hutangulia bila msaasa wa yeyote atakaye weza kutokeza toka sifuru vitu mbali mbali

24. Milki yake hiyo iliyo muwezesha kutangulia bila kuanza ndiyo itakayo muwezesha kutokeza ambacho hakikua popote.

25. Hakika ni kawaida mtokezaji kutangulia bila kutokezwa, hasipo tangulia hawezi kutokeza toka sifuru, maana atakua mzaifu.

26. Maana uzaifu ule ulio mfanya ashindwe kutangulia mwenyewe bila kufanyika ndio utakao mfanya ashindwe kuumba.
27. Kama kweli kuna viumbe vilivyo fanyika, ni kwamba kweli kabisa kunapitakana mtangulizi asiye fanyika aliye wafanya.
28. Haiwezekane kiumbe, ambae ni zaifu na pungufu, kujitokeza chenyewe; kitajitokezaje na hali hakikua ila sifuru?
29. Hakutokee chochote bila utangulizi wa milki kibusara, milki yenyi ukamilifu ambae haifanyikake ajili ya kuenea.
30. Hufanyika ambae nizaifu na pungufu, ambae hukosewa milki ya kujieneza mwenyewe, ambae kabla ya kufanyika hakuwaka ila sifuru.
31. Uzaifu na upungufu huo wa kuwa sifuru muda Fulani haumgusi kamwe mwenyi uzima ambae pekee hutangulia.
32. Hakika utangulizi ndio mamlaka ya uumbaji; kwamba atanguliaye ndio aumbaye.

## SURA YA INE

1. Ulimwenguni kumepatikana viumbe vingi sana: baadhi miongoni mwao ni wenyi maisha na wengine hawana maisha.
2. Ni umbiko ambaye kafanyika na mwenyi busara kamilifu, ambae hutokezwa bila yao yenyewe kufahamu wala kutaka, wala haikuwa na la kufanya ajili ya kutokuwa chochote.

3. Kiumbe ni zaifu sana mbele ya muumbaji wake, sio chochote wala lolote, wala kisingeli patikana bila idhini ya mfinyanzi wake.
4. Kuumba ni tendo la ajabu ,namna ya kugeuza sifuru kua kitu Fulani sambamba na idhini, maajabu ya kutokeza ambae hakikua popote.
5. Ni mamlaka kubwa kadiri ya uwezo wa vyote ambae idhini yake hutenda.
6. Milki kuu isiyo patikana katika upungufu, ambae hupatikana katika ukamilifu peke yake.
7. Ni kwamba anaye stahili kuumba ni Yule aliye mkamilifu.
8. Na mkamilifu ni yule asiye na upungufu kimilki na kibusara, asiye zaufika kwa kuanza na kukoma, ambae hashindwake na chochote.
9. Na yule mkamilifu ambae hupatikana pasipo upungufu wa kuanza na kukoma ndio aliye tangulia, na atanguliae ndio mwenyi uzima.
10. Muujiza wa kutangulia ndio maajabu ya kuumba, yaani uwezo wa kupatikana bila kuanza ndio uwezo wa kutokeza ambae hakikua popote.
11. Kuona kama Mungu peke yake ndio aliye tangulia ulimwenguni ndiye peke yake aliye umba kila kitu.
12. Ni mwenyi milki kibusana izidiayo, yenyi uwezo wa kufanya kila kitu kadiri apendavyo, bila tatizo wala shuruli.

13. Ni yeye aliye mkubwa wa vyote ku yote wala hakuna wa sawa yake, mtukufu wa daraja.
14. M’bora wa kuumba aliye na milki ya ushindi, chemchem ya upatikanaji wa kila aina.
15. Kuumba sio kuunda ; kwani kuunda ni kubadiri umbo iliyo kutwa. Ni namna ya kutumia kitu ambae hakukianzisha.
16. Kwa kuunda chuma, hutumia jiwe ambae yeye hawezi kuifanya.
17. Hakika kuunda sio kutokeza toka sifuru, bali ni kubadiri umbo iliyo fanyika zamani.
18. Kuumba ni tendo la mwenyi ujuzi ; na kuunda ndio tendo la mwenyi fikara
19. Kilicho «umbwa» ndio umbo, na kilicho undwa ndio << chombo >>, ni tafauti kabisa umbo na chombo.
20. Umbo hutokezwa na mjuzi toka sifuru, lakini chombo hutokezwa na mwanahewa tokea umbiko.
21. Hakika Mungu mwenyenzi ni m’bora wa kuumba, wapekee katika daraja hiyo, mshindi aliye juu.

**SURA YA TANO**

1. Mwenyenzi Mungu ndio husabidisha ulimwengu namna ya kuutokeza katika kuumba kwake.
2. Ni yeye awezaye ndio mwanzo wa yote, yaani ndiye mwanzishaji wa kila kitu.

3. Mwanzo wa vyote ndio chemchem ya upatikanaji wote na maisha yote katika ulimwengu.
4. Ni yeye mtangulizi ambae hutangulia awali peke yake namna ya kuenea kabla ya vyote, na baadaye hutokeza kila kitu ambae hupatikana ulimwenguni.
5. Ni hiyo milki yake ambae ni mamlaka kubwa sana na zaidi ndio kamfanya atangulie na pia atokeze kila kile kadiri ya mapenzi yake
6. Milki ya ushindi ni mamlaka juu ya kila kitu ambae huweza yote bila kushindwa na chochote
7. Haiwezekane Mungu kuanza sababu ya ushindi wa milki yake ambae hukamilika katika kuweza yote, maana kuanza ni alama ya uzaifu na upungufu wa kutopatikana hapo awali. Na ilihali uzaifu na upungufu haumgusi kamwe mwenyi ushindi kimilki.
8. Ni kwamba habari ya kuanza kwa kitu ni habari ya uzaifu na upungufu wake ambae hupatikana katika umbiko, haistahili kamwe kupatikana katika umungu.
9. Hakika tendo kuanza ndio alama kubwa sana ibainishayo uzaifu na upungufu wa kitu.
10. Na tendo kutangulia ndio alama kubwa iyakinishayo uwezo na ukamilifu wa kitu.
11. Maajabu kadiri ya muujiza wa kutangulia kwake huwasangaza sana watafiti ambae hujaribu kupapasa utukufu wa uzima, hata wakifikia kubisha sababu ya kushindwa, hata wakikubali umbiko peke yake.

12. Kama italazimika kila kitu kianze, ni kwamba hulazimika kila kitu kiumbwe
13. Na kama italazimika kupatikane viumbe peke yao, ebu tuambie ginsi vitakavyo umbwa pasipo muumbaji.
14. Ni muimu, lazima na kawaida muumbaji kutangulia mbele ya vyote, na baadaye ndipo hutokeza kila umbo kadiri apendavyo.
15. Maana kwa kiumbe kuumbwa, inatakika kutangulie milki kibusara itakayo weza na itakayo jua kutokeza umbo.
16. Viumbe haviwezi kamwe kutangulia ajili ya ukosefu wa milki kamilifu, na ndio maana hudai msaada kwa wao kupatikana.
17. Watatangulia je wenyewe na hali hapo awali hawakua ispokua sifuru?
18. Hakika umungu ni muujiza wa kutangulia ulimwenguni kwa walimwengu kupatikana.
19. Hakika umungu ni muujiza wa maajabu, milki isiyo fananishwa, fahamu isiyo na kipimo, mamlaka ya maajabu ulimwenguni.
20. Utangulizi wake ni muujiza una staajabisha viumbe ajili ya udogo wa fahamu yao ; na ilihali hii ndiyo hakika ya kawaida ya umungu.
21. Ni haki na kawaida kusangaa kuenea kwake ambae ni utukufu wa ajabu sana, mamlaka ya kutangulia hali ya kua yote katika yote, milele na melele
22. Mola wa anga na ukiwa, M’bora wa kuenea ambae hakosekane kamwe muda wowote ule, wa pekee aliye huru, mtukufu aliye na uzima

## SURA YA SITA

1. Mwenyenzi Mungu aliumba kila umbo kwa haki, katika usawa wa kawaida ya umbiko.
2. Huwafanya katika utafauti, ajili ya uwingi wao, kufatana na upungufu wao.
3. Haiwezekane viumbe kua namna moja ajili ya kua na upungufu.
4. Na upekee ndio utukufu ambae hupatikana kwake mwenyi ukamilifu.
5. Kadiri ya umbile fulani ndio kadiri ya upungufu fulani ajili ya ukosefu wa milki kamilifu.
6. Jumuiya la upungufu mbalimbali hutimiza umbiko.
7. Ujuzi wa muumba ambae ni fahamu ya ajabu ndio humfanya atokeze viumbe vya kila aina, bila kurudishia ; maana busara yake ni kubwa sana, haitafute sura ya kutokeza wala kushindwa na utokezaji upya.
8. Ndio maana kumepatikana sura nyingi sana, ijapokua ni katika umbile moja lakini tafauti.
9. Utafauti wa hali zao hutokana na uzaifu pamoja na upungufu ambae ni asili ya umbiko.
10. Hakika hakiumbwe ispokua kipungufu ambae hakina ukamilifu.

11. Ijapokua viumbe huzidiana, sio kwamba muumbaji alipendelea baadhi miongoni mwao, bali kawaida ya umbiko

12. Maana pasipo uzidiano, utafauti usingeli patikana kati yao ; na kama utafauti usingeli patikana kwao bila shaka uwingi usingeli kua kwao.

13. Na kama uwingi usingeli kua kwao, kama wangeli kua katika upekee.

14. Na ilihali upekee haugusike kamwe na upungufu, wala haufanyikake, bali ndio utukufu wa muumbaji kadiri ya ukamilifu.

15. Eti itawezekana viumbe kua muumbaji? Ama ni kweli wote wawili wakuwe wakamilifu katika upekee?

16. Kumbe ya faa kukiri upungufu wa kila umbo kwamba ni kawaida kabisa, wala sio kosa wala upendelevu wa muumbaji.

17. Ni kweli kabisa mutu ni mwenyi makosa ajili ya kutengeneza kiato na kofia?

18. Lau kuma kiato kingeli zingatia kazi yake na kuilinganisha na kazi ya kofia kingelisema: hakika mutu hupendelea kofia sababu huiheshimu kwa kuibeba na hunizarau mimi kwa kunitesa na uzito wake kuni kanyaka.

19. Ebu tuambie ni kweli kabisa uyu mutu alifanya kosa kuunda kiato ? ama ni kweli kabisa alipendelea kofia?

20. Ndivyo pia kuhusu muumba na viumbe vyake. Hakika Mungu mwenyenzi hana hatia yoyote ajili ya kuumba umbo fulani na upungufu Fulani

21. Hakika kila umbo ilifanyika katika kawaida ya umbiko, ikifaa kadiri ya kipaji chake ulimwenguni.
22. Thamani ya umalaika ni katika utetezi wa uzuri katika kupinga ubaya.
23. Na thamani ya ushetani ni katika utetezi wa ubaya katika kupinga uzuri.
24. Haiwezekane kutetea uzuri katika kupinga ubaya  wakati hakuna ubaya ulimwenguni.
25. Na pia haiwezekani kutetea ubaya katika kupinga uzuri wakati hakuna uzuri ulimwenguni.
26. Umbile zao zisingeli timilika pasipo wote wawili kuumbwa, wala maisha yao isingeli timilika katika kawaida yake.
27. Ni kwamba maisha ya malaika isingeli patikana bila ubaya kuumbwa.
28. Na pia maisha ya shetani isingeli patikana bila uzuri kuumbwa.
29. Maana utetezi baina yao ndio maisha yao walio pewa mfano wa kazi yao maalumu.
30. Na kama mmoja kati yao asingeli umbwa, bila shaka maisha ya mutu isingeli patikana, kwani maisha ya mutu ni utetezi baina ya uzuri na ubaya.
31. Uhai hupatikana katika uzuri ajili ya kuimarika katika kupinga ubaya.
32. Na pia mauti hupatikana katika ubaya ajili ya kuimarika katika kupinga uzuri.

33. Hakika mwenyezi Mungu ni M'bora wa kuumba, mwenyi busara kamilifu; ni haki kumsifu na kumshukuru kuliko kumlaumu; ni upumbafu ulio-je kumlaumu ajuaye?
34. Ametakasika mwenyezi Mungu bingwa wa kufahamu, atendaye katika kawaida ya kutenda, M'bora wa kukadiria.

## SURA YA SABA

1. Tukuzeni mwenyenzi kila siku maishani mwako, wala usipitiwe hata siku moja bila kumsifu na kumshukuru, maana ndiye pekee anaye stahili kuhimidiwa.
2. Mola mshindi wa walimwengu, mtukufu apangaye na apanguaye kadiri ya idhini yake, wala hakuna kilicho njee ya mipangilio yake, yaani hakuna kilicho kinyume na idhini yake.
3. Hupangilia katika kujua kila umbo; akifahamu bila kusahau yote yatakayo tenda kila umbo kabla ya kuziumba.
4. Na ndio maana huwaagiza yale watakayo tenda, na ilihali huyafahamu kabla ya kuwatokeza; ili kutimiliza kawaida ya umbile zao.
5. Ni maagizo yake ndio hutimiliza maisha ya kiumbe, maana kuagiza kwake ndio kuumba kwake, ni kuyaruhusu yapatikane kadiri ya idhini yake.
6. Hapana kulaumu amri ya Mungu, kwamba ni namna gani huwa agiza watu kuwawekeeni sheria;

7. Hayo ni kwa sababu alipenda kupatikane watakatifu miongoni mwao, ambae wata wa fuata wakaaji wa mbingu, ndio maana aliweka maamrisho yake.
8. Na pia kupatikane wachafu miongoni mwao ambae watafuata wakaaji wa hadeze; ndio maana aliweka makatazo yake.
9. Maana kauli yake tukufu hutenda kwa ajabu ya kutimiza idhini yake, yaani kutokeza kwa rafla kama apendavyo.
10. Na maagizo yake hayabadiri kamwe mapenzi yake wala kutafautiana, maana agizo lake hutokea mapenzini mwake.
11. Mapenzi yake hupangiliwa naye kabla ya kutukiza, na hutimilizwa na kauli yake kadiri ya agizo lake.
12. Nayo mapenzi yake haikadiriwake, lakini hukadiriana katika usawa bila hatia yoyote.
13. Wala hadondokake katika kupenda kwake, na ndio maana haifai kushakia kawaida ya idhini yake tukufu wala kulaumu lolote katika tendo lake.
14. Maana yeye hujua na viumbe hawajui lolote, na huweza vyote na ilihali viumbe hawawezi lolote.
15. Je! Utamkosoa ambae hukuzidia? Ama ni kweli jembe itamuongoza mlimaji?
16. Ni lazima na kawaida kupatikane utafauti mkubwa katika umbiko sababu ya upungufu uliye asili ya umbo zao.
17. Huinuka juu ya viumbe maisha urakibuni, na pia hushuka chini ya viumbe, maisha uatiduni.

18. Kila kiumbe kinayo neema ya namna yake, lakini kuna daraja mbali mbali katika neema yao.
19. Hakika hupokea ujira mkubwa tokea mbinguni, katika urakibu.
20. Ni njia ya kwendea mbinguni, bustanini mwake mola karima.
21. Njia yenyi Baraka, ambae husalimisha umbo, ujira na faraja maishani.
22. Pendeni Mwenyenzi Mungu aliye tangulia kukupendeni kabla yako na kukutokezeni toka sifuru, na kukujaalieni maisha na vifaa vyake na nuru ili upate kushukuru.

## SURA YA NANE

1. Shuudieni utukufu wa mapenzi ya mwenyenzi ambae hujaza tabaka la anga na tabaka la ukiwa.
2. Hakutukie chochote wala lolote ulimwenguni ila ni ndani ya mapenzi ya Mungu mwenyenzi.
3. Na ambae hupatikana njee ya mapenzi yake Mungu, hukosekana ulimwenguni.
4. Ni timilifu sana mapenzi yake, ajili ya kutokea katika ukamilifu mfano wa uvuli wake.
5. Kuona kama upumbafu haupatikani katika mapenzi yake tukufu ndio maana hupatikana katika usawa kila atendalo.

6. Ni yeye mtendaji mkuu, wa kweli na haki, aliye na shani kamilifu mumiliki wa ulimwengu.
7. Hakika mambo yote hutendeka kwa niaba ya mjuzi, ni ajabu ilioje utimilifu wa tendo lake.
8. Kuona kama hakuna aliye na fahamu kama yeye ambae angeli fahamu siri ya uwezo wake huo wa ajabu, ndio maana hakuna awezaye kutefua ajabu ya kutenda kwake.
9. Mwenyezi huchipua toka sifuru shuruli ya kila namna kadiri ya kawaida ya umbiko.
10. Na huifadhika katika mwongozo wake, ndani ya kanuni tokea ukamilifu ambae ni nuru takatifu.
11. Nuru ya Mwenyenzi ni katika mapenzi yake, kadiri ya sehemu ya utukufu wake.
12. Kuona kama nuru ya Mungu ni uvuli wa utukufu wake yeye aliyeko milele, ndio maana nuru yake pia ni milele.
13. Tumieni maishani mwenu nuru ya enzi takatifu ili mupate karama ya uhai, maana ni nuru ya taa isiyo zimika.
14. Nuru yenyi ladha umboni kadiri ya usalama, zawadi ya utimilifu wa maisha
15. Na katika maisha, nuru hupatikana katika ibada ya Mwenyenzi.
16. Matumizi ya ibada ndio matumizi ya nuru takatifu ambae ni uadilifu kitendo kadiri ya usilimu.
17. Heri mutu aliye silimu maishani mwake, maana huchagua uhai ambae ni neema kubwa ya kuishi salama milele.

18. Ni neema na rehema kutoka kwa Mungu Mwenyenzi, kiongozi pekee wa jumla ya viumbe.
19. Usilimu ni mwenendo wa wakaaji wa sehemu ya kwanza ya bahazi la juu angani, ambae ni uadilifu na ustaarabu katika unyenyekevu.
20. Ni mila ya wakaaji wa mbinguni wenyi hidaya kadiri ya nuru maishani, ambae hutimiliza umutu.
21. Katika mpango ulio imarishwa na idhini tukufu, huko juu ya maala pa juu, ambae hujaa fahamu yote.
22. Kutenda adili na zamiri safi, katika unyenyekevu, ndio matumizi ya nuru katika njia iliyo nyooka.
23. Na aliye katika njia iliyo nyooka amekwisha faulu katika utetezi wake, na mambo yake yote ni katika usalama.
24. Maana ni katika mapenzi ya Mungu, na aliye katika mapenzi ya Mungu ni roho takatifu ya Mungu mwenyenzi.
25. Hakuna lisilo wezekana enzini ajili ya milki ya ushindi iliyemo na ndio maana hutawala yote milele.
26. Milki hiyo ni mamlaka ya ajabu katika kutaka, ambae utasi wake ni huru katika kutenda, ambae tendo lake ni utokezaji upya sambamba na idhni yake tukufu, mola hodari aliye na utukufu wa ajabu.
27. Mkamilifu aliye na ushindi, msamehevu na mrehemevu, m’bora wa kuenea ulimwenguni.

## SURA YA KENDA

1. Hii ni habari ya uzima wa Mungu Mwenyenzi.
2. Mola wa anga na ukiwa, m'bora wa kuenea, aliye na shani kuliko vyote ulimwenguni.
3. Mtukufu aonaye yote pasipo kutazama; asikiaye yote pasipo shuruli ya kutekeleza, m'hodari aliye na ujuzi.
4. Ni yeye pekee aliye na uhuru, atendaye yote bila sharti wala shuruli ya yeyote, ambae uzaifu na upungufu wa kufikiri haumgusi kamwe
5. Msaafu aumbae katika usawa, akiongoza peke yake vilivyomo angani na vilivyomo ukiwani; taa tukufu ya ulimwengu
6. Nuru humfumuka kwa wingi, hidaya ya anga na ukiwa ambae humulika kadiri ya kuzagaa juu ya ulimwengu
7. Mtakatifu wa ajabu, aliye stawi arshini peke yake, akijaa utukufu na heshima.
8. Ameinuka kuliko vyote, wala hakuna mwengine mfano wake katika daraja; mufalme wa wafalme wote
9. Mwenyi milki ya ajabu isiyo tokea wala kuendea, kupungua wala kuongezeka, wa pekee anaye enea kabisa.
10. Mamlaka juu ya kila kitu, utukufu wa milele, thamani ya ulimwengu

11. Hakuna mfano wake angani na ukiwani, mteza nguvu, afanyaye apendavyo
12. Mwenyi kujaa hali ya kua yote katika yote akienea pote, katika milki na katika busara
13. Ni yeye aliyeko daima na imara pasipo kufanyika wala kufanyiwa mtukufu atanguliaye
14. Akienea peke yake awali hali ya kua mwanzo wa vyote ulimwenguni
15. Mshindi asiye tanguliwa na yeyote ku vyovyote, ambae ukamilifu wake hukosekanisha kabla na baada dhatini mwake.
16. Muhimidiwa aliye na sifa kamilifu, ambae utukufu wake huienea mbingu na dunia.
17. Mkuu aliye juu, mola wa nyakati zote, aliye tayari muda wote kumiliki ulimwengu.
18. Niyeye peke yake asiye fikiwa na yale asiyo ya taka, ambae huhukumu yanayo tendeka ulimwenguni.
19. Hakika Mungu ndio mzima, ajaaye utukufu wakuenea, wala hakuna mfano wake wala wakutaniana naye, mkuu aliye na uwezo wote.

## SURA YA KUMI

1. Ametakasika mtukufu aliye na ushindi, mola mshangiliwa, bingwa wa mabingwa ulimwenguni.
2. Mwenyi ufalme wa ajabu, ambae hukamilika pekee, juu ya maala pa juu, hali ya kujaa fahamu yote, enzini.
3. Aliye kwa siri bila mfanano, mtegemewa wa haki.
4. Ndiye mjengaji wa umbiko, atendaye kwa kasi la idhini yake .
5. Msifiwa wa ajabu aliye na mamlaka ya kumiliki, ambae viumbe humtaja kwa majina mengi kadiri ya kutenda kwake.
6. Wakali anapo jenga umbiko humuita; M’bora wa kuumba, m’neemeshaji mwingi wa rehema, baba wa salama...
7. Na wakati wa ubamoaji humuita: M’kali wa kuadhibu, mdhikishaji na mkomeshaji, bingwa wa banashari...
8. Na kujenga kwake na kubomoa kwake ni katika baadhi la juu angani
9. Maala ambae muumbaji kawa kadirieni maisha na mauti, katika mpango ulio imarishwa na idhini tukufu.
10. Akaweka uhai juu ya maki ya mbingu, na mauti chini ya mbingu
11. Na hulinda siri ya umbiko la wanahewa haramu katika maunganio ya mbingu na hadeze.
12. Ni maala mfano wa baraza la kambi, hujumuika humo kabla na baada ya kuishi duniani, kwa muda muchache tu
13. Na badaye hujumuika kila yule kambini mwake ambae zamiri yake hutegemea.

14. Mwenyenzi huwaneemesheni kuwatayarishieni kambi iliyo bora sana kwao wafanyao ibada duniani. Na pia iliyo mbovu sana kwao wafanyao uovu duniani.
15. Akikupambieni bustani na nuru kubwa; nuru yenyi ladha umboni, pumzi yenyi manukato.
16. Huninginia ndani mwake, mfano wa nyota katika kumeremeta, wajumuikao.
17. Hakika shukrani ni zake mwennyenzi Mungu, mola wa majeshi yote, aliye na mamlaka yote.
18. M'bora wa wapodoaji ambae rangi yake huokoa umbo ijipakaayo, mpanaji wa daraja.
19. Mzima aliye muujiza katika kutangulia, na maajabu katika kuumba mtukufu asiye linganishwa.
20. Hufanya apendavyo ajili ya kujaa milki kamilifu ambae huweza yote.
21. Ni mkubwa saana mwenyenzi mungu, mwingi wa baraka ambae hujaa heshima na sifa kamilifu.
22. Na humtukuza vilivyomo angani na vilivyomo ukiwani, mola wa kila umbo, mkamilifu katika yote.

## SURA YA KUMI NA MOJA

1. Sifa na heshima humustahili mwenyenzi Mungu aliye kikweli ambae hualikwa na walimwengu kuhitaji msaada wake, mlezi wa viumbe.
2. Mjuzi asiye sahau wala kusinzia, muonaji na msikiaji wa jumla ya viumbe
3. Ameona yote ulimwenguni na ilihali hana kiungo chochote kiitwacho jicho ndani mwake.
4. Na husikia yote ulimwenguni na hakuna kiungo kiitwacho sikio ndani mwake.
5. Na pia husema na ilihali hana kinywa dhatini mwake.
6. Ujuzi wake huzidia macho kwa kuona, na huzidia masikio kwa kusikia, na pia ujuzi wake huzidia kinywa kwa kusema.
7. Hakika kujua ni kuweza yote, hakuna kisicho fanyika na mjuzi.
8. Ni mwenyi utukufu sana ambae macho ya viumbe hayawezi kumzingantia, ispokua kwa njia ya vitimbi vyake, machoni kiroho.
9. Maana kinacho onaka umboni mwa mutu ni huo mjengo kihewa ambae ni pumzi.
10. Pumzi ni mjengo kihewa, kuona kama hewa ndio fikara, ni kwamba mjengo kihewa ndio mjengo kifikara.
11. Kuona ni kufahamu, na kusikia pia ni kufahamu
12. Maana pumzi ni fikara, na fikara ni fahamu ; kumbi kinacho onaka katika umutu ni hiyo fikara ambae hufahamu, ni yao ndio macho ionayo.

13. Na pia kinacho fanya mutu asikie ni fikara, ni yao ndio masikio isikiayo.
14. Jicho na sikio kimwili ni viungo mfano wa njia ambae fikara hupitia kwa kuona na kusikia, yaani kwa kufahamu.
15. Katika umbo la mwanahewa-haramu, kuna aina tano ya mapito ya fikara yake kwa kufahamu jambo.
16. Ni katika viungo vitano vya utambuzi, na vyao ni ; jicho, sikio, ulimi, pua, na mwilini mwake.
17. Mapito ya fikara katika jicho ndio utazamaji ; na katika pua ndio unusaji ; na katika ngozi ama mwilini mwake ndio ugusaji ; na katika ulimi ndio uonjaji.Na katika sikio ndio utekelezaji.
18. Mutu huzingatia kimwili kwa njia ya utazamaji, utekelezazi, unusaji, ugusaji na uonjaji.
19. Uzingatiaji kimwili hutambua umbiko peke yake, wala hauwezi kuzingatia enzi tukufu ambae ni tafauti sana na umbiko.
20. Huzoroteka uzingatiaji kimwili ajili ya ujinga upatikanao mwilini.
21. Na ndio maana kwa kumuona Mungu Mwenyenzi sio kawaida kumtazama kimwili, lakini ni kawaida kabisa kutumia utaalamu kifikara ambae ni akili, kadiri ya utazamaji kiroho kwa ku zingatia uzima wa Mungu.
22. Hushukiwa na nuru akili urakibuni, na pia hufunikwa na giza akili uatiduni.

23. Akili hutimilika katika matumizi ya ibada, hakika huzingatia bayana utukufu wa Mwenyenzi, yule afanyaye ibada katika mustari wa neno la Mungu.
24. Akipata kuzingatia utukufu wa enzi kwa njia ya mbingu takatifu, akionana na watakatifu, wa mbinguni ambae humnukulu mola wa walimwengu.
25. Hakika fikara huzingatia kidogo tu katika kupapasa, ispokua ujuzi ndio uonao kikweli.
26. Na ndio maana muonaji wa kweli ulimwenguni ni Mungu peke yake, mshindi ajuaye.

## SURA YA KUMI NA MBILI

1. Ushindi ni wake Mwenyenzi Mungu, ambae peke yake katangulia ulimwenguni kadiri ya kuenea.
2. Mwenyi kuwako kikamilifu kwa ushindi wa milki yake, akitawala juu ya yote ulimwenguni kwa mamlaka yake mwenyewe
3. Mtukufu zaidi ya vyote hodari aliye na sifa na heshima, mkuu na m’bora wa mashujaa katika kutenda, chemchem ya baraka ulimwenguni.
4. Aliye mwanzo wa vyote ajili ya kutangulia, mamlaka ya ajabu itokezayo, wa pekee aliye na ujuzi, mshindi aliye juu.

5. Hakuna aliye mtangulia yeye ajili ya kutokuanza, maana hutangulia kabla ya matukio yake.
6. Hakuna «kabla» yake ajili ya kutokuanza ; angeli kua na mwanzo wake kama kungeli patikana kabla yake, maana kungeli kua muda wa mbele ya tarehe ya kuanza kwake.
7. Na pia hakuna «baada» yake ajili ya kutokua na mwisho wake, angeli kua na ukomo wake, kama kungeli patikana baada yake ; maana kungeli patikana muda wa nyuma ya upatikanaji wake kiisha tarehe ya ukomo wake.
8. Mwenyenzi hushinda maanzio na hushinda makomeo, mtukufu aliye na shani ya ajabu, ambae hupatikanisha vyote ulimwenguni
9. Hutangulia namna ya kuenea, kadiri ya ukamilifu akihepukana na upungufu wote.
10. Hakika ni bahati na furaha kwetu enzi tukufu kutangulia, kama sivyo sifuru ingeli tawala milele, maana hakungeli patikana watu wala kufanyika lolote.
11. Ni muujiza ulio-je kutangulia kwake? hakika hali kama hiyo ndio utukufu wake huo wa ajabu ya kuenea katika yote.
12. Na utukufu wake huo wa ajabu ya kuenea katika yote ndio ukamilifu ambae ni uzima
13. Na ukamilifu ni katika upekee ajili ya ushindi wa milki yake
14. Ndio maana kuna Mungu mmoja tu bila mshirika ambae hutawala ulimwenguni, milele na milele.

15. Kama kungeli kua mwengine wa namna yake hasingeli kua na ukamilifu, maana uwezo wake ungeli kua na mipaka, kwani hasingeli kua na utasi juu ya mwenzake.
16. Na hali kama hiyo ya uzaifu wa kushindwa na fulani ndio upungufu ambae haumgusi kamwe mkamilifu.
17. Na kama angeli kua na mipaka kimilki na kibusara hasingeli kua na uwezo wa kuumba, bali angeli kua na ginsi ya kubadiri kimatumizi umbo aliyo ikuta tayari imekwisha umbika, wala hasingeli tangulia bali angeli anza .
18. Ni kwamba ukosefu wa milki kamilifu hufanya kitu kiwe na mwanzo wacho hali ya kua kiumbe sambamba na makadirio ya mshindi aliye kamilika .
19. Hasingeli enea mshindi lau kama kungeli kua mwengine, maana katika ukamilifu hakuna utafauti wala mipaka, kufanana wala kulingana na chochote

## SURA YA KUMI NA TATU

1. Ametakasika Mwenyenzi Mungu-m’bora wa kukadiria, mola mtukufu, mkuu wa wapanaji
2. Ni yeye aliye enea ulimwenguni, ambae peke yake huepukana kabisa na asili.
3. Asili hupatikana kwao viumbe, ambae hukosewa milki kamilifu.

4. Viumbe wenyi fikara timamu hutafuta ufahamu wa asili yao, wakijifunza hakika ya matokeo yao na maendeleo yao katika ulimwengu
5. Umbo zao na maisha zao ni karama kutoka kwa Mwenyenzi Mungu, mola wa walimwengu.
6. Hutokezwa toka sifuru, viumbe vyote, pasipo matakwa yao, wakikadiriwa umbo bila kuichangua wala kuhelewa mradi wake.
7. Wakitayarishiwa vifaa vya maisha yao kabla ya umbo zao kufanyika, hata wakitokezwa sambamba na idhini yake.
8. Hakika viumbe ni zaifu sana, umbiko kiusaidizi, ambae hudai msaada kwa wao kuishi.
9. Kuona kama wamepatikana ulimwenguni pasipo manuizi yao, ndio maana maisha yao hupangiliwa na yule aliye watokeza toka sifuru.
10. Kwani wao wenyewe na maisha yao ni mpango ulio pangwa na muumba aliye kwa siri.
11. Na pasipo mpango wake mwenyenzi, maisha yao ni bure hali ya kukosekana .
12. Wote kwa jumla huishi kwa idhini tukufu ya muumba wao wala hakuna maisha njee ya idhini yake tukufu.
13. Kuona walifanyika pasipo wao wenyewe kutambua wala kutaka ,mamlaka ni kwake Mwenyenzi kuwakadiria ginsi apendavyo.
14. Huwakadiria umbo, maisha na sheria kadiri ya mapenzi yake, kwa njia ya neno lake.

15. Hupatikana wote kwa njia ya neno lake na pia huishi kadiri ya neno lake.

16. Ndio maana kila mutu hulazimishwa kutumia neno la Mungu ili apate uhai, maana maisha kinyume na nuru ya Mungu hukoma namna ya kupotea.

17. Mwenyenzi Mungu aliwatokeza wote namna moja, katika idhini yake tukufu, lakini ka fanya utafauti katika umbile zao ili uwingi upatikane kwao.

18. Huandalia katika kawaida ya umbiko, shuruli fulani kadiri ya kipaji fulani, utimilifu wa karama.

19. Haimjuzu Mungu kutokeza umbo moja peke yake maana upekee haustahili kwake yule asiye na uwezo wa vyote, maana ni mzaifu ambae hudai msaada, bali hustahili yeye aliye mkamilifu, ambae huweza vyote bila shuruli wala tatizo lolote.

20. Na hii ndio kawaida : "upekee katika umungu, na uwingi katika umbiko"

21. Uwezo wa vyote husababisha upekee katika ukamilifu kadiri ya uzima ambae ni umungu.

22. Na upungufu ndio husababisha utafauti, na utafauti ndio husabisha uwingi, katika umbiko.

23. Ni kawaida kila umbo kupatikana na upungufu fulani, maana upungufu ndio asili yake, yaani alitokea katika upungufu.

24. Hakiumbwe ulimwenguni ispokua kipungufu, ambae ni zaifu kinyume na uwezo.

25. Ni hiyo hali pungufu kadiri ya sifuru ndio uzaifu ambae hugeuzwa na milki kamilifu kua kitu fulani.

26. Kimegeuzwa ajili ya kua zaifu, maana kisingeli kua pungufu na zaifu kama kisingeli umbwa, kwani kingeli kua kamilifu kadiri ya kuenea kimilki na kibusara.

27. Kilicho umbwa ni kitu pungufu na zaifu, hakika umbo fulani ni upungufu fulani.

28. Kilicho kamilika hakiumbwake ajili ya kuenea pasipo maanzio wala makomeo.

29. Ni kwamba haifai kumlaumu muumbaji ajili ya kuumba umbo fulani na upungufu fulani.

30. Kama italazimika umbo fulani isiwe na upungufu wowote, ni kwamba hulazimika umbo ile kua kamilifu.

31. Na kama umbo fulani italazimika kua na ukamilifu, ni kwamba umbo iyo hulazimika kua muumbaji, maana ukamilifu haupatikani ispokua katika umungu.

32. Eti viumbe havistahili kujumuika ulimwenguni ispokua muumba peke yake?

33. Wapumbafu humlaumu Mola wa walimwengu ajili ya utafauti wao usababishwao na upungufu wao, wakitarajia ukamilifu hali tukufu ya upekee kadiri ya umungu.

34. Bila kutambua ya kama ukamilifu haufanyikake wala kufanana na yeyote munamna yoyote ile ajili ya kuenea.

35. Hakika aliye na anaye stahili ukamilifu ni Mungu peke yake, lakini viumbe vyote ni katika upungufu.

## SURA YA KUMI NA INE

1. Utakatifu ni wake Mwenyenzi Mungu, kiongozi pekee wa jumla ya viumbe; Mola wa wanahewa na wazila hewa, mshindi aliye juu.
2. Huongoza kwa kauli yake tukufu, m'bora wa kutenda ambae hutokeza kila upatikanaji ulimwenguni.
3. Ni yeye mkadiriaji wa kila umbo, aongozaye umbo baada ya kuipatikanisha .
4. Ameinuka sana zaidi ya yote, mwenyi mamlaka ya kuenea katika ulimwengu.
5. Akihukumu kihakika vilivyomo angani na vilivyomo ukiwani pasipo msaada wala shauri la yeyote
6. Ni kwa sababu hakuna mwengine aliye kamilika kama yeye ndio maana husalia peke yake katika utukufu wa ajabu
7. Mjuzi wa siri, ambae hutefua ndani ya kila zamiri, tajiri wa habari ulimwenguni

## SURA YA KUMI NA TANO

1. Ni nani anaye mkanusha Mwenyenzi Mungu?
2. Ni nani yule anaye shakia uzima wa muumba wake?
3. Je! Amejidai mwenyewe kwa dalili gani?
4. Eti ni yeye ndio katangulia bila kuanza ambae hustaili kuumba walimwengu?
5. Ama ni yeye ndio muweza wa vyote na Mjuzi wa vyote vilivyomo ulimwenguni?
6. Ama ni kweli yeye ndio mkamilifu asiye gusika na upungufu wowote?
7. Ama huzani kama ulimwengu na walimwengu hujitokeza vyenyewe katika sifuru?

## SURA YA KUMI NA SITA

1. Humkanusha Mwenyenzi, kwamba hakuna utukufu wa namna hiyo, ajili ya uchache wa elimu.
2. Fikara yao hukomea katika mwili, kwamba kilicho na mwili ambae njia tano ya fikara kupitia hudhatiti ndio kipatikanacho.

3. Huo ndio upumbafu wa kweli, hawazingatie ila kidogo tu.
4. Tazama!m kunapatikana sehemu zingine kubwa saana kuliko dunia, namna ingine ya upatikanaji kinyume na hali ya dunia, ambae utazamaji kimwili hauzingatie hata kidogo.
5. Katika sehemu hizo hupatikana baadhi tukufu kabisa la ‟Enzi”, ambae hujaa milki kibusara.
6. Ni milki hiyo ndio huweza kufanya yote, ambae haigusike na uzaifu wala upungufu wowote ajili ya ushindi.
7. Na milki hiyo ya ajabu, yenyi kujua na kuweza yote ndio enzi yake Mungu.

**SURA YA KUMI NA SABA**

1. Shuudieni uzima wa mwenyenzi ulimwenguni.
2. Hakika viumbe vyote ni hunusu na vipande, ambae kafanyika muda falani.
3. Hawakuwa muda fulani na hawata kuwa muda fulani.
4. Ni wavuguvugu katika upatikanaji wao ajili ya kukosewa milki kamilifu.
5. Ni milki hiyo ndio hustiri upatikanaji pasipo kutingizika wala kubadirika.
6. Ni hali tukufu sana kadiri ya utangulizi ambae huenea katika yote, pekee.

7. Utangulizi ni namna ya kupatikana bila mwanzo wala mwisho ni hali tukufu sana kadiri ya ukamilifu, na ukamilifu ndio uzima; na uzima ndio umungu.

## SURA YA KUMI NA NANE

1. Mutu hukosewa milki ya ushindi, ni umbo zaifu kabisa, yenyi kuzoroteka kimilki na kibusara, ajili ya kuvaa mwili.
2. Maana mwili ni ujinga, hushirikishwa fikara na ujinga ndani mwake.
3. Ndio maana mutu hufikiri na husahau, namna ya kuzingatia na kulala.
4. Kupitiwa namna ya kulala ndio tunda la mwili, na pia kufikiri namna ya kuzingatia ndio tunda la pumzi.
5. Hakika mutu ni umbo pungufu sana, ambae haina uwezo wowote wa kupatikana bila msaada.
6. Ni umbo zaifu sana isiyo weza lolote.
7. Umbo yenyi kufuata kanuni ya mshindi, ambae peke yake bila msaada isingeli patikana ulimwenguni.

## SURA YA KUMI NA KENDA

1. Ulimwenguni kuna utangulizi wa milki kibusara ambae ni mamlaka ya kuweza na kujua yote, ambae uzaifu haupatikani ndani mwake.

2. Mamlaka yake huenea katika yote kimuujiza bila kuanza wala kukoma. Mola mshindi, uwezo wa milele.
3. Ni kwa sababu huenea (katika yote) ndio maana hakuna maanzio yake, maana huanza kile kisicho enea ambae ni kipungufu.
4. Milki hiyo ya kuenea pasipo mipaka ndio daraka kubwa sana na zaidi kadiri ya uwezo wa vyote.
5. Na uwezo wa vyote ndio mamlaka ya uumbaji ; haumbe ispokua yule aliye na uwezo wa kutenda yote.
6. Muujiza wa kuenea ndio maajabu ya kutokeza ambae hakikua popote ulimwenguni ; ni uwezo wa ajabu ambae hakuna kiumbe kiwezacho kuukagua ajili ya udogo wa fikara mbele ya ujuzi.
7. Hakika mjuzi ndio hutangulia, kadiri ya kuenea ; na pia pekee hutokeza, kwa mamlaka yake, ambae hakikua popote ulimwenguni.

**SURA YA MAKUMI MBILI**

1. Ujuzi ni busara kamilifu, fahamu ya ajabu sana ambae haishindwe wala kusahau kitu.
2. Na fahamu ya vyote ndio milki kibusara, ambae ni ushindi juu ya kila kitu.
3. Na ushindi juu ya kila kitu ndio uwezo wa vyote, mamlaka ya kumiliki kila jambo.

4. Hakuna mwengine aliye na mamlaka mfano wake, wa pekee aliye stawi arshini.
5. Viumbe vyote ulimwenguni hulindwa naye, wala hakipatikani chochote kinyume na idhini yake.
6. M'bora wa kutenda, aliye na kasi ya ajabu mapenzini mwake.
7. Mungu mwenyi uzima, ajaaye utukufu mkuu asiye zembea wala kuchoka, mtakatifu wa kweli, aliye juu.

## SURA YA MAKUMI MBILI NA MOJA

1. Mwenyenzi huenea maala pote katika yote, mwenyi utukufu usiye pungukiwa kitu, mshindi ulimwenguni.
2. Ni mwenyi uhuru kiupatikanaji, ambae hujaa katika kua, akistirika milele na milele.
3. Hupatikana pasipo mipaka namna ya kutawala pasipo ukomo ulimwenguni.
4. Ni mwenyi kuwako daima, ambae hakukosekana wala hata kosekana muda wowote ulimwenguni.
5. Ni kwa sababu Mungu pekee ndio mkamilifu mwenyi kuenea katika uwezo na katika busara.
6. Milki yenyi ushindi kibusara aliyo nayo ndio humkamilisha namna ya kuhepukana na upungufu wote.

7. Hakika mkamilifu ni mbalimbali kabisa na mpungufu, maana yule ni muweza yote, na uyu ni zaifu sana ambae hawezi chochote.

## SURA YA MAKUMI MBILI NA MBILI

1. Haiwezekane kamwe sifuru kutenda, na ndio maana inatakika, kwa hakika, utangulizi wa milki yenyi ushindi ili tendo ipatikane.
2. Ni kwa sababu sifuru ni ujinga ndio maana haina ginsi ya kutenda.
3. Ujinga hauwezi kutenda lolote sababu ya kujaa uzaifu na upungufu ndani mwake, ispokua ujuzi ambae hujaa uwezo na ukamilifu ndio uwezao kutenda, ajili ya kuenea.
4. Kuenea ndio kukamilika, namna ya kutokua na upungufu wowote
5. Na ambae huenea ulimwenguni ndio yule ajaaye ujuzi, mwenyi mamlaka yote ku vyote, mtukufu wa ajabu.
6. Ni yeye atanguliaye na aumbaye, aliye shinda ; ambae utukufu wake na mamlaka yake humtenganisha na sifuru milele.
7. Ni lazima milki ya ushindi itokeze vitu mbali mbali toka sifuru, kwa umbiko kupatikana, kama sivyo hakungeli tukia chochote wala lolote katika sifuru.

## SURA YA MAKUMI MBILI NA TATU

1. Kuona ni kufahamu, na kuonekana ni kufahamika.
2. Sio kwamba kuzingatia na kiungo cha mwili kiitwacho jicho peke yake ndio kuona.
3. Fahamu hupatikana kwa njia nyingi, maana fikara ni shuruli kubwa sana
4. Ni utaalamu ndio huleta ufahamu wa aina nyingi ambae mwili hauwezi kuzingatia.
5. Ni kwamba anaye zingatia utukufu wa mwenyenzi amemuona Mungu, maana amefahamu ya kwamba kuna Mungu.
6. Na yule asiye zingatia utukufu wa Mwenyenzi ndio kipofu asiye muona Mungu wala hawezi kufahamu ya kwamba kuna Mungu ajili ya uchache wa fikara yake.
7. Mutu hawezi kuonana na Mungu uso kwa uso sababu hawalingane kibusara; maana kuonana uso kwa uso ni kufahamiana sawa sawa; na kufahamiana sawa sawa ni kua katika daraja moja ya busara, kwamba kadiri ya fahamu ya uyu ndio pia kadiri ya fahamu ya yule, hata wakifahamiana namna moja
8. Mungu hujua lakini mutu hajui ; ndio maana mutu huzingatia tu utukufu wa mwenyenzi bila kuonana naye, maana kuonana ni kufahamiana
9. Haiwezekane kufahamiana na yule asiye kua na daraja moja nawe katika busara.
10. Mungu kutoonekania viumbe ni hasa ajili ya ukubwa wa daraja ya busara yake mbele ya viumbe.

11. Daraja ya busara yake ni kubwa sana na zaidi ambae viumbe hawaoni hata pa kuanzia wala pa kukomea katika utafiti wao ; na ndio maana uzima wa Mwenyenzi ni muujiza mkubwa sana mbele ya viumbe .
12. Viumbe hustaajabu sana hali hiyo tukufu ya mwenyenzi Mungu, ambae, haikurubiane kamwe na hali zao zaifu.

## SURA YA MAKUMI MBILI NA INE

1. Ulimwengu ni jumla ya tabaka tatu : la enzi, la anga na la ukiwa.
2. Katika enzi hupatikana utukufu wa ajabu sana ; maana ndio shina kadiri ya chemchem ya vilivyomo angani na ukiwani.
3. Enzini hujaa ujuzi pekee, milki kuu ajabu ambae haifanane na chochote.
4. Na angani hupatikana fikara ya kila aina, na utukufu haupatikane humo ispokua chembe ya huko juu katika sehemu ya kwanza ya bahazi la juu angani.
5. Na ukiwani hupatikana ujinga, hamna utukufu wowote ajili ya giza, ni maala pa zaifu sana ambae hapafanyike lolote.
6. Na anaye patikana enzini ndio Mungu pekee mtukufu na mbora wa kuenea ambae hustawi katika uhuru. Hakuna maikalio yake kwani hana kiungo chochote ndani mwake wala kimo. Hakae wima wala chini sababu ya kuto fanana na kiumbe.

7. Ni mkamilifu wa ajabu ambae hafanane na maikalio ya yeyote miongoni mwa viumbe; maana maikalio fulani ni namna ya upungufu fulani.
8. Mungu muweza atafananishwaje na umbo alizo ziumba ? kila umbo ni pungufu na zaifu tafauti kabisa naye mkamilifu aliye na uwezo wa vyote.
9. Hakika uzima wa Mungu ni jambo kubwa sana na zaidi kadiri ya muujiza usio fananishwa wala kulinganishwa na upungufu wowote.
10. Ndio maana haifae kulinganisha uzima na maisha maana maisha ni upungufu na uzima ni ukamilifu.
11. Wala Mungu hakae angani wala ukiwani; maana yeye sio mwanaanga wala muzilahewa.
12. Lakini kuona kama Mungu hustawi enzini pekee ndio maana huitwa kwa jina la Mwenyenzi.

## SURA YA MAKUMI MBILI NA TANO

1. Aliye na uwezo wa vyote hataabikake wala hashurulikake ajili ya chochote, mola mshindi apatikanaye enzini.
2. Atakavyo hutukia bila kazi yoyote; ni mwenyi mamlaka ya kutenda bila shuruli.
3. Kazi hufanyika na wazaifu wasio kua na milki ya ushindi.

4. Hushurulikia utimilifu wa umbo zao ajili ya kusongwa na upungufu.
5. Ndio maana hutetea muda wote maishani ajili ya kutokamilika.
6. Na utetezi wao ndio maisha yao kadiri ya kazi maalumu walio pewa, namna ya shuruli kubwa ya kutafuta ginsi ya kutimiliza umbo zao ambae hutatizwa namna ya kuzoroteka na upungufu.
7. Na upungufu huo ambae huzikumba umbo zao ndio asili yao.
8. Na asili yao hiyo ya upungufu ndio msingi wa umbiko lao, maana wasingeli umbwa bila kua upungufu.
9. Hakiumbwe ispokua kipungufu; maana kilicho kamilifu hakifanyikake kwa namna yoyote ile.
10. Ni asili ya umbo, ambae ni upungufu, ndio humtatiza kiumbe namna ya kutetea, akifanya kazi mbalimbali ili apate utimilifu.
11. Lakini kwake aliye kamilifu hakuna tatizo lolote wala shuruli, wala hafikiwake na asiyo ya taka, wala hatumikake kwa kutenda jambo.
12. Mwenyenzi mtukufu hutenda kwa idhini yake, atakavyo hutukia kwa rafla, mumiliki aliye na shani ya ajabu.
13. Na ndio maana Mungu peke yake ndio aliye stawi hali ya kuwa huru kabisa, ambae hataabikake kwa kufanya kazi yoyote ile.
14. Huko mwenyenzi huongoza umbiko baada ya kuitokeza toka sifuru.
15. Na uongozi wake huo sio kazi mfano wa uongozi wao viumbe, bali kwake hufanyika kila jambo kwa idhini, bila shuruli yoyote.

16. Ni ajili ya kua na milki ya ushindi ndio maana Mungu hagusike na shuruli yoyote ile.

## SURA YA MAKUMI MBILI NA SITA

1. Ni upumbafu sana kulinganisha uzima na maisha.
2. Maisha ni uzaifu mkubwa, ni upungufu usio na thamani pasipo msaada.
3. Na uzima ndio milki ya ajabu sana, namna ya kuenea katika yote, thamani ya ulimwengu ambae pasipo yeye kusingeli fanyika chochote ; ni ukamilifu kimilki ambae hutenda kwa idhini bila shuruli.
4. Kumfananisha mzima na yule anaye ishi ni upumbafu kabisa.
5. Ni uchache wa akili ndio hufanya watu wamfananishe Mola wao na hali zao zaifu, maana wamezani ya kwamba hufanana na wao.
6. Mungu muumba hana maisha ya aina yoyote ile ajili ya kuenea, ni mwenyi uwezo wa yote ambae hagusike kamwe na uzaifu huo wa kuishi, kwani kuishi ni kutetea kadiri ya shuruli kifikara.
7. Mtukufu asiye gusika na shuruli yoyote, ambae mapenzi yake hutimiza bila kazi, mshindi aliye na mamlaka ya ajabu.
8. Mwenyenzi ni mwenyi uzima tafauti na maisha ; ni mwenyi kuenea, katika kuwako, ambae hutangulia ulimwenguni.
9. Wanahewa ndio wenyi maisha, ambae hutaabika na shuruli ya kutetea, ambae hutumika kazi ili kudumisha umbo zao.

10. Hutaabika ajili ya uzaifu na upungufu katika busara, hawana milki kibusara.
11. Hakika kutamka tu «maisha ya Mungu» ni kukufuru kabisa ni kama kumtusi kadiri ya kuunajisi utukufu wake wa ajabu.
12. Hakuna mwengine aliye kamilifu ulimwenguni kama vile Mungu ; ni yeye pekee aliye na uzima, ambae uzaifu na upungufu wa kuishi haumgusi kamwe.

## SURA YA MAKUMI MBILI NA SABA

1. Enzini kuna heshima kubwa sana ; hakuna ila utukufu mtupu kadiri ya upekee.
2. Naye mwenyenzi hustawi katika heshima kubwa sana, msifiwa aliye inuka zaidi, mkuu.
3. Hakupatikane utafauti, shuruli wala uwingi wala upungufu ndani mwake.
4. Ni kwa sababu humo ni eneo la milki kibusara ambae haina kasoro wala doa, hakuna palipo wazi ambae pangeli jazwa.
5. Uwingi hupatikana angani na ukiwani, maala penyi uzaifu na upungufu, ambae hujazwa na mumilki aliye yatokeza toka sifuru
6. Mungu mwenyenzi ni mkamilifu ambae uwingi hauna fasi kwake, ni mwenyi upekee ajili ya kuenea
7. Na ndio maana hukamilika peke yake enzini bila wa kuchangia naye fasi.

8. Kama huitwa Mwenyenzi ni kwa sababu ya kupatikana peke yake humo enzini, hakuna wenyenzi, bali kuna mwenyenzi ajili ya upekee.
9. Enzi ni kambi la ajabu, humo hujaa uwezo wote wenyi ushindi namna ya muujiza wa maajabu.
10. Ni upumbafu sana kulinganisha enzi na vitu vipungufu ambae hupatikana angani na ukiwani.
11. Ni viumbe ndio hutumia namna ya kula anga na ukiwa ili vipate kusikimiza umbo zao za kihewa na za kimwili, kimaisha.
12. Asiye kula miongoni mwa wanahewa hawezi kuishi, maana chakula ndio hujenga umbo za kihewa na za kiukiwa.
13. Aliye wa hewa hutumia hewa namna ya kula kadiri ya kupumua, na aliye wa mwili hutumia mwili namna ya chakula.
14. Hayo ni kwa sababu ni wapungufu na wazaifu ambae hutafuta vifaa ili kusaidia umbile zao.
15. Lakini mkamilifu hatumiake kifaa chochote ili kusaidia uzima (wake), bali yeye ni mwenyi kuenea katika yote, bila kiu wala njaa, shida wala tatizo lolote.
16. wala uweji wake haudai kifaa chochote wala msaada wowote ajili ya kukamilika namna ya kuenea kiushindi.
17. Wala yeye mtukufu hatumiake enzi kama vile wanahewa hutumia hewa namna ya kupumua.
18. Hakika mwenyenzi ni mwenyi ukamilifu wa ajabu, ni yeye mwenyewe katika upekee namna ya utupu wa enzi.

19. Hakuna sehemu mbili kwamba uyu ndio mwenyenzi na hii ndio enzi, lakini utupu wa ajabu;
20. Enzi ndio dhati yake mwenyewe, hakuna utafauti wa maki ndani mwake.
21. Kungeli kua utafauti kati yake na enzi kama vile wanahewa na hewa yenyewe walivyo bila shaka asingeli itwa mwenyenzi bali mwanaenzi, na upekee usingeli kua kwake.
22. Lakini kuona kama yeye ni utupu wa enzi, ndio maana hakuna Wanaenzi ispokua mwenyenzi peke yake.

## SURA YA MAKUMI MBILI NA NANE

1. Ametakasika mwenyenzi Mungu, M’bora wa kuumba, Mola wa pahali pote, mufalme aliye juu.
2. Hakuna mwengine ila yeye, mshindi aliye tangulia kadiri ya kuenea kabla ya ulimwengu.
3. Ni yeye aliye kua, aliyeko na atakaye kua, namna ya muujiza ambae mipaka haipatikani ndani mwake
4. Hakuna kabla yake wala baada yake, maanzio wala makomeo ; kuzaa wala kuzaliwa, kuchoka wala kushindwa.
5. Mwenyi milki ya ajabu ambae hushinda maanzio na makomeo mtukufu asiye badirika

6. Haimjuzu muweza kuzaufika kwa kuanzishwa na kukomeshwa.
7. Ni yeye ndio muanzishaji wa kila umbo, la wazi na siri.
8. Mtangulizi wa vyote ulimwenguni, ambae peke yake hutokeza kwa idhini yake vilivyomo angani na ukiwani, mkuu asiye kua na wa zaidi yake.
9. Milki yake humfanya atangulie pekee bila mfanano, na aumbe kila kiumbe bila msaidizi, na atawale juu ya yote bila mshirika.
10. Bingwa mkuu, aliye na kasi la uwezo wa kutenda, mkamilifu wa ajabu
11. Kuumbwa na kuzaliwa ni uzaifu mkubwa sana, ambae haumgusi wala kumkurubia mwenyenzi aliye jaa milki ya ushindi.
12. Kila kilicho zaliwa ni kiumbe zaifu kabisa, ambae ni tafauti kabisa na Muumbaji (wake).

## SURA YA MAKUMI MBILI NA KENDA

1. Ushindi ni wake mwenyenzi Mungu ; mudiriki wa ulimwengu.
2. Mungu wa wanahewa na wazilahewa, mtegemewa, aliye inuka kuliko yote, ambae hutawala kwa ushindi wa milki yake.
3. Ni yeye mkuu wa masiku, mkongwe, ambae huzidia wote ajili ya kutangulia.
4. Ni mkubwa sana na zaidi ajili ya kuenea kiupatikanaji pasipo kabla wala baada yake.

5. Ni hali tukufu sana hiyo ya kukamilika katika kuwako ndio jambo ambae humfanya ainuke juu ya yote bila wa kulingana naye
6. Ni mwenyi mamlaka kubwa ajabu, ambae hupindukia walimwengu wote kwa jumla.
7. Hakuna mwengine akurubiaye utukufu huo wa ajabu wenyi kupatikana kadiri ya muujiza, ambae fikara haiwezi kamwe kukagua hakika ya kadiri yake
8. Milki katika busara ijaayo utukufu na ushindi kadiri ya kuzidia, juu ya maala pa juu ulimwenguni.
9. Hujieneza mwenyewe kadiri ya kujienelea kiutangulizi namna ya mamlaka ya milele kadiri ya ukamilifu.
10. Na ukamilifu ndio uzima, na uzima ndio umungu, na umungu ndio ufalme wa milele.
11. Hakika Mwenyenzi Mungu ni mkubwa kabisa, mtukufu anaye stahili kusifiwa, ambae peke yake hujaa mamlaka ya milele.
12. Ametakisika Mwenyenzi Mungu, kiongozi pekee wa jumla ya viumbe, ambae hustawi katika uhuru, mkadiriaji wa karama, aliye pasipo yeyote, milele na milele.

## SURA YA MAKUMI TATU

1. Ulimwengu sio chochote pasipo enzi ; isingeli kua ukamilifu wake kama ulimwengu usingeli patikana.

2. Ukamilifu wake humueneza pasipo maanzio wala makomeo, hali ya kua yote katika yote.
3. Ni lazima kabisa kumshukuru Mwenyenzi, maana bila yeye kusingeli patikana yeyote wala chochote miongoni mwa viumbe.
4. Na watu hujiuliza, ni wapi enzi hupatikana katika ulimwengu?
5. Na ni namna gani hustawi enzi ulilmwenguni?
6. Ni gani rangi ya enzi tukufu?
7. Hakika kila ulizo  iko na jibu yake.

## SURA YA MAKUMI TATU NA MOJA

1. Ametakasika Mwenyenzi aliye inuka juu ya maala pa juu ulimwenguni, Mungu mwenyi ushindi, mtukufu wa daraja.
2. Hupatikana juu ya ulimwengu na walimwengu sababu ya kua na mamlaka kubwa ajabu, ambae hutokana na ujuzi uliye busara kamilifu.
3. Kama husemekana enzi ipo juu, sio kwamba ni juu duniani ama juu mbinguni, wala kuhusikana na kuketi kwa kiumbe chochote.
4. Enzi tukufu hupatikana juu sana ajili ya busara yake kubwa, ni daraja ya busara yake ndio huzidia yote na kuzidiya yote ndio kuinukia yote kadiri ya kua juu ya yote.
5. Kuona kama ameshinda vyote vilivyomo ulimwenguni ndio maana huinuka juu kabisa, na viumbe vyote hupatikana chini yake.

6. Milki kamilifu ambae humjaa ndio utukufu na mamlaka kubwa yenyi kumfanya atukuzike zaidi ya vyote ulimwenguni.
7. Kwa kutambua juu na chini ulimwenguni ni lazima kutambua kwanza ginsi enzi ilivyo katika ulimwengu.
8. Enzi tukufu ni taa ya ulimwengu isiyo zimika ; na taa huzingatiwa katika mwangaza wake ; upande wa taa hupatikana mwanga mkubwa, na mbali na taa upande wa giza hupatikana mwanga mdogo sana wenyi kufifia.
9. Kuona kama enzi ndio iliye juu, upande wa enzi ndio juu na upande wa giza, mbali na enzi, ndio chini.
10. Ndio maana mbingu ipo juu na dunia ipo chini, ulimwenguni.
11. Viumbe waliyemo mbinguni ndio waliye juu kuliko viumbe vingine vyote.
12. Hakika daraja ulimwenguni hutokana na busara ; aliye na busara kubwa hupitikana juu na aliye na busara ndogo hupatikana chini.
13. Na aliye juu katika watu ni nabii na walii wa Mungu, ambae hujazwa na nuru tokea mbinguni, ajili ya hayo huinuka juu sana mfano wa wakaaji wa mbinguni.
14. Wala sio kwamba masulutani na matajiri ndio waliye juu, ispokua miongoni mwao atakaye amini Mungu mwenyenzi na kuishika kimakini dini yake
15. Kweli kabisa ukubwa wa imani ndio ukubwa wa daraja ya mutu.

## SURA YA MAKUMI TATU NA MBILI

1. Enzi tukufu, huko juu, hustawi katika utukufu wa mamlaka yake mwenyewe.
2. Hairuke kama yenyi mabawa, wala kuketi kama yenyi miguu, wala kusegamia katika chochote kile.
3. Je! Umesangaa kustawi kwa enzi bila kugusa chochote wala kutokea popote kadiri ya utukufu wa upekee?
4. Eti hauone ginsi alivyo weka mbingu bila nguzo! ebu niambie yeye mwenyewe!!!
5. Milki yake ya ajabu humstawisha katika ukamilifu namna ya kua shina la vilivyomo ulimwenguni.
6. Wala uzaifu wa kujumuika na kuitaji haumkurubie kamwe.
7. Ni yule aliye zaifu ndio hujumuika, namna ya kufaa na kufaidika kimatumizi, katika umbiko.
8. Anacho kiruhusu kuketi bila kusegamia wala kuninginia hutii amri yake sababu ya ushindi wa mamlaka yake, kefule yeye mwenyewe!
9. Mamlaka yake ni ya ajabu sana ambae ni utasi juu ya kila jambo ; umemfanya astawi kikamilifu katika upekee utangulizini kadiri ya mwanzo wa vyote.
10. Mtukufu wa ajabu ambae hakae ndani ya chochote cha utafauti naye mwenyewe, lakini hustawi enzini hali ya kua utupu wa enzi tukufu.

11. Maana enzi ndio yeye mwenyewe, na ndio maana hustawi katika utukufu wake huo wa ajabu.
12. Ni yeye aliye msingi wa ulimwengu, ambae katokeza vyote vilivyomo, atanguliaye pasipo msaada wa mwengine.

**SURA YA MAKUMI TATU NA TATU**

1. Utakatifu ni wake Mwenyenzi Mungu, mshindi wa yote, ambae humiliki kila jambo.
2. Utukufu wa enzi ni muujiza usio fananishwa na chochote, mamlaka yenyi kuenea.
3. Kila kilicho umbwa kilipewa umbile yacho fulani ili kidhihirike kwayo : kama vile hulka, kimo na rangi, kadiri ya sura fulani.
4. Usizani ya kama enzi ipo na rangi mfano wa hiyo rangi ya umbiko ; haiwezekane muumba kufanana na kiumbe.
5. Kama husemekana «rangi ya Mwenyenzi», sio mfano wa rangi yenu, bali utajo wa nuru yake takatifu, namna ya kungaa kwake.
6. Hakika Mola wako ni tafauti kabisa na kila jambo ; hafanane wala kulingana na chochote ku vyovyote.
7. Ametakasika Mwenyenzi mtukufu aliye muujiza kiutangulizi na maajabu kiutokezaji, Mola mshindi, mufalme aliye kamilika.

**SURA YA MAKUMI TATU NA INE**

1. Utakatifu ni wake Mungu Mwenyenzi, Muumbaji wa ulimwengu.
2. Mkuu anaye tawala maala pote, akijaa hekima ya ajabu.
3. Hana shida ya msaidizi, wala hachokake kusimamia viumbe vyake.
4. Ni mwenyi uwezo wa kufanya kila jambo, wala tatizo la kutetea halimkurubie kamwe.
5. Ujuzi wake umemfanya amiliki aina yote ya fahamu, bila shuruli yoyote.
6. Hasahau wala hadondoke, mtakatifu aliye na busara kamilifu.
7. Mola wa jumla ya viumbe, mtukufu aliye juu.

## SURA YA MAKUMI TATU NA TANO

1. Mungu alitangulia mwenyewe kabla ya viumbe kupatikana, hakukua kitu kingine kinyume na dhati yake tukufu.
2. Amekua yote katika yote mwenyi kukamilika
3. Alitangulia peke yake bila kuanza, kadiri ya kuenea ulimwenguni, katika mamlaka yake mwenyewe.
4. Maana uwezo wake ni mwingi ajabu ambae humfaya akamilike bila upungufu wowote.

5. Ni upungufu ndio unao sababisha uzaifu wa kushindwa
6. Lakini kwake yeye mkamilifu asiye gusika na upungufu, huweza yote bila uzaifu wa kushindwa.
7. Amejaa uwezo wa ajabu, mamlaka ya utendaji ambae hukadiriana pasipo kukadiriwa na yeyote, mola mtukufu, mfalme wa ajabu.

## SURA YA MAKUMI TATU NA SITA

1. Kuna ukamilifu na pia kuna upungufu, katika ulimwengu.
2. Ukamilifu ni hali tukufu sana, kadiri ya uzima, upatikanaji wenyi kuenea.
3. Ameenea katika uwezo hali ya kua muweza wa vyote, na ameenea katika fahamu hali ya kua mujuzi wa vyote
4. kuenea kiupatikanaji ndio kua na uzima, yaani (kupatikana) bila ku anza na bila kukoma, katika upatikanaji, na katika uwezo na katika fahamu.
5. Upungufu ndio hali dhalili sana, namna ya kutoeneana katika yote.
6. Haeneane katika upatikanaji wala katika uwezo wala katika fahamu.

7. Na hali ya kutoeneana ndio kupungukiwa kadiri ya hunusu na kipande, jambo lisilo endelea mbele na nyuma kiupatikanaji na kiufahamu

## SURA YA MAKUMI TATU NA SABA

1. Ukamilifu umepatikana katika tabaka la Enzi
2. Ni utukufu wa ajabu usio jumuika wala kunajisika, na ndio maana hauko angani wala ukiwani.
3. Ispokua upungufu ndio upatikanao angani na ukiwani
4. Na kuona kama ukamilifu umepatikana enzini peke yake, ndio maana aliye enzini ndio mkamilifu, wala hakukua na hakuna na akutakua mwengine mfano wake popote ulimwenguni.
5. Kuona kama ukamilifu umepatikana kwake aliye enzini na aliye enzini ndio Yule anaye itwa mwenyenzi Mungu, ni kwamba aliye mkamilifu katika ulimwengu ni Mungu mwenyenzi peke yake.
6. Ni yeye anaye jaa utukufu, namna ya kupatikana kadiri ya kuenea, mtangulizi aliye na uzima.

7. Mwenyi kujaa kadiri ya kuenea katika kua, katika kuweza na katika kujua, mola wa siku yote katika yote, mshindi aliye juu.

## SURA YA MAKUMI TATU NA NANE

1. Upungufu umepatikana katika tabaka la Anga na pia katika tabaka la ukiwa.
2. Ni hali zaifu sana isiyo kua na milki ya ushindi, imekosewa mamlaka ya kujieneza bila msaada.
3. Kuona kama upungufu umepatikana angani na ukiwani ambae mumejaa wakaaji wengi.
4. Ni kwamba wanaanga na wakiwa ndio wapungufu katika ulimwengu.
5. Ni wao ndio wadhalili, wenyi kupatikana bila kueneana, ambae hutaabika na shuruli ya utetezi.
6. Wamepatikanishwa na kupangiliwa kimaisha, wala hawakua ispokua sifuru.
7. Hali yao hutokana na sifuru ambae ni uzaifu mkubwa, wamekua mfano wa makadirio yake yeye aliye kamilifu.

## SURA YA MAKUMI TATU NA KENDA

1. Utukufu wa ukamilifu ni mamlaka ya ajabu ambae huzidia kila kitu.
2. Ni muujiza wa maajabu upatikanishao kila kitu ulimwenguni.
3. Haukuanza mu namuna yoyote ile lakini ulitangulia wenyewe kadiri ya kuenea bila mwanzo wala mwisho
4. Ni utukufu wa ajabu usio linganishwa na chochote ajili ya ushindi wake, hakuna mfano wake ulimwenguni.
5. Hali kama hii ndio uzima, mamlaka ya kuenea kadiri ya utangulizi.
6. Na uwezo wa kutangulia ndio mamlaka ya uumbaji
7. Haumbe ispokua aliye tangulia, na hatangulie ispokua aliye mkamilifu.

## SURA YA MAKUMI INE

1. Upungufu ni dhati ya umbiko, maana kinacho fanya aumbwe ni ajili ya kupungukiwa kimilki na kiufahamu.

2. Hakuwaka chochote kabla ya kuumbwa kwake sababu ya kupungukiwa, angeli kua kamilifu kama angeli tangulia kuwako kadiri ya kuenea bila kuanza mu namuna yoyote ile.

3. Ndio maana yule anaye umbwa, ametokezwa tokea upungufu na kufanyika umbile fulani.

4. Kama hasingeli tokezwa bila shaka asingeli patikana ulimwenguni.

5. Maana hakuwa na uwezo wowote ila sifuru tu, humu hamna ila ujinga mtupu.

6. Hakika katika ulimwengu huu umbiko imetokana na upungufu na uumbaji ndio unao tokana na ukamilifu.

7. Ni kwamba muumbaji ndio mwenyi ukamilifu na kiumbe ndio mwenyi upungufu.

## SURA YA MAKUMI INE NA MOJA

1. Ukamilifu ndio uzima, ni hali tukufu ya upekee inayo tokana na milki ya ushindi, hakuna cha zaidi yake.

2. Amekua yote katika yote, hasinzie wala halali, na hachoke wala kushindwa, na hakosekane wala kubadirika

3. Amekua yote katika kupatikana, hakuna aliko tokea wala aliko endea, mtangulizi wa mbele na nyuma

4. Mwenyi sifa kamilifu ajuaye yote zaidi ya woote ulimwenguni ,m’bora wa kuenea

5. Hii ndio hali tukufu ya yule aliye enzini ambae hujaa mamlaka ya ajabu

6. Sifa yake imeachana sana na sifa ya viumbe maana kiumbe ni chenyi upungufu ambae ni uzaifu

7. Hakika hali ya mwenyenzi ni muujiza wa maajabu, na ndio maana viumbe wamestaajabu sana ukubwa wake hata wengine wenyi uzaifu kififikara wamefikia kubisha.

**SURA YA MAKUMI INE NA MBILI**

1. Hakungeli patikana chochote bila mwenyenzi kutangulia ulimwenguni.

2. Maana yeye ndio mwanzo wa vyote, ambae hutokeza toka sifuru.

3. Milki yake ya ajabu humfanya aenee maali pote katika kuweza na katika kujua, kadiri ya ushindi katika yote.

4. Kwa kuweza kutokeza kitu ambae hakikua inabidi kua mkamilifu, yaani kutokua na upungufu ao uzaifu wowote.

5. Kwani yeyote aliye na upungufu ni mzaifu, na aliye zaifu hana uwezo wowote, hajiweze na hawezi kitu.

6. Ni kwamba atakaye kanusha utukufu wa ukamilifu na kukubali tu uzaifu wa upungufu ni pumbafu kabisa.

7. Hakungeli patikana chochote bila mkamilifu kutangulia, na mkamilifu ndio yule aliye enzini anaye itwa Mungu.

**SURA YA MAKUMI INE NA TATU**

1. Ulimwengu, ambae ni jumla ya tabaka tatu, umefanyika na yule aliye kamilifu atanguliaye katika mamlaka yake mwenyewe.

2. Mbingu, hadeze na dunia vilifanyika kwa idhini yake wala hakuna kilicho njee ya mapenzi yake.

3. Kinacho fanya kitu kijumuike ulimwenguni ni ruhusa yake inayo tokana na mapenzi yake.

4. Maadamu umbo Fulani imepatikana ni kwamba huruhusiwa naye.

5. Na ambacho hukataliwa naye hakiwezi kujumuika.

6. Na kama umbo Fulani hujumuika lakini imetumia makatazo ya Mungu, hufupisha maisha yacho namna ya kipande, na baadaye kitafutwa katika hesabu ya walimwengu.

7. Hakuta bakia ispokua dhati yake Mtangulizi aliye juu.

**SURA YA MAKUMI INE NA INE**

1. Kila kiumbe asili yake ni upungufu, hakuna umbo iliyo kamilika kamwe.

2. Kilicho kamilifu hakiumbwake, maana ni chenyi kuenea, hakina shida ya msaada wa yeyote.

3. Kama unaona kitu ao umbo angani ao ukiwani, ijapokua kikue kya kustaajabisha, katika uwezo ao katika fahamu ama dalili yoyote ile, tambua ya kama ni kiumbe kilicho umbwa na mwenyenzi.

4. Kitu kile kingeli kua kamilifu kama macho yako haingeli weza kukizingatia ana kwa ana, wala hakingeli jumuika angani wala ukiwani, bali kingeli stawi katika enzi tukufu.

5. Enzi haigawanyikake wala kujumuika, mfano wa hewa; hakuna kitu kitakacho jazwa enzi ndani mwacho angani wala ukiwani.

6. Musidanganyike na mwanahewa yeyote yule atakaye jidai ujuzi, hakuna kujumuika kwa mjuzi ; angeli kua mjuzi asingeli pumua hewa wala kupatikana duniani ama mbinguni ama hadezeni,

lakini angeli patikana enzini maala penyi kuhifadhika ambae macho ya kiumbe haizingatie bayana.

7. Hakika mwenyenzi Mungu hafanane na umbo yoyote ile wala haamake kutoka enzini kusafiri angani Mufalme wa ajabu anaye stawi kiushindi, wa pekee aliye juu.

**SURA YA MAKUMI INE NA TANO**

1. Enzi ni tabaka kuu zaidi ya yote, eneo tukufu ijaayo mamlaka imepatikana kadiri ya kutangulia bila mwanzo wala mwisho.
2. Ni yenyi upekee ajili kutogusika na kitu, na ndio maana haiwezi kujumuika wala kuingia ndani ya chochote cha umbalimbali na dhati yake
3. Inabidi vitu vyote viliokutwa huko viondoshwe namna ya kupotezwa, ili dhati yake isalie huko peke yake
4. Kama ni angani inatakika hewa na wakaaji wake wote wapotee namna ya kutopatikana kwa enzi kuketi maala hiyo
5. Taa haiwezi kuingia ndani ya mwangaza wake ama kutokea humo
6. Na kama ni ukiwani inatakika ukiwa na wakaaji wake wote wapotee namna ya kufutwa kwa enzi kuketi maali hapo
7. Hakika enzi tukufu ya Mungu haijumuikake katika umbiko, lakini yao ni katika upekee, na ndio maana hakuna kitu cha kumfanana wala cha kumkurubia katika milki.

## SURA YA MAKUMI INE NA SITA

1. Utakatifu wa mbingu umetokana na nuru ya enzi inayo mjaa, ambae huangazia bila kufifia wala kuzimika
2. Nuru hiyo ni kifaa kikuu cha maisha ambae hutimiliza umbo
3. Ni neema kubwa kupatikana karibu na chemchem ya nuru
4. Ole kwao waliyeko njee mbali sana na kisima cha nuru, maana huko ni hatari ya giza yenyi kufunika wala hawazingatie lolote katika utukufu wa taa ya ulimwengu
5. Hufanikiwa sana na mwangaza huo aliye wa roho, akimeremeta kama tungi kandokando mwa taa ya ulimwengu
6. Nuru yenyi ladha ya ajabu nafsini, zaidi ya yote ambae hunusuru na hustiri umbo.
7. Elekeeni kwenyi enzi tukufu ili mupate kukurubishwa, hakika bustani ni fasi bora ya kujumuika.

## SURA YA MAKUMI INE NA SABA

1. Nini kinacho kufanya ukanushe uzima wa Mungu?

2. Bila kutangulia kwake kama ulimwengu na walimwengu visingeli patikana kamwe.

3. Upatikanaji wa umbiko humaanisha utagulizi wa mjuzi awezaye kufanya mambo yote kwa mamlaka yake mwenyewe.

4. Kutangulia kwake ni muujiza, na kutenda kwake ni maajabu.

5. Ameenea katika upatikanaji na pia huenea katika utendaji, mzima aumbaye.

6. Milki yake ni yenyi ushindi katika yote bila mfano wake ulimwenguni.

7. Hakika Mungu ndio mwenyi uzima ambae hukamilika peke yake ulimwenguni.

**SURA YA MAKUMI INE NA NANE**

1. Mungu ni mwenyi haki ambae hutenda haki, hakuna atakaye mkosoa.

2. Yeye ni chemchem ya kweli na haki ajili ya ukamilifu wake, maana uzaifu wa kudondoka haumkurubie kamwe

3. Na kama ametokeza umbo mbalimbali yenyi uzidiano katika neema yake sio upendelevu wala makosa

4. Hayo hutokana na upungufu ambae ndio asili ya kila umbo

5. Kule kutokamilika kwao ndio jambo liletayo utafauti kati yao, na utafauti huo ndio kisa cha uwingi kupatikana kwao ili kila yule ajazikishe maala pake, kupatikane kawaida ya umbiko

6. Angeli umba wote namna moja bila utafauti wala uzidiano kama maisha isingeli timilika kwao na haistahili upekee katika uzaifu wala upekee haufanyikake, maana ndio alama ya ukamilifu.

7. Ndio maana umbali mbali umepatikana kwao wapungufu ajili ya kutojieneza, wamefanyika kadiri ya mapenzi ya muumba ; kila yule na hali yake na kazi yake ijapokua ni aina moja kiumbile.

## SURA YA MAKUMI INE NA KENDA

1. Katika ukamilifu ambae ni uzima, hakuna utafauti wala uwingi bali ni upekee ajili ya kuenea.

2. Utafauti usababishao uwingi hupatikana katika upungufu ajili ya uzaifu wa kutoeneana

3. Uwingi ndio jambo linalo timiliza maisha yao, ni kifaa kikuu katika utetezi wao.

4. Mutu asingeli ishi bila maji kuumbwa, na hewa, udongo, mimea, wenziwe...

5. Hakuna maisha wala thamani ya upatikanaji wa kiumbe peke yacho bila aina zingine, maana ni katika uzaifu.

6. Na utafauti fulani ni uzaifu fulani. Ndio maana haifae kulazimisha kuwa sawasawa katika upungufu ambae ni jambo lisilo sawa, ispokua ukamilifu ambae ni uzima ndio jambo lenyi usawa.

7. Kumbi ni vema kukubali uzidiano baina yenu maana asili yenu ni upungufu ambae ni uzaifu.

## SURA YA MAKUMI TANO

1. Mzima aliye juu alipangilia vema ajili ya kuwapelekeni katika utimilifu.

2. Amewawekeeni neno lake kuwa nusura ya tatizo la upungufu asilia.

3. Atakaye amini kweli atapata bahati ya kuingia katika utimilifu wa umbo.

4. Nafsi yake itatulizwa kutokana na tatizo yote kwa jumla.

5. Shida yake yote itatimilizwa bila yeye kutaabika na shuruli yoyote ile, wala mauti haita mufikia kamwe

6. Hali hii ndio utimilifu wa umbo, sio ukamilifu, lakini neema kubwa yenyi kustiri umbo

7. Basi tumieni neno la Mungu kama inavyo stahili ili mupate kutimilika nafsini.

## SURA YA MAKUMI TANO NA MOJA

1. Atakaye amini Mungu, na malaika zake, na mitume yake, na vitabu vyake, bila shaka umbo lake litatimilizwa
2. Atapewa uhai kadiri ya hunusu, zaidi ya kipande, kama kistari cha usawa kilicho na mwanzo bila mwisho
3. Aliumbwa lakini hata kufa tena, ameondolewa mipaka katika upatikanaji wake
4. Amekuwa mfano wa nuru ya taa isiyo zimika ambae huangaza milele na milele
5. Hii ndio neema kadiri ya mshahara wa wale watakao pokea neno la Mungu na kulitumia kama kawaida
6. Hakika mwenyenzi ni mwema, mkweli, mwenyi haki, m’bora wa kukadiria, atakasikaye na ajuaye
7. Ni muimu kwenu kuamini kweli hii ambae kafunuliwa na mola wenu aliye juu.

## SURA YA MAKUMI TANO NA MBILI

1. Mungu alijua ya kwamba hali yake ni muujiza mbele ya watu, ndio akafanya muusiano kati ya mbingu na dunia, ili wapate kuzingatia utukufu wake.

2. Akaagiza malaika na roho ili wawaonye watu, wakiwaletea habari nzuri kutoka kwake.

3. Ndio maana kumuamini mjumbe wa Mungu inakua ni jambo muimu kwa mutu .

4. Hata tumwa bayana malaika wala roho kutoka mbinguni kua mtume wenu, ispokua watu wenzenu tu ndio watakao inuliwa na kupewa neema hiyo .

5. Ni amri kwenu kuwaamini wote, wala musibague baina yao .

6. Na yule anaye muamini yesu masiya kiisha akamkataa nabii mtukufu muhamadi, imani yake ni ya bure kabisa ; na pia yule anaye muamini Muhamadi na kiisha akamkataa Nabii mutukufu yesu masiya, bila shaka imani yake ni ya bure kabisa

7. Mungu ni mumoja na ujumbe wake ni mmoja na dini yake ni moja ya usilimu

**SURA YA MAKUMI TANO NA TATU**

1. Nuru ya Mungu ni jambo kubwa sana katika maisha ya mutu .
2. Ni rehema ya Mungu inayo timiliza umbo iliyo jazwa
3. Hakuna umati pasipo nabii, wala nabii pasipo umati .
4. Nuru imewaka na kungara sana katika rangi mweusi, maana huzagaa katika kifaa maalumu.
5. Huu ni ukweli kutoka kwa mola wenu mzima aliye juu .
6. Basi itumieni na hekima wala musiichafue kwa kuichanganya na upuuzi wa shetani, ni rehema ya muumba kwa wakaaji wa Dunia.
7. Roho ni tayari kuwashukia wale watakao amini ujumbe huu.

**SURA YA MAKUMI TANO NA INE**

1. Hapana kubisha uzima wa Mungu muumba anaye stawi katika enzi tukufu
2. Ni upumbafu kupinga uzima na kukubali tu maisha .
3. Hakungeli patikana maisha yoyote bila utangulizi wa uzima ulimwenguni .

4. Lau kama ni upungufu ndio ulio kutwa hapo awali, bila shaka viumbe vyote visingeli umbwa ; sifuru ingeli bakia milele.

5. Utangulizi wake ndio Muujiza mkubwa unao staajibisha, na ili hali ndivyo anavyo stahili kwa maana yeye ni uzima tafauti kabisa na kila umbo.

6. Ili bidi kutangulie ujuzi mbele ya vyote, fahamu ya ajabu isiyo shindwa na lolote, ambae hutokeza toka sifuru.

7. Hakika Mungu ni mwenyi mamlaka ya ajabu kuliko walimwengu wote, ni muweza wa vyote na mjuzi wa vyote, ambae hastahili kufanana na kitu kipungufu.

**SURA YA MAKUMI TANO NA TANO**

1. Ujumbe wa Mungu haukuteremushwa ispokua kwa wenyi akili.

2. Ni raisi watu kuzingatia uzima wa Mungu kwa njia ya neno lake.

3. Lakini neno lake ni ngumu sababu hutumiwa katika lugha ya watu isio kua yake, maana kutenda kwa Mungu ni mbalimbali sana na kutenda kwa watu.

4. Kwa kusikilizisha watu ilibidi kuyalinganisha na kusema kwao ili wapate kufahamu.

5. Na ndio maana hutumia lugha ya watu katika ujumbe wake namna ya mifano.

6. Lugha yote ni yake Mungu ni yeye ndio kawafunza watu lugha mbalimbali, na ndio maana imeruhusiwa kuomba ao kusali katika lugha unayo fahamu.

7. Mungu hana kabila wala lugha, hana upungufu huo wa kiumbile sababu yeye sio kiumbe ; atakuaje na lugha na ilihali hakuna mwengine wa namna yake ambae wangeli kua na zungumza katika lugha hiyo?

## SURA YA MAKUMI TANO NA SITA

1. Mungu ni mwenyi uwezo wa kufanya kila kitu, mtukufu aneemeshaye kila kabila na kila umati.

2. Na ndio maana kila lugha ipo na jina la Mungu ndani mwake.

3. Ni alama ya neema yake ku watu wote kwa jumla, kwani kila kabila imepatikana na vipenzi vyake.

4. Wala sio lazima aitwe tu katika jina yake ya mu lugha fulani.

5. Ni bora kumtaja katika lugha unayo tumia ao unayo penda miongoni mwa lugha zake.

6. Ameyapenda ma lugha yote na majina yake yote aliyo iweka ndani mwayo, mjuzi wa ya siri na ya wazi.

7. Hakika Mungu mwenyenzi ni m’bora wa kukadiria na ni mwenyi hekima kamili.

## SURA YA MAKUMI TANO NA SABA

1. Mungu ni uzima kadiri ya ukamilifu, amepatikana katika utangulizi bila mwanzo wala mwisho
2. Ni milki kiujuzi yenyi ushindi ndio inayo mfanya awe na utukufu huu wa ajabu.
3. Milki hiyo, ndio dhati yake mwenyewe, mamlaka kuu yenyi kumiliki shuruli na wakati.
4. Na ndio maana hana shida wala umri maalumu, mtukufu anaye tangulia kuenea ulimwenguni.
5. Alikua, yuko na atakua, mwenyi uzima ulimwenguni.
6. Maisha na muda hukadiriwa naye, amempa umri mrefu amtakaye na pia humpa umri mfupi kadiri ya idhini yake, na vivihivyo kuhusu maisha yao.
7. Hakuna mola mwengine mfano wa Mungu mwenyenzi, m’bora wa kuumba anaye jaa mamlaka, mtakatifu aliye juu.

## SURA YA MAKUMI TANO NA NANE

1. Umungu ni mamlaka ya ajabu, milki kamilifu isiyo badirika, ushindi katika yote milele na milele.
2. Ni mwenyi uwezo wa vyote ambae idhini yake hutimiza, hakuna upatikanaji njee ya mapenzi yake .
3. Kama mutu anapatikana duniani ni kwa ruhusa yake mumiliki aliye juu.
4. Basi shangilieni uzima wa mola wenu aliye enzini, mtangulizi wa vyote anaye jaa utukufu.
5. Msifiwa wa ajabu anaye miliki ulimwengu, bingwa wa mabingwa, muheshimiwa aliye juu.
6. Ametangulia kadiri ya kuenea, mwenyi uwezo na ushindi, mtakatifu aliye enzini.
7. Hakuna mola mwengine sawa na Mungu mwenyenzi, wa pekee aliye na uzima.

## SURA YA MAKUMI TANO NA KENDA

1. Ametakasika mwenyenzi Mungu, m’bora wa kuumba aliye umba shetani kwa ulimi wa moto, kadiri ya kapi iliyo anguka .
2. Akashirikisha pumzi na mwili mwepesi wa moto ambae hupatikana ndani mwake kama uchafu unao fanya afifie kadiri ya pumzi chafu angani
3. Utazani kwamba ni mwanahewa-Halisi aliye najisika ajili ya ukubwa wa pumzi yake, na ilihali yeye ni mwanahewa-haramu.
4. Mwili wake hauzingatiwe ila mfano wa giza, kadiri ya uchafu ndani ya anga
5. Amepatikana mbali na chemchem ya nuru ndio maana hufifia pumzi yake pasipo nuru.
6. Hayo ni kwa maana amepatikana na mwili asilia ijapokua huogelea angani.
7. Hakika shetani ni mwanahewa-haramu anaye ishi njee ya dunia, katika hadeze.

## SURA YA MAKUMI SITA

1. Utakatifu ni wake mwenyenzi Mungu, mubora wa kuumba, aliye umba malaika kwa anga tupu, kadiri ya idhini yake.

2. Akamfanya kua pumzi tupu isiyo shirikishwa na chochote.
3. Na ndio maana yeye ni mwanahewa-halisi, asiye changanya hewa na mwili wowote,
4. Ni pumzi timilifu na takatifu kadiri ya nuru, ndio maana humeremeta.
5. Ni umbo kubwa isiyo fikiwa na kifo maana hakuna mtengano wa pumzi na mwili wowote ndani mwake.
6. Amepatikana karibu na chemchem ya nuru, ndio maana humeremeta, mwangaza wa taa isio  fifia wala kuzimika.
7. Hakika malaika ni umbo hai, kadiri ya uvuli wa enzi, ambae huishi njee ya dunia, katika mbingu takatifu.

## SURA YA MAKUMI SITA NA MOJA

1. Mwenyenzi Mungu ni m'bora wa kuumba, ambae katokeza uzuri na ubaya angani.
2. Amefanya mila mbili ambae hutenganisha wanahewa, humo angani.

3. Moja ni alama ya uvuli wake na ingine kinyume cha huo.
4. Uvuli wa ukamilifu ndio utimilifu, na utimilifu ndio chemchem ya uzuri.
5. Na kinyume cha utimilifu ndio uaribifu, na uaribifu ndio chemchem ya ubaya.
6. Anaye timiliza mambo hufanya uzuri ; na anaye haribu mambo hufanya ubaya.
7. Hii ndio njia mbili ambae umbiko hupitia angani.

**SURA YA MAKUMI SITA NA MBILI**

1. Mwenyenzi Mungu hana mila yoyote ile, maana yeye ni tafauti kabisa na umbo.
2. Maana mila ni umbo, ambae kafanyika kwa wakaaji wa anga.
3. Na ndio maana utakuta katika wanaanga mila hii mbili.
4. Uzuri kwao wahelekeaye taa, na ubaya kwao wahelekeaye giza.
5. Ni mila ya watetezi, ambae hupatikana na pumzi nafsini mwao.
6. Haipatikane kwao wasio na pumzi kamwe.
7. Hakika mila ndio umbo la wanaanga, haipatikane kwa mwenyenzi wala kwa wakiwa.

## SURA YA MAKUMI SITA NA TATU

1. Mwenyenzi Mungu sio muzuri wala yeye sio mubaya.
2. Hafanane na umbo yoyote maana yeye ni wa pekee anaye zidia kila kitu.
3. Uzuri ni adui wa ubaya, na ubaya pia ni adui wa uzuri ; uyu huangamiza yule, na yule pia huangamiza uyu.
4. Mungu angeli kua na mila fulani, bila shaka angeli angamizwa na ile ingine.
5. Upekee wake wa kuto jumuika wala kulingana unamfanya awe huru kabisa mbali na kuangamia.
6. Ni mwenyi mamlaka ya ajabu sana ambae huepukana na uzaifu wa aina yote.
7. Sifa yake huzidia vilivyomo angani na vilivyomo ukiwani, maana yeye ndio mwanzo wa vyote.

## SURA YA MAKUMI SITA NA INE

1. Mungu muumba sio muzuri wala sio mubaya, bali yeye ni mkamilifu.

2. Amezidia uzuri maana, uzuri ni utimilifu wa jambo.

3. Na utimilifu ni uvuli wa ukamilifu, yaani ni miongoni mwa nuru yake takatifu .

4. Hawezi kulingana na uvuli wake, lakini yeye huzidia.

5. Ndio maana Mungu amezidia uzuri, maana uzuri ni katika umbiko ambae haina ukamilifu.

6. Ukamilifu ndio hali tukufu sana isiyo na doa, utakatifu wa ajabu, kadiri ya usawa wenyi kuenea.

7. Hakika umungu ni utukufu wa ajabu sana, muujiza wa maajabu ulimwenguni.

**SURA YA MAKUMI SITA NA TANO**

1. Uzuri ni mfano wa rangi ya enzi, humeremeta wote wajipakao.

2. Malaika na roho ndio umbo timilifu, kadiri ya nuru ya Enzi tukufu.

3. Na ndio maana ni wenyi mila nzuri kabisa, utimilifu wa pumzi katika eneo la anga.

4. Na mutu yeyote atakaye fuata malaika na roho atafanyika nuru ya Enzi tukufu.

5. Nuru isiyo zimika wala isiyo fifia, mwangaza wa mbinguni.

6. Matumizi ya mila hii ni matumizi ya nuru ya Mungu, namna ya kujipakaa rangi yake.

7. Ametakasika mwenyenzi Mungu, mkamilifu tena wa pekee m'bora wa kuumba.

**SURA YA MAKUMI SITA NA SITA**

1. Uzuri umetokana na nuru, na ubaya umetokana na giza.

2. Aliye katika nuru hutumia silaha za nuru, na aliye katika giza hutumia silaha za giza.

3. Nuru ni ufahamu na giza ni upumbafu.

4. Nuru ni sehemu ya utukufu wa taa ya ulimwengu.

5. Na taa ya ulimwengu ndio ujuzi ambae ni enzi kadiri ya uzima.

6. Hupungukiwa sana yeyote aliye mbali na chemchem ya nuru, ambae huelekea giza.

7. Hakika neno la mjuzi huangazia kila nafsi inayo litumia.

**SURA YA MAKUMI SITA NA SABA**

1. Mungu hafanane na umbo yoyote ile lakini amezidia sana kila kitu.

2. Kile kilicho kitukufu katika umbiko ni kitu dhalili sana mbele ya mwenyenzi aliye «uzima».

3. Na ndio maana lugha zenu hazitakase kweli yake ispokua katika mifano.

4. Kutenda kwenu sio sawa na kutenda kwake muumba, na ilihali hamsemi ila kadiri ya utendaji wenu.

5. Fikara ya watu wa dunia ni chache sana, haizingatie ila kidogo tu.

6. Na ndio maana «umungu» huwastaajabisha sana na wengi miongoni mwao hawauzingatie wala kuukubali.

7. Hakika kulitangulia milki kamilifu yenyi ujuzi ambae hujaa mamlaka ya ajabu yenyi kutokeza kitu ambae hakikua popote, na ambae hujieneza bila msaada ajili ya kukamilika ambae imeitwa «mwenyenzi Mungu».

**SURA YA MAKUMI SITA NA NANE**

1. Ametakasika mwenyenzi Mungu muumbaji wa kila umbo, mkuu anaye tawala milele na milele.

2. Vyote huanzia kwake na vyote kukomea kwake.

3. Hakuna cha utafauti na idhini yake wala upatikanaji njee ya uumbaji wake.

4. Mbingu na dunia hufuata kanuni yake, wala hakuna cha kumpinga wala cha kumuhukumu.

5. Na kama hajumuike duniani na pia mbinguni, sio kwamba hukosekana, bali yeye hustawi katika enzi tukufu, katika upekee.

6. Utukufu wake wa ajabu umemfanya atengane na vitu visio kua na ukamilifu, maana kugusana na upungufu ao kuchangikana na huo ni kupungukiwa ao kuzaufika.

7. Ameketi mbali sana na viumbe, lakini ameona na ameweza kutenda vya huko kwenyi viumbe zaidi ya wenyi kambi hilo ; hakika Mungu ndio muweza wa vyote tena mjuzi wa vyote.

## SURA YA MAKUMI SITA NA KENDA

1. Nuru ya Mungu ni sehemu ya utukufu wake, kama vile mwanga ulivyo sehemu ya utukufu wa taa.

2. Kuona kama mwenyenzi ni mkamilifu, nuru yake ni utimilifu.

3. Na pia kwa maana mwenyenzi ni mjuzi, nuru yake ni fikara.

4. Na kuona kama Mungu ni enzi tukufu, nuru yake ni anga(hewa).

5. Kwa maana mwenyenzi ni uzima, nuru yake ni maisha.

6. Na kuona kama Mungu ni muumba, nuru yake ni umbiko.

7. Hakika nuru ya Mungu huzingatiwa kwa namna mbali mbali, kadiri ya matazamio, bila shaka mwenyenzi ni Muujiza wa maajabu ulimwenguni

## SURA YA MAKUMI SABA

1. Enyi watu wa dunia, aminini Mungu mwenyenzi aliye wa umbeni kwa udongo.

2. Ni yeye aliye tangulia kupatikana ulimwenguni bila msaada wa yeyote.

3. Mtukufu wa ajabu ajaaye mamlaka yote, ambae hutenda kwa idhini bila kutumika kazi.

4. Yeye ndio mwenyi kuwako daima muda wote, hana mwanzo wala mwisho, mkamilifu aliye juu.

5. Hapana kushakia uzima wake, maana amepatikana juu sana hatua na viumbe.

6. Na ndio maana haifae kulazimisha kumgusa ao kumtazama kama munavyo gusana na kutazamana (ana kwa ana) nyinyi kwa nyinyi, kwani yeye ni tafauti sana nanyi tena kuna hatua kubwa ajabu baina ya dunia na enzi.

7. Mimi ni shaidi wa uzima wake, maana nimeagizwa maneno naye tukizungumza sauti kwa sauti.

## MULANGO WA TATU : NURU TAKATIFU

### 1.UITO

1.huu ni ujumbe kutoka kwa Mungu mwenyenzi:

2.Mimi Kalonda , nilisikia sauti toka juu kuniita nilipo itika akasema: ni mimi Mungu wako! nime kubariki kama nilivyo mubariki ibrahim.

3.Na nimekutuma uwaubirie wale utakao wa kuta wakibishana kuhusu uzima wangu.

4. Ni kamuuliza, nikisema:niwahubirie maneno gani?

5.Mungu akanijibu akisema:yale utakayo fahamu kuhusu uzima wangu.

6.Kwelikweli ninakwambia hauta fahamu lolote kunihusu mimi ispokwa ukweli peke yake.

7.Akaniambia, akisema, unasikia ninayo kuagiza?nikajibu, nikisema ndio nimesikia.

8.Mungu akaniambia, akisema:usikose kuwafikishia kweli yangu.

9.Nilipo maliza kuzungumuza na Mungu maneno hayo, nikaona nuru kubwa mbele yangu.

10.Ni katazama, katika nuru ile, nikaona mwanamuke mumoja ameketi chini udongoni.

11.Alikua mtu mweusi mnene mwenye kimo cha kadiri, akivaa kanzu ya kitenge.

12.Alikua ndani ya jengo la msingi wa nyumba, iliyo jengwa kwa matofari ya kuchomwa.

13.Tulikua na tazamana, mimi na mwanamuke huyo.

14.Punde kidogo, nikaona maji tokea juu mbinguni, ikamushukia kichwani pake, ikimimilika kama vile maji itokavyo katika mulonge.

15.Wakati maji hiyo ilimushukia toka juu, ni kamuona kama mwenye mimba.

16.Na maji ile ilitiririka mwilini mwake akalobana wote, mpaka udongoni.

17.Na ilipo gusa udongo, maji ile ikasambaa bila kulobanisha udongo wala kuzama.

18.Wakati huo, nilisikia mzozo wa watu wengi wakipiga kelele kwa kishangwe, wakisema:amebarikiwa..

19. Nikasikia sauti toka juu kuniambia, ikisema:tazama, ewe kalonda, kadiri baraka yako itakavyo patikana.

## 2.UVULI

1.Ametakaslka Mwenyenzi Mungu, m'bora wa kuumba aliye umba nuru kadiri ya uvuli wake.

2.Kinvuli cha mwenyenzi huzingatiwa kadiri ya matazamio yenu, na ndio maana nuru yake hutajwa namna tafauti.

3.Kama matazamio yako humzingatia Mungu kadiri ya enzi tukufu, nuru yake huzingatiwa kadiri ya hewa (anga)

4.Na kama utazamaji wako humzingatia Mungu kadiri ya ujuzi, uvuli wake ama nuru yake nifikara.

5.Na kama humemzingatia kadiri ya uzima, nuru yake ao uvuli wake ni maisha (uhai)

6.Mbingu ni kambi takatifu, sehumu ya kwanza ya bahazi la juu angani;

7.Ndio sehemu kubwa ya tabaka la anga, tukufu inayo jumuisha falme mbili takatifu;

8.Kuna mahala anapo  patikana malaika, na pia sehemu anapo keti roho humo mbinguni.

9.Malaika na roho ni pumzi hai yenye fikara timilifu iliyo umbwa kwa uvuli wa enzi tukufu.

10.Kuona kama ilifanyika kwa nuru ya taa ya ulimwengu, umbo hizi ndio nuru ya mwenyenzi inayo angazia dunia.

11.Hiyo fikara timilifu kadiri ya neno lake takatifu iliye ndani mwao ndio mwangaza unao angazia.

12.Ufunuo wake ndio mwangaza mboleo ya maisha ya watu.

13.Wamefaulu kabisa walio silimu kwa shaada yao, ambae umpelekea mola wao shukrani.

14.Ni mkubwa sana mwenyenzi Mungu m'bora wa kukadiria anaye jaa mamlaka.

15.Utukufu wa dhati yake umezienea mbingu na ardhi, na vilivyomo hutamania uvuli wake.

16.Mufalme wa wafalme aliye na ushindi, ambae kauli yake hufanya yote pasipo shuruli, m'bora wa kuumba.

## 3.M'BORA WA KUUMBA

1.Ametakasika mwenyenzi Mungu, m'bora wa kuumba ,mtukufu ambae hatumiake kifaa chochote cha njee ya alivyo viumba kwa kuumba.

2.Lau kama angeli tumia kifaa ambae hajue kukitokeza hasingeli itwa muumbaji bali angeli itwa muundaji.

3. Mumilki anaye tokeza ambacho hakikua kwa kutumia idhni yake peke yake.

4.Kustawi kwake katika dhati yake mwenyewe humfanya upekee pasipo kuchangikana na chochote wala ku fanana na chochote wala kutumia chochote cha umbali mbali naye.

5.Mufalme anaye enea katika yote kwa mamlaka yake mwenyewe, mtukufu aliye na miliki kamilifu.

6.Wengi miongoni mwa watu hawawezi kuamini ambae njia tano ya fikara kupitia mwilini haidhatiti.

7.Ndio maana wamepatikana mbali sana na nuru: sehemu moja ya watu humkanusha Mungu.

8.Na sehemu ingine ya watu humpachika mujumbe wa Mungu daraja isio yake ya umungu.

9. Awa wote ndio wasio amini kweli kikweli, nivema kushuudia kweli vilivyo kihakika.

10.Kumpachika mtume fulani umungu ni sawa na kuabudu sanamu ,zambi kubwa zaidi ya yote.

11.Mshindi katika yote hujitenga mbali na upungufu wote, hakuna kilicho mfanana.

12.Jihadharini sana maishani mwenu na ibada ya masanamu, hakika ushirikina ndio upotevu wa bayana.

13.Umungu ni katika upekee, tafauti na umbo zote, wala uzaifu wa kujumuika haumkurubie kamwe mtukufu aliye enzini.

14.Hakika utakatifu ni wake mwenyenzi, mtukufu ambae nuru humfumuka kwa wingi, vikijipakaa viumbe utukufu wa dhati yake.

15.Mwenye kuenea katika yote kuliko wote, mufalme wa wafalme wote.

16.Hakuna mwengine kama yeye, mwenyi mamlaka ya ajabu, anaye weza yasio wezekana kwa viumbe, m'bora wa kuumba.

## 4.AKUNA LAWAMA

1.Ametakasika mwenyenzi Mungu m'bora wa kuumba anaye fanya yote kwa usawa bila hitaji ya msaidizi.

2.Mkamilifu ajaaye utukufu, anaye podoa na anaye tuliza nafsi ya walio silimu.

3.Mjuzi anaye kadiria jumla ya viumbe pasipo kudondoka, kiongozi mwenye kukamilika.

4.lakini watu wa dunia humlaumu Mungu muumba kwa kuwaumbia shetani ambae huwaangamiza.

5.Na ilihali maisha yao(watu)pia ni mfano wa maisha ya shetani mbele ya viumbe vingine.

6.hayo hutokana na upungufu asilia ambae huzikumba umbo zao wote kwa jumla.

7.Na wanapo angamiza viumbe ajili ya starehe ya nafsi zao, hufurai bila kujali kilio chao.

8.Kadiri watu wanavyo laumu kuumbwa kwa shetani ,ndivyo pia viumbe vingine vinavyo laumu kuumbwa kwa mutu.

9.Minyama ,ndege,samaki,vidudu...wanalia kwa uchungu wanapo uwawa na watu .kama vile watu wanavyolia kwa uchungu wanapo vamiwa na shetani.

10.Kama kweli Mungu hakustaili kuumba shetani sababu huangamizana ,ni kwamba hakustaili pia kuumba mutu sababu huangamizana pia.

11.Viumbe vyote huangamizana ajili ya upungufu asilia unao tafautisha maisha yao.

12.Ambae ni mbaya kwa uyu ni nzuri kwa yule,katika maisha ya jumla ya viumbe.

13.Hakuna kisicho pendeza wala kisicho chukiza miongoni mwa viumbe.

14.Eti ni kweli kabisa Mungu alifanya makosa kuumba viumbe?

15. Hapana kumlaumu Mungu kwa lolote maana mola wenu ni mjuzi wa vyote anaye tenda katika usawa kila jambo.

16.Wala usitafute kua mkamilifu kama Mungu ambae hagusiwake na upungufu wowote ,na ilihali wewe ni tunda la upungufu.

17.Ni amri kwa kila mutu kumsifu sana Mungu na kumshukuru kwa wingi ,hapana kumlaumu Mungu ku vyovyote.

18. Mutu atakaye amini Mungu kwa moyo wake wote na kumuabudu kila siku,na akawa na moyo safi ,bila shaka nafsi yake itageuzwa roho atakapo ihama dunia.

19.Tetea namna ya kupata utimilifu wa nafsi yako ,sio ukamilifu,lakini neema ya kupata maisha ya milele.

## 5.MTENDAJI

1.Ametakasika yeye aliye umba mbingu na ardhi pamoja na vilivyomo.

2.Mwenyi kustawi katika utukufu ,juu ya palipo juu ,hakuna mfano wake ulimwenguni.

3. Amejaa katika kua,nyuma na mbele ,bila mabadiriko yoyote.

4. Hakuna macho iwezayo kumtazama ana kwa ana ajili ya utukufu wake wa ajabu.

5. Macho itakayo jaribu kumtazama,hupofoka bila mafanikio yoyote .

6. Nuru juu ya nuru mtukufu anaye angaza kadiri ya taa ya ulimwengu .

7. Mkamilifu asiye gusika na upungufu wowote ,m'bora wa kuenea .

8. Baba wa siri aliye kwa siri kadiri ya muujiza wa maajabu, ambae hali yake hustaajabisha walimwengu.

9.Amejaa uwezo wa vyote wala hakuna asilo liweza,mwenyi mamlaka ya utendaji.

10. Kila tendo  liko na tafsiri yake inayo maanisha ujuzi wake.

11. Hatendi lolote ispokua katika kujua,muweza na mjuzi,anaye wezesha na anaye fahamisha kila umbo la kihewa .

12.Watu wangeli fahamu mradi wa kuumbwa kwa kila umbo, hakika wange muogopa Mungu na kumsifu na kumshukuru.

13.Ameumba kadiri ya kufumba, wala hakague ispokua aliye funuliwa naye.

14.Mkuu aliye na ushindi juu ya kila kitu, shina la vilivyomo ulimwenguni.

15.Majira ya ulimwengu, imetokana naye, ni yeye anaye badiri kipindi katika wakati.

16.Hakuna Mungu mwengine kama yeye, bwana wa mabwana, anaye hifadhi kwa milele.

17.Mola wa anga na ukiwa, mumilki, ambae nguvu yote hutokea kwake.

18.Wa pekee katika utukufu usio kurubiwa, msifiwa aliye kamilika, anaye patikana juu ya daraja zote,mwenyi uwezo na ushindi.

19.Wengine wote walifanyika naye, wala hakuna mwengine kama yeye, mzima, anaye pimiana muda bila yeye kupimiwa na yeyote.

20.Mwenyi kuenea katika tendo kua, kuzidia wakati, m'bora wa kutangulia.

## 6. SIMAMA IMARA

1.Utukufu ni wake mwenyenzi Mungu, kiongozi mwenyi hekima kamilifu.

2.Amejifunua kwao wanaadamu kwa namna tafauti, wamaajabu anaye fanya raisi jambo ngumu, na kuifanya ngumu jambo raisi.

3.Hawamzingatie ila kidogo tu, kwani nuru yake aiwafikie kama kawaida ajili ya giza ambae ni mwili ujengao nafsi zao.

4.Anga ndio sehemu ya ulimwegu kadiri ya mwangaza wake na wanaanga wamekuwa na ginsi ya kujikusuru kadiri ya kutenda.

5.Pumzi zao zimekua nguvu na zimekua fahamu, ndio maana ni wenyi maisha.

6.Hii ni miongoni mwa faida ya nuru yake, ambae huthamanisha umbiko.

7.Watu wa dunia wamekataa neno la Mungu lenyi nuru na baraka, wamekubali vishawishi vya shetani ambae hufunika.

8.Ni kwa sababu hawamzingatie shetani bayana kadiri alivyo umbwa, anayo desturi ya kujificha.

9.Shetani ni umbo mbaya ajabu, yenyi kutisha, lau kama angelikua na onekana bayana, hakuna mutu ambae angeli penda imusogelee.

10.Umbo lake ni uchafu, na matendo yake ni machafu, na kambi lake ni chafu ajabu, maana yeye ni kapi.

11.Ubaya wa aina yote ni ndani mwake, mfano wa yalala, ambae hulinda uchafu wa aina yote.

12.Pahali ya pumzi yake kuleta ladha nafsini mwake iliyo mjaa, yao humletea maumivu na wasiwasi.

13.Matendo yake yote ni kinyume na usawa, wala hatendi ispokua ubaya.

14.Yeyote anaye sharikiana naye ndio anaye fanana naye, katika mila na matendo, analeta wasiwasi katika jamii la watu.

15.Amewafunza urozi  wa kila namna na kuwapambia hata wakiupanga majina mazuri ili watu wautamanie.

16.Na pia huuingiza katika dini;kuwafananishia ramli na utabiri wa maono,na kuwafananishia zinguo la kizimu na uponyaji wa maombi.

17.Hayo ndio mafunzo ya shetani, mambo ya giza ambae mwisho wake ni hasara.

18.Ole kwao watembeaye  gizani ,hakika ni mbaya sana makao yao siku ya mwisho.

19.Na wana pupia kusukumana gizani ajili ya chuki, wala hawataki uongofu.

20.Na wanapo karibiza watu mezani, hutia urozi ndani ya chakula ili wawaambukize wengine.

21.Hakika kupatiana uchawi ni zambi kubwa sana zaidi ya kuuwa mutu.

22.Ni kujiwekea akiba ya zambi, maana zambi yote atakao ichuma na uchawi ulio mupa, nawe pia utapewa sehemu.

23.Na yule uliye mupatia urozi kama unapatiana pia, utapewa pia na zambi ya yule mpaka mwisho.

24.Usitafute kurudisha kisasi kwa kupezana uchawi kama walivyo kupatia wewe, na ili hali wale unao wapatia sio yule alio kuambukiza.

25.Na kama wana kuambukiza uchawi(urozi) bila kutambua wala kutaka, usikate tamaa, lakini zidisha ibada na usimame imara mpaka mwisho wa umri wako.

26.Hakika mola wako atakutakasa na kukuneemesha, ukipewa bustani kua makao yako ya milele.

27.Atakaye simama imara katika urakibu pasipo kurogana na uchawi walio muambukiza ndio shujaa anaye pewa daraja ya kiroho, ambae ameshinda majaribu.

28.Na yule atakae shindwa kusimama imara katika njia ya Mungu baada ya kuambukizwa uchawi, kiisha akaanza kurogana, ndio maskini kiroho anaye shindwa na jaribu.

29.Simameni imara enyi walio silimu ili mupate kupokea zawadi ya kiroho.

30.Aliye pokea roho takatifu hawezi kunajisika(kiroho) ijapokua wakusudie kumunajisi.

31.Giza aifukuzake nuru lakini nuru ndio yenye nguvu ya kusukuma giza mbali.

32.Imani ya kweli humfanya mutu ateremkiwe na watakatifu wa mbinguni.

## 7. USHAIDI

1.Shuudieni kweli hii, enyi watu hakika mola wenu yupo pamoja na washuudiao.

2.Mungu amenifunulia kweli hii na kuishuudia mwenyewe ,hakuna shaka ndani Yake.

3. Mimi ni shahidi wa Mungu mwenyenzi ,nimetumwa ku watu wote bila ubaguzi.

4. Nimeleta ushahidi wa uzima wa Mungu ili kila yule atakaye upokea apate uzima wa milele.

5. Hapana kushakia habari hii ya ukweli,wala usizanie kama ni akilia ya kibinaadamu.

6. Wala usizani kama kutomuona na macho ya mwili wako ndio kukosekana kwake,hayo humaanisha ukubwa wa daraja yake pia na utafauti uliyeko baina ya wewe na yeye.

7. Mungu ni uzima kadiri ya Enzi tukufu,lakini wewe ni changachanga ya pumzi na mwili.

8. Mwili ni ukiwa kadiri ya utupu wa ujinga,yaani uzaifu na upungufu,ganda isiyo Linda fahamu yoyote.

9. Na pumzi ni mjengo kihewa ambae kafanyika kwa uvuli wa enzi,yaani fikara kadiri ya uvuli wa ujuzi.

10. Fikara yenyi thamani ya uvuli ichangikane tena na mwili ulio ujinga mtupu ,itawezaje kuzingatia bayana umungu ambae ni muujiza wa maajabu?

11. Ndio maana Mungu mwenyi ujuzi alichugua hatua ya kuwatumieni ujumbe na watu wenzenu ili mupate kuzingatia uzima wake.

12. Wajumbe wake ndio mashahidi wake ambae humsikia na masikio yao na huona utukufu wake na macho yao.

13. Neno ni ngumu kimwili ,lakini mwepesi kufahamika kiroho.

14. Mwili ni giza na roho ni nuru,aliye wa mwili hutembea gizani,na aliye wa roho hutembea nuruni.

15. Aliye wa roho ni mwepesi kuzingatia uzima sababu yeye ni katika mapambazuko.

16. Alie wa mwili  hawezi kuzingatia uzima maana yeye ni gizani,macho yake imefumbwa na ujinga.

17. Na ijapokua musilimu azaufike katika maisha ya dunia,yeye ndio chombo halisi,umbo tukufu la mbinguni.

18. Na ijapokua kafiri atukuzike katika maisha ya dunia ,sio kwamba anakua chochote,yeye ni kapi tu ,umbo dhalili ya hadezeni.

19. Hakika Mungu ni mwenyi kuwako,mzima,anajua yote na anaweza yote,halingane na yeyote.

20. Makafiri wanafikiria ya  kwamba Mungu amefanana na kiumbe ,ndio maana wamelazimisha yafanyike kwake kama inavyo fanyika kwenyi viumbe.

21. Hakika kupatikana kwake kadiri ya kutangulia pia na kutenda kwake kadiri ya kutokeza toka sifuru ni muujiza wa maajabu,tafauti sana na kupatikana pia na kutenda kwao viumbe.

22. Mungu ni mwenyi mamlaka ya ajabu ,anga na ukiwa vilifanyika naye bila kutumika kazi.

23. Akaamuru kitu fulani kifanyike mara moja kinakua.

24. Uzima wake hauna asili,Bali yeye alitangulia kadiri ya kuenea bila mwanzo wala mwisho,wala hakudai msaada wowote kwa yeye kuwako.

25. Utukufu wake huu umemtafautisha na vitu vyote kwa jumla,wa pekee bila mfano wake.

26. Kama unafikiria kuhusu hali yake ,tambua ya kama hakuna umbo yenyi kumfanana ku vyovyote.

27. Hayo ni kwa sababu yeye peke Yake ndio mwenyi ukamilifu ,na wengine wote ni wapungufu,hakuna ginsi ya wao kulingana.

28. Mchoraji haweze kulingana na chombo kilicho chorewa naye.

29. Ndio maana mutu hawezi kumuona muumba wake ana kwa ana;kitu kilicho fanyika kina patikana chini sana,mbali kabisa na daraja ya yule aliye kifanya,hawawezi kulingana kamwe.

30. Kama yule aliye fanyika angeli pewa ginsi ya kuzingatia hali ya yule aliye mufanya,Angeli staajabu sana.

31. Hali ya yule aliye mfanya ni tukufu ajabu kubwa sana na zaidi tafauti kabisa na yule aliye fanyika.

32. Hakika uwezo wa muumbaji ni mwingi mno hakuna hâta namna ya kuukagua.

33. Kweli kabisa mwenyenzi ni muujiza wa maajabu,hakuna ginsi ya kumkurubia ku vyovyote.

## 8. MASIYA

1. Ametakasika mwenyenzi Mungu,mneemeshaji ,anaye mtukuza amtakaye miongoni mwa watumishi wake.

2. Mimi kalonda nilikua na zoezi ya kuamuka usiku kwa kusali.

3. Siku moja roho akanijia katika ndoto ,akaniambia akisema:hakika ibada unayo fanya ni kubwa na malipo yake ni kubwa .

4. Na kama utapenda kuinuliwa,basi upande mlimani,ukafanye ibada kama hii usiku na mchana kadiri ya uwezo wako.

5. Nilipo amuka,nikajiandaa kwenda mlimani kwa ajili ya ibada ya Mungu muda wa siku tatu.

6. Nilipo kua katika kisimamo ndani ya sala,usiku huko mlimani,nilisikia sauti toka juu kuniita :kalonda!

7. Nilipo itika akasema:kati ya zawadi hiyi mbili chagua unayo penda upewe:

8. Kuna zawadi ya kimalaika na zawadi ya kiroho.

9. Zawadi ya malaika ni hii:jibrilu ,mikailu na asrafilu.

10. Na zawadi ya roho ni hii: Yesu masiya,Mussa na Eliya.

11. Nikajibu ,nikisema :Mungu mwenyewe anichagulie île iliye bora kwangu anipatie.

12. Ni bora kwako île utakayo ichagua mwenyewe,chagua unayo penda upewe.

13. Akaanza kunifasiria kuhusu zawadi ya kimalaika:akamtapa jibrilu hali yake na kazi yake na daraja yake.na akamtapa mikailu,kuonesha hali yake na ufalme wake na vivihivyo kwa malaika asrafilu.

14. Kiisha akanifasiria kuhusu zawadi ya kiroho kunionesha utukufu wa nabii Mussa ,daraja yake na kazi yake.

15. Na akanionesha utukufu wa Yesu masiya daraja yake na kazi yake humo mbinguni, hakika Yesu ni mfalme.

16. Na pia akanionesha utukufu wa nabii Eliya,daraja yake na kazi yake humo mbinguni.

17. Ndio akaniambia,akisema:baada ya  kufahamu ubora wa zawadi yote mbili,chagua sasa zawadi unayo penda upewe.

18. Nikataka kuchagua ya kimalaika lakini nilipo tizama ukubwa wa daraja ya Yesu masiya nikachagua zawadi ya kiroho,yaani Yesu masiya,Mussa na Eliya.

19. Ma nabii hawa ni wenyi utukufu wa namba ya juu mbinguni.

20. Wakati huo nilikua nimeendelesha sala mpaka mwisho.

21. Kiisha nikalala,nikaona katika ndoto,mwangaza mkubwa umeniangazia,

22. Nilipo tazama juu,nikaona nuru mfano wa jua ya asubui.

23. Nikatazama ndani ya île nuru iliye kua mfano wa jua ya asubui,nikaona mutu humo ndani.

24. Nuru île ilikua na teremuka toka juu mbinguni.

25. Wakati huo nilijikuta juu ya  muti mkubwa,katika majani ya chongo ya tawi lake .

26. Mutu yule aliye kua na poromoka ndani ya nuru ,alishangiliwa sana na watu walio kua chini ardhini.

27. Wakisema:yesu masiya ! mwana kondoo wa Mungu ! Mfalme wa mbinguni, mpenzi wa Mungu,njia ya mbinguni,roho ya Mungu...

28. Roho akaniambia,akisema:tazama Yesu masiya, mwana kondoo wa Mungu aliye haï,anaye kuja duniani ili kuondoa zambi za watu .

29. Na tazama ,alikua na shukia upande ambae uguta ulitenganisha upande nilio kua na upande alio kua na shukia hewani.

30. Alipo kurubia sehemu hiyo ,tawi nilio kua ili nepa upande huo alikua na shukia,kutambuka ukuta huo ulio tutenganisha.

31. Ndipo Yesu masiya alipo ni chugua,akinishika na mikono yake miwili na kunipitisha upande wake wa kulia pembeni yake.

32. Tukawa tumeketi ,kadiri wanavyo keti juu ya kiti ,hewani.

33. Watu walio kua huko chini ardhini waka shangilia sana ,wakimtukuza sana Bwana Yesu.

34. Hakika karibu na Yesu masiya kuna hewa yenyi ladha nafsini.

## 9. MALINGANIO

1. Utakatifu ni wake mwenyenzi Mungu ,m'bora wa kuumba.aliye umba anga na ukiwa na ilihali hakukua kwa yeye kuigia mfano.

2. Vilivyomo angani na vilivyomo ukiwani hushangilia dhati yake,mkuu aliye na ushindi.

3. Heri mutu anaye mnyenyekea muumba wake na kuitakasa dini yake ,maana atatukuzwa kuanzia duniani mpaka mbinguni.

4. Hakika makafiri ni wapumbafu ,kama wanasikia jina la Mungu hutukuzwa ,nyoyo zao hujaa huzuni na hasira.

5. Na kama wana sikia sifa ya shetani huburudika nyoyoni mwao.

6. Wao ndio wajinga ,wanao fanya nyoyo zao kua makao ya shetani.

7. Ni wenyi mioyo migumu ajabu,yenyi kujaa kiburi,wala hawata amini ijapokua waubiriwe ao hapana.

8. Hawafikiri ispokua ubaya:huchukia kila jambo nzuri,na hutamania kila jambo mbaya,umbo dhalili ya hadezeni.

9. Waaminifu ndio wanao furahi sana wanapo sikia sifa ya Mungu mwenyenzi.

10. Neno la Mungu ni chakula ya kiroho nafsini mwao,wameitumia kila siku ili kuzijenga roho zao.

11. Na huchukizika sana wanapo sikia maneno ya upuuzi wa shetani ,maana kwao ni mfano wa sumu ambae huaribu afya ya roho zao.

12. Waliumbwa kwa kauli tukufu na wameishi kwa matumizi ya kauli tukufu ,umbo tukufu ya mbinguni.

13. Wamechukia mabaya yote ,na wametamania  mazuri yote;wao ni mfano wa mboleo ya  uzuri,vipenzi vya Mungu.

14. Anaye zingatia uzima wa Mungu na kuushuudia ni mwenyi akili.

15. Na yule asiye zingatia uzima wa Mungu ndio pumbafu.

16. Utimilifu hupatikana mbinguni na uaribifu hupatikana hadezeni.

17. Ndio maana wanao silimu na kutenda mema ,hujumuika mbinguni ,na wanao kufuru na kutenda mabaya,hujumuika hadezeni,baada ya kuihama dunia.

18. Mola wenu ametakasika zaidi ya kila kitu,hakuna wa zaidi yake wala wa sawa yake ambae Angeli msaidia.

19. Shuudieni uzima wa mwenyenzi katika yakini,ndiye mtawala wa ulimwengu anaye kamilika.

20. Amekua yote katika yote,mwanzo wa vyote,chemchem ya upatikanaji na maisha ulimwenguni.

## 10. MAFUNDISHO

1. Ametakasika mwenyenzi  Mungu, mtangulizi anaye jumuisha kila apendacho ulimwenguni.

2. Ni yeye anaye angazia mbingu na ardhi ,chemchem ya mwangaza kadiri ya taa ,ujuzi wa kila kitu.

3. Nuru ya Mungu sio mfano wa mwangaza kimwili,lakini fahamu ambae huondoa ujinga.

4. Kitu ambae ni nuru kimwili ni giza kiroho,hakika mwili na roho ni umbo mbili tafauti kabisa.

5. Nuru ya Enzi imewahusu wanahewa ambae kaumbwa kwa baki la uvuli wake.

6. Enzi ni ujuzi,na nuru yake ni hewa kadiri ya fikara.

7. Naam ! Fahamu ambae huondoa ujinga.

8. Neno la Mungu huzagaa namna ya kuelimisha viumbe.

9. Kutumia neno la Mungu ndio kutumia nuru maishani.

10. Haikuja nuru kwa mjumbe ila ajili ya watu wote bila ubaguzi.

11. Tumieni wote ukweli huu ili mupate Kufanyika roho takatifu mutakapo ondoka duniani.

12. Mutu anaweza kufahamu kwamba Mungu yupo kwa njia ya ufunuo ao kwa njia ya mafundisho.

13. Kama mutu ana amini Mungu bila kuhubiriwa na mutu yeyote ni msaada wa roho takatifu.

14. Roho anaweza kumkurubia mutu na kumsaidia katika shuruli zake bila mutu mwenyewe kutambua.

15. Huzingatia msaada wa roho yule aliye wa roho.

16 . Mutu ni mfano wa kipofu ,macho yake imefumbwa na giza.

17. Mungu ni baba wa siri aliye kwa siri,inabidi kumtazama kiroho kwa kuzingatia uzima wake.

18. Ujumbe huu ni nuru kubwa ambae humsaidia mutu kwa kuzingatia uzima wa Mungu.

## 11. TOBA

1. Ametakasika mwenyenzi Mungu,hakimu mkamilifu,anaye tenganisha adili na batili.

2. Mutu halaumike ajili ya kutenda zambi ispokua yule aliye pewa akili.

3. Ujuzi wake ambae ni busara kamilifu ndio unao jua yule anaye stahili kusamehewa na pia yule anaye stahili kuhukumiwa.

4. Na ndio maana maamzi ya watu inafanyika na Mungu peke yake.

5. Mungu mujuzi amekuwekeeni maamrisho na makatazo.

6. Amekuwekeeni maamrisho ili ukutane na Heri,na amekuwekeeni makatazo ili uhepukane na shari.

7. Katika vile alivyo viumba ,kuna ambae husalamisha nafsi yako na ambae huhatarisha nafsi yako.

8. Kadiri sumu inavyo haribu mwili wa mutu,ndivyo pia zambi inavyo haribu roho ya mutu.

9. Kama upo yakini kwamba Mungu ni mjuzi wa yote,mbele na nyuma,haustaili kumpinga kwa lolote,Bali unastaili kumtii.

10. Na kama haufaamu mradi wa amri yake fulani,ni ajili ya upungufu wako unao tokana na asili ya umbo lako.

11. Kila asemalo Mungu ni kweli na haki maana yeye ni mkamilifu.mpungufu hastaili kumlaumu kamwe.

12. Utazania upo katika kundi ya wanao stahili kusamehewa kumbi wewe ni katika kundi la wanao stahili kuhukumiwa.

13. Na mara utazani utaangamia ,kumbi utaokolewa.

14. Hakika ataangamia yule anaye tenda maovu kwa kusudi,ambae hataki kuacha wala kutubu.

15. Yule atendaye zambi kwa ujinga ama kwa kukazwa bila ya idhini yake ndio anaye samehewa upesi.

16. Fanyeni toba namna ya kujilaumu kwa matendo yako,na kunuia kutoirudilia tena,hali yakua umejisihi sana kwa mola wako ili akusamehe.

17. Kiisha ujitolee kuzidisha wema,na pia kumtukuza mola wako kwa wingi.

18. Bila shaka mola wako atakutakasa,hakika yeye ndio msamehevu na mrehemevu.

19. Muaminifu ni yule anaye muamini Mungu na mitume yake ,na pia anaogopa kutenda zambi.

20. Anaye tenda zambi kwa siri ao kwa wazi,sio muaminifu,ijapo kua ajidai mwenyewe.

21. Na wengi huzingiziwa na makafiri ili kuwaaibisha na pia kuwavunja moyo wanao hitaji kauli tukufu.

22. Kila aliye tumwa na Mungu alizingiziwa,kama wanavyo mzingizia Kalonda yale asiyo ya fanya.

23. Kumsemea aliye tumwa uwongo ni kumkebei yule aliye mtuma,zambi kubwa sana.

24. Haisamehewe zambi hii mpaka atubu mbele ya watu kwamba alimsemea wongo mjumbe .

25. Utukufu unatokana na nuru ya Mungu:mutu anaye jazwa malaika ao roho ndio mutukufu.

26. Na kitabu ambae huandikwa ujumbe,ambae malaika na roho humfundisha Mjumbe ni kitukufu.

27. Na Fasi ambae hujumuika malaika na roho ni maala pa takatifu.

28. Mungu ndio bwana wa ulimwengu wote mfalme wa ajabu,anaye simamia wote sawa sawa.

29. Hakuna upatikanaji wala maisha njee ya idhini yake.

30. Wala hakuna anaye tukuzika ulimwenguni kama yeye, bwana wa mabwana.

31. Alikua, yuko na atakua,mwenyi kuenea;hakuna mwengine kama yeye,wa pekee aliye juu.

## 12 UNAFIKI

1. Ametakasika mwenyenzi Mungu ,anaye endelea kuleta mwongozo wake duniani.

2. Huu ni uma bora wenyi majira ya bustani,ambae roho huninginia hewani kutafuta wa kumshukia .

3. Humshukia mnyenyekevu ,anaye amini ujumbe huu mwenyi yakini na uzima wa Mungu.

4. Atakaye hifadhi kauli tukufu ya kitabu hiki,na kuyafanya kama dhikri namna ya kuyarudilia kwa wingi katika kisomo,ataona miujiza ya Mungu.

5. Mwenyenzi atatosheleza maitaji yake kwa namna ya ajabu,lau kama yeye sio mshirikina wala mnafiki.

6.wanafiki ndio wanao zalalisha kazi ya Mungu ajili ya unafiki wao.

7. Ni mfano wa mayatima wasio kua na mlinzi ,ambae hudanganyia kwamba ulinzi wao ni Mungu na ilihali hawafuate sheria ya Mungu.

8. Wamemkimbilia adui wao mkubwa ili awalinde,bila kutambua kama wamejitoa wenyewe mateka.

9. Wamesema tume amini na ilihali katika nyoyo zao hamna hâta chembe ya imani.

10. Na wamesema tumeokoka na hali wao ndio kuni ya jahanamu.

11. Shetani amewataabisha ajili ya kukosa imani,ndio maana wamekosa msaada wa Mungu kwani wao ni wanafiki.

12. Muaminifu wa kweli hataabishwe na shetani ispokua katika kipindi cha majaribu.

13. Shetani hana uwezo wowote mbele ya Mucha Mungu ,maana uyu ni nuru ambae humuondoa yule aliye giza.

14. Hapana kutia unafiki katika imani yako usije ukanyimwa fadhila yote.

15. Na atakaye amini kweli ataona msaada wa Mungu.

16. Ishara kubwa kutoka kwa Mungu itafanyika naye,sio kwa mapenzi yake,lakini kwa idhni ya mola wake.

17. Mungu ndio mtendaji mkuu ,ambae vyote hutokana na idhni yake.

18. Mtukufu anaye tawala bila mpinzani,na kuhukumu bila faragha,m'bora wa viongozi.

19. Utukufu wa Mungu unaendelea kuonekana kila siku kwa ukarimu wa jaza lake.

20. Ajabu ilioje matendo yake Mungu anaumba aina nyingi sana ya viumbe,wala hakuna kwa yeye kuigia mfano.

21. Muumba wa anga na ukiwa kadiri ya pumzi na mwili.

22. Akitokeza asili ya kila umbo kadiri ya idhni yake, na ilihali mwenyewe hana asili yake,mola wa juu ya daulati ,mshindi aliye juu.

23. Mwenyi uzima ,anaye inukia kila kitu,mamlaka katika yote milele na milele.

24. Ni mutukufu wa daraja anaye stawi katika arshi ,asiye kurubiwa na yeyote.

25. Hakuna mwengine mfano wake ulimwenguni,mumilki wa kila jeshi.

26. Ameenea bila kasoro ,juu ya maala pa juu,kadiri ya kistari cha usawa bila mwanzo wala mwisho,na bila fundo wala lukumba.

27. Hakuna wa kumbuguzi wala wa kumsaidia katika uzima wake,amejitosheleza mwenyewe katika yote namna ya kukamilika.

28. Ni mkubwa wa wakubwa wote,aliye na utasi wote ,pahali pote ulimwenguni.

## 13. MLIMA WA HEKIMA

1. Ametakasika mwenyenzi Mungu,mjuzi ,ajengaye umutu baina ya anga na ukiwa.

2. Sehemu ya anga umboni mwake ndio pumzi, na sehemu ya ukiwa ndani mwake ndio mwili.

3. Ukiwa sio sifuru ,lakini upatikanaji usio kua na fikara ndani mwake,kadiri ya ujinga mtupu.

4. Ni umbo isio kua na maisha ajili ya ukosefu wa pumzi ndani mwake.

5. Na ndio maana anaitwa muzilahewa,umbo isiyo linda pumzi ndani mwake.

6. Muumba alifanya mwili wa mutu mfano wa ardhi,wenyi mboleo ioteshaye viungo.

7. Kadiri maji itokayo mawinguni inavyo fufua mimea iliyo kufa,ndivyo pia neno litokalo mbinguni linavyo fufua matunda ya kiroho iliyo kufa nafsini.

8. Mutu ni umbo la kati na kati,changachanga kiumbiko,amekumbwa na uzaifu wa mwili sababu ya kuketi duniani.

9. Na hujaa nguvu nafsini ajili ya pumzi,umbo la angani.

10. Hufanikiwa na mazao ya zamiri yake yule aonekanaye katika sehemu ya kwanza ya bahazi la juu angani.

11. Utaalamu wake ndio hunyanyua umbo lake juu,kwani ametumia nuru itokayo mbinguni.

12. Jengeni mlima wa hekima duniani,na aina tatu ya udongo:kadiri ya mnara wa uongozi katika uharamu kihewa.

13. Sehemu ya udongo mweusi na sehemu ya udongo mweupe na sehemu ya udongo mwekunda.

14. Hakika ardhi husimama sawa pasipo kuyumbayumba majini ajili ya milima.

15. Ujuzi ni wake mwenyenzi Mungu m'bora wa kuumba atanguliaye ulimwenguni.

16. Hakuna alipo anzia wala atakapo komea,mwenyi mamlaka ya ajabu,mshindi aliye juu.

17. Hazaufikake hâta kidogo maana yeye ni mkamilifu,tafauti na wapungufu wote.

18. Hutendeka kwa rafla anacho idhinia,mwenyi uhuru wa milele.

19. Yeye ndio mwanzo wa vyote kadiri ya muujiza,anaye fanya yote kadiri ya maajabu.

## 14. KISIMA

1. Ametakasika mwenyenzi Mungu Chemchem ya nuru ,anaye funulia watumishi wake siri ya mbinguni.

2. Niliona katika ndoto,roho amenikurubia ,akaniambia ,akisema:kuja twende nikuoneshe kisima cha Mungu.

3. Nikaenda pamoja naye ,tukafika kwenyi kisima.

4. Roho aliye nipeleka akaniambia :hiki ndio kisima cha Mungu,tazama ginsi kimechafuka!

5. Nikatazama ndani mwake, nikaona mumejaa uchafu,na majani imeota juu ya maji .

6. Na sehemu ndogo ndio iliyo safishiwa vizuri na maji yake ili kua safi kabisa.

7. Roho aliye ni peleka akaniambia,akisema:sehemu île iliyo safishwa ndio kazi aliyo ifanya nabii muhamadi.

8. Nabii uyu alifanya kazi kubwa ya kusafisha kisima cha Mungu, ili watu watumie maji safi.

9. Lakini hakumaliza,Bali alisafisha sehemu ndogo tu.

10. Na wewe ingia ndani ya kisima, usafishe pia sehemu utakayo wezeshwa na Mungu.

11. Akanipatia upanga ,nikaingia ndani ya maji ya kisima,nikaanza kusafisha lakini siku maliza,Bali sehemu ndogo tu.

12. Roho aliye nipeleka akaniita,akisema: ewe Kalonda ! Tazama ,akafungua kitanga chậke cha kuume kunionesha.

13. Na tazama,nikaona wembe unageuka nuru mfano wa mwezi.

14. Nikatazama ndani ya mwezi ule ,nikaona watu wawili ndani mwake.

15. Mmoja alikua amevaa mfano wa kamanda wa jeshi,na mwengine mfano wa roho mwenyi sura ya urembo sana.

16. Roho aliye ni peleka akaniambia ,akisema:uyu unaye muona ndio nabii muhamadi.

17. Akasema:kweli ninakuambia muhamadi ndio bwana wa wote.

18. Nilipo amuka nikaenda mlimani kwa ajili ya ibada muda wa siku tatu.

19. Nikanuia kuomba Mungu zawadi ya kiroho , ambae nilikua nimekwisha chagua:yaani Yesu,Mussa na Eliya. Na anipatie pia muhamadi .

20. Nilipo kua katika kisimamo cha sala ya usiku ,mlimani, nilisikia sauti toka juu kuniita,akisema:Kalonda ! unapenda Muhamadi akushukie?nikasema,ndio.

21. Mungu akaniuliza, akisema:unapenda aje katika upepo ao aje katika nvua?chagua

22. Nikajibu nikisema :aje katika nvua.

23. Nikasikia watu wengi wameshangilia ,chini ya mlima,wakisema:amebarikiwaa , amebarikiwaa...barakaa,barakaaa...

24. Kiisha wakaanza kusema: Laa ilaha ila laha,muhamadi rasululah,laa ilaha ila laha,kalonda rasulu laha...

25. Mungu akaniambia,akisema:" tangu leo umepewa usanii ".

26. Nilikua nasikia masauti yao lakini sikua na waona.

27. Kiisha nikamalizia sala yangu,na nikafanya dhikri kwa wingi ,ndio nikalala.

## 15. KISOMO

1. Ametakasika mwenyenzi Mungu, muanzishaji wa ulimwengu.

2. Kadiri alivyo tangulia bila hitaji ya msaada,ndivyo alivyo umba viumbe bila hitaji ya msaidizi.

3. M'bora wa kuumba anaye fanya kawaida ya umbiko,hâta kukipatikana usawa katika maisha ya jumla ya viumbe.

4. Hakuna kudondoka kwa mjuzi,vyote hufanyika kwa usawa.

5. Kiumbe hâta kimoja hakifahamu ispokua kwa msaada wake,mwalimu wa siri na wazi.

6. Mtukufu anaye stahili kusifiwa ,mwenyi hâtua na lawama yote.

7. Karibu naye hupatwa na mwangaza,na mbali naye hufinikwa na giza.

8. Mola mwenyi hekima ya ajabu ,ambae hustaajabisha ajili ya kuzidia , mjuzi.

9. Ameendelesha maisha ya dunia ajili ya kutohukumu papu kwa papu.

10. Maisha ya mbingu ni utetezi wenyi kutimia,kazi maalumu ya nuru ambae ni kufukuza giza.

11. Starehe ilioje katika sehemu ya kwanza ya bahazi la juu angani.

12. Ni kambi lenyi utukufu ,ambae ndani mwake hupatikana Maisha ya milele.

13. Tetea namna ya kujumuika mbinguni ,ukipata kufuzu kwa mazao ya zamiri yako.

14. Utetezi bora ni matumizi ya neno la Mungu:ukifanya aliyo kuamrisha na kuacha aliyo kukataza.

15. Hakika aliye silimu ndio mwenyi akili na aliye kufuru ndio mjinga.

16. Someni maandiko matakatifu ya kitabu cha ukweli ili mupate kujazwa.

17. Na itakapo somewa kauli tukufu ya kitabu hiki, ndipo huwafikia nusra kutoka kwa mola wao.

18. Kisomo kinayo faida kubwa huwapatieni nguvu na ushindi, na huwarejesha nyuma wanao shindana nanyi.

19. Amefaulu kabisa yule anaye tumia maneno ya kitabu hiki kadiri ya kifaa maalumu cha maisha.

## 16. TUMAINI

1. Ametakasika mwenyenzi Mungu, bwana wa kila jeshi,anaye neemesha wote walio amini.

2. Tumaini ndio iletayo heri nyingi maisha ni,maana ndio msingi wa imani.

3. Mutu anaye kosa tumaini ya Mungu moyoni mwake ndio maskini,hakuna la Heri maishani mwake.

4. Ni bora kumtumainia Mungu katika kila jambo ,ukawa yakini kwamba ndiye anaye raisisha na ndiye anaye kwamisha.

5. Moyoni mwako usijiweke mbali naye,lakini karibu naye,katika ulinzi wake.

6. Helekeza mawazo yako yote kwake,ukijiuliza moyoni mwako kama yote unayo tenda ni katika mapenzi yake ao hapana.

7. Kuweni na zoezi ya kumkumbuka na kumtukuza moyoni,na tumaini ya kua hauko peke yako Bali malaika na roho wamekuzunguuka.

8. Kama unafaulu katika shuruli zako umshukuru Mungu yakini kwamba ni msaada wake.

9. Na kama unakosa usimlaumu mola wako wala usikate tamaa,lakini umshukuru Mungu na kumuomba masamaha na msaada wake.

10. Na uzidishe ibada hali ya kua na tumaini ya kutoshelezwa na Mungu peke yake.

11. Usiwe na wasiwasi kutaka kujibiwa palepale,wala usisahau ya kama mjuzi ni yeye peke yake,mara utazani ni shari kumbi ni Heri.

12. Wala usijali zarau ao lawama ya watu ,lakini kumbuka ya kama uchoraji wa pumzi yako unabidi makapi kuanguka kandokando yako.

13. Simama imara katika kumuabudu mola wako,ijapokua ugumu wa maisha.

14. Mpelekeeni mola wenu shukrani kwa wingi,mufalme tajiri, anaye miliki vyote kwa jumla.

15. Ndiye mwenyeji wa ulimwengu, mchana ni wake na usiku ni wake,wala hakuna kisicho kua chake.

16. ukategemea umbo fulani,umetegemea kile alicho kiumba,wewe sio ila pumbafu wa kweli.

17. Vyote vitapita,itabakia dhati tukufu ya mola wa ulimwengu.

18. Tukuza jina la mola wako kila siku,na umsujudie na kumshukuru kwa wingi,hakika yeye ndio anaye stahili kuabudiwa.

19. Angeli penda ukosekane duniani kama aungeli zaliwa,lakini amekujaalia maisha kwa ukarimu wa jaza lake.

20. Na akapenda kubadiri hali yako ,utageuzwa kwa rafla,hakuna mwengine aliye na utasi kama yeye.

21. Basi kumbatia kauli ya mola wako kwa kishangwe ,wala usiritadi baada ya kusilimu, wala usiabudu kinyume na muumba wako.

## 17. UJENZI

1. Ametakasika mwenyenzi Mungu,hakimu mkamilifu ,anaye jua Yale ambae wanahewa hawafahamu.

2. Mutu asitafute kujiamua mwenyewe wala kumuamulia yeyote na ilihali hafahamu ya nyuma wala ya mbele ya wakati.

3. Wala usifanye kiburi sababu mola wako anajua yote na hali wewe haujue kama yeye.

4. Ni bora kwako kuamini na kutenda mema na kumuomba.

5. Hayo huonesha matunda mazuri ya  zamiri yako na msimamo wako katika imani.

6. Kadiri unavyo tumika kazi ili upate kujenga mwili wako ,ndivyo unavyo pashwa kufanya ibada ili upate kujenga roho yako.

7. Kama mutu anakataa kuoga maji,na kufua nguo yake,mwili wake utaharibika .

8. Na vivihivyo kama mutu anakataa kusilimu na kutenda mema,roho yake itaharibika,hawezi kuishi milele kamwe.

9. Mwenyi akili ni yule anaye tumia vifaa vya mwili wake na pia vifaa vya roho yake ,kadiri mola wake alivyo muamrisha.

10. Na mjinga ni yule anaye tenda kinyume na maamrisho ya mola wake.

11. Umbalimbali wa mutu na mnyama ni akili:atakaye amini na kutenda mema ndio mwenyi akili.

12. Na atakaye kufuru na kutenda mabaya ndio mjinga,asiye kua na akili,mfano wa mnyama.

13. Neno la Mungu ndio chakula ya roho , itumieni katika kawaida yake ili roho zenu zipate afya njema ya kuishi salama milele.

## 18. MUTI WA UNABII

1. Utakatifu ni wake mwenyenzi Mungu, mkadiriaji wa karama, aliye pasipo yeyote.

2. Nilijikuta katika ndoto, chini ya muti mukabambi wa rangi ya kimanjano,na majani ya mayiyasombe.

3. Muti île ulikua na Matawi tatu ,yenyi kuzidiana unene.

4. Nikamuona roho pembeni yangu, akaniambia,akisema:huu ndio muti wa unabii,panda juu yake.

5. Nikapanda juu ya muti île katika tawi moja,nikatokelea njiani mpaka mbinguni.

6. Nikakutana na mutu aliye vaa kanzu mweupe, aliye kua na kimo cha kadiri.

7. Mutu yule akanikaribisha kwa furaha,akisema:mimi ndio nabii Mussa.

8. Nimetumwa ili nikuoneshe nyumba ya nabii ibrahimu ,tazama nyumba yake kadiri ilivyo.

9. Nyumba île ili kua nzuri sana ambae sijapata kuona,katika bustani ya karibu yetu.

10. Na kiisha ,akanifundisha maneno mengi. Alipo maliza,tuka agana,nami nikarudia.

11. Nikajiona nimeteremuka kwenyi muti huo nilio pandia,na kushuka mpaka chini ardhini.

12. Vijana wa wili ,walio kua na tembea kwa ushujaa wakanikaribia,walivaa mikalabanda kuvikanyako,na mashati na masuruhali.

13. Mmoja kati yao akaniuliza,akisema : nabii Mussa alikua na kuzungumuzia maneno gani mbinguni ?

14. Nikamufasiria kwa kifupi,wote wa wili wakaamini, nao wakajiandaa kupanda katika muti huo wa unabii.

## 19. WAZI WAZI

1. Ametakasika mwenyenzi Mungu mufalme wa ajabu,aliye ni chagua na kunituma ili nipate kufasiria wazi wazi habari yake.

2. Wengi miongoni mwa watu wamenajisi utukufu wa mola wa ulimwengu kwa kumufananisha na viumbe.

3. Mungu mwenyenzi hafanane na yeyote ,yeye sio roho ,wala sio neno ,wala nabii ,wala malaika,wala yeye sio shetani wala muzimu.

4. Amepatikana kadiri ya kuenea,mamlaka yenyi uzima,hakuna anako tokea wala anako endea.

5. Wote mnao wataja walifanyika kwa idhni yake ,kuwatokeza toka sifuru.

6. Pahali alipo hakuna mwengine, mshindi anaye stawi arshini.

7.. Ingieni wote katika usilimu,dini ya Mungu mwenyenzi;ni vema kumuabudu yeye peke yake ,msifiwa aliye juu.

## 20. USALAMA WA NAFSI

1.Shuudieni kwayakini mwenyenzi Mungu,mumoja,atanguliaye ulimwenguni.

2. Anaye amini Mungu peke yake hawezi kuabudu kingine ispokua muumba peke yake,wala hachanganyi nuru na giza.

3. Na ameamini mitume wote,wala hamkanushe yeyote miongoni mwa wale waliotumwa na Mungu.

4. Kuamini mitume ni kusadiki maneno waliyo kuja nayo na kuitumikisha.

5. Na kuamini maneno ya mitume wote ndio kuamini vitabu vya Mungu vyote.

6. Anaye tumia vilivyo maneno ya vitabu vya Mungu amesalamisha nafsi yake kuingia mbinguni.

7. Na kusalamisha nafsi katika mapenzi ya Mungu,ndio kua katika dini ya Mungu.

## 21. SHABAA

1. Enyi walio silimu,unganeni katika kamba moja wala musiachane,mola wenu huwapenda sana walio na umoja.

2. Hapana kuunda kikundi cha kidini ajili ya shabaa ya kidunia.

3. Wala musitumie neno la Mungu kama kizingizio na ilihali shabaa yenu ni mambo mengine.

4. Tumieni neno la Mungu ajili ya kutafuta wokovu wa roho zenu ,mupate kuingia mbinguni baada ya kuihama dunia.

5. Mambo ya kimwili yote ni ya bure,maana itabaki duniani,ispokua mambo ya kiroho ndio inayo dumu milele.

6. Dini nyingi hutokana na uchache wa imani pia na uchache wa elimu.

7. Mungu ni mumoja na sheria yake ni moja ,haipinganake kamwe.

## 22. WA PEKEE

1. Shuudieni ukweli huu,enyi watu wa dunia,hakika hii ni nuru tokea Enzini.

2. Ni kauli tukufu yenyi utimilifu ,mwongozo na wokovu kutoka kwa Mungu.

3. Mungu ndio mwenyi uzima peke yake,mufalme wa ajabu asiye lingana na yeyote.

4. Mtukufu asiye kua na mwili wala pumzi ndani mwake.

5. Na ndio maana hachangie fasi na yeyote,wa peke aliye enzini.

6. Wengine wote ni tafauti sana naye, pumzi yao na miili yao huwafanya wajumuike angani na ukiwani.

7. Mungu amehepukana na upungufu wote , maana amestawi arshini milele.

## 23.SILAHA

1.Mamlaka ni yake mwenyenzi Mungu m'bora wa Viongozi.

2.Mungu wa maajabu anaye tendea waja wake miujiza ya kila namna.

3.hakuna unaso utakao nasa wa chaguliwa wake.

4.wachawi hubaki bumbuwazi wakati waaminifu wanapo okolewa kimuujiza.

5.neno lake hupanguza uchafu wa aina yote, kadiri nuru ipanguzavyo giza.

6.pakizeni nguvu ya ushindi nafsini mwenu kwa ibada ya sala na dhikri, hakika neno la Mungu ndio silaha ya wachamungu.

7.Mola wenu ni muweza wa kila jambo, mwenyi mamlaka kuliko vyote ulimwenguni.

## 24 . WALII

1.Nilipo kua nime lala, roho alinichugua na kunipeleka, katika ndoto, akanifikisha kwenyi mukutano mkubwa wa watu wengi sana.

2.wengi miongoni mwao walivaa mavazi matakatifu makanzu na viremba ma Juba....

3.roho alisimama mbele ya mukutano akaanza kuhubiri neno la Mungu.

4.Alipo maliza, akinisimamisha mbele ya mukutano na kuniruhusu niwaubirie neno la Mungu.

5.Nika wa ubiria kuhusu umungu, na nilipo maliza nikaona yule mkubwa aliye keti katika kiti cha ufalme, akasimama, wakati huo watu wote walistaajabu sana elimu yangu.

6.Na kuni kurubia na kunipatia mukono wake wakulia, akisema: sikiliza, ewe mpenzi wa Mungu:

7.utakapo hubiri ujumbe huu, watu wa dunia wata kuuliza:wewe u' nani ?usiseme ' u' nabii, sema : u' walii.

8.maana wewe ni mtoto wa walii, baba yako mzazi ni walii wa Mungu mwenyenzi.

9.nikaona roho ya uwalii inakuja na ninginia hewani, ikanisogelea na kunieleza, ikisema:

10.Ewe mpenzi wa Mungu usiongeze wala usipunguze katika yale unayo funuliwa.

## 25 .BABA WA SALAMA

1.ametakasika mwenyenzi Mungu, m'bora wa kuumba, mtukufu anaye ondoa aibu na kuleta heshima kwa mtumishi wake aliye zingiziwa.

2.Na ni yeye mjuzi anaye konyeza mutu aliye tetwa na kumsimamia aliye achwa.

3.Mola mtatuzi wa shida zote, mwokozi, anaye nusuru kutokana na shari ya shetani.

4.ameondoa, kwa kauli yake, mashaka na wasiwasi moyoni, hali ya kua mfariji wa milele.

5.baba wa salama aliye salama, mlinzi mwema anaye simamia wote kwa usawa.

6.Neno lake ndio chakula ya roho, mtukufu wa kauli na matendo, ajengaye pumzi urakibuni.

7.Mungu mwenye enzi tukufu, anaye sikia na anaye jibu maombi ya watumishi.

## 26. HODARI

1. Mwenyenzi Mungu peke yake ndio aliye tangulia kadiri ya kuenea bila mwanzo wala mwisho.

2. Lau kama Alianza ,hasingeli kamilika ,maana Angeli kumbwa na upungufu fulani ,namna ya kukosekana muda fulani.

3. Na angeli kua na uzaifu fulani,hasingeli weza kuumba chochote,maana angeli kosewa milki itokezayo toka sifuru.

4. Uwezo wa kuumba ni mamlaka ambae haistahili hata chembe ya uzaifu wowote ndani mwake.

5. Alama ya uzaifu fulani ni dalili ya umbile fulani,na ilihali kiumbe hakina uwezo wa kuumba.

6. Mwenyi uzima ni muujiza wa maajabu,mutukufu anaye patikana kadiri ya kuenea,ambae idhini yake kutenda.

7. Hakika Mungu ni wa peke,hodari asiye jumuika.

## 27. MLINZI MWEMA

1. Abuduni Mungu Mwenyenzi aliye umba kila kitu,unacho kiona na usicho kiona

2. Yeye ndio bwana wa mabwana,ambae maisha na mauti hutokea kwake.

3. Mlinzi mwema,asiye sinzia wala kulala,anaye okoa kutokana na vitimbi vya shetani.

4. Dunia haimzingatie kabisa ,ispokua mbingu ndio humzingatia kidogo tu.

5. Malaika na roho humsujudia kwa unyenyekevu,namna ya kutetemeka mbele yake.

6. Watu wa dunia hawamuabudu kama inavyo stahili,ispokua walio silimu kwa shaada zao za uyakini.

7. Umbo iliye njee ya nuru haizingatie uzima wa Mungu sababu hufunikwa na giza.

## 28..M'BORA. WA. WAFUNDI

1. Ametukuzika sana na zaidi mufalme anaye stawi arshini milele.

2. Mtakatifu mwenyi ujuzi wa yote,anaye jaa kweli na haki ndani mwake.

3. Muweza aliye tandaza mbingu angani na dunia ukiwani kadiri ya kambi mbili tafauti.

4. Na kujaza ndani mwake viumbe vya kila aina,m'bora wa wafundi,asiye iga kwa yeyote,ambae wote huiga kwake.

5. Mutu hagundue wala haunde chochote pasipo mwongozo wake,mwalimu wa walimu wote.

6. Heri yule anaye funuliwa na Mungu maana hufundishwa na mjuzi,na ndio maana ni mwenyi kuinukia .

7. Watakieni rehma na Amani mitume wote ,ni kubwa tena bora kabisa kazi waliopewa na Mungu.

## 29. UTATUZI

1. Ametakasika mwenyenzi Mungu,mwokozi ,anaye fungua maisha iliyo fungwa,na kumponesha aliye gonjwa ,ushindi wa neno lake.

2. Hakuna utata pahali penyi utatuzi wake mutukufu aliye enzini.

3. Mujibu wa dua anaye  anaye rehemu viumbe.

4. Amemnusuru muja wake kutokana na majaribu,falme ya giza haina Fasi ndani mwake ajili ya ibada.

5. Kisomo na maombi hukinga na huponya kwa namna ya ajabu.

6. Someni kila mara kitabu hiki cha ukweli ili mujazwe nguvu ya ushindi.

7. Na kusali kila siku asubui na jioni,na kumtukuza Mungu usiku na mchana.

### 30. MTOTO ( WA  KALONDA)

1. Niliona,katika ndoto ,nimeingia nyumbani.

2. Nikamukuta roho ndani ,kati ya sebule,na watu wengi pamoja na ndugu zangu muma pembeni.

3. Roho akaenda ku kona ya sebule maala ambae kulikua kashiki ya maji ya kunywa.

4. Akaingiza mikono yake miwili ndani ya kashiki iliyo kua na maji ya kunywa.

5. Akatoa mtoto mchanga ndani ya kashiki ,alikua mtoto mwanaume.

6. Kiisha akamuweka mu sahani iliyo kuwa na maji safi, kati ya sebule.

7. Mtoto akafungua kinywa chake,maji ikatokota midomoni pake.

8. Roho akawaambia: Tazameni kadiri anavyo sema.

9. Kweli kweli Nina waambia,mtoto uyu atasema .

10. Ndugu zangu wakaanza kujiuliza,uyu ni mtoto wa nani?

11. Roho akawajibu ,akisema:uyu ni mtoto wa Kalonda atakaye sema maneno.

12. Roho akaniambia ,akisema:habari hii hata wa kubwa yako walio kutangulia zamani waliipokea :

13. Nilikua natembea njiani,nikakutana na mwanamuke kigumba.

14. Ni kamuchugua,katika siku tatu akabeba mimba ,akazaa mtoto mwanamuke jina lake Mariamo.

15. Roho wa Mungu akaandika jina hili hewani,maandiko meupe yakaonekana hewani yakiandikwa "Myriam".

16. Roho wa Mungu akaniambia,akisema:soma jina unayo iona hewani.Nikasoma ,nikisema :Myriam.

17. Roho akaniambia, akisema:utampanga mtoto wako jina hili atakapo zaliwa.

## 31. URAKIBU

1. Ukubwa ni wake yeye anaye stawi arshini,Mola wa karne na karne,mkukufu atanguliaye kadiri ya kuenea .

2. Ni yeye aliye na utasi juu ya kila kitu,mumilki ,ambae hashindwake na chochote.

3. Watu ndio wazaifu katika fikara,hawawezi kabisa kumtegemea vilivyo ajili ya upungufu asilia.

4. Ndio maana hufikiwa na madhara mbalimbali ajili ya udhalili wa dunia .

5. Lau kama wangeli weza kusimama imara kama walivyo wakaaji wa mbinguni,tatizo lisingeli msibu yeyote.

6. Maisha yao ingeli timilika kadiri ya starehe ya milele ,hakuna kilio mbinguni .

7. Basi tumieni njia bora ya urakibu,yenyi kujaa nuru,ili mupate kurithi ufalme wa mbinguni.

## 32. MSAADA

1. Utukufu ni wake Mwenyenzi Mungu,Muumba wa roho na mwili,anaye bariki wachaguliwa wake.

2. Atakaye tumia nuru bila kuichanganya na giza maisha yake yote,hubarikiwa pamoja na uzao wake.

3. Jitengeni na upuuzi wa shetani :usimuendee mpiga ramli wala usimshirikishe na chochote.

4. Hakuna"msaada"njee ya radhi yake Mwenyenzi,maana vyote hutokana na idhni yake.

5. Magumu ya maisha ni kawaida kumgusa kila mutu,imetokana na uzaifu wa mwili,asili ya mwanaadamu.

6. Kama ni msiba shukuru Mungu bila kurombokeza, Na kama ni magonjwa,tumia maombi ao matunzo,hapone yeyote ispokua kwa ruhusa yake.

7. Na kama ni ukosefu ama tatizo lolote,fanya ibada na kazi,ukijaa tumaini ya msaada wa Mungu.

## 33. MPONYAJI

1. Amini Mungu Mwenyenzi ,aliye umba mbingu na ardhi pamoja na vilivyomo bila kuitaji ya msaidizi.

2. Hakuna anaye ishi pasipo ruhusa yake,muweza wa vyote .

3. Kila yule amehitaji msaada wa Mola wake,tumaini na kimbilio,tajiri wa vyote.

4. Mungu ndio mponyaji wa kila nafsi,mkarimu anaye ondoa machungu moyoni.

5. Tumieni neno lake,katika kawaida yake,ili upate kuona utukufu wa Mola wako.

6. Linapo tukuzwa sana jina lake ,ndipo hufanyika ishara yake ya kila namna.

7. Mwenyenzi ni mfariji wa milele,Mufalme mkamilifu,asiye hitaji chochote kwa yeyote.

## 34. AKILI

1. Ametakasika Mwenyenzi Mungu,mpenzi wa watu,amemtukuza kila anaye amini uzima wake na kutii sheria yake.

2. Makafiri hawana yakini na uzima wa Mungu ajili ya kuto mzingatia kimwili.

3. Huzingatiwa kimwili kile kilicho na mwili ,na huzingatiwa kiroho kile kisicho kua na mwili.

4. Kuona kama Mungu hana mwili ,ni lazima kumtazama kiroho ili upate kuzingatia uzima wake.

5. Akili ndio macho ya kiroho inayo zingatia Enzi tukufu namna ya kudhatiti uzima wake.

6. Ni kwamba waaminifu ndio mwenyi akili ,ambae wameona bayana kiroho ndio maana wamemuamini Mungu.

7. Kuona kama makafiri hawana akili ndio maana hawaamini uzima wa Mungu ajili ya kuto zingatia kiroho.

## 35. BAYANA

1. Mutu aliye na akili ni yule anaye zingatia uzima ulimwenguni bila kulazimisha muujiza kwa yeye kusilimu. .

2 .Muujiza mkubwa uliye"bayana" ni kuumba kwako na pia kuumba kwa viumbe vyote uvionavyo.

3. Hakungeli patikana kiumbe chochote ,angani na ukiwani,pasipo muumbaji kutangulia kupatikana,maana kungeli kosekana fundi.

4. Kuna utafauti mkubwa kati ya Muumba na kiumbe.

5. Muumba ni mwenyi ukamilifu ,na kiumbe ni mwenyi upungufu.

6. Ukamilifu ni namna ya kuenea katika uwezo na katika fahamu,na upungufu ni namna ya kutoenea katika milki na katika busara.

7. Kuenea katika uwezo na katika fahamu ndio kuweza yote na kujua yote, mamlaka itokezayo kuujaza ulimwengu.

## 36. NYOTA

1. Niliona ,katika ndoto, mwangaza mkubwa umeniangazia toka juu.

2. Nikanyanyua macho yangu juu, nikatazama, nikaona nyota ine kubwa yenyi kuunganishwa na vistari vine.

3. Nyota moja upande wa mashariki na nyota ingine upande wa mangaribi ,na ingine upande wa kaskazini na ingine nyota upande wa kusini.

4. Humo ndani ya vistari vilio unganisha zile nyota ine,mulikua makundi ya nyota ndogo,na mwezi uliandama ndani ya kundi moja ya nyota humo ndani ya jengo lile la zile nyota ine kubwa.

5. Roho akanichapia nyota zile ine kubwa ,pahali pa vistari akachapa nyota ndogondogo zilizo unganisha zile nyota ine kubwa .

6. Roho akaniambia ,akisema:vile vistari ni mufululizo wa nyota ndogo ndogo zinazo unganisha zile kubwa.

7. Roho akaniambia akisema:hakika nyota hizi unazo ziona ndio watoto.

## 37. KARAMA

1. Sema:kuna daraja ya kiroho na pia kuna kazi ya kiroho .

2. Daraja ya kiroho ni unabii na uwalii .

3. ,Na kazi ya kiroho ni utume na utumishi .

4. Unabii ni daraja kubwa ,karama ya nuru kubwa ,ambae humfanya azingatie mambo yatakayo tokea mbele ya wakati,na kuwaonya watu.

5. Na utume ni kazi kubwa sana ya kiroho ,ya kufundisha watu neno la Mungu kwa njia ya ufunuo,yaani kwa kupokea ujumbe kwa Mungu.

6. Mtume anaweza kua na daraja ya uwalii ao anaweza kua na daraja ya unabii .

7. Na yule anaye tumikisha ao anaye fundisha watu neno la Mungu kwa njia ya maandiko, yaani bila kupokea ujumbe kwa Mungu ,yeye ndio Mtumishi.

## 38. UZAO WA MBINGUNI

1.Mwenyenzi Mungu ni nuru ya anga na ukiwa,mjuzi atawalaye ulimwenguni.

2.Yeye ndio chemchem ya kila upatikanaji ,mufalme wa pekee anaye enea kadiri ya uzima.

3. Ameletea watu mwangaza namna ya upodozi wa nafsi.

4. Tumieni wote nuru hii,ili nafsi zenu zipate kufikia utimilifu,mupate kua watukufu wa mbinguni.

5. Mbinguni hakuna kuzaa wala kuzaliwa,lakini wakaaji wa bustani huzaliwa duniani.

6. Atakaye amini Mungu na mitume yake yote,ndio mzaliwa kiroho wa mbinguni.

7. Atageuka roho takatifu,atakapo ihama dunia,na kujumuika mbinguni.

## 39. JITIHADA

1. Mwenyenzi ni mshindi aliye na mamlaka ya ajabu, mwenyi uwezo wa kuokoa ijapo kua dakika ya mwisho.

2. Hapana kukata tamaa ajili ya maovu iliyo tangulia ,ni bora kujitaidi kutubu na kutenda mema ili upate kusamehewa.

3. Usijiamulie mwenyewe kua wa hadeze na ilihali hauja kufa,kukingali wakati wa kukuokoa lau kama utaamini .

4. Wala usijiamulie mwenyewe kua wa mbingu na ilihali ungali na ishi duniani,labda imani yako haikubalike ,na wenda utadondoka baadaye.

5. Usiwe na majivuno wala usiwe na unyonge,lakini ujitaidi kuzidisha wema ili upate ushindi.

6. Kama uko katika jitihada ya kutumia nuru vilivyo,usisahau kwamba unaweza kujaribiwa .

7. Na utakapo jaribiwa na yule mwovu ,ujitolee kushinda majaribu kwa subira na ibada, ukiomba masamaha na wokovu .

## 40. ZAMIRI

1. Imani ya kweli ni kusadiki uzima wa Mungu ,na pia kutumikisha mafundisho ya mitume wote.

2. Kinacho haribu imani ya watu ni uchafu wa nyoyo zao pamoja na ushirikina .

3. Ni lazima kutakasa zamiri yenu kwa kuondoa :kiburi,chuki ,nongo,choyo,hila,fitna,na tamaa mabaya .

4. Na utakapo jitenga na mambo haya na yaliyo mfano wa hayo, ujitolee kufanya ibada kwa wingi .

5. Usijidai utumishi na ilihali moyo wako umejaa takataka ya kila namna .

6. Mbingu ni pahali patakatifu,hakuwezi kuingia kichafu .

7. Mwenyenzi Mungu huchunguza zaidi zamiri ya watu,anafahamu sana yaliyo moyoni mwa kila mutu .

## 41. MATUMIZI

1. Abuduni Mungu mwenyenzi peke yake wala usiabudu mwengine badala yake .

2. Watumishi wa Mungu wengi wamepotea ajili ya kutumia kafara ya shetani .

3. Kutumikisha mizimu (ma jini) kwa siri ao kwa wazi ,ni ujinga wa kujitoa mateka .

4. Kwa nini kutumikisha jeshi la hadezeni na hali munatambua matata ya hadeze ?

5. Kwa nini hamutumikishe tu jeshi la mbinguni na hali munatambua fadhila ya mbingu?

6. Mara ni kushindwa kutumia njia nzuri ya urakibu;maana kutumia maamrisho ya Mungu ni vigumu kwa wenyi wasiwasi na tamaa ya dunia .

7. Na mara ni kukosa tumaini ajili ya uchache wa imani ,hawana yakini na uzima wa Mungu Mwenyenzi .

## 42. MILKI ICHIPUAYO

1. Ametakasika Mwenyenzi Mungu,M'bora wa kuumba,aliye muumba Shetani kwa ulimi wa moto,na akamuumba Malaika kwa Anga takatifu.

2. Na akamuumba Mutu kwa udongo .

3. Hakuna Mjuzi mwengine kama yeye na ndio maana hakuna anaye weza kuumba ispokua yeye peke yake .

4. Anatokeza viumbe vingi sana ,wala hasahau hâta kitu kimoja,mlezi wa jumla ya viumbe .

5. Anajua na anatosheleza haja ya kila umbo inayo ishi .

6. Mtukufu atanguliaye kimuujiza ,afanyaye maajabu ,aliye na uhuru , aliye na ushindi .

7. Chemchem ya upatikanaji na maisha , kadiri ya milki ichipuayo ,kadiri ya taa iangazayo .

## 43. MUSKITI MTAKATIFU

1. Roho wa Mungu alinikurubia ,akaniambia,akisema:maono haya hâta wakubwa yako walio kutangulia waliyaona .

2. Nikatazama juu , nikaona mbingu imefunguliwa ,naangalia ,nikaona jicho mfano wa jicho la mutu ndani ya mbingu ambae hutazama ku dunia .

3. Roho akaniambia ,akisema:furahi sana,Kalonda,maana umepata kuona siri ya ufalme wa mbingu .

4. Na tazama nikajikuta ndani ya Muskiti mkubwa sana ,ambae ndani yake mulikua sehemu tatu;sehemu mbili ku wanaume na moja kuwanawake.

5. Humo ndani mulikua watu wengi,ma rangi pia ma Kabila ya dunia yote.Mulikua watu walio vaa makanzu na viremba ,na mwengine walikua na ndevu ndefu.

6. Baada ya sala ,roho akanichugua,tukatoka ili turejee nyumbani;tulipo toka njee nikajikuta mbele ya muskiti wetu wa benye kadingila .

7. Nikastaajabu sana ,nikamuuliza roho aliye nipeleka,nikisema:ni namna gani hivi?tulikua katika muskiti mkubwa ,wenyi majengo mapya ya kudumu ,kutoka inje tunakua mbele ya muskiti wetu wenyi majengo ya kiasili na nyasi juu.

8. Roho akaniambia ,akisema:muskiti huu ndio uleule tulio kuwamo.

9. Hakika nimekuambia ,Muskiti huu ni utakatifu .

10. Ni lazima ujengewe kadiri ulivyo uona,kuunenepesha mpaka ngambo ya njia.

11. Heri Mutu atakaye jumuika katika sala ndani ya muskiti huu.

## 44. M'BORA WA VIONGOZI

1. Utukufu ni wake Mwenyenzi Mungu,m'bora wa viongozi .

2. Anaye helekeza fikara ya musilimu kwenyi haki na kweli,na kumpitisha katika njia iliyo nyooka hadi mbinguni.

3. Amemzindua aliye jingikiwa na kumsimamisha aliye anguka katika imani .

4. Mutu anaweza kuzania kufanya haki kumbi sivyo.Lakini mwenyenzi humuhelekeza kulingana na zamiri yake.

5. Ni lazima kuomba kwa Mungu mwongozo wa zamiri yako,na akuhepushe na vishawishi.

6. Mungu ni msamehevu na mrehemevu ,mjuzi anaye sikia manongonezo ya moyoni mwa kila Mutu.

7. Ogopeni Mungu kwa siri na kwa wazi,hakika mamlaka yake ni kubwa ajabu,hakuna kwa kumfichamia .

## 45. MTUNZAJI

1. Utakatifu ni wake mwenyenzi Mungu,mtunzaji,anaye ponya walio rogwa na kuwapanguza machozi wanao lia .

2. Mola wa miujiza mwenyi mamlaka ya ajabu,anaye ondoa uchawi kwa kauli yake tukufu.

3. Anapo taka jambo husema: liwe na linakuwa .

4 . Hakuna ligumu kwake yeye mufalme, hakika vyote ni chini ya uwezo wake.

5. Muweza yote anaye pana nguvu ya ushindi kwa waja wake,kama alivyo mupa Kalonda nguvu ya kumshinda Waileshi.

6. Mtukufu anaye jengea vipenzi vyake ngao ili mizinga ya maadui isiwapate.

7. Mungu hawaachake waaminifu ajili ya kudondoka,lakini huwarudilia baada ya toba yao kwa huruma wake ,hakika Mungu ni msamehevu na mrehemevu.

## 46. MUAMUZI

1. Ametakasika Mwenyenzi Mungu, mutukufu anaye tawala ulimwenguni bila mipaka..

2. Mola wa jumla ya viumbe aliye na milki kamilifu ,atendaye kwa idhini bila kazi.

3. Mutu hazae wala hafiwe ispokua kwa mapenzi yake ,bingwa aliye na kasi la uwezo wa kutenda.

4. Mungu ndio anaye bariki waaminifu na ndiye anaye laani makafiri.

5. Hazulumu yeyote miongoni mwa viumbe vyake,m'bora wa kukadiria.

6. Muumba wa vyote aliye fanya roho kadiri ya utimilifu na akafanya muzimu kadiri ya uharibifu.

7. Muamuzi anaye jua yote bila kuambiwa na yeyote,kiongozi pekee wa jumla ya viumbe.

## 47. MWANZO WA VYOTE

1. Ukamilifu ni wake Mwenyenzi Mungu anaye enea ulimwenguni.

2. Mwanzo wa vyote anaye tangulia kwa mamlaka yake mwenyewe bila msaada wa yeyote.

3. Amepatikana na ujuzi wa vyote pia na uwezo wa vyote sababu ni mwenyi kukamilika.

4. Hali yake ni uzima, utukufu wa ajabu usio kua na mfano, m'bora wa kuumba.

5. Angeli kua na mfano wake kama hasingeli kua na ukamilifu,na kama angeli kosa ukamilifu bila shaka angeli kua mpungufu.

6. Upungufu hutokana na umbiko, uzaifu unao dai msaada kwa kujumuika na kwa kutenda ulimwenguni.

7. Mwenyi Enzi ndio bwana wa ulimwengu, mshindi aliye na milki kamilifu.

## 48. ENZI

1. Utangulizi wa Mungu ni muujiza mkubwa sana,namna ya kuenea bila mwanzo wala mwisho.

2. Ni mamlaka ya ajabu kadiri ya uwezo wa vyote, ambae humkamilisha bila upungufu wowote.

3. Uwezo wa vyote ndio milki kamilifu, ambae haishindwake na chochote.

4. Milki hiyo ndio inayo itwa:Enzi ,jambo la upekee pasipo mfano wake ulimwenguni.

5. Enzi ndio hutokeza ulimwengu na walimwengu maana hujua yote na huweza yote.

6. Hakuna kinacho patikana bila ya idhni yake,mutukufu aliye na mamlaka ya kutokeza toka sifuru.

7. Yeyote aliye na upungufu hana uwezo wa kutangulia wala uwezo wa kutokeza toka sifuru ajili ya uzaifu.

## 49. AHMADI

1. Sema:Ahmadi ni mkweli,alitumwa na Mungu.

2. Na wewe ni shahidi wa Mungu Mwenyenzi.

3. Na maneno unayo andika ni ukweli, na kitabu hiki ni kitukufu.

4. Kwa nini umesoma maneno ya wengine katika sala na ilihali umekwisha funuliwa maneno ma takatifu zaidi ?

5. Ushuuda unao toa juu ya uzima wa Mungu ndio wa kweli kabisa.

6. Basi shaidilia, Mungu mwenyenzi yu pamoja nawe ,pia na wote wanao kubali ushuuda wako.

7. Hakika mwenyenzi Mungu amewapenda sana wanao toa shaada, ambae huamini ujumbe wake.

## 50. UTAZAMAJI

1. Mola wa ulimwengu amestawi juu ya maala pa juu arshini.

2. .Amepatikana mbali sana na dunia maana yeye ni tafauti kabisa na mwili, mwenyi kuhepukana na upungufu wote.

3. Mungu haiko mashariki wala mangaribi,haiko kaskazini wala kusini,Bali mutukufu amestawi juu sana kupita mbingu.

4. Kumuhelekea ni kumtumainia ,kumpenda kwa moyo wako wote ,yakini kwamba ndiye mwenyi mamlaka ya vyote.

5. Ukamtazama kimwili hauweze kuzingatia, ni kawaida kumtazama kiroho ili upate kuzingatia uzima wake.

6. Akili yako ikazingatia utendaji wake ni kwamba umemuona.

7. Mungu ni mwenyi kuwako bila kukosekana wakati wowote wala kushindwa na chochote , m'bora wa kuenea.

## 51. MAJI YA. UHAI

1. Mwenyenzi Mungu ni nuru ya anga na ukiwa, busara kamilifu ambae hujua yote.

2. Neno lake huangazia akili urakibuni,kadiri ya upodozi wa nafsi.

3. Enyi walio silimu, jisafisheni na neno la Mungu ,hakika kauli tukufu ni mfano wa maji ambae husafisha roho.

4. Huondoa takataka yote ya moyo na kugeuza pumzi ya mutu hali ya kua roho takatifu.

5. Yesu Masiya ni Nabii na mitume mkubwa aliye jazwa kauli tukufu na kulingana nayo kihakika zaidi ya wenzake.

6. Na ndio maana yeye ni mfano wa neno la Mungu.

7. Kauli tukufu ni mfano wa maji ya uhai,ambae hutakasa moyo wa mutu,kutumia neno la Mungu ndio kuamini unabii wake.

## 52. WEMA

1. Amejaa utukufu wa ajabu Mwenyenzi aliye juu, mkuu anaye wezesha na anaye zaufisha.

2. Kila tendo lake linao mradi wake na maana yake,sababu hufanyika na busara kamilifu.

3. Ulemavu na utimilifu watokea kwake, wala hana hatia yoyote katika kuumba kwake.

4. Kama watu wangeli fahamu sababu ya kutokeza kwake umbo fulani na upungufu fulani, bila shaka wangeli shangilia ujuzi wake.

5. Heri mutu anaye saidia maskini bila kumshimangi wala kurombokeza ,maana yeye pia atalipwa makubwa na Mola wake.

6. Tendeni wema ili Mungu akulipe mema zaidi ,wala usitende wema ili watu wakulipe ao wakusifu.

7. Dunia haina wema,atakaye tumaini malipo ku dunia atavuna sifuru.

## 53. MASINGIZIO

1. Enyi walio silimu ! Jiepusheni na zana pia na masingizio ku watu wenzenu.

2. Atakaye mzingigizia muaminifu ili kutaka kumzalalisha,ataingizwa hadezeni atakapo ihama dunia.

3. Ogopeni Mungu ukweli wa kuogopa ,hakika hukumu ya Mola wenu haina maondoleo.

4. Katika uwezo wake wa ajabu hakuna wa kupimana naye ulimwenguni.

5. Mwenyenzi ni bingwa anaye zidia wote katika yote,vyote hupatikana kadiri ya idhni yake wala hakuna kilicho njee ya hukumu yake.

6. Hapana kumushambulia muaminifu bure musije mukaanguka pembeni yake mfano wa makapi,msije mukachomwa motoni.

7. Kila mutu atavuna Yale aliyo ya panda,maana Mola wenu ni hakimu mkamilifu.

## 54. VIFAA

1. Uzima ni wake Mwenyenzi Mungu,mwalimu wa wanahewa wote.

2. Yeye ndio anaye angazia fikara ya watu ili wagundue vifaa mbali mbali.

3. Matumizi ya vifaa katika shida mbali mbali sio mubaya,Mola wenu amewatakieni usalama.

4. Ni makosa kutumia chombo ajili ya kuangamiza watu bure bila ya haki.

5. Kama musilimu anagonjwa,ni bora aanze na maombi na kiisha atibiwe bila kumshirikisha Mola wake na chochote.

6. Mutu anaye kataa kutunzwa ni sawa na majununi anaye kataa kuoga na hali mwili wake umechafuka,na ndio mfano wa muovu anaye kataa kutubu.

7. Usimjaribu Mola wako kamwe ,wala usilazimishe Mungu akufanyie jambo ambae amekwisha kupa ginsi ya kujifanyia mwenyewe.

## 55. TAJI LA UTUKUFU.

1. Ewe muaminifu ,acheni watu wa dunia wakuzarau ajili ya imani yako,hakika heshima yako ni kubwa sana mbinguni.

2. Mola wako atakuvika taji la utukufu, na furaha kwako haitakua na ukomo.

3. Zaidi umeshambuliwa duniani ,zaidi umeneemeshwa mbinguni.

4. Usivunjike moyo sababu ya kutohukumiwa duniani waovu wanao kubuguzi,kuna wakati ulio wekwa ,ambae haki itainuliwa juu,ndio kilio chao kitaanza bila ukomo.

5. Maisha ya dunia ili wadanganya ,walizani ujanja kumbi upumbafu .

6. Muovu asiye azibiwa na watu duniani,azabu yake ni kubwa zaidi siku ya mwisho.

7. Ole kwao wanao tenda zambi kwa uficho,wamezani kunusurika kumbi kuhatarika zaidi hiyo siku ya hukumu.

## 56. KADI

1. Roho alinikurubia, akaniita akisema:Kalonda ! Twendeni pamoja nikuoneshe.

2. Nikaenda naye ,tukafika katika uwanja,ambae mutu mmoja alikua amekaa chini juu ya udongo .

3. Mutu yule alikua mwenyi kuzoroteka kiafya,akivaa suruhali ya rangi mweusi yenyi vumbi,na shati mweupe yenyi kufifia na uchafu.

4. Roho akaniambia, akisema : mutu uyu anaye kaa katika mavumbi ya ardhi ndio Kadi ,yaani Kadima.

5. Mutu uyu amejidai unabii na utume na ili hali Mungu hakumtuma.

6. Roho akaniambia, akisema : tazama kilicho mbele yake.

7. Nikatazama mbele yake, nikaona kumewekwa marimbarimba ,juu yake mafulushi na mapiki makundi.

8. Punde kidogo nikaona chombo kile kikaanza kutingizika na nguvu sana.

9. Roho akaniambia, akisema : kitu hiki ndio uchawi wake, kama kinafanya hivi,ishara hufanyika.

10. Hakika mutu uyu ni nabii wa uwongo tena muchawi,miujiza yake sio ila urozi mtupu.

11. Angalisho na walimu wa mafumbo,maana ndio wajumbe wa masih jadali.

12. Zama hizi watu wengi wamejidai utume na ilihali hawakutumwa na Mungu.

## 57. WA MIUJIZA

1. Mwenyenzi Mungu ndio mwanzo wa vyote ulimwenguni, chemchem ya upatikanaji na maisha.

2.Ujuzi wake ndio ulio kutwa kabla ya ulimwengu na walimwengu,kadiri ya ukamilifu pasipo kabla yake wala baada yake.

3. Mwenyi uzima, mtukufu aliye na uwezo wa vyote, anaye simamia viumbe kwa usawa.

4. Vitu vyote njee ya dhati yake ni miongoni mwa viumbe alivyo viumba.

5. Mungu hafanane na yeyote wala hachangie fasi na yeyote, wala hana shauri na yeyote kwani ni wa pekee.

6. Bingwa aliye tokeza vitu vyote bila kutokezwa na yeyote, mkamilifu.

7. Mufalme wa ajabu anaye stahili kuabudiwa peke yake, wa miujiza aliye huru kuliko wote.

## 58. LENGO

1. Mungu amempenda sana aliye nuruni kuliko aliye gizani.

2. Aliye nuruni hutumia vyote kiroho matendo ya mwili wake huangaziwa na roho yake.

3. Hutumia mwili sababu ndio unao fanya adhihirike duniani,lakini mradi wake ni kiroho.

4. Umungu hauzingatiwe ispokua kiroho ,yaani kwa njia ya roho.

5. Utazamaji kimwili hauzingatie ispokua miili peke yake.

6. Anaye sumbukia dunia hutumikia tu maisha ya dunia ,wala hakumbuke maisha ya mbinguni.

7. Mutu wa namna hii ndio mwenyi hasara kubwa ya kukosa maisha ya milele.

## 59. ASIYE ONEKANA

1. Enyi wanaadamu ! Aminini Mungu kama vile mungeli kua na muona na macho yenu,wala musiwe na shaka ajili ya kuto onekana kimwili.

2. Watu wengi hawana imani sababu ya kuto muona na macho yao kimwili, wamezani wamefanana naye.

3. Hapana kulazimisha kumuona kimwili yeye ambae hana mwili, tena aliye mbali sana na dunia.

4. Kiungo cha mwili kiitwacho jicho hakizingatiake kisicho kua na mwili, wala kilicho njee ya dunia.

5. Mwili ni umbo zaifu sana ambae hujaana na ujinga,ndio maana fikara inayo changana na ujinga ndani ya mutu ni zaifu,yenyi kufubala.

6. Hali yake Mungu ni tukufu ajabu,tafauti kabisa na umbo zote,maana yeye ni katika ukamilifu na viumbe ni katika upungufu.

7. Kama unapenda kuona utukufu wa Mungu ,basi amini kikweli utaona bayana utukufu wake na hâta kumsikia sauti yake.

## 60. MWAMBA USIO VUNJIKA

1. Mwenyenzi Mungu ndio mwokozi,ni lazima kuhitaji msaada kwake,mkubwa aliye na uwezo wa vyote.

2. Atakaye tegemea viumbe katika shida yake yote ndio pumbafu atakaye shindwa.

3. Tumaini ya Mungu moyoni ndio husadikisha imani ndani ya mutu.

4. Baada ya dhikri urakibuni ni faraja,hapana kukata tamaa, maana uwezo wa Mola wenu ni tayari kila fasi na kila muda.

5. Kama unajitupa kwa Mola wako na moyo wako wote hauta pata haya lakini ushindi na heshima.

6. Mwenyenzi ndio mwamba usio vunjika ,shikeni kwa bidii mwamba huu ili mapate kufuzu.

7. Hakika Mwenyenzi Mungu ametosheleza kua mlinzi.Hakuna mwengine kama yeye.

## 61. USAFI WA MOYO

1. Safisheni moyo wako,ewe mwanaadamu, wala usilinde kamwe wazo mbaya ndani mwako.

2. Hauwezi kulipwa malipo ya mtenda mema na ilihali wewe ni mtenda zambi.,Mola wako ni m'bora wa mahakimu.

3. Usiunge urafiki na shetani na hali wewe umekwisha silimu.

4. Hakika unafiki ni mila mbaya ambae humfanya mutu anyimwe fazila zote.

5. Ondoa upuuzi na uvivu katika utumishi wako ,bila shaka ujasiri wako humaanisha ukubwa wa imani yako.

6. Na usifanye ibada kama anaye mjaribu Mola wa walimwengu.

7. Mola wako huchunguza zaidi sana yaliyo moyoni, wala hapitiwe na lolote.

## 62. UMUTU

1. Mutu asiye tumia neno la Mungu pumzi yake sio urakibuni lakini uatiduni,,ndio maana nafsi yake sio asili ya roho lakini asili ya muzimu.

2. Matunda yake ni mabaya ajili ya kupatikana gizani ametumia wazo lisilo faa na kisa kisicho faa.

3. Na fikara yake hukomea katika mambo ya kidunia peke yake ,na ilihali dunia ni ya muda mfupi.

4. Na yule anaye tumia wazo inayo stahili na kisa kinacho stahili, ndio pumzi urakibuni, asili ya roho takatifu.

5. Kuona kama yeye ni nuruni, ndio maana huwanukulu wakaaji wa mbinguni,utimilifu wa umutu.

6. Yule asiye amini Mungu ndio mwenyi kukosa akili , amewanukulu wakaaji wa hadezeni,uaribifu wa umutu.

7. Mutu asiye kua na utaalamu kifikara ni sawa na mnyama, kukosa imani ndio kukosa akili.

## 63. MLIMA KAROMBWE

1. Niliona, katika ndoto, mlima mrefu ambae juu yake kulisimama mutu mrefu,akivaa koti na suruhali na mtama.

2. Mutu yule alikua na teremuka kuhelekea upande wetu mpaka mbele yangu,kicheko midomoni.

3. Roho akaniambia, akisema : mutu uyu unaye muona ndio Nabii Saleh .

4. Nilipo mtazama ,moyoni mwangu mulijaa furaha.

5. Roho aliye ni peleka, akaniambia, akisema : furahi sana ewe mpenzi wa Mungu, hakika kuonana na nabii uyu ni neema kubwa.

6. Roho akaniambia, akisema : karombwe ni mlima mtakatifu,lakini haija funuliwa kwa yeyote, kama ilivyo kwenyi muji Seule.

7. Mlima huu na muskiti wa benye kadingila ni maala pa takatifu .

## 64. ONDOA SHAKA

1. Ametakasika Mwenyenzi Mungu ,mwalimu mkamilifu, anaye funulia watu siri ya mbinguni.

2. Dunia isingeli ongoka pasipo ujumbe wake, amelea viumbe na hekima ya ajabu.

3. Kupokea kauli yake ndio kusalamisha nafsi yako, namna ya kustiri maisha yako.

4. Mungu anaendelea kuongoza watu ili wasipotee,wenyewe wasingeli faulu ajili ya  uzaifu kibusara.

5. Lakini ijapokua msaada wake, mashaka haimalizike katika nyoyo zao.

6. Huwapinga wajumbe wa Mola wao na kulazimisha Mwenyenzi apate kuishi kama wanavyo ishi.

7. Ni ujinga sana kulazimisha utendaji wa Mungu ulingane na utendaji wa kibinaadamu.

## 65. ANAYE STAAJABISHA

1. Mwenyenzi ni mwenyi uzima, mtukufu anaye kamilika peke yake ulimwenguni.

2. Nafsi yenu na maisha yenu ni tafauti kabisa na dhati yake uzimani.

3. Matendo yote ya viumbe ni upungufu,tafauti kabisa na matendo yake ya ukamilifu.

4. Ni vema kufikiri mbele kama yale unayotaka Mungu ayatende humustahili ao hapana, maana yeye ni mkamilifu.

5. Uzaifu wa kuishi mfano wa viumbe haumkurubie kamwe.

6. Utendaji wake ni wa pekee kadiri alivyo wa pekee bila mfano wake.

7. Mufalme anaye staajabisha ulimwenguni.

## 66. CHEMCHEM YA FAHAMU

1. Ametakasika Mwenyenzi Mungu, mufalme anaye stahili kuhimidiwa usiku na mchana.

2. Amepatikanisha kila kitu kwa ujuzi wake na uwezo wake, m'bora wa kuumba.

3. Akapenda kugeuza umbiko, anaweza kufuta upatikanaji huu na kutokeza umbiko lipya la aina ingine.

4. Busara yake ni kamilifu,chemchem ya fahamu yote ulimwenguni.

5. Hakuna asilo lijua,mtukufu aliye tayari muda wote kutokeza mapya bila kuiga wala kujifunza.

6. Anafahamu mambo yote inayo fanyika na kila viumbe muda wote pahali pote.

7. Tajiri wa habari yote ulimwenguni, mzima asiye sinzia wala kulala,mfinyanzi wa umbo za walimwengu.

## 67. BARAZA

1. Ujuzi ni wake Mwenyenzi, wa pekee anaye endelesha maisha ya pumzi ya wanahewa_haramu.

2. Miili yao huaribika duniani, lakini pumzi yao hujumuika barazani.

3. Viumbe vikali katika baraza la hadeze,na viumbe vipole katika baraza la mbingu.

4. Baraza la hadeze hufikiwa na chembe ya utesi wa shetani,.

5. Na baraza la mbingu hufikiwa na chembe ya ulinzi wa malaika.

6. Kifo cha duniani ndio mwanzo wa starehe kwa waaminifu, na pia ndio mwanzo wa mateso kwa makafiri.

7. Hakika Mwenyenzi ndio m'bora wa mahakimu,humlipa kila mumoja wenu sawa na matendo yake.

## 68. KABURI

1. Sema:kaburi ni kambi la kimwili udongoni ambae hulinda mauti ya mutu.

2. Humo ndani ya kaburi hamuna maisha ingine Bali mwili huaribika kwa haraka na kugeuka udongo.

3. Umbo la mutu linayo sehemu mbili : mwili na pumzi.

4. Baada ya kifo,mwili ndio huingizwa na watu kaburini ,na pumzi ndio huingizwa na Mungu barazani.

5. Pumzi huzidi kuishi barazani hadi kiyama,na mwili ndio huoza namna ya kufutika kaburini

6. Sehemu ya baraza inayo gusana na mbingu ndio baraza la mbingu, na sehemu ya baraza inayo gusana na hadeze ndio baraza la hadeze.

7. Kama kweli kaburi ingeli kua na Linda pumzi, ingelikuaje kwa yule ambae mauti yake haikuzikwa kaburini ?

### 69. MAPAMBAZUKO

1. Nuru ndio kifaa ambae huondoa giza,kadiri fahamu inavyo ondoa ujinga.

2. Ni utukufu utokao ndani mwake kadiri ya uvuli wake ambae huleta mapambazuko.

3. Kinacho pambanua fikara ya mutu ili maisha yake itimilike sawasawa ni neno la Mungu.

4. Kauli tukufu ni nuru ya busara kamilifu inayo tua mbinguni na kuzagaa angani pote na ukiwani.

5. Malaika na roho wanapo pokea neno la Mungu ndio kuzagaa kwa nuru mbinguni.

6. Na ma nabii na mitume wanapo pokea ujumbe ndio kuzagaa kwa nuru duniani.

7. Asiye tumia neno la mola wake hupatikana gizani maisha yake yote, atajumuika hadezeni mikononi mwa falme za giza.

### 70. KIMBILIO

1. Utakatifu ni wake Mwenyenzi Mungu, m'bora wa kuumba.

2. Mola wa miujiza aliye na mamlaka ya ajabu

3. Mtukufu apangaye na apanguaye majira ya ulimwengu.

4. Vilivyomo angani na vilivyomo ukiwani hutarajia msaada wake.

5. Mwingi wa rehema na mwingi wa ukarimu, anaye fariji maisha ya kila mutu.

6. Baba wa salama aliye salama ,helekeo na kimbilio la wasilimu.

7. Hakuna Mola mwengine apasaye kuabudiwa kwa haki ispokua Mungu Mwenyenzi peke yake.

## MULANGO WA INE : CHEM CHEM

## (1)

1. Ametakasika mwenyenzi Mungu aliye tangulia bila kuanza ajili ya kukamilika.

2. Ni mwenyi kuenea katika yote tafauti na upungufu wote.

3. Amejaa milki kamilifu ambae huweza yote na hujua yote.

4. Mamlaka kubwa ajabu ya utendaji wa vyote yenyi kuongoza ulimwengu.

5. Bila yeye kutangulia hakungeli patikana chochote, ndio maana ameitwa "chemchem" ya upatikanaji wote na maisha yote.

6. Mwanzo wa vyote, kadiri ya milki ichipuayo ,kadiri ya taa iangazayo.

7. Hakika ametukuzika sana Mwenyenzi Mungu, mzima peke yake ulimwenguni.

## (2)

1. Mwenyenzi ni mtawala wa wote pahali pote, bwana wa majeshi asiye jumuika angani wala ukiwani.

2. Kutojumuika katika upungufu sio kukosekana, hayo husababishwa na ukamilifu wake.

3. Mkamilifu hastahili kuchangikana na wapungufu asiye kunajisika.

4. Hali yake hii tukufu hutokana na ukubwa wa daraja yake, bwana wa mabwana.

5. Ndio maana hazingatiwe katika upungufu sababu ya kutojumuika humo wala kufanana na chochote.

6. Kadiri hewa inavyo zingatiwa

kwa vitimbi vyake, ndivyo pia enzi inavyo zingatiwa kwa matendo yake.

7. Hakika Mungu Mwenyenzi ni mkubwa sana mwenyi mamlaka ya ajabu,mutakatifu asiye najisika.

# (3)

1. Ametakasika Mwenyenzi Mungu, wa  pekee anaye jumuisha pasipo kujumuika.

2. Mkombozi anaye fungua waja wake kutokana na vifungo vya shetani.

3. Na kuwajaza afya kimwili na kiroho ,na kuwaingiza katika bustani ya neema.

4. Mtukuzeni Mola aliye umba kila kitu, chemchem ya nuru ulimwenguni.

5. Hakuna aliye juu yake, muheshimiwa,anaye stahili kupelekewa shukrani zote.

6. Mumilki aliye imara na daima katika tendo kua kadiri ya uzima kinyume na maisha.

7. Hakuna aliko tokea wala anako endea ,mtangulizi kadiri ya mwanzo wa vyote, mwenyi kuenea.

# (4)

1. Enyi wanaadamu, abuduni wote Mola wa ulimwengu aliye enzini.

2. Wala usiweke kiumbe pa fasi ya muumba wako.

3. Wala usifanye zihaka katika ibada usije ukaangamia.

4. Wala kuimba na kucheza sio kusali, wala mlio wa vyombo vya mziki sio dhikri.

5. Kila ibada iko na kawaida yake ambae Mola wenu kawafunzeni.

6. Kumsifu Mungu katika nyimbo ni jambo nzuri sana, lakini iko na fasi yake pia na wakati wake, katika mpango maalumu.

7. Watu wasio abudu vilivyo ni wale wasio amini vilivyo wameamini sehemu na wamepinga sehemu ya ujumbe wa Mola wao.

# (5)

1. Ushindi ni wake Mwenyenzi Mungu, mkamilifu, anaye miliki vyote ulimwenguni.

2. Vyote huanzishwa naye na vyote hukomeshwa naye.

3. Ni yeye peke yake anaye jua sababu ya kuumbwa kwa kila kiumbe.

4. Kumbi usimlaumu mola wako ajili ya kuumba kiumbe fulani.

5. Hakuna ukamilifu katika umbiko : kama uyu ni chukizo maishani mwako, nawe pia ni chukizo maishani mwa wengine.

6. Hayo hutokana na asili ya umbiko ambae ni upungufu, lakini Mungu aliwawekeeni silaha ya kuchora nayo upungufu.

7. Silaha hiyo ya nuru ndio neno la Mungu, ambae huchora pumzi kadiri ya roho takatifu.

# (6)

1. Ametakasika mwenyenzi Mungu, mjuzi wa kila kuumba.

2. Mwingi wa huruma anaye samehe watumishi wake kadiri ya toba zao.

3. Heri Mutu anaye acha makosa yake bila kuirudilia tena.

4. Jitihada ya kujenga imani itawale maisha yote.

5. Sala na dhikri ifanyike kila siku popote ulipo ,ili nafsi yako ijae nuru ya Mungu.

6. Mola wenu ametosheleza haja ya kila kiumbe wala hakuna msaada badala yake.

7. Mungu wa miujiza anaye tenda kwa idhni : mumilki na mshindi aliye na uzima.

# (7)

1. Ametakasika Mwenyenzi Mungu, mwokozi,anaye jaa mamlaka ya kila namna.

2. Kauli yake imeokoa wote wanao itumia kama dira ya maisha.

3. Zoezi ya kuisoma kauli yake hii kila mara kadiri ya dhikri inaleta heri ya kila namna kufatana na manuizi.

4. Hakika amefaulu kabisa mutu anaye hifadhi moyoni mwake sura na aya kadhaa ambae huisoma kila mara.

5. Ujumbe wake ndio nuru kubwa ambae huondoa ujinga unao tokana na vitimbi vya shetani.

6. Nuru yake ni elimu ambae huteketeza ujinga, ndio maana ni sharti kutumia neno lake ili mupate kuzingatia bayana uzima wake.

7. Hakuna kimbilio ingine badala yake, bwana wa majeshi anaye miliki vitu vyote.

# (8)

1. Utukufu ni wake Mwenyenzi Mungu, mlinzi mwema, anaye tosheleza haja zote wakati wote.

2. Pasipo msaada wake hakuna ambae angeli okolewa,Mola wa karne na karne,muhifadhi wa milele.

3. Ametenda yote kwa idhni yake, wala hazaufike kwa kufanya shuruli yoyote.

4. Milki yake ni juu ya vitu vyote, hakuna mfano wake wala Diko mwenzake,wala jerani yake.

5. Amestawi milele kiushindi tafauti na kuishi, m'bora wa kuenea kadiri ya uzima.

6. Hana mwanzo wala mwisho, wa pekee anaye kamilika.

7. Hakika utukufu wote unamustahili yeye peke yake, wala hakuna mwengine kama yeye,wa muujiza aliye juu.

# (9)

1. Enyi wanaadamu ! ,ingieni wote katika dini ya Mungu.

2. usilimu ndio usalama wa nafsi katika mapenzi ya Mungu.

3. Atakaye kataa kusilimu amekataa kuingia katika dini ya Mungu.

4. Hatua ya kwanza katika usilimu ni shaada.

5. Kukiri moyoni na kushaidilia waziwazi kwamba Mungu Mwenyenzi ni m'moja tu,hakuna mwengine kama yeye.

6.Na hatua ya pili ni kupokea ujumbe wake wote na kuutumia maishani.

7. Mwenyenzi ndio mkamilifu anaye tawala angani na ukiwani, baba wa salama aliye salama milele na milele.

# (10)

1. Amejaa utukufu Mwenyenzi Mungu,mkamilifu anaye jitenga na upungufu wote.

2. Kutenda kwake sio sawa na kutenda kwao viumbe. Hawa hutenda kizaifu na yeye hutenda kimilki.

3. Kwa wao kuzingatia uzima wa Mungu ilibidi wa pewe ujumbe wake kadiri ya kusema kwao.

4. Matendo yote ya viumbe ni katika upungufu, hayapatikane kamwe katika ukamilifu.

5. Kama kutenda kwake hufananishwa sio ila namna ya kusikilizisha ili mupate kutimilika.

6. Kuona kama lugha ni umbo, ndio maana hakuna lugha ya Mungu.

7. Na kama Mungu Angeli kua na lugha fulani bila shaka angeli kua na umbo fulani, lakini mutukufu wa daraja amejitenga mbali na uzaifu huo.

# (11)

1. Mwenyenzi Mungu ndio tumaini la wanahewa wote, mlinzi wa maisha.

2. Mtukufu wa kauli anaye jaa milki kamilifu ambae huongoza wote kwa njia ya neno lake.

3. Ole wao wanafiki wanao geuzageuza neno la Mungu, wamefikia hata kubadiri maana ya andiko kwa kuzingizia tafsiri ya kiroho.

4. Hafahamu mambo ya kiroho ispokua aliye jazwa roho takatifu.

5. Tafsiri ya neno la Mungu pasipo ufunuo ni uwongo mtupu.

6. Wameangamia wote wanao jidai unabii pia na utume kwa ugumu wa nyoyo zao na ilihali hawakufunuliwa na Mungu.

7. Tumieni wote kweli yake hii na hekima : musiongeze wala musipunguze.

## (12)

1. Mwenyenzi ndio mufalme wa siku ya kiyama,hakuta bakia ispokua enzi tukufu peke yake.

2. Nani anaye kanusha matukio ya kiyama ? Hakika ni upumbafu kushakia kauli ya mjuzi wa yote.

3. Mungu ndio mkweli wa kauli,hasemi ispokua ukweli peke yake.

4. Siku hiyo Mwenyenzi atawafufua wote wapumuao baada ya kuwauwa.

5. Kufufua sio tendo la ajabu kuzidia kuumba:hakuna kigumu kwake yeye aliye na milki kamilifu.

6. Atakapo idhinia jambo ndipo hutukia kwa rafla jambo hiyo sambamba na idhni yake.

7. Siku hiyo ndio siku ya malipo kila mutu atavuna Yale ambae alipanda.

# (13)

1. Tumsifu Mungu aliye na ujuzi wa kuumba, mufalme wa ajabu tafauti sana na kila kitu.

2. Kutokeza toka sifuru ni tendo la ajabu ambae hufanyika na mwenyi ukamilifu.

3. Mpungufu hana uwezo wala fahamu ya kutokeza toka sifuru sababu amekumbwa na uzaifu mkubwa.

4. Heri Mutu anaye nyenyekea mbele ya muumbaji wa pumzi na mwili.

5. Hakika mamlaka yake ni kubwa zaidi ambae hutenda kwa idhni bila kutumika kazi.

6. Ombeni yote kwake mumilki, utapewa kwa wingi bila hesabu,kimwili ao kiroho.

7. Mwenyenzi ndio tajiri wa vyote, mwenyi uwezo wa vyote, hakuna mwengine kama yeye.

# (14)

1. Mwenyenzi Mungu ndio mufalme wa ajabu anaye zidia wote ulimwenguni.

2. Hakuna mfano wake popote kwani yeye tu ndio mkamilifu wengine wote ni wa pungufu.

3. Ole kwao wapumbafu ambae humlinganisha muumba na kiumbe fulani.

4. Hakika anaye muita mjumbe wa Mungu kua ndio Mungu wake ni sawa na kafiri anaye abudu sanamu.

5. Mungu hagusanake na umbo yoyote wala hageukake hali wala hapumuake hewa.

6. Ukamilifu wake humtenganisha na kila kitu, hawezi kujumuika mbinguni wala hadezeni wala duniani.

7. Kwa yeye kuketi maala fulani inabidi vyote vilio kutwa huko vipotee namna ya kukosekana, maana milki yake kamilifu hufuta upungufu wote kandokando yake.

# (15)

1. Uzima wa Mungu ni muujiza wa maajabu : ametangulia kimuujiza na ameumba kwa maajabu.

2.. Mola anaye stawi katika dhati yake mwenyewe hali ya kua Mwenyenzi.

3. Ukaona kiumbe kinacho ishi mbinguni kiumbe hicho ni mwanahewa_halisi.

4. Na kinacho ishi duniani bila shaka nimwanahewa_haramu.

5. Na vivihivyo pia kinacho ishi hadezeni ni mwanahewa_haramu.

6. Usilinganishe umbo yoyote na Mola wa ulimwengu ,hafanane na yeyote wala chochote.

7. Hakika mola wenu ni tafauti sana na kila kitu : yeye ni mkamilifu na wengine wote ni wapungufu.

# (16)

1. Ametakasika Mwenyenzi Mungu, chemchem ya baraka ambae hupatiana sifa na heshima kwa amtakaye.

2. Usiku ni wake na mchana ni wake, ameona muda wote pahali pote, wala hapitiwake na chochote.

3. Uhai na kifo hutokea kwake, ni yeye anaye fufua wafu kwa neno litokalo kwake na kumjaza roho takatifu amtakaye.

4.. Hakuna mwengine kama yeye ,muumba wa anga na ukiwa atawalaye Milele na milele.

5. Ombeni idhni ya Mwenyenzi ipate hufanyika maishani mwenu.

6. Hakika idhni yake juu ya jambo fulani, ni utimilifu wa jambo hiyo.

7. Ee Mola wangu ! Unizidishie elimu,na unizidishie nuru na unizidishie riziki,yote kadiri ya idhni yako.

# (17)

1. Mwenyenzi Mungu ndio taa ya ulimwengu, mjuzi wa mambo yote.

2. Ndiye msimamizi wa kila kitu, mwenyi mamlaka isiyo pungua wala kuongezeka ajili ya kuenea.

3. Muanzishaji na mkomeshaji ,aliye pasipo yeyote milele na milele.

4. Ole wake yule asiye zingatia uzima wa Mola wake.

5. Tumieni utaalamu kifikara ili upate kuzingatia njee ya mwili.

6. Akili ndio macho ya kiumbe ambae huzingatia kiroho

7. Yeyote asiye zingatia kiroho hana akili ndio maana hana imani.

# (18)

1. Utakatifu ni wake Mwenyenzi Mungu, mfariji,anaye ruzuku kila kiumbe.

2. Mungu wa miujiza anaye tenda kwa maajabu.

3. Mlinzi mwema anaye tosheleza haja za waja wake, anaye rehemu na anaye kirimu.

4. Alikua, yuko na atakua,mwenyi kuenea.

5. Mtukufu afanyaye apendavyo,hakuna wa kumsambisha wala wa kumuhukumu.

6. Upende haupende upo chini ya mamlaka yake, mteza nguvu, aliye na uwezo wa kuenea.

7.. Bingwa wa mabingwa anaye miliki falme zote  ulimwenguni, wa pekee aliye juu.

# (19)

1.Shukrani kwa Mwenyenzi Mungu, mpanaji wa pumzi, anaye kadirisha maisha ya kila kiumbe.

2. Umri ni zawadi kutoka kwake yeye anaye patikanisha kwa idhni bila kutaabika na kazi.

3. Hakuna mbele yake wala nyuma yake, mtangulizi wa milele.

4. Tajiri wa vyote, anaye pagaa watumishi wake mafuta ya kiroho na kuwapandisha katika daraja.

5. Chemchem ya nuru ambae humulika ulimwenguni.

6. Hana baba wala mama,si mwanaume wala si mwanamuke, hana ukoo wala Kabila ...

7. Hafanane na yeyote maana yeye ndio mkamilifu wengine wote ni wapungufu.

# (20)

1. Mwenyenzi Mungu ni uzima kadiri ya ukamilifu.

2. Mamlaka yenyi kuenea katika yote itokezayo kwa idhni ambae hakikuwa popote.

3. Dhati yake ni uwezo wa vyote, namna ya kuenea katika yote.

4. Mtukufu wa ajabu asiye kurubiwa na uzaifu wowote, Mutakatifu aliye peke yake enzini.

5.Hakuna mwengine kama yeye ,mzima, anaye tangulia katika yote imara na daima.

6.. Mumilki wa anga na ukiwa, kiongozi pekee wa jumla ya viumbe.

7. Mola wa pekee anaye stahili kuabudiwa, mwenyi milki kamilifu, anaye kirimu wanahewa wote na wazila hewa wote.

# (21)

1. Kitabu hiki ni ufunuo kutoka mbinguni, ukweli usio na shaka.

2. Maneno yake huletewa na malaika saba,kila yule na ujumbe ambae hujenga kweli moja.

3. Mungu amefanya mawasiliano baina ya mbingu na dunia katika dhati yangu nipate kua muonyaji.

4. Uchoraji wa pumzi ufanyike katika maunganio ya anga na ukiwa ili mutu apate utimilifu.

5. Yeyote atakaye tumia kauli tukufu ya kitabu hiki pumzi yake itafanyika roho takatifu.

6. Kuzingatia uzima wa Mungu ndio kumuona Mungu, yeye hazingatiwe kimwili sababu hana mwili.

7. Mwili ni umbo zaifu sana, ujinga mtupu, kadiri ya uchafu ambae haumkurubie kamwe mtukufu aliye enzini.

# (22)

1. Shukrani yote inamustahili Mwenyenzi Mungu, mkamilifu, anaye chagua miongoni mwa watumishi wake na kumtuma atakaye.

2. Masingizio na mazarau ya makafiri na wanafiki haiwezi kubadiri chochote katika neema ya Mungu iliye juu ya shahidi wake.

3. Yule ambae Mungu amemtukuza ,hakuna atakaye weza kumzalalisha.

4. Na yule ambae Mungu amemzalalisha hakuna atakaye weza kumtukuza.

5. Kinacho tatiza watu sana ni chuki na kiburi, hawataki kavumu ya mutu mwengine.

6. Ole wao makafiri na wanafiki wanao wa tungia uwongo mitume, hakika hadeze ndio makao yao,humo itakua ni kilio na kusaga meno.

7. Heri wanyenyekevu wanao pokea ujumbe kwa furaha, hakika wao ndio vyombo halisi vya mchoraji ,watarithi bustani ya neema kwa kishangwe.

# (23)

1. Neno la Mungu ni mfano wa maji Safi,na ibada ni mfano wa matumizi yake.

2. Uchafu wa shetani ambae hujaribu kunajisi watumishi wake hutakaswa na neno la Mungu katika ibada.

3. Tegemeeni kwa Mola wenu katika shida yote, hakika hakufanyike lolote ispokua kwa idhni yake.

4. Kuto kua urakibuni pia na kukosa tumaini ya Mungu ndio mambo ambae hutenganisha watu na karama ya Mola wao

5. Neno la Mungu ni kinga na utajiri maishani,jikingeni kwa kuisoma aya zake kwa wingi.

6. Na itumieni aya zake kama chakula pia silaha ya kuteketeza falme za giza zinazo taka kujiinua.

7. Kauli tukufu ya kitabu hiki imeleta nguvu na ushindi kwa yule anaye isoma kila mara.

# (24)

1. Mwenyenzi Mungu ndio tumaini la walimwengu ambae hulea viumbe vyote kwa usawa.

2. Ni amri kumuabudu kila siku asubui na jioni na kumtukuza usiku na mchana.

3. Wanafiki wameabudu kwa udanganyifu na ilihali moyoni hakuna hata chembe ya imani.

4. Abuduni Mungu kwa moyo wako wote na nia ya kupata wokovu hiyo siku ya mwisho.

5. Uwe katika usalama ama katika magumu,simama imara, usibadirike sababu ya vitimbi vya dunia.

6. Mola wako atakuvika taji la utukufu,na kukuweka katika kundi ya walio heshimishwa.

7. Tumainia Mungu peke yake katika shida zote ,wala usimchanganye na yeyote wala chochote

# (25)

1. Mwenyi enzi ni tafauti sana na kila kitu, hakuna mfano wake popote ulimwenguni.

2. Yeye sio umbo maana kila kilicho umbwa ni kipungufu.

3. Amepatikana kadiri ya kuenea, mtukufu anaye zidia wote kwa jumla.

4. Mshindi anaye kamilika bila mwanzo wala mwisho.

5. Ukamilifu umetokana na Enzi ambae ni uwezo wa vyote na pia ujuzi wa vyote.

6. Kuweza yote na kujua yote ndio kumiliki vyote.

7. Hakika Mwenyenzi Mungu ni mshindi juu ya kila kitu ,mufalme wa ulimwengu.

## (26)

1. Uzima ni wake Mwenyenzi Mungu, mtukufu anaye kamilika milele.

2. Mola ndio mwanzo wa vyote, chemchem ya kila fahamu.

3. Mfano wa taa ya ulimwengu, mwenyi kujua yote.

4. Elimu yote hutokea kwake, anaye patikanisha na anaye kosekanisha.

5. Usimlaumu mola wako kwa lolote yeye anaye kamilika katika busara.

6. Hauzingatie chochote ispokua kwa ruhusa yake.

7. Mola wa miujiza anaye jaa mamlaka ,hakuna mwengine kama yeye,wa pekee aliye juu.

## (27)

1. Enyi wanaadamu ! Aminini Mungu ukweli wa kuamini.

2. Kua na imani ni kua katika mapenzi ya Mungu.

3.Kutumia maamrisho yake na kujitenga mbali na makatazo yake.

4. Mungu amewaalikeni wote katika nuru yake ndani ya dini yake.

5. Mujichugulie fadhila nyingi kutoka kwa Mola wenu.

6.. Mungu ndio tajiri wa vyote anaye ruzuku wanahewa wote, hakuna maisha pasipo msaada wake.

7. Hakika mwokozi ni Mungu peke yake, wala hakuna mwengine kama yeye wa milele aliye juu.

# (28)

1. Ujuzi ndio chemchem ya umbiko ulimwenguni.

2. Mjuzi ndio mtokezaji wa kila umbo, la wazi na la siri,kadiri ya mwanzo wa vyote.

3. Hakuna kisicho kua chake,angani na ukiwani, tajiri wa vyote, m'bora wa kuumba.

4. Ni yeye aliye kutwa hapo awali tayari amekwisha Tangulia bila msaada wa yeyote.

5. Mwenyi uzima, anaye jaa milki kamilifu, kiongozi pekee wa jumla ya viumbe.

6. Amepatikana kadiri ya kuenea bila maanzio wala makomeo,jalali ulimwenguni.

7. Hakika Mungu ni mkubwa sana, tegemeo na kimbilio la wa silimu.

# (29)

1. Sauti ya Mungu ni yenyi mamlaka ya ajabu, yenyi kutimiliza kwa rafla jambo anaye idhinia.

2. Mungu hasemake kifikara Bali yeye husema kiujuzi,hali ya kuenea katika fahamu.

3. Kusikia sauti ya Mungu ni neema ya kukutana na wokovu.

4. Ametakasika kabisa yule aliye msikia Mola wake ,maana ameingia katika nuru yake.

5. Mutu anaye sema na Mungu ni mwenyi kuinukia;laiti mungeli muzingatia Nabii Mussa.

6. Kuzungumuza naye ndio kukurubishwa sana naye, zaidi ya wengine wote.

7. Amejumuika katika sehemu ya kwanza ya bahadhi la juu angani.

# (30)

1. Ushindi ni wake Mwenyenzi Mungu, hakimu mkamilifu.

2. Mtukufu anaye tenganisha adili na batili pasipo kasoro.

3. Ni yeye atakaye ingiza makafiri hadezeni na kuwakosekanisha baadaye.

4. Na ni yeye atakaye waingiza waaminifu mbinguni na kuwapatia maisha ya milele.

5. Amekufuru yeyote anaye kanusha moto wa jahanamu,bila shaka hadezeni ndio motoni.

6. Kadiri moto unavyo poteza kuni,ndivyo pia hadezeni inavyo poteza umbo.

7. Hakika sifa zote zina mustahiki Mwenyenzi Mungu ,muumba wa viumbe vyote.

## (31)

1. Mungu amestawi juu sana mbali na viumbe vyote, hakuna jerani yake.

2. Ukamilifu wake umemtenganisha kabisa na upungufu wa aina yote.

3. Ametangulia kadiri ya kuenea, hakuna alipo anzia wala alipo komea.

4. Enzi yake imewaka na kurarua upungufu wa aina yote kandokando yake.

5. Mamlaka yake imetawala pahali pote ulimwenguni, wala hatumikake kazi kwa kutenda.

6. Mapenzi yake hutosheleza kiutendaji,hodari aliye na starehe ya ajabu.

7. Hakuna Mola mwengine kama yeye,mwokozi, anaye rehemu na anaye kirimu.

# (32)

1. Aliye arshini haonekanake kimwili sababu ya kutokua na mwili.

2. Macho ya kimwili hayazingatie ispokua miili peke yake.

3. Kumbi usitumie macho ya mwili wako kwa kutaka kumuona kimwili sababu yeye hana mwili wala pumzi.

4. Mutu hawezi kumuona Mungu kimwili , Mola wenu ni tafauti kabisa na umbo zote ,wa pekee aliye enzini.

5. Mungu hana mwili wala pumzi, na ndio maana haiwezekane kumuona ana kwa ana maana yeye ni wa pekee.

6. Kukosa mwili na pumzi sio kukosekana Bali kuko hali ingine tukufu ajabu tafauti kabisa na umbiko,inayo itwa Enzi kadiri ya uzima wake Mungu.

7. Ni kawaida kumtazama Mungu kiroho ili upate kuzingatia uzima wake, ndio maana mutu hawezi kuamini ispokua aliye na akili.

# (33)

1. Enyi walio amini ! Fanyeni ibada kwa wingi ili mupate kujazwa nuru ya Mungu .

2. Aliye na nuru ya Mungu huzingatia bayana uzima wa Mungu, maana yeye ni katika mapambazuko .

3. Amefunuliwa wazi_wazi siri ya ufalme wa mbingu, akiwasiliana na wa takatifu wa mbinguni.

4. Ndio maana mitume wa Mungu ndio mashaidi wa uzima wake humu duniani.

5. Ni amri kwa kila mutu kumuamini Mungu Mwenyenzi na pia kuwaamini mitume wake wote.

6. Kila mtume iko na kitabu, yaani iko na maneno aliyo funuliwa na Mungu.

7. Hakuna mjumbe pasipo ujumbe, wala hakutumwa yeyote pasipo elimu ya neno la Mungu.

# (34)

1. Mwenyenzi ni mwenyi mamlaka ya ajabu, ametenda yote, zaidi ya wote, pahali pote.

2. Hazaliwe wala hakufe yeyote pasipo ruhusa yake.

3. Uwingi wa viumbe haumusumbue kwa kutosheleza haja zao, tajiri wa vyote.

4. Milki kamilifu hutimiza mambo yote kwa rafla, bila kutumika kazi.

5. Hakuna wa kumfichama wala wa kumponyoka,maana uwezo wake umezienea anga na ukiwa.

6.Daraja yake hailingane na yeyote, mshindi, anaye kusanya vyote katika ujuzi wake.

7. Hakika mwenyenzi Mungu ni mkubwa sana, bwana wa mabwana, hakuna mwengine kama yeye.

# (35)

1. Mola wa ulimwengu ndio tegemeo la haki,amekua yote katika yote, mwenyi kutosheleza.

2. Katika shida yote, weka tumaini lako kwa Mungu, mapenzi yake ikafanyika tu shida yote humalizika.

3. Ametibu magonjwa isiyo tibika na watu, mganga mkamilifu, anaye umba kila magonjwa na dawa yake.

4. Kisomo kitukufu kadiri ya dhikri ,katika kitabu hiki ,ni tiba ya kila magonjwa.

5. Uchache wa imani ndio jambo ambae husababisha uzaifu wa kila aina pia na majaribu.

6. Juhudi ya ibada katika urakibu inaleta wokovu maishani mwa watu.

7. Muweza wa vyote ni Mungu peke yake, tumkimbilie na tumaini letu lote katika mambo yetu yote, hakuna mwengine kama yeye.

# (36)

1. Mwenyenzi ni mufalme wa ulimwengu mwenyi uwezo wa ajabu.

2. Amepatikana kadiri ya kutangulia bila mwanzo wala mwisho.

3. Ni ajili ya kua na milki ya ushindi, ndio maana amekamilika mbali na upungufu wote.

4. Kua na mwanzo pia na mwisho ni kua na upungufu, namna ya kuto kamilika.

5. Utukufu wa kujua yote na kuweza yote ndio unao mfanya aeneane katika yote hali ya kua mwanzo wa vyote.

6. Hakuna Kitakacho mtokeza yeye aliye tangulia vyote, wala kitakacho mkomesha yeye anaye kamilika katika yote.

7. Hali yake hii ya kuenea ndio uzima ambae ni umungu, bingwa mshindi anaye miliki vitu vyote.

# (37)

1. Enyi walio amini ! Mtukuzeni Mungu na kumshukuru kwa wingi ajili ya neema aliye wapeni.

2. Kuamini Mungu ni neema kubwa, hakuna bahati maishani zaidi ya kufikiwa na imani moyoni.

3. Hakuna mwenyi akili kumzidia yule anaye amini uzima wa Mungu.

4. Asiye amini Mungu ni sawa na mnyama ambae hukosewa akili.

5. Kule kutokua na utaalamu kifikara, ndio humfanya ashindwe kuzingatia kiroho.

6. Yeye ni mfano wa kipofu ambae uzingatiji wake hukomea katika mwili, hawezi kutazama kiroho.

7. Kama angeli kua na akili bila shaka angeli mzingatia Mungu Mwenyenzi, baba wa siri aliye kwa siri.

## (38)

1. Ulimwengu ni jumla ya sehemu tatu :Enzi, Anga na Ukiwa.

2. Wanahewa wote huzingatia ajili ya fikara iliye ndani ya pumzi zao.

3. Fikara yao huzidiana kulingana na umbile zao.

4. Pumzi isiyo changikana na chochote ni kubwa tena bora zaidi ya ile inayo changana na mwili.

5. Ndio maana wanahewa_halisi ni pumzi takatifu, kubwa tena yenyi utaalamu kifikara ambae huzingatia  vema zaidi ya wenzao.

6. Amezingatia bayana mbinguni, hadezeni na duniani na hata kuzingatia njee ya umbiko, enzini, ajili ya kupatikana na macho ya kiroho inayo itwa akili.

7. Mutu atakaye jazwa pumzi halisi atakua na ginsi ya kuzingatia umbiko na pia muumba wake.

# (39)

1. Mutu anaye silimu ni mfano wa nuru inayo meremeta ,amezaliwa upya kiroho.

2. Amejaaliwa neema yakujumuika katika hesabu ya wanyenyekevu ambae hufanikiwa na jaza la mbinguni.

3. Muumba wa anga na ukiwa ni mwingi wa rehema,msaada wake hutarajiwa na wote wanao pumua.

4. Ibada ndio charamata ya nuru, kila anaye abudu Mungu vilivyo hukurubiwa na roho takatifu.

5. Hakuna aliye mwema kama vile Mungu mwenyi rehema ya kuenea.

6. Heri mutu anaye mshukuru kwa kila jambo, kila ulicho nacho ulipewa na Mungu.

7. Hakika nampenda Mola aliye ni umba, bila yeye kama mimi si chochote.

# (40)

1. Mola wangu amenipa kazi ya kutangaza habari ya uzima wake.

2. Watu wengi hawana yakini na uzima wake, wamejaa mashaka ajili ya kutomzingatia kimwili.

3. Wengine wanasilimu kwa udanganyifu na ilihali hawana yakini (na uzima wake ) moyoni.

4. Atakaye amini ujumbe huu,bila shaka atakua yakini kwamba Mungu yupo na atajazwa roho takatifu itakayo mfanya aishi milele.

5. Katika daraja ya kiroho mimi ni walii wa Mungu.

6. Na katika kazi ya kiroho mimi ni mjumbe wa Mungu Mwenyenzi.

7. Hakika shukrani zote zinamustahili Mwenyenzi Mungu, mufalme mwema, anaye jua yote na anaye weza yote.

# (41)

1. Ametakasika Mwenyenzi Mungu, Mola wangu na Mola wenu pia na Mola wao.

2. Mungu wa ma nabii na mitume wote, chemchem ya upatikanaji wote na maisha yote.

3. Aliye mtuma Ahmad ili asadikishe qur'ani na pia atabiri ujio wa Kalonda.

4. Hakika Ahmad ni mjumbe wa Mungu aliye kuja baada ya Nabii mutukufu Muhammad ,kabla ya kuzaliwa kwake Kalonda; asema roho wa Mungu.

5. Mutu anaweza kua Nabii na ilihali yeye sio mtume, na pia anaweza kua mtume na ilihali yeye sio Nabii.

6. Na mwengine anaweza kua Nabii pia mtume, na ndio mutukufu zaidi : kama vile ,Mussa ,Yesu masiya, na Muhamadi...

7. Mtume asiye kua Nabii ni miongoni mwa mawalii watukufu.

# (42)

1. Musifuni yeye aliye umba kila kitu, mtegemewa ,anaye sitiri kila nafsi, angani na ukiwani.

2. Maisha pasipo nuru yake haiendelee lakini hukoma,maana giza ni mfano wa uchafu ambae huchafua nafsi.

3. Aliye nuruni hufikiwa na heri nyingi na aliye gizani hufikiwa na shari ya kila namna.

4. Nuru imeleta usalama ajili ya uzuri wa malaika na roho.

5. Na giza imeleta hasara ajili ya ubaya wa Shetani na muzimu.

6. Amefaulu kabisa mutu anaye amini mjumbe wa Mungu, ijapokua hafafanue baina ya Nabii na Mtume.

7. Kinacho hitajika ni imani, mutu anaye kubali ujumbe wa Mola wake hujazwa nuru ya mbinguni.

# (43)

1. Mponyaji ni Mungu peke yake, mganga wa magonjwa yote, wala hapone yeyote ispokua kwa idhni yake.

2. Ee Mola wangu ! Uniponye kwa rafla kadiri ya idhni yako ibakie ishara kwa watu watakao kuja nyuma.

3. Na unikinge na kila uchawi:wakutia na wakupuliza,hakika wewe ndio mujibu wa dua.

4. Mungu ndio ukingo wangu ngao ya miujiza anaye ni kinga na hatari ya kila namna, usiku na mchana.

5. Watu wa dunia hawamsadiki Mungu ila kwa mashaka na ndio sababu wamekanusha ujumbe wake.

6. Ondoeni mashaka ,enyi watu wa dunia, kwa nini hamuamini na hali mumezingatia?vyote munavyo viona vilifanyika naye bila msaidizi.

7. Amepatikana kadiri ya kuenea, bila maisha wala mauti,bila kimo wala kipimo,lakini mkamilifu awezaye na ajuaye.

# (44)

1. Enzi, Anga na Ukiwa ndio hujenga ulimwengu.

2. Enzini hupatikana utukufu wa ajabu, ukamilifu kadiri ya uzima.

3. Na Anga ndio kambi la Hewa, maala penyi shuruli ya kila namna ambae hupatikana maisha.

4. Na Ukiwa sio sifuru lakini utupu kimwili kadiri ya ganda,umbo isiyo Linda pumzi ndani mwake.

5. Aliye Enzini hafanane na yeyote, yeye ndio mkamilifu lakini wengine wote ni wapungufu.

6. Mungu hafanane na yeyote wala chochote, amepatikana kadiri ya kuenea.

7. Mamlaka yake ni juu ya kila kitu, mteza nguvu anaye zidia kushinda,wa miujiza aliye juu.

## (45)

1. Mwenyenzi Mungu peke yake ndio mwenyi kuenea katika tendo kua hali ya kua mzima.

2. Kupatikana ao kujumuika ao kuishi sio kua na uzima.

3. Unaweza kupatikana namna ya kujumuika ulimwenguni na ilihali hauna uzima.

4. Kua na uzima ni kua na ukamilifu, namna ya kuenea kimllki na kibusara,yaani kuweza yote na kujua yote.

5. Wala kuishi sio kua na uzima maana sio kukamilika.

6. Anaye ishi ni yule anaye pumua hewa yaani yule anaye fikiri.

7. Shuruli ya aina yote ni uzaifu na ndio maana ni kwao viumbe, haipatikane kwa Muumba kamwe.

## (46)

1. Neno la Mungu ni nakala ya ufunuo ambae hujaa kweli.

2. Ni ujumbe wa mjuzi ambae ndani mwake hamna kasoro wala doa lakini ukweli usio na shaka.

3. Kila atakaye tumia neno lake, atakua mtaalamu ,mwenyi nguvu ya ushindi .

4. Mungu atafumbua macho yake kwa kumjaza nuru ya mbinguni.

5. Pumzi yake itakomazwa na roho takatifu na ndio maana ukaguzi wa andiko itakua jambo raisi kwake.

6. Mengi ni mafumbo ambae hudai tafsiri, na pia mengi ni wazi_wazi, ndio maana hudai mwenyi akili.

7. Kutumia neno la Mungu ndio kutumia nuru ya Mungu namna ya kujitenga na giza.

# (47)

1. Mwenyenzi yupo,ndiye mwenyi uzima katika ulimwengu.

2. Amepatikana kadiri ya kuenea hatua na upungufu wa aina yote.

3. Mungu hawezi kujumuika na vitu vizaifu asije kulingana nao katika kuzaufika.

4. Mola wenu ni yote katika yote zaidi ya yote kuliko wote, mufalme wa wote.

5. Macho yako haiwezi kumuona ana kwa ana,sababu ya kua tafauti sana naye.

6. Wewe ni mwenyi mwili na pumzi, lakini yeye hana mwili wala pumzi.

7. Amepatikana katika upekee,njee ya Anga na ukiwa, katika utukufu usio kurubiwa na yeyote, Enzini.

# (48)

1. Macho ya mwanaadamu haizingatiake vitu vyote vilivyomo ulimwenguni.

2. Sio kwamba jumla ya vitu unavyo viona ndio walimwengu wote.

3. Kuko aina nyingi ya viumbe ambae mwanaadamu hazingatiake bayana, utazamaji kimwili ni wenyi uzaifu mkubwa.

4. Mwilini hamna ispokua ujinga mtupu, na ilihali ujinga hauzingatiake Bali hupitiwa.

5. Viumbe vyenyi kua karibu naye angani na ukiwani hawezi kuzingatia vyote bayana kefule yeye mshindi aliye njee ya umbiko ! .

6. Hapana kujingikiwa ajili ya kuto mzingatia kimwili yeye asiye kua na mwili,tena aliye mbali sana na dunia.

7. Mola wenu amejifunua ku watu kupitia wajumbe wake ili watu wapate kuzingatia uzima wake.

# (49)

1. Mwenyenzi Mungu ni mumoja hana baba wala Mama, sio muzila hewa wala mwanahewa.

2.. Mungu hafanane na yeyote wala chochote katika ulimwengu, yeye peke yake ndio mkamilifu lakini wengine wote ni wapungufu.

3. Dhati yake ni tukufu ajabu, haigusanake na chochote wala haigeukake hali.

4. Kitu kinacho badiri hali ni zaifu,hubadirika ajili ya uzaifu wa kuto eneana.

5. Mungu hawezi kugeuka kiumbe, kua kiumbe ni kua zaifu.

6. Hasara ilio_je kwao wanao abudu mtume wa Mungu ! Wanamshirikisha Muumba na kiumbe alicho kiumba .

7. Ingawa kama hawata acha ibada hiyo ya sanamu,bila shaka wataangamia siku ya kiyama.

# (50)

1. Ametakasika Mwenyenzi, m'bora wa wanao bariki,mjuzi anaye geuza pumzi kua roho takatifu.

2. Mapenzi yake ndio msaada mkubwa ambae kutosheleza haja zote,mwingi wa rehema na mwingi wa ukarimu.

3. Mjuzi anaye kadiria maisha ya kila anaye pumua.

4. Alitangulia mwenyewe kadiri ya kuenea pasipo uzaifu wa kuanza na kukoma.

5. Kupatikana milele bila mwanzo wala mwisho ndio kukamilika hali ya kua na uzima.

6. Mungu ndio mwanzo wa vyote ambae huenea katika tendo kua, hakuna kabla yake wala baada yake.

7. Hakika ushindi ni wake Mwenyenzi Mungu aliye na uhuru : anaye miliki shuruli na wakati, m'bora wa kuenea.

# (51)

1. Mutu wa dunia amekanusha uzima wa Mola wake sababu y'a kupatikana pasipo kuanza namna fulani.

2. Hali hii ya kutangulia ndio ukamilifu, namna ya kuweza yote na kujua yote.

3. Kuanza ni uzaifu wa kua sifuru kabla yake ,na pia kukoma ni uzaifu wa kua sifuru baada yake.

4. Kua na mwanzo pia na mwisho ni kua mpungufu kadiri ya umbiko, ambae asili yake ni sifuru.

5. Kama italazimika kila yule kuanza namna fulani, ni kwamba imelazimika kila yule kuumbwa ,na ilihali haiwezekane viumbe kupatikana pasipo muumba kutangulia.

6. Muumba ni yule asiye umbika , anaye kamilika kimilki kinyume na uzaifu wa kushindwa.

7. Milki yake hiyo ya ajabu isiyo shindwa na chochote ndio inayo mkamilisha pasipo upungufu wa kuto kua muda fulani, na pia ndio inayo mfanya atokeze ambacho hakika popote.

# (52)

1. Ole wao wajumbe wa Shetani, ambae baada ya kutumia njia mbali mbali ya ushirikina ,hutumia kwa unafiki kitabu cha Mungu ili wa pate hanasa ya dunia.

2. Wamejidai unabii na utume na ilihali wao ni mishirikina .

3. Na wanapo piga ramli,watu wa dunia wamezani ni unabii.

4. Na wanapo fuma ufumu wao kwa kutibu ,watu wa dunia wamezani ni maombi.

5. Udanganyifu kama huo ndio mafunzo ya Shetani ili wapate kuwapoteza walio amini.

6. Alama yao ni kutowaletea watu "maneno ma takatifu, na ndio maana hawana vitabu kadiri ya nakala ya ufunuo wao.

7. Wamezingizia kusoma vitabu vya Mungu,na kudanganya kufanya ishara ndogo kutokana na muzimu yao, ajili ya upofu wa watu wa dunia.

# (53)

1. Umungu ni uzima, yaani ukamilifu.

2. Ni utangulizi kadiri ya kuenea katika yote.

3. Kutangulia vyote ndio kupatikana milele.

4. Na hapatikane milele ispokua yule asiye kua na upungufu (uzaifu) wowote.

5. Na asiye kua na upungufu wowote ni yule awezaye yote na ajuaye yote.

6. Na yule awezaye yote na ajuaye yote ndio mkamilifu, kadiri ya " mwanzo wa vyote "

7. Naye ndiye muanzishaji wa kila kitu aliye muumba wa vyote anaye itwa Mungu Mwenyenzi.

# (54)

1. Ametakasika Mwenyenzi Mungu, m'bora wa kuumba, aliye tokeza kila kinacho patikana ulimwenguni.

2. Milki yake kamilifu ni mamlaka ya ajabu ambae huhukumu kila upatikanaji na maisha ulimwenguni.

3 .Utukufu wake huu wa ajabu unamtenganisha na vitu vyote, hafanane na chochote wala hachangie fasi na yeyote.

4 .Amestawi katika utukufu wa dhati yake mwenyewe hali ya kua wa pekee.

5. Alitangulia kila kitu, namna ya kuenea kadiri ya uzima.

6. Hakuna kabla yake wala baada yake sababu ya kuenea namna ya kukamilika.

7. Hakika Mungu Mwenyenzi ndio mwenyi uzima, mufalme mkamilifu,hakuna mwengine kama yeye.

# (55)

1. Ujumbe wa Mungu ni mfano wa nuru ambae huondoa giza,yaani elimu ambae huondoa ujinga.

2. Atakaye kanusha ujumbe wa Mungu, atakua gizani siku zote wala hawezi kuzingatia.

3. Kila mara baada ya mtume, Mola wenu analetaka Mja nyuma ili kusadikisha ujumbe wake.

4. Roho takatifu anasaidiaka waaminifu katika njia mbali mbali,lakini sio kwa kuwapatia karibuni wote kazi ya utume.

5. Waaminifu na waubiri wote sio ma Nabii wala Mitume ,hapana kujidai unabii ao utume ajili ya kufanya kazi ya Mungu.

6. Dini ambae waubiri wote wameitwa ma Nabii ao mitume ni dini ya uwongo.

7. Ogopeni Mungu ukweli wa kuogopa,wala usimzingizie kwa lolote, wala usipinge lolote katika kauli yake.

# (56)

1. Ushindi ni wake Mwenyenzi Mungu, mtukufu wa daraja, anaye inukia walimwengu wote kwa jumla.

2. Ameteremsha nuru yake hii katika umati huu ili ukweli upate kutawala duniani pote.

3. Ukafiri wa kukanusha uzima wa Mungu hauna tena fasi kwani uwongo umekwisha toweka.

4. Someni wote kitabu hiki ili mupate kuzingatia uzima wa Mola wenu.

5. Hakungeli patikana yeyote wala chochote bila Mungu kutangulia ulimwenguni, maana ndiye muanzishaji.

6. Mumilki asiye hitaji kwa yeyote, ambae wote huitaji kwake.

7. Alikua, yuko na atakua, mwenyi kuenea ; hakuna mwengine kama Mungu.

# (57)

1. Mola wa ulimwengu amekua yote katika yote kuliko vyote, m'bora wa kuenea.

2. Ukamilifu ni hali tukufu ajabu, uwezo wa vyote kadiri ya mamlaka ya milele.

3. Fikara ya viumbe ni fahamu ndogo sana, haiweze kukagua siri ya utukufu wa ujuzi.

4. Upungufu hauwezi kupatikana bila ukamilifu kutangulia, kamwe upatikanaji na maisha pasipo utangulizi wa uzima.

5. Hakika viumbe haviwezi kupatikana pasipo Muumba kutangulia, ndiye chemchem ya upatikanaji na maisha.

6. Pasipo Mungu kama sifuru ingeli tawala milele, maana kungeli kosekana mwanzo wa vyote.

7. Umungu ni utukufu wa ajabu tafauti sana na kila kitu, hakuna mwengine kama yeye.

# (58)

1. Abuduni Mola wa ulimwengu kila siku kwa kusali : asubui na mangaribi pia na usiku. Na umtukuze mchana kadiri ya uwezo wako.

2. Ni lazima kwa kila mutu kuonesha shukrani na heshima kwa Muumba wake Aliye juu.

3. Nabii Muhamadi alifundisha watu sala ili wapate kukurubishwa na Mola.

4. Mwalimu wa usilimu,aliye kua na silimusha watu kwa maneno na matendo.

5. Heri mutu anaye amini mjumbe uyu na kuitumia qur'ani kama chakula ya roho.

6. Mungu alimupa kazi kubwa katika nuru kubwa na kumpa heshima kubwa mbinguni.

7. Anaye silimu ndio anaye muamini,hatua ya kwenda mbinguni.

# (59)

1. Ametakasika Mwenyenzi Mungu, chemchem ya nuru, anaye angazia mitume na nuru itokayo dhatini mwake.

2. Kama alivyo mjaza yesu masiya nuru kubwa sana, na kumfanya umbo laini yenyi imani timilifu kadiri ya mapenzi yake.

3. Akamtakasa kadiri ya neno lake, na kumtukuza kadiri ya roho yake.

4.Mnyenyekevu na mpole wa moyo,hapazake sauti anapo sema ,lakini maneno yake imeikia ya wenzake.

5. Hiyo siku ya kiyama, bwana Yesu atasaga milima kuisawanisha ardhi sawa sawa, hakuta baki bonde wala kisuguu.

6. Hakika Yesu masiya ni bwana, mufalme mwenyi daraja kubwa na heshima kubwa sana mbinguni.

7. Anaye silimu ndio anaye muamini,hatua ya kwenda mbinguni.

# (60)

1. Enzi sio sifa yake Mungu, lakini dhati yake Mungu. Na dhati yake Mungu ndio umungu.

2. Hakuna kiumbe chenyi kua na Enzi ndani mwake.

3. Umungu ni katika upekee kadiri ya ukamilifu,hakuna wana_Enzi ispokua "Mwenyenzi" peke yake.

4. Ni kwamba habari ya Enzi tukufu ndio habari ya Mwenyenzi Mungu.

5. Katika umungu ndio Enzini, umoja tafauti sana na uwingi.

6. Hakika Mungu ni wa pekee, hachangie fasi na yeyote wala hafanane na chochote.

7. Yule atakaye mfananisha Mungu na mwanahewa ao muzila hewa, atakamatwa na kutupwa hadezeni, kadiri kapi inavyo ogotwa na kutupwa motoni.

# (61)

1. Dini ya Mungu ni usilimu,kuingia katika dini ya Mungu ndio kusilimu ,na anaye silimu ndio musilimu.

2. Dini ingine yote ni ya uwongo maana imetokea kwa yule mudanganyifu.

3. Mungu ni mumoja na dini yake ni moja, wala jumuiya la kidini sio dini ya Mungu.

4. Kila Nabii ao mtume anaye hubiria watu kwamba mwanakondoo wa Mungu ndio Mwenyenzi bila shaka ni Nabii ao mtume wa uwongo.

5. Dini ambae hawaabudu Mungu mwenyenzi ,wala hawaamini mitume, wala hawaamini siku ya kiyama ni dini ya uwongo.

6. Dini ambae hawashaidilie uzima wa Mungu ,wala hawasome sura za ufunguzi,wala hawasujudu katika sala, ni dini ya uwongo.

7. Kutoa shaada ndio tendo la msingi wa imani, na kusujudu ndio tendo la msingi wa ibada.

# (62)

1. Ujumbe wa Mungu umepatikana katika vitabu vyake vitukufu.

2. Vitabu vitukufu ni nakala ya ufunuo wa Mungu, sio fikara ya kibinaadamu.

3. Kitabu chochote kinacho andikwa pasipo kufunuliwa na Mungu sio kitabu kitukufu.

4. Neno la Mungu ni mfano wa maji ya kunywa ,ambae hupatikana katika kisima cha Mungu.

5. Kuona kama kisima kinaweza kuchafuka,ndio maana Mwenyenzi anatumaka wajumbe ili kusafisha kisima chake mara na mara.

6. Ole wao waandishi wadanganyifu,ambae huongeza ao hupunguza katika maandiko ma takatifu.

7. Tumieni wote kitabu kitukufu hiki, "ukweli" ambae Mungu mwenyewe kaushuudia,ili mupate kuokolewa.

# (63)

1. Kauli tukufu hii "ukweli" ni ujumbe wa Mungu ku watu wote.

2. Asiye amini Mungu ,na yule anaye amini Mungu, wao wote wamealikwa kusoma kitabu hiki ili wapate kuzingatia uzima wa Mola wa ulimwengu.

3. Kukosa yakini moyoni kunaleta unafiki katika imani.

4. Elimu ndogo inaleta uzaifu katika imani, na ndio maana matendo ya musilimu asiye kua na elimu haiachane na matendo ya kafiri.

5. Kama Mungu haonekane kimwili ni kwa sababu hana mwili, sio kwamba kukosa mwili ndio kukosekana.

6. Tazameni kiroho ili mupate kuzingatia uzima wa Mola wenu.

7. Mola wa ulimwengu sio mwili wala pumzi, lakini mwenyi "Enzi".

# (64)

1.Utukufu ni wake Mwenyenzi Mungu, mwenyi uzima, atanguliaye kadiri ya kuenea.

2. Kauli yake ni tukufu ajabu, imefadhilisha kila nafsi inayo itumia.

3. Atakaye mtukuza Mungu katika kuzisoma aya za kitabu hiki kwa wingi,atakua miongoni mwa wazaliwa wa sehemu ya kwanza ya bahazi la juu angani.

4. Sifa ya Mungu inayo andikwa katika kitabu hiki ndio tukufu zaidi,kifaa maalumu cha maisha.

5. Ni bora zaidi kufanya dhikri ya kisomo cha kauli hii hali ya kua na matendo mazuri,ili upate kuzingatia utendaji wa Mola wako bayana.

6. M'bora katika watu ni yule aliye katika mapenzi ya Mungu, hatakiwe amani mbinguni ispokua yule anaye takia watu wenzake amani duniani.

7. Kilicho muimu maishani ni mapendo :hamfitini ndugu yake ispokua yule asiye mpenda nduguye.

# (65)

1. Ushindi ni wake Mwenyenzi Mungu, mtukufu aliye na mamlaka ya ajabu.

2. Ndiye mneemeshaji ,anaye bariki mchaguliwa wake pamoja na uzao wake bila ukomo.

3. Ma Nabii na mawalii wanaweza kuzaa kimwili na pia wanaweza kuzaa kiroho.

3. Mungu ndio mkweli wa kauli,hakuna atakaye vruga mpango wake wala kuiba baraka yake.

4. M'bora wa kuumba anaye tokeza,kadiri ya matamshi yake, kila kitu kinacho patikana.

5. Ameporomosha ujumbe wake kwa kila umati maana yeye ni taa isiyo fifia wala kuzimika.

6. Mjuzi na mshindi anaye kadirisha kila kinacho fanyika ulimwenguni.

7. Hakuna mwengine apasaye kuabudiwa kwa haki ispokua Mungu Mwenyenzi peke yake.

# (66)

1. Mwenyenzi Mungu ndio chemchem ya nuru, kadiri ya taa ya ulimwengu.

2. Neno lake ndio nuru maishani,litumieni kwa kila jambo kauli tukufu ya kitabu hiki, ili mupate ushindi.

3. Heri mutu anaye amini uzima wa Mola wake ,na pia anaye amini neno lake na kulitumikisha katika kawaida yake.

4. Mungu Mwenyenzi atamjaza roho takatifu pamoja na malaika yule atakaye zoelea kusoma kitabu kitukufu hiki katika mpango maalumu.

5. Na atakapo ihama dunia, roho yake itapokelewa kwa shangwe mbinguni.

6. Jitengeni na mambo ya giza, wala usimtegemee Shetani,wala usikose kusilimu maishani mwako, wala usiritadi baada ya kusilimu.

7. Onesha shukrani yako kwa Mola wako aliye kuumba kwa bure na akakupatia neema ya kila namna kwa bure.

# (67)

1. Uwezo ni wake Mwenyenzi Mungu, mufalme anaye tawala Anga na Ukiwa milele.

2. Ni yeye peke yake anaye pana cheo kwa amtakaye,hakuna mamlaka kinyume na idhni yake.

3. Unabii na utume umetoka kwake, ameteremsha ujumbe kwa muja wake kuhusikana na majira ya umma wake.

4. Amekadirisha neno lake kulingana na ukaguzi wa watu wa ule umati ili wapate kuzingatia.

5. Mola wenu hawatakieni kamwe yaliyo mazito ispokua yaliyo mwepesi.hakika Mungu ni mwema sana na zaidi.

6. Roho takatifu ndio zawadi ya Mungu kwa watumishi wake, ambae husindikiza nafsi zao hadi utimilifu.

7. Ni karama ya Mungu kutoka mbinguni, ili walio silimu wasiangamie lakini wapate wokovu.

# (68)

1. Ametakasika Mwenyenzi Mungu,mwalimu mkamilifu anaye fundisha wanahewa wote kwa njia mbali mbali.

2. Ujumbe wake huu ni elimu ya namba ya juu inayo wa husu watu wenyi akili.

3. Utazamaji kiroho unafanya wazingatie duniani pia na inje ya dunia.

4. Ni mwenyi nuru ya Mungu, musilimu anaye soma sura ao aya kadhaa ya kitabu hiki kitukufu, usiku kama vile mchana.

5. Sema : Yesu masiya ndio simamizi la neno la Mungu, na Muhamadi ndio simamizi la ibada ya Mungu:umpende nani na umkatae nani?

6. Muaminifu wa kweli ni yule anaye amini Mungu na mitume yake wote pia na vitabu vyake vyote.

7. Hakuna mtume wa dini fulani wala Hakuna kitabu cha dini fulani,mitume wote na vitabu vyote ni vyake Mungu mumoja katika dini yake moja ya usilimu.

# (69)

1. Uzima ndio ukamilifu, ni uwezo wa vyote tafauti sana na uzaifu wote.

2. Mwenyi uwezo wa kumiliki kila kitu, hakuna mfano wake popote ulimwenguni.

3. Utukufu wa ajabu usio kadiriwa na yeyote ndio umungu, ushindi katika yote milele na milele.

4. Kulazimisha Mungu aanze mu namna fulani ni kulazimisha Mungu apungukiwe ao azaufike mu namna fulani.

5. Ni upofu wa kuto zingatia mwanzo wa vyote,hakungeli patikana chochote pasipo Muumba kutangulia ulimwenguni.

6. Milki kamilifu ndio mamlaka ya umungu ambae katangulia vyote bila msaada wa yeyote.

7. Utangulizi ndio ukamilifu kadiri ya uzima, mamlaka itokezayo kuujaza ulimwengu.

# (70)

1. Ametakasika Mwenyenzi Mungu, muhitajiwa ,anaye tosheleza walimwengu wote maala pote.

2.. Uwezo wake Mwenyenzi hauna kipimo ,ndiye mtokezaji wa mapya asiye dondoka wala kushindwa.

3. Mjuzi anaye jua yaliyo mbele yao na yaliyo nyuma yao, pasipo shuruli yoyote wala msaada wowote.

4. Alikua, yuko na atakua, mwenyi kuenea hali ya kua uzima.

5. Mtukufu asiye onekana kimwili, aliye tafauti sana na umbiko.

6. Pahali pake hakuna mwengine,Mwenyi kumiliki walimwengu wote milele.

7. Mwenyenzi Mungu ni mkubwa sana, chemchem ya upatikanaji na maisha, hakuna mwengine kama yeye.

-

## MULANGO WA TANO : NJIA YA MUNGU

# (1)

1. Utukufu ni wake Mwenyenzi Mungu, mkamilifu anaye jitenga na upungufu wote milele.

2. Mkweli wa kauli ambae tamko lake hutokeza kitu ambae hakikua popote.

3. Mutu atakaye amini na kutenda mema bila shaka ataingizwa mbinguni.

4. Na yule atakaye kufuru na kutenda mabaya ndio atakaye ingizwa Hadezeni.

5. Ole kwao wanao tumainia kuokolewa kwa neema, hakika kila mutu atavuna yale aliyo panda.

6. Kilicho muimu katika imani ni matendo mazuri.

7. Imani pasipo matendo mema ni unafiki mtupu.

8. Kila mutu analazimishwa kutenda mema, haimufae mutu ispokua matendo yake mwenyewe.

9. Matendo ya mutu mwengine haiingie katika hesabu ya mutu mwengine, ispokua mazao yake.

10. Kama unaingiza mutu katika dini, utapewa pia sehemu katika yale atakaye ya chuma ndani ya dini.

11. Na kama unaingiza mutu katika urozi, utapewa pia sehemu katika yote atakaye ya chuma ndani ya urozi ulio mupa.

12. Mitume wote walifanya kazi moja ya kuondoa watu kwenyi giza na kuwapeleka kwenyi nuru.

13. Kuamini mtume wa Mungu fulani ni kutumia mafundisho yake bila kuongeza wala kupunguza.

14. Atakaye ongeza ao kupunguza katika mafundisho yake, amemsea uwongo mtume wake .Na kumsemea uwongo mtume ni kumsemea uwongo Mungu aliye mutuma.

15. Mwenyenzi Mungu ni baba wa salama aliye salama, tendeni salama ili mupate usalama wa milele.

16. Mungu ni mkubwa sana, mufalme wa ulimwengu wote, asiye lingana na yeyote ajili ya ushindi.

17. Maagizo yake ndio nguvu inayo tokeza,hakipatikane chochote ispokua kadiri ya agizo lake.

18. Enzi inayo patikana ndani mwake ndio mamlaka yake ya ajabu ambae humiliki vyote.

19. Atakaye abudu Mungu vilivyo atajazwa nguvu ya ushindi ndani mwake, na kuinuliwa katika sehemu ya kwanza ya bahazi la juu angani.

20. Pumzi yake itajazwa nuru mfano wa mkaaji wa mbinguni, kinvuli cha Enzi tukufu.

21. Mungu Amestawi arshini kiupekee,milki yake ndio hutawala vitu vyote fasi yote.

22. Nuru ya Mungu haipatikane fasi yote wala ndani ya viumbe vyote.

23. Ndio maana kuna patikana maala pa nuru na maala pa giza,na pia viumbe vya nuru na viumbe vya giza.

24. Mola wa ulimwengu ni wa pekee ,mwenyi uhuru, umbalimbali na viumbe vyote kwa jumla.

25. Mwenyi uwezo wa kuenea, ambae milki yake imewaka kimuujiza na kupoteza kwa rafla uzaifu wa aina yote kandokando yake.

26. Mwenyenzi ni mumilki, mutukufu na mshindi, bingwa wa ma bingwa.

27. Ee Mola wangu ! Unijaalie kuacha yote ninayo chupa,na unipatie nguvu ya kushinda tamaa ya nafsi yangu.

28. Wala usiniache kua na chuki mbele ya wale ulio wa neemesha.

29. Wala usinifanye kua na kiburi ajili ya neema ulio nipa.

30. Mola wangu ! Unifanye kua mnyenyekevu na mpole wa moyo, CVmiongoni mwa wachagwpuliwa wako.

31. Roho alinichugua na kunipeleka,tukafika katika uwanja wenyi nuru kubwa.

32. Nikatazama, naangalia,nikaona mtoni mbele yetu.

33. Roho akaniambia, akisema : tazama kule ngambo ya mtoni.

34. Nikatazama ngambo ya mtoni,nikaona watu wengi walio vaa makanzu na viremba na mitama.

35. Watu wale walikua na hali ya upole sana, walipo niona ,wakaanza kuniita kwa kunisihi sana ili nipate kuvuka upande huo.

36.:Roho aliye nipeleka akaniambia, akisema : wasilimu wale unao waona upande huo ndio wa Ahmadiya.

37. Wasilimu wale walikua wapole sana, wengi ,na pia upande huo kulikua nuru pia.

38. Wakati walipo zidi kunisihi ili nipate kujumuika kambini mwao ,nikaanza kufikiri kama ni vuke ao hapana.

39. Roho aliye nipeleka, akaniambia ,akisema:tazama pia upande wetu. Nikatazama. Nikaona nuru kubwa tena maala ambae humeremeta sana.

40. Punde kidogo nikaona watu wote wananyamaza hali ya kutetemeka,wakaanza kutazama juu.

41. Na mimi pia nikatazama juu, nikaona roho mfano wa mutu aliye vaa kanzu mweupe ,anakuja akiporomoka toka juu mbinguni.

42.Roho yule akateremuka na kutua juu ya maji ya mtoni huo ulio tenganisha upande wangu na upande wa Ahmad.

42. Alipo tua juu ya maji ya mto hakugusa maji ya mto huo,lakini alininginia hewani namna ya kuketi kwa kukunja miguu.

43. Akaita watu wa pande zote mbili, upande wetu ulikua kuume kwake, na upande wa Ahmadi ulikua kushoto kwake, maana alihelekeza uso wake chini ya mtoni.

44. Akasema : Nimetumwa na Mungu ili ni pate kuwaamua.

45. Nimemupa mkubwa wa Ahmadiya talantha hii ili amupokeze kijana uyu (Kalonda),

46. Kama kijana uyu (Kalonda) anaipokea bila ayo kugusa maji ya mtoni, ni kwamba imeruhusiwa Kalonda kwenda upande wa Ahmadiya.

47. Lakini kama talantha hii inagusa maji ya mtoni mbele ya Kalonda kui pokea ,ni kwamba haistahili Kalonda kwenda upande huo.

48. Kiisha roho aliye tua juu ya maji akainua vitanga vyake na kunyanyua macho yake juu, akaomba Mungu bila kupaza sauti.

49.Alipo maliza kuomba,akachugua talantha hiyo na kumupokeza mkubwa wa Ahmadiya ili anipokeze, ilikua mfano wa kalamu.

50. Wakati huo wasilimu wa pande zote wakaanza kuomba Mungu ili nipate kujumuika upande wao.

51. Mkubwa wa Ahmadiya kiisha kuipokea ,akaninyooshea mkono wake wa kuume ili anipokeze pia.

52. Na mimi pia nikamunyooshea mkono wangu wa kuume ili nipate kuipokea.

53. Nilipo karibia kuipokea ,ikamuponyoka na chongo yake ikagusa maji kabla ya mimi kuipokea,ndipo nikaikamata baada ya yao kugusa maji.

54.Roho aliye tua juu ya maji akasema:Kalonda ameketi upande wake huu ,na Ahmadi upande wake ule.

55. Wasilimu walio kua na niita upande wa Ahmadi walisikitika sana,

56. Na wasilimu walio kua upande wangu pamoja na roho aliye nipeleka wakafurai sana.

57.kiisha roho aliye tua juu ya maji ya mto akanyanyuka na kupaa juu mpaka mbinguni.

58. Nilipo amuka wakati wa sala ya asubui.

59. Niliona umbo ,mfano wa mutu ,yenyi sura ya urembo sana zaidi ya wanaadamu .

60. Alikua amevaa nguo mweupe yenyi kufunika kiwiliwili chake tangu kumabeka mpaka kuvikanyako .

61. Fasi ya mikono yake kulikua kwenyi kuvimba utazani ni mabawa.

62. Alikua na ogelea hewani bila kutembea na miguu yake.

63. Alipo ni kurubia ,nilifunga macho yangu kwa kuogopa, lakini nilikua na muona kama anaye tazama, nilipo fungua macho nikazidi kumuona.

64. Hakika shukrani na heshima humustaili Mwenyenzi peke yake, Hakuna Mola mwengine kama yeye.

65. Ee Mola wangu ! Unipe kila la heri na unikinge na kila la shari na unijaalie mwisho mwema.

66. Usiku ni wako na mchana ni wako, wala Hakuna kisicho kua chini ya uwezo wako.

67. Mungu wa Ibrahimu na Kalonda, aliye pasipo yeyote juu ya maala pa juu.

68. Muumba wa viumbe vyote, aliye tangulia kadiri ya kuenea,mwenyeji wa ulimwengu.

69. Heri mutu anaye amini Mungu Mwenyenzi peke yake.

70. Hakuna Mola mwengine apasaye kuabudiwa kwa haki ispokua Mungu Mwenyenzi peke yake.

# (2)

1. Mwenyenzi Mungu amenipatia kazi ya kuhubiri habari ya uzima wake.

2. Watu wengi hawasadiki kwamba Mungu ni mwenyi uzima.

3. Hawaamini kwamba Mungu yupo sababu hawamuonake kimo chake,wala kumsikia sauti yake, na pia ajili ya kuto jibiwa palepale pindi wanapo muomba.

4. Watu hawa humuitaji kimwili kulingana na hali zao,wamezani amelingana na umbo.

5. Hawatambue ya kama Mola wao ni wa pekee tafauti sana na vyote kadiri ya Muujiza wenyi kustaajabisha.

6. Huonekana kimwili yule aliye na mwili.

7. Mungu haonekane kimwili ajili ya kuto kua na mwili wala pumzi mfano wao.

8. Hayo ni kwa sababu yeye ni tafauti sana na umbo zote,sio mwanahewa wala sio muzilahewa

9. Amepatikana mbali sana na viumbe, katika upekee, enzini.

10. Hakuna anaye lingana naye katika tendo kua, peke yake ndio mwenyi uzima na mwenyi uwezo wa kufanya kila kitu, na peke yake ndio anaye jua yote.

11. Huonana  ana kwa ana wanao lingana katika busara : kwamba kadiri ya fahamu ya uyu ndio pia kadiri ya fahamu ya yule.

12. Na ndio maana Mutu hazingatie bayana ispokua viumbe vyenzake,maana wote hulingana.

13. Fikara yao ni ndogo sana, haiwezi kuzingatia bayana njee ya anga na ukiwa.

14. Ndio kisa cha mutu kuto muona ana kwa ana Mola aliye njee ya anga na ukiwa, mtukufu anaye hifadhika katika Tabaka la Enzi.

15. Na kusema ni tendo la wanahewa, la muusiano baina yao ambae huweka wazi mawazo yao.

16. Ajili ya uchache wa fikara yao, watu hawafahamiake yaliyomo vifuani mwa wenzao pasipo kusema nao kwa sauti ao kwa mfano.

17. Wametumia misemwa kadiri ya lugha mbali mbali ili wapate kusikilizana,namna ya kusaidiana katika utetezi wao (maisha yao).

18. Haya hutokana na uzaifu wa umbo zao, ambae huitaji msaada kwa kuishi.

19. Na pia hayo humaanisha uchache wa fahamu yao ambae hudai mafunzo kwa kufahamu.

20. Kuzungumuza baina yenu ni miongoni mwa utetezi kifikara, namna ya kuishi.

21. Kua na sema na watu sauti kwa sauti katika haja za watu ni namna ya kuishi pamoja nao.

22. Mungu Mwenyenzi hagusike na uzaifu huo wa kuishi hata kidogo,maana yeye ni mkamilifu mwenyi uzima.

23. Wala hasemake kifikara maana yeye hana fikara, ndio maana haongeake na viumbe vyake kuhusikana na shuruli zao kama anaye fikiri mfano wao.

24. Kusema kwake sio sawa na kusema kwao viumbe, maana Mungu haseme ila kijuzi,bila kazi ya kufikiri wala kutamka kwa pumzi wala kwa ulimi.

25. Akapenda mutu asikie maneno fulani kwa jina lake, sauti hutokelea kwa rafla kutamka maneno Yale kadiri ya idhni yake.

26. Sio kwamba hutamka kwa pumzi ama kwa kufungua kinywa ;Mola wenu hana pumzi wala kinywa hana mdomo wala ulimi,wala kiungo chochote, atakalo hutukia kwa rafla.

27. Na kama mutu anasikia sauti yake sio kwamba hutokea dhatini mwake, lakini mapenzini mwake.

28. Na mapenzi yake ni miongoni mwa nuru yake, : kadiri ya roho yake, kadiri ya neno lake.

29. Roho yake na neno lake sio uzima wake, lakini nuru yake takatifu.

30. Sauti yake ingeli kua na tokea dhatini mwake, kama angeli kua na shurulika katika kutamka mfano wao viumbe.

31. Hapo angeli kua na ishi namna ya kujitetea mfano wao viumbe,maana shuruli ao kazi haifanyike ila na mwenyi fikara, yaani kwake aliye na maisha.

32. Na maisha haipatikane ispokua kwao viumbe wasio kua na ujuzi, ambae kufikiri.

33. Kwake yeye asiye kua na fikara, hakuna shuruli ao kazi yoyote,atakalo hutukia kwa rafla kadiri ya idhni yake bila kutumika kazi.

34. Kuonekana kimwili na kusema kifikara ndio kua kiumbe chenyi maisha, hali dhalili tafauti sana na Muumba.

35. Kutenda kwake Mwenyenzi ni kwa ajabu hakulingane hata kidogo na kutenda kwao viumbe, maana hawa ni wa zaifu na yeye ni muweza.

36. Watu wa dunia hulazimisha umungu ulingane na umutu, bila kutambua kama uzima ni utukufu wa ajabu usio lingana hâta kidogo na hali dhalili ya maisha.

37. Kama utamlaumu Mungu ajili ya kuto fanya jambo fulani ni vema ujibashiriye mwenyewe kama ni kweli tendo lile hustahili kutendeka na mkamilifu.

38. Mengi wanao mlaumu Mungu haya stahili katika uzima Bali hustahili katika maisha.

39. Mungu ni mwenyi milki kamilifu : anaweza yote na anajua yote, hali ya kua na uhuru, mbali na shuruli yote.

40. Kama Mwenyenzi hufananisha tendo fulani na utendaji wao ni katika mfano ili mupate kuzingatia.

41. Lugha yao viumbe sio ila tafsiri ya utendaji wao ambae ni tafauti kabisa na utendaji wake Mwenyenzi.

42. Hakuna kosa katika uumbaji wake, maana ujuzi wake unao umba ni fahamu kamilifu isiyo gusika na upungufu wowote.

43. Kilicho muimu kwao viumbe ni utiifu ,kutumia maamrisho na kutupilia mbali makatazo, ili wapate wokovu.

44. Majibu ya Mwenyenzi huzingatiwa rasmi na watu kiroho, maana hutendeka kwa njia ya ujuzi tafauti kabisa na fikara.

45. Aliye na roho ndani mwake huzingatia bayana utendaji wa Mola wake kwani yeye sio kipofu.

46. Na yule asiye kua na roho dhatini mwake ndio kipofu asiye zingatia chochote katika ukarimu wa Mola wake.

47. Kwa kujazwa roho takatifu inabidi utumie neno la Mungu katika kawaida yake.

48. Neno lake ndio nuru yake ambae huondoa giza, namna ya kufumbua macho.

49. Muaminifu ni mwenyi kua na ginsi ya kuwasiliana na watakatifu wa mbinguni kwa njia mbali mbali wakati wowote.

50. Anaweza kuonana na malaika pia na roho na Kuzungumuza nao bila panzia ao nyuma ya panzia.

51. Wakaaji wa mbinguni ni wenyi kazi ya kuwasaidia wale wanao amini uzima wa mungu na kutii sheria yake.

52. Mutumishi wa Mungu anajibiwaka na Mola wake kwa njia mbali mbali kulingana na daraja ya imani yake.

53. Na majibu ya Mola wenu sio katika fikara, lakini katika ujuzi.

54. Kila atendalo mjuzi ni la ajabu maana huzidia fikara ya viumbe.

55. Na ndio maana matendo ya Mola wenu haiheleweke wala kuzingatiwa ispokua na wenyi akili.

56. Na yeyote asiye amini uzima wa Mungu hana akili, ispokua yule anaye tumia neno la Mungu kama dira ya maisha yake ndio mwenyi akili.

57. Mwenyi akili ni yule aliye wa roho ambae hujaa nuru ya taa ya ulimwengu isiyo zimika.

58. Utaalamu wake unamufanya ahepukane na shari na kumukutanisha na Heri.

59. Amepata maisha ya milele sababu amefanyika roho ambae ni miongoni mwa nuru yake Mwenyenzi.

60. Heri mutu anaye pokea karama kutoka mbinguni.

61. Atakaye shika maneno ya kitabu hiki, hali ya kua amejitenga na ushirikina pia na unafiki, atapewa zawadi ya kiroho.

62. Roho amemkurubia yule anaye amini ujumbe huu na kukaa ndani mwake.

63. Mungu Amestawi enzini, juu kupita mbingu, mbali sana na dunia.

64. Ni wa pekee asiye kurubiwa na asiye jumuika, mumilki aliye tangulia kadiri ya kuenea.

65. Yeye ndio mwanzo wa vyote, anaye tokeza bila kutokezwa ,mfinyanzi wa ulimwengu.

66. Mamlaka yake imetawala pahali pote ulimwenguni, wala hakuna asiye milikiwa naye.

67. Uzima wake ni muujiza, na utendaji wake ni maajabu.

68. Mwenyi ujuzi, anaye ona yote na anaye sikia yote.

69. Anga na ukiwa vilifanyika naye bila msaidizi, muweza wa vyote.

70. Hakuna Mola mwengine apasaye kuabudiwa kwa haki ispokua Mungu Mwenyenzi peke yake,na Kalonda ni mjumbe wake.

# (3)

1. Amejaa utukufu Mwenyenzi Mungu, mjuzi wa kuumba, hakuna kilicho patikana bila hufanyika naye.

2. Uzima wake ni muujiza wa maajabu mbele ya viumbe ajili ya kuenea kimilki.

3. Kuenea ndio kukamilika, yaani kuto kua na upungufu wowote.

4 .Hali yake hii ya kuenea katika tendo kua ni milele kadiri ya kutangulia.

5. Utukufu wa kuto pungukiwa hâta kidogo ndio ukamilifu.

6. Uwezo wake Mwenyenzi umestaajabisha watu ajili ya kuzidia fikara yao.

7. Uzingatiaji wao hutokana na asili yao ya upungufu.

8. Neno la Mungu huletewa katika mifano maana umungu ni muujiza wa maajabu mbele yao viumbe.

9 mithali ili kufahamisha ,maana lugha zenu sio ila namna ya kufikiri kwenu na kutenda kwenu, ambae ni tafauti sana na ujuzi wake pia na uwezo wake.

10. Kuna patikana tafsiri ya kimwili na pia tafsiri ya kiroho, sambamba na umbo lake mutu.

11. Pumzi yake ni sehemu ya anga, na mwili wake ni sehemu ya ukiwa, yaani changachanga ya pumzi na mwili.

12. Utazani imepingana kimwili na ilihali haipingane kiroho,maana **mwili** ni mfano wa giza na roho ni mfano wa nuru.

13. Gizani munamo mashaka ajili ya upofu wa kuto zingatia ; lakini nuruni hakuna ma shaka ajili ya kuzingatia bayana.

14. Kuona kama umungu ni utukufu wa ajabu, ndio maana nuru yake pia sio jambo ndogo.

15. Nuru yake inayo tafsiri nyingi, maana ni jambo kubwa, inahusikana na matazamio.

16. Enzi kadiri ya taa na hewa kadiri ya nuru yake.

17. Ama ujuzi kadiri ya taa na fikara kadiri ya nuru yake.

18. Katika taswira ya ulimwengu inabidi tafsiri zote ili watu wapate kuzingatia.

19. Pumzi anaweza kua nuru na pia anaweza kua giza kulingana na umbile pia na kazi yake.

20. Mwenyenzi aliweka kifaa maalumu ambae hutakasa uchafu unao najisi pumzi.

21. Neno la Mungu ndio hutakasa kabisa pumzi inayo itumia katika kawaida yake.

22. Hâta ikifikia kugeuka roho takatifu hali ya kua nuru yake Mwenyenzi.

23. Watu wote wamealikwa katika nuru yake, na wote wanaweza kua nuru yake ispokua watakae kataa wenyewe.

24. Heri mutu anaye silimu na kutubu, maana ameingia katika nuru, hatua ya kwanza katika njia iliyo nyooka.

25. Kuamini Mungu na malaika zake na mitume yake wote, na vitabu vyake vyote ndio imani ya kweli.

26. Neno la Mungu ni kweli moja inayo fundisha Mungu mmoja na dini moja ya usilimu.

27. Niliona katika ndoto, mutu ananikurubia,na kuniambia,akisema : kuja twende ili nipate kukuonesha !

28. Akaniuliza, akisema : unanifahamu?nikamjibu ,nikisema : hapana. Akasema : hakika mimi ni Roho takatifu wa Mungu.

29. Akanichugua,tukaenda pamoja, tukafika kwenyi mukutano wa watu wengi .

30. Nikaona kumewekwa meza kubwa ya muviringo mbele ya uwanja wa mukutano,ambae juu yake kuliketi watu wa tatu.

31. Nikaona mumoja wa wale watu watatu walio keti juu ya meza akasimama,alikua amevaa kanzu mweupe ; akaanza kuhubiri neno la Mungu kwa kupaza sauti.

32. Wakati huo watu wote walio huzuria mukutano walikaa kimya wakimtekeleza;alipo maliza kuhubiri ,akaketi chini juu ya meza.

33. Ndio yule mwengine aliye kua pa kati yao akasimama,naye pia alivaa kanzu mweupe, akaanza kuhubiri neno la Mungu namna ya kupaza sauti.

34. Naye alipo maliza kuhubiri, alikaa chini juu ya meza,ndipo alipo simama yule wa tatu :

35. Alikua amevaa kikwembe kyeupe(weupe wa kadiri),akifunika bega lake la kushoto pamoja na mkono ispokua kitanga.

36. Na akaacha wazi bega lake la kuume na mkono wake wote,pasipo kufunika na nguo hiyo mweupe.

37. Akaanza kuhubiri neno la Mungu na sauti ya chini sana na hali ya upole sana tena mwenyi kulainika sana na zaidi, ili bidi kutega sikio kwa kusikia aliyo kua na hubiri.

38. Roho aliye nipeleka akaniambia, akisema :uyu unaye muona akiubiri kwa sauti ya upole sana ndio bwana Yesu.

39. Ameubiri na sauti ya upole sana lakini maneno  yake ni yenyi kuinukia ya wenzake wote.

40. Nilipo zidi kumtazama,moyoni mwangu muliingia ulainifu na unyenyekevu.

41. Roho akaniambia, akisema : kuja twende,tukaenda katika njia mbukani,mbuka île ili kua na visuguu vingi na miti mirefu mingi.

42. Nikasikia shindo kubwa sana nyuma yetu, nikageuka na tazama,nikaona ardhi inakuja na geukageuka namna ya kupinduliwa.

43. Milima,miti na mabonde vyote vinageuzwa na kusawanishiwa sawa sawa, nyuma yake hakukubakia bonde wala kisuguu.

44. Roho akaniambia akisema : kweli Nina kuambia ,hiyo siku ya kiyama, bwana Yesu atasaga milima na kusawanisha ardhi, hakuta bakia bonde wala kisuguu.

45. Roho akaniambia akisema : twende. Tukaenda, tukafika kwenyi muji ambae sikuona humo ispokua wanaume.

46. Watu wale walikua kikundi wima uwanjani:walikuja kutupokea na shangwe kubwa, baada ya kusalimiana tukaanza kupita ;

47. Nikaona mutu mumoja aliye keti chini barazani akasimama,akaja kutupokea kwa furaha, akisema : karibu mpenzi wa Mungu, tunafurahi sana kukupokea katika muji wetu, maana tulikua na kungojea ,basi subiri nikuletee chakula, hauta pita na njala.

48. Tukamsubiri,akaingia nyumbani, akaleta muhogo mubichi ambae hauja menyewa,akanipatia akisema : pasula na ukule.

49. Nikachugua muhogo ule ,nikaupasula na vidole vyangu ,na tazama ndani ya muhogo, nikaona mume jaa maandiko ma takatifu yenyi sifa kubwa ya Mungu.

50. Nikamuuliza roho aliye nisindikiza ,nikisema :ndani ya muhogo huu mume jaa maandiko ma takatifu yenyi sifa ya Mungu.

51. Roho akaniambia akisema : soma maandiko Yale yote na imetosha kwako.

52. Nikasoma maandiko Yale yote,ambae yalikua na ongezeka kama nikafika ku mwisho mpaka vile niliimaliza yote.

53. Nikatazama ndani ya muhogo huo, nikaona mizizi tatu, nikamuuliza roho aliye nisindikiza,nikisema : muhogo huu uliumbika namna gani ? Ndani mwake hupatikana maandiko matakatifu pia  na mizizi tatu pahali la muzizi mmoja kama kawaida ?

54. Roho akaniambia akisema : sikia maana ya hii mizizi tatu.:huu muzizi wa kwanza ndio bwana Yesu. Na huu muzizi wa pili ndio bwana yesu.na huu muzizi wa tatu ndio bwana Yesu.

55. Nikaona kama nimeamuka,nikaanza kufasiria Yale nilio yaona,kumbi nilikua bado sija amuka,nikingali katika usingizi ndotoni.

56. Mumoja kati yao akasimama akisema : sikia maana ya maono yako:

57. Maneno ya  Mungu yenye unafundishaka, inapandaka huko juu, hiyo siku ya kiyama itakua ndio chakula chako, hauta sikia njaa wala kiu.

58. Nilipo amuka sasa kikweli ,ni kasali rakaa mbili, ni kamuomba Mungu anifunulie wazi maana ya maono haya.

59. Nilipo jitandaza tena kwa kulala, nikamuona tena roho mtakatifu aliye nipeleka,akaja kunichugua na kunipeleka, tukaenda tukafika katika muji ambae watu walikua na zungumuza neno la Mungu barazani.

60. Aliye kua mkubwa kati yao akasimama,  akawakataza kelele, akisema : ivi mume zoza kijana uyu( Kalonda )hâta sikia maana ya Yale aliyo funuliwa.

61. Kiisha kutupokea,akamsimamisha mumoja kati yao akisema : ewe mukristu,simama umufasirie Kalonda maana ya maono yake.

62. Yule aliye amrishwa akasimama na kunihelekea akisema : sikia maana ya ndoto yako ewe mpenzi wa Mungu.

63. Fungua kitabu cha warumi sura yake ya kumi na tatu, aya yake ya kumi na mbili, ili upate kufahamu maana ya maono yako.

64. Sema : Yesu masiya ndio njia ya kwendea mbinguni.

65. Hakuna atakaye ingia mbinguni pasipo kutumia neno la Mungu Mwenyenzi.

66. Kuamini Mungu na mitume yake na vitabu vyake vyote, ndio kutumia neno la Mungu.

67. Imani ikaingia ndani ya mutu na kuketi moyoni mwake ,pumzi ya mutu uyu ni miongoni mwa roho takatifu.

68. Yesu masiya ni neno la Mungu, na ni roho ya Mungu. Na ni njia ya Mungu.

69. Jihadharini na imani mbaya ya kumpachika aliye tumwa daraja ya yule aliye mtuma.

70. Mungu ni mumoja, hakuzaa wala hakuzaliwa,mkamilifu asiye zaufika wala kubadirika,wa

pekee aliye juu.

# (4)

1. Ametakasika Mwenyenzi Mungu, mumoja, atanguliaye ulimwenguni.

2. Mola mwenyi uwezo wa ajabu kuzidia vyote, wala hakuna kilicho mkurubia katika mamlaka.

3. Ni yeye anaye nusuru muja wake kwa namna ya miujiza.

4. Na kuwaangamiza mahasidu na wanafiki wanao piganisha maisha ya mtumishi wake bila sababu.

5. Shetani ni adui wa watu, anaye ingia katika nyoyo za watu wasio tumia urakibu.

6. Na kuwaimiza kufanya ufisadi wa kila namna, ambae ndani mwake hamna ispokua ubaya.

7. Ni muimu kwa kila mutu kujitenga mbali na adui yake (shetani) asiye onekana kimwili.

8. Anaye onekana kiroho peke yake, ambae hujificha ndani ya umbo ingine ili apate kudanganya watu.

9 . kujitenga na adui uyu ni kunusuru nafsi yako na shari ya kila namna.

10. Ukingo wa kweli ili adui uyu asivamie nafsi yako hasa ni imani na ibada ya Mungu.

11. Kuwa  yakini moyoni na uzima wa Mola wako, na kumkumbuka kila wakati popote ulipo.

12. Na kumsifu kwa wingi na kumshukuru kwa yote anayo kufanyia.

13. Hakika shukrani zote zinamustahili Mwenyenzi Mungu, muweza wa yote.

14. Na umsujudie Mungu peke yake, wala usisujudie mwengine badala yake.

15. Na ndio maana ni amri kwa kila mutu kuhelekeza mawazo yake yote kwa Mungu katika sala.

16. Hakika sala ndio ibada kubwa, tendo kubwa la unyenyekevu mbele ya Muumba.

17. Hali yake Mungu ni muujiza ambae fikara ya viumbe haiwezi kuukagua.

18. Amezidia wote katika mambo yote maana Hakuna mwengine aliye na milki kamilifu kama yeye.

19. Watu wamestaajabu sana uzima wake ambae ni tafauti sana na maisha yao.

20. Vyote vinavyo patikana katika umutu ,havipatikane hata kidogo katika umungu.

21. Watu wa dunia wamestaajabu sana hali yake ya ukamilifu ya kutokua na mila.

22. Kua na mila fulani ni kua na umbo fulani hali ya kua kiumbe.

23. Mila ni jambo ambae hupatikana katika upungufu ,haina fasi katika ukamilifu.

24. Usawa wenyi kuenea haupatikane ispokua katika umungu

25. Vyote ambae hupatikana katika umutu sio katika usawa wenyi kuenea ajili ya kuto kamilika.

26. Fikara sio ila shuruli kadiri ya utetezi ,namna ya utafiti wa utimilifu.

27. Uzuri huangamiza ubaya ,na ubaya pia huangamiza uzuri.

28. Mkamilifu ni mtukufu aliye huru kabisa hakuna cha kumuangamiza ,wa pekee aliye tafauti kabisa na mila yote.

29. Mungu aliye juu ni mwenyi uwezo wa vyote,na ndio maana inabidi kumpelekea ,yeye peke yake, maitaji yenu yote .

30. Maombi ya muaminifu sio katika shari lakini katika heri ,amemtukuza mola wake na kujisihi kwake kwa siri na kwa wazi.

31. Hawezi kumuendea mchawi kwa shida ya kiroho ,asije akavamiwa na shetani.

32. Mola wenu amewapendeni sana na ndio maana huwaleteeni ujumbe ili mupate wokovu.

33. Pasipo uzima wake hakungeli patikana yeyote miongoni mwa viumbe.

34. Ni amri kwa watu wote kumuamini na kumuabudu yeye aliye tangulia,mfalme anaye miliki upatikanaji wote na maisha yote.

35. Heri mutu anaye vumilia pindi anapo jaribiwa ,bila shaka atavikwa taji la utukufu baada ya ushindi.

36. Katika maisha kuna kupanda na kushuka ,wala usimlaumu Mola wako ajili ya madhara fulani kukupata.

37. Asili ya kila umbo ni upungufu ,hakuna ukamilifu katika umbiko.

38. Mungu ndio mufalme wa ulimwengu anaye anzisha na anaye komesha kila kitu .

39. Ni yeye atakaye mtuma Yesu masiya siku ya kiyama na kazi kubwa ya kusawanisha ardhi sawasawa ,ikuwe yenyi unyoofu kabisa.

40. Kuifanya ardhi ikuwe nyoofu,katika usawa pasipo utafauti wowote ndio kugeuza dunia kua bustani ,namna ya kuondoa matatizo yote na kuleta amani ya milele.

41. Watu wema ndio watakao keti katika ardhi hii mupya nyoofu,kadiri ya bustani,na kuishi humo milele.

42. Na waovu ndio watakao tupwa njee ya usawa ,katika uharibifu hadezeni.

43. Humo hadezeni ,hufikiwa na kifo cha pili ,kadiri ya upotevu wa nafsi.

44. Katika bustani hupatikana uhai kadiri ya utimilifu wa umbo .

45. Kuichora ardhi kadiri ya bustani sio jambo ngumu kwa Muumba.

46. Wala kuichora pumzi ya mutu hali ya kua roho takatifu sio jambo ngumu kwa muumba.

47. Siku ya kiyama nafsi ya mutu haita kua kama ilivyo kua baada ya kifo .

48. Muumba atamurudishia mutu umbo lake ,yaani atamfufua.

49. Mutu hata kua tena mwili peke yake kama alivyo kua kaburini ,wala hata kua tena pumzi peke yake kama alivyo kua barazani baada ya kuihama dunia.

50. Mwanaadamu atakua kama alivyo kua duniani,changachanga ya pumzi na mwili .

51. Mwenyenzi Mungu ni mwenyi uwezo wa kufanya yote ,wala hakuna mfundi mwegine zaidi yake.

52. Mola wenu ni mwenyi uwezo wa kuweka bustani katika ardhi hii mupya ,hata mukipatikana starehe ya milele .

53. Kadiri bustani ilivyo leo huko mbinguni hailinde ndani mwake ispokua pumzi tukufu ,yaani mwanahewa halisi peke yake.

54. Kwa ginsi ipate kulinda mutu ambae amekwisha kufufuliwa kadiri alivyo kua duniani ,huchanga bustani na ardhi nyoofu.

55 Kama alivyo changa ardhi yenyi usawa na bustani ,na hata ikapatikana Edeni,eneo lenyi kua na ginsi ya kumlinda Adamu na Eva ,ambae ni wanahewa_haramu.

56. Mwenyenzi ndio m'bora wa wanao ruzuku ,,mwenyi rehema za milele.

57. Amebarikia wanao amini bila wasiwasi wala mashaka,ambae hujitaidi kwa kutenda mema.

58. Wanao simama katika kisomo cha ufunguzi ,na kumsujudia pia na kushaidilia upekee wa Mungu mwenyenzi .

59 .Asiye abudu Mungu kwa kutumia taratibu kama hii imani yake ni ya bure kabisa .

60. Musilimu ni mnyenyekevu anaye abudu Mungu mfano wa wakaaji wa mbinguni.

61. Muskiti ndio nyumba inayo jengwa ajili ya ibada ya Mungu mwenyenzi.

62. Ibada inayo fanyika humo muskitini ni :sala,maubiri,dhikri,kisomo na maombi.

63. Matandiko bora ndani mwake ni misala ,na mfano wa hayo humo hamustahili viti na mameza ao vitanda,maana ni maala pa kumsujudia Mungu.

64. Kumsifu Mungu katika kisomo ao katika nyimbo ni jambo la kawaida kabisa ,panafasi yake .Hapana kuimba ndani ya sala.

65. Ni lazima moyo wa musilimu kufanana na muskiti ,ambae ndani mwake hufanyika ibada ya Mungu.

66. Muskiti ni nyumba tukufu ya ibada ya jamaa la kidini,kuacha kujumuika muskitini ni kuvunja alama ya dini ya Mungu.

67. Mungu mwenyenzi ndio tajiri wa vyote ,ma kabila yote ni yake wala hakuna lugha isiyo kua yake .

68. Kila mtume wa Mungu alifunuliwa katika lugha yake yenye anasemaka,ili asikie na afahamishe watu.

69. Kauli tukufu hii imefunuliwa katika kiswahili sababu Kalonda anasemaka kiswahili,sio mkazo ku watu kutumia lugha ya mjumbe wao katika sala ,ispokua kipenda_roho.

70. Heri yule anaye tumia ukweli huu maishani mwake.

# 5)

1. Mwenyenzi Mungu ndio mshindi ,hakuna mwengine kama yeye ,muumba wa anga na ukiwa ,wa milele aliye juu.

2. Ujuzi wake unamfanya atokeze aina nyingi sana ya pumzi ,halisi na haramu ,kadiri ya idhini yake.

3. Kila anaye pumua hewa ,ndani mwake hupatikana fikara ,na ndio maana ni mwenyi maisha.

4. Umbo la kihewa linalo itwa pumzi humfanya apumue na afikiri ,yaani apate kuishi.

5. Nafsi isiyo kua na pumzi sio kihewa lakini kimwili ,na ndio maana ni miogoni mwa wazilahewa ,njee ya maisha.

6. Heri mutu anaye kagua baina ya nafsi kihewa ,ambae hutafautisha wakaaji wa mbingu na wakaaji wa hadeze.

7. Mungu aliumba mbingu na thamani kubwa,na wakaaji wake pia ni watukufu.

8. Malaika na roho ni viumbe vitukufu maana hutokana na nuru yake takatifu.

9 Pumzi zote sio roho ,kunapatikana umbile za kihewa tafauti.

10. Nafsi kihewa inayo patikana ao inayo fanyika ,kadiri ya neno ao kwa njia ya neno la Mungu ndio "Roho".

11. Nafsi kihewa ,yaani pumzi,inayo patikana ao inayo fanyika kinyume ama tafauti na neno la Mungu sio roho,lakini muzimu.

12 .Na malaika sio roho,bali ni umbo mbili tafauti.

13. Na shetani sio muzimu,bali ni umbo mbili tafauti sana.

14. Malaika ni mwenyi mabawa,lakini roho hana mabawa.

15. Na shetani ni mwenyi mapembe ,lakini muzimu hana pembe.

16. Roho ni jaza la nuru ,na muzimu ndio jaza la giza.

17. Mungu amestawi peke yake arshini,hakuna wa kujumuika naye wala jerani yake.

18. Wengine wote ni umbo alizo ziumba ,hakuna atakaye weza kukurubia dhati yake tukufu.

19 .Roho ni miongoni mwa viumbe vyake vitukufu ambae hupatikana mbinguni

20. Enzini hamuna roho wala malaika ,wala kiumbe chochote .

21. Ni maala pa upekee penyi kujaa milki kamilifu, umbo zote huyeyuka ,namna ya kufutika,kandokando mwake ,hakuna ginsi ya kujumuika enzini.

22. Watu wasio kua na elimu wamemfananisha Mola wao na roho ,bila kutambua kama mwenyenzi halingane na umbo yoyote.

23. Roho ni nafsi kihewa kadiri ya pumzi tupu.ndani mwake hamna Enzi bali hewa ambae ni nuru ya Enzi

24. Ni mwanahewa_halisi aliye umbwa kwa hewa ,anaye ishi hewani kwa kupumua hewa,kadiri ya neno lake.

25. Mola Aliye pasipo yeyote, juu ya maala pa juu ni mjuzi wa kutokeza mapya wakati wowote kadiri apendavyo .,

26. Kama anaruhusu upatikane kua mutu wakati huu kadiri ulivyo ni amri kwako kumshukuru kwa wingi

27. Angeli penda usijumuike ulimwenguni kama wewe ni sifuru ,haungeli kua chochote .

28. Na kama Mungu anaita mutu fulani kua ndio roho yake, ni kwa kuonesha ukubwa wa imani ya mutu yule, ameishi kwa njia ya neno lake kadiri ya neno lake.

29. Ndio maana Mungu amemuweka katika fungo la viumbe vyake vitukufu vinavyo itwa Roho.

30. Na kama Mungu anajitapia kiumbe fulani kua chake,sio kwamba viumbe vingine sio vyake, wala haimaanishe ya kwamba kiumbe hicho ndio yeye.

31. Hayo humaanisha ukubwa wa daraja ao thamani ambae Mola kajaalia umbo île.

32. Ametakasika kabisa Mwenyenzi Mungu na Yale yote wanao mshirikisha nayo.Mola mwenyi ukamilifu, wa pekee aliye juu.

33. Mbingu, hadeze na dunia ni mazao ya idhni yake mwenyewe, pasipo mshauri  wala msaidizi wa kazi.

34. Ni yeye anaye Lea maisha ya wanahewa wote, kiongozi pekee wa jumla ya viumbe.

35. Kumuabudu yeye peke yake na kuacha maovu yote ndio kuichora pumzi yako kua roho takatifu.

36. Mungu ndio mwenyi uzima, kujiuliza kama ni kweli Mungu iko ,ni alama ya kukosa akili, hali ya upofu.

37. Pasipo Mungu kutangulia, hakungeli patikana chochote ulimwenguni.

38 .Kwa kitu kutokezwa toka sifuru ,inatakika kupatikane kabla ya yote,yule awezaye yote na ajuaye yote, atakaye kitokeza.

39. Hakuwezi kutokezwa kitu bila fundi wa kukitokeza kutangulia kupatikana mbele ya  yote.

40. Kitu kisicho dai wa kukitokeza ni kîle kilicho kamilifu, ambae hujieneza katika yote bila upungufu wowote.

41. Kingeli dai msaada kwa kyao kupatikana kama kisingeli weza kutokeza toka sifuru, maana kingeli kua na uzaifu mfano wao viumbe.

42. Hakika kushakia uzima wa Mola na hali uko na zingatia viumbe alivyo viumba, ni upofu, hali ya kukosa macho ya kiroho inayo itwa "akili".

43. Mungu Mwenyenzi ndio m'bora wa kutenda, mjuzi anaye jaza tabaka la anga na maisha ya kila namna.

44. Kujiuliza kama Mungu anaweza ni kukosa imani, amejaa ma shaka ajili ya kukosa yakini.

45. Vyote kwa jumla hutendeka kwa idhni yake, lau kama hasingeli Patiana nguvu ya utendaji, bila shaka viumbe visingeli weza kufanya lolote.

46. Na kama viumbe visingeli weza kujikusuru kiutendaji kama hakungeli patikana maisha yeyote ulimwenguni.

47. Kilicho mfanya atangulie bila kuanza na atokeze ambacho hakikua popote ni île milki kamilifu aliyo nayo ambae ni mamlaka ya kufanya anayo penda,pasipo kushindwa na chochote.

48. Mungu ndio muweza yote kadiri ya mwanzo wa vyote, pasipo yeye hakungeli patikana wala kufanyika chochote.

49. Mungu ndio mjuzi wa vyote ,ambae vyote ni vyake, wala hakuna kisicho kua chake,kwani ndiye muanzishaji wa kila kitu.

50. Yeye ni mwenyi mamlaka ya utendaji, anaye anzisha na anaye komesha .

51. Hakuna mwengine kama Mungu, wa miujiza na wa milele.

52. Alitangulia kadiri ya kuenea katika mamlaka yake mwenyewe, kabla ya ulimwengu na baada ya ulimwengu,mwenyi kukamilika.

53. Mufalme anaye enea katika tendo kua,mtukufu asiye badirika.

54 .Mungu Mwenyenzi sio mwenyi maisha wala sio mwenyi ukiwa, lakini mwenyi uzima.

55. Ni mwenyi kuenea katika yote mbali na upungufu wote.

56. Mamlaka yake humiliki kila kitu, vitu vyote ni chini ya uwezo wake.

57. Hakuna mwengine kama yeye ,wa pekee atanguliaye ulimwenguni.

58. Ukamilifu wake unamfanya aenee katika tendo kua pasipo kabla yake wala baada yake, na atokeze vilivyomo angani na vilivyomo ukiwani bila kuiga mfano popote wala kutumika kazi yoyote .

59. Kama si ukamilifu wake,hakungeli patikana chochote Bali sifuru ingeli tawala milele.

60 . Mpungufu hawezi kutokeza toka sifuru maana ni mwenyi uzaifu hafahamu chochote wala hawezi lolote bila msaada wa mfinyanzi wake.

61. Ujumbe huu ni ukweli usio kua na shaka ambae Mungu kaushuudia mwenyewe.

62. Kuna patikana umungu ambae ndio ukamilifu kadiri ya uzima.

63. Ni utukufu wa ajabu, mamlaka ya milele inayo patikana kimuujiza bila msaada wa yeyote.

.64 Hakungeli patikana yeyote wala chochote bila milki kamilifu kama hii kutangulia ulimwenguni.

65. Mutu asiye amini Mungu ni sawa na mnyama ambae hukosewa akili.

66. Na waaminifu wote ni katika fungo moja na wanahewa_halisi, watakatifu wenyi hidaya kadiri ya jaza la nuru yake Mungu.

67. Tumieni wote ukweli huu ili mupate kuzingatia uzima na kujumuika mbinguni.

68. Hakika Mungu iko mzima,mufalme wa milele, aliye tangulia kadiri ya kuenea.

69. Heri mutu anaye silimu na kutubu maishani mwake,ambae humsujudia Mola wake usiku kama vile mchana.

70. Hakuna Mola mwengine apasaye kuabudiwa kwa haki ispokua Mwenyenzi Mungu peke yake.

(6)

1. Ametakasika Mwenyenzi Mungu,Mjuzi aumbaye ,wa pekee anaye stawi katika dhati yake mwenyewe .

2. Mwokozi aliye na mamlaka juu ya kilakitu, mwalimu wa wote.

3. Ni yeye anaye letea watu ujumbe kuwanusuru na shari ya giza

4. Kumuamini aliye tumwa na Mungu mwenyenzi ni neema,jambo muimu kwa watu wote .

5. Kama ni wa uwongo mutamutambua kwa matunda yake .

6. Na Hakika kumzingizia Mungu kwamba kakutuma na ilihali hakukutuma ni zambi kubwa sana, wala mutu hafikie kiasi hicho ispokua kafiri mkubwa.

7. Na wengine walio kufuru hawaamini mtume yeyote sababu hawa kujionea wala kujisikilia wakati walipo funuliwa na Mungu.

8. Usilazimishe kukutanika wanapo funuliwa kwa wewe kuamini ,utajionea ao kujisikilia namna gani na hali sio wewe ulio funuliwa?.

9. Lau kama ni ushahidi wa mambo ya kidunia anakubali kwa haraka bila kulazimisha kukutanika yeye mwenyewe .

10. Hayo humaanisha ukafiri mtupu ,amejaa kiburi sababu ya kupewa muda ,hakika atajuta kwa yale aliyo kua akiyafanya.

11. Mjumbe wa Mungu ni mwenyi elimu ya juu,mwenyi utaalamu wa kiroho.

12. Ameinukia wengine maana ni uvuli wa ujuzi, nuru ya taa ya ulimwengu.

13. Neno anaye toa sio lake Bali la yule aliye mtuma, na ndio maana ni lenyi kuinukia.

14. Basi jihazarini na upinzani musije kuwapinga mitume wa Mola,musifikie kuanguka pembeni yao mfano wa makapi.

15. Na wanao kanusha wajumbe wote ndio makafiri wanao kanusha uzima wa Mola wa walimwengu.

16. Aminini Mungu Mwenyenzi aliye umba mbingu na ardhi pamoja na vilivyomo.

17. Ni yeye aliye tangulia kadiri ya kuenea bila mwanzo wala mwisho.

18. Hakuna mwengine apasaye kuabudiwa kwa haki ila Mwenyenzi peke yake.

19. Hakika wengi miongoni mwa watu waliingia katika hasara alipo tumwa Ahmad, kila mutu aliye mpinga ni mwenyi hasara.

20. Mungu amemtuma malaika aniagize neno hili:hakika Ahmad ni mjumbe wa Mungu, wala musiwe na shaka juu yake.

21. Basi aliye na masikio ya kusikia asikie .

22. Mwenyenzi ndio mumilki, mpanaji wa nguvu anaye tegemewa na walimwengu wote kwa jumla.

23. Mola wa karne na karne,Hakuna kisicho milikiwa naye, mshindi wa popote na milele.

24. Ni yeye anaye fanya muusiano baina ya sehemu zote za ulimwengu ili maisha ipate kutimilika.

25. Amejaa utukufu wa ajabu, mchungaji mwema anaye rehemu na anaye kirimu .

26. Achanikaye mbinguni huonana na watakatifu wa mbinguni na kusharikiana nao pia, wakingara namna moja kama matonge ya nuru.

27. Na yule achanikaye hadezeni, huonana na wakaaji wa hadezeni na kusharikiana nao pia, wakififia wote kama matonge ya giza.

28.muusiano wa mbingu na dunia ndio ufunuo ambae huambatanisha mutu na nuru.

29. Na muusiano wa dunia na hadeze ndio ushirikina ambae huambatanisha mutu na giza.

30. Mutu atakaye wasiliana na mbingu atatukuzika mpaka kufikia daraja ya juu ya viumbe vyote.

31. Na mutu atakaye wasiliana na hadeze atazalalika mpaka kufikia daraja ya chini ya viumbe vyote.

32. Muusiano na mbingu umeleta baraka,na muusiano na hadeze umeleta laana.

33. Hakika ni bora kwa mutu kuchagua Heri kuliko shari.

34 .Mola wenu amekua yote katika yote, juu ya yote kuliko wote ,m'bora wa kuenea.

35. Ukamuomba heri atakupatia ,na ukimuomba shari atakupatia.

36. Maisha ya mutu ni utetezi baina ya mema na na mabaya.

37. Akili yako ndio itakayo kuweka huru ao mtumwa.

38. Lau kama watu wangeli ona ginsi mizimu inavyo taabishwa na shetani humo zimuni,kama watu wote wangeli ogopa kutenda zambi.

39. Na lau kama watu wangeli ona ginsi roho inavyo shangiliwa na malaika humo mbinguni, kama watu wote wangeli pupia kutenda mema.

40. Maana Hakuna furaha sawa na hiyo ya mbinguni.Na pia Hakuna mateso sawa na hiyo ya hadezeni.

41. Hakika Mola wenu ni m'bora wa mahakimu, humlipa kila mmoja wenu sawa sawa na matendo yake.

42. Tumieni urakibu maishani mwenu,enyi walio silimu, hakika hii ndio njia iliyo nyooka.

43. Aliye katika njia iliyo nyooka hana tegemeo ingine badala ya Mungu Mwenyenzi.

44. Matendo yake imeambatana sana na maamrisho ya Mungu ,tafauti kabisa na makatazo yake.

45. Mnyenyekevu ni yule anaye fuata sheria ya Mungu, ameogopa kutenda zambi asiye kupotea njia.

46. Mwenyenzi ni mkaguzi wa mambo ya siri na ya wazi, Hakuna asilo lijua.

47. Mtefuzi wa kila zamiri, chemchem ya fahamu ulimwenguni.

48 . Ufunuo utokao mbinguni ndio mwongozo wa maisha ya watu.

49. Hakuna utimilifu wa maisha pasipo imani, wala hakuna wokovu njee ya nuru yake.

50. Cha muimu mbele ya yote ni kusilimu na kutubu.

51. Dini inayo undwa pasipo ufunuo ni makila ya shetani.

52. Watu wengi wamefichamia katika neno la Mungu, wakidanganyia kuhubiri na kuombeana .

53. Wanapo piga ramli, hudanganyia kutabiri maono,wamezani kupata kumbi kupatikana .

54. Hakika hawadanganye ispokua nafsi zao wenyewe ,watajuta kwa Yale walio kua wakiyafanya.

55.Mutu atakaye ingia katika dini isiyo fundisha umoja wa Mungu, amepotea njia.

56. Na yule atakaye ingia katika dini isiyo fundisha namna ya kumsujudia Mungu peke yake ameangamiza nafsi yake mwenyewe.

57. Hakuna imani moyoni mwa mutu pasipo matumizi ya shaada na sijida.

58. Mungu amewapenda sana wanyenyekevu wanao muabudu yeye peke yake.

59. Mitume wote walikua na shaidilia umoja wa Mungu na pia wote walikua na msujudia yeye peke yake.

60. Atakaye tenda umbalimbali na mafundisho ya mitume ya Mungu ni miongoni mwa makafiri, pumbafu anaye potea njia.

61.Roho aliniita,tukaenda,tukafika maala ambae mutu alikua na hubiri ,alikua mnene,akivaa shati na suruhali,ya rangi ya kahawa.

62. Roho akaniambia akisema :mutu uyu anaye hubiria hili kundi la watu ndio Kadima ya Nzambi.

63. Mutu uyu amedanganya watu kwamba alitumwa na Mungu na ilihali Mungu Mwenyenzi hakumutuma .

64. Maneno anaye hubiri inasikilika na watu wa dunia kama ni maubiri ,lakini mbinguni maneno yake imesikilika kama matusi makubwa anayo mtusi Mola wa ulimwengu.

65. Hakika nakuambia mutu uyu ni Nabii wa uwongo tena mchawi mwenyi laana kubwa .

66. Nilipo sikia hayo nikamuambia roho tuondoke pahali hapo ,tulipo anza kwenda ,yule Nabii wa uwongo akageuka kutuangalia,akaanza kututukana na kutukania kutuiba sehemu ya nyota yetu .

67. Roho akaniambia akisema : usiogope hana uwezo wowote mbele yetu.

68. Zama hizi watu wengi wamemzingizia Mungu kwamba kawatuma na ilihali Mungu hakuwatuma .

69. Uwaambie watu wafanye angalisho na ma nabii wa uwongo,

70. Wajumbe wa uwongo wamewadanganya wale wanao amini kwa kuona miujiza ,ambae huamini ya kama Mungu anaweza kujigeuza mutu,wao ndio mateka ya masih jadali.

# (7)

1. Ametakaskka mwenyenzi Mungu ,mfalme wa ajabu anaye patikana kadiri ya kuenea,bila mwanzo wala mwisho.

.2 Utangulizi wa dhati yake ulimwenguni ndio uzima ambae ni umungu.

3. Mshindi anaye zidia wote kimilki na kiufahamu.,ambae vyote humuitaji .

4. Pahali alipo hakuna mwengine, wa pekee bila mfano wake wala diko mwenzake ,wala jerani yake.

5. Mtukufu wa ajabu aliye yote katika kujua na yote katika kuweza ,muujiza wa maajabu ulimwenguni.

6. Mola wa mashariki yote na magharibi yote,mwenyi mamlaka ya milele.

7. Katika ulimwengu kunapatikana hali mbili tafauti:kunapatikana ukamilifu na kunapatikana upungufu.

8. Ukamilifu ndio uzima ,kadiri ya kuenea.Hali tukufu ya kumiliki vyote pasipo uzaifu wowote.

9. Na upungufu ndio hali dhalili ya Ukosefu wa Mamlaka ya kuenea .Na kuto enea ndio uzaifu wa kushindwa.

10. Ukamilfu ni utukufu ,mamlaka ya kuweza yote na kujua yote

11. Na upungufu ni udhalili ,uzaifu wa kushindwa na yote ,ambae hudai msaada kwa kufanyika na kwa kufanya .

12. Kuanza husababisha kua sifuru kabla yake.

13. Na kukoma husababisha kua sifuru baada yake.

14. Kuanza na kukoma ndio alama kubwa ya uzaifu wa kitu ,upungufu wa kutokamilika

15. Na ndio asili ya kila umbo ,tafauti kabisa na muumbaji .

16. Kuona kama Mungu hana uzaifu wowote ndani mwake, ndio maana hakuna kabla yake wala baada yake

17. Mungu ni mwenyi kukamilika tafauti sana na upungufu wa aina yote.

18. Na ndio maana yeye peke yake ndio mwanzo wa vyote,yaani muanzishaji wa kila kitu.

19. Pasipo ukamilifu wake kama sifuru ingeli tawala milele.

20. Katika upungufu hamna ispokua uzaifu mkubwa ,na ilihali uzaifu hauwezi kutokeza toka sifuru.

21. Kama kuna patikana ulimwengu na walimwengu (yaani umbiko)ni kwa sababu Mwenyenzi Mungu alitangulia namna ya kuenea pasipo uzaifu wa kuanza na kukoma.

22. Shangilieni uzima wa Mola wenu aliye juu ,muweza yote na mujua yote ,wa pekee anaye kamilika.

23. Mungu peke yake ndio mwenyi uzima tafauti kabisa na kila kitu, hakuna anaye fanana naye .

24. Fikara ya viumbe ni jambo dhalili mbele ya ujuzi wake, wala haizingatie chochote ispokua kwa ruhusa yake.

25. Mwenyenzi ni mkamilifu anaye stirika milele ,ambae hafikiwake na asicho kitaka kamwe.

26. Na ndio maana huzuni na hasira hukomea kwao viumbe ,alama ya uzaifu kama hii haipatikane enzini kamwe .

27. Amelinganishwa na viumbe katika hayo kupitia mapenzi yake ambae huzingatiwa kadiri ya nuru yake.

28. Malaika na roho ni mfano wa nuru yake ambae hutimiza mapenzi yake,

29. Katika ubinaadamu ,kile kinacho wa huzunisha ao kinacho wa kasirisha ,husemekana ni vivihivyo pia na kwake mwenyenzi maana wao ni uvuli wake.

30. Kwa kufikia mapenzi yake mshindi lazima kuiga mila ya malaika na roho ,ambae humnukulu.

31. Atakaye tenda kinyume na mila ya watakatifu wake ,bila shaka atakua amepotea njia .

32. Watakatifu wake wa mbinguni ni mfano wa nuru yake lakini sio mfano wa Enzi yake

33. Ni tafauti sana na dhati yake,maana wao ni viumbe na yeye ni muumba.

34. Matendo ya viumbe hailingane na matendo ya muumba kamwe

35. Mila nzuri huwaingiza watumishi wake katika utimilifu sio katika ukamilifu.

36. Kama malaika na roho hupatwa na huzuni pia na hasira sio kwamba uzaifu huo utamgusa mtukufu wa daraja aliye enzini.

37. Mwenyenzi ni muujiza wa maajabu aliye pasipo yeyote ,juu ya maala pa juu,hafanane na yeyote .

38. Amekua na milki kamilifu ambae hutenganisha kutenda kwake na kutenda kwao viumbe.

39. Kutenda umbalimbali na mafunzo ya watakatifu wa mbinguni ni kutenda sawa na mafunzo ya Shetani.

40. Kinacho tafautiana na nuru kimelingana na giza.

41.Tumieni maamrisho ya Mungu na itupilieni mbali makatazo yake ili mupate wokovu.

42. Mungu ndio anaye stahili kutumainiwa zaidi ya wote maana ndiye peke yake awezaye yote.

43. Heri mutu anaye simama imara katika njia ya Mungu.

44. Hasara ilio je kwao vigeugeu wenyi kua mguu njiani mguu porini .

45. Unafiki ni sumu maishani ,maana hufupisha umri wa mwanaadamu .

46. Mungu ni mwenyi uwezo juu ya kila kitu  ni vema kua yakini naye.

47. Vyote viliumbwa naye  na vyote humilikiwa naye na pia vyote hukomeshwa naye.

48. Ni amri kwa watu wote kuamini kwamba Mungu iko.

49. Hakuna Mola mwengine kama yeye,mkamilifu aliye pasipo yeyote ,milele na milele..

50. Ni mtukufu wa ajabu ambae dhati

yake huunguza kadiri ya kufuta umbo zote kandokando yake.

51. Amengara zaidi ya nuru ,taa tukufu ya ulimwengu isiyo lingana na chochote .

52. Nuru yake ni kubwa ajabu ambae hupofoa jicho linalo jaribu kumchungulia.

53.Amejidhihirisha kwao kwa namna ya mifano na pia kwa njia ya neno lake.

54. Bila yeye kujifunua kwenyi wajumbe wake kama watu hawangeli zingatia uzima wake.

55. Anaye sikia sauti ya Mungu ndio anaye muona Mungu ,amemzingatia kupitia kauli yake.

56. Hapana kulazimisha ukamilifu ukuwe sawa na upungufu,ambae ni kamilifu ni muujiza mbele ya wapungufu.

57.Anaye kanusha ujumbe na kulazimisha tu kumuona kimwili ni kafiri anaye mkanusha Mola wake kwa kusudi .

58. Katika maisha ya watu kuna patikana kipindi cha majaribu, ni lazima kuizingatia na kuihepuka.

59. Shetani anajipindaka na ushambulizi kujaribu kuwaangusha wasilimu katika imani yao.

60. Kupatwa na madhara fulani ni jambo la kawaida kwa watu wote,hapana kumkufuru Mungu.

61. Shari na mema yote imetoka kwa Mungu, kilicho muimu kwako ni kuamini na kuabudu na kuomba Mungu.

62. Na kupewa uchawi bila wewe kutaka pia ni jaribu .kilicho muimu kwako ni kuukataa,yaani kutoutumikisha kwa kurogana.

63. Atakaye utumikisha baada ya kuambukizwa atakua ameshindwa na jaribu .

64. Ni lazima kwako kuzidisha ibada ya sala na Saumu na dhikri ya kisomo cha kitabu hiki kitukufu.

65. Mola wako atakusafisha ,mamlaka yote ni yake, wala hashindwake na chochote kamwe.

66. Kauli tukufu ya kitabu cha ukweli ni yenyi nguvu na ushindi ambae huunguza kila falme za giza.

67. Kama unajitenga na mabaya na kutumia kauli tukufu hii katika mpango maalumu, bila shaka utafanikiwa katika maombi yako.

68. Hakika dawa ya kutibu nayo jaribu ni subira na ibada .

69 Kitabu hiki ni ukweli kutoka kwa Mola wa ulimwengu.

70. Hakuna Mola mwengine apasaye kuabudiwa kwa haki ispokua Mungu Mwenyenzi peke yake

# ***Mlango wa sita : UZIMA***

## I. MWANZO WA VYOTE

1. *Mungu ni mmoja sababu yeye ndio mwanzo wa vyote.*

2. *Hakuna ginsi mwanzo wa vyote upatikane tena na mwanzo wake ungine.*

3. *Ni wa pekee ajili ya kua na milki kamilifu,fahamu ya vyote ambae hutokeza toka sifuru.*

4. *Hakuna kinacho patikana bila kufanyika naye.*

5. *Ni Mungu pekee aliye na ujuzi,fahamu isiyo shindwa na lolote;mamlaka ya uumbaji.*

6. *Mungu ni mwenyi uzima sababu ya kupatikana na milki kamilifu.*

7. *Milki yake hufanya atangulie ; yaani apatikane bila kuanza wala kukoma.*

8. *Hakuna wa Mungu wengi sababu umungu ni ukamilifu,Hakuna utafauti wala mipaka,Hakuna maanzio wala makomeo,ajili ya kuenea.*

*9. Uwingi ni katika viumbe,na upekee ni katika umungu.*

*10. Ni yule aliye umbwa ndio kawekewa wenziwe wa kushiriki naye katika matumizi.*

*11. Na yeye asiye umbika hawezi kua  na wenzake sababu hakuna wa kuwajaza ili wawe wengi.*

*12. Muumba ndio mwenyi mamlaka ya kuwajaza (ili wawe wengi) kadiri apendavyo.*

*13. Mungu ni kama taa ya ulimwengu,ambae huangaza maala pote kwa nuru yake.*

*14. Pahali penyi kua taa hupatikana sehemu tatu: taa,nuru na giza.*

*15. Kila sehemu ni tabaka,na jumla ya hizo tabaka tatu ndio ulimwengu.*

*16. Mgawanyiko huu wa ulimwengu umesababishwa na busara ambae katangulia.*

*17. Taa hiyo ndio ujuzi na nuru yake ndio fikara,na giza ndio ujinga.*

*18. Hakutukie chochote pasipo  fahamu kamilifu kuya tenda.*

*19. Kuona kama busara kamilifu ndio ujuzi,na aliye na ujuzi ni Mungu peke yake,ndio maana Mungu peke yake ndio aliye fanya ulimwengu upatikane.*

*20. Ni lazima watu kugundua jambo ambae husababisha upatikanaji wa viumbe ili wapate kuzingatia ulimwengu ambae ni uzima,maisha na mauti.*

*21. Ni mwenyi uzima aliye na ujuzi,na ni mwenyi maisha aliye na fikara,na ni mauti aliye na ujinga.*

*22. Kupatikana bila uzima wala maisha ndio kua mauti,yaani kua bila ujuzi wala fikara ndio kua na ujinga kadiri ya mauti.*

*23. Hakika upatikanaji ( mauti) na maisha ni matunda ya idhni yake Mjuzi;*

*24. Hakufanyike lolote pasipo utangulizi wa fahamu ya vyote pia na uwezo wa vyote.*

*25. Hakukua,hakuna na hakutakua mwengine badala ya Mungu Mwenyenzi.*

*26. Hakuna nguvu wala fahamu bila msaada wa ujuzi maana vyote ni katika fahamu ya mtangulizi*

*27. Ujuzi ndio taa,na uvuli wake (ao mwangaza wake ) ndio fikara,na kinyume cha mwangaza wake ndio giza ambae ni ujinga.*

*28. Katika matazamio ingine: ujuzi ndio Enzi ,na fikara ndio Anga yaani hewa,na ujinga ndio ukiwa.*

*29. Kuona kama ujuzi ndio ukamilifu,ndio maana Mjuzi ni mwenyi uwezo wa vyote,hashindwake na yeyote wala chochote.*

*30. Mwenyi mamlaka ya uumbaji,atokezaye mapya ambae hayakua popote,bila shuruli kupatikana ndani mwake.*

*31. Mola wa jumla ya viumbe,aliye hodari na wasaa ,anaye stawi enzini katika uhuru,aliye na kasi la uwezo wa kutenda,mzima.*

*32. Enzini ni maala pa juu hupita mbinguni,wala hakuna kilicho inuka mfano wake ulimwenguni.*

*33. Mwenyi daraja la juu kuliko vyote,mtukufu atanguliaye kadiri ya kuenea.*

*34. Hodari asiye jumuika katika umbiko,M'bora wa katangulia.*

*35. Mbingu ni bahazi la kiroho linalo patikana angani.*

*36. Na dunia ni bahazi (kambi) la kimwili linalo patikana ukiwani ku maunganio na anga.*

*37. Katika utazamaji kiroho:dunia imefunikwa na giza, na mbingu*

*imemeremeta na nuru.*

*38. Hakika anga (hewa) ndio nuru na ukiwa ndio giza.*

*39. Utakatifu ni wake Mwenyenzi,M'bora wa kuumba Mola wa anga na ukiwa,haimjuzu kutokea wala kuendea, muhodari juu ya arshi yenyi heshima ,imara kukadiria; mtukufu mwenyi uwezo na ushindi.*

*40. Mustawi aliye na mamlaka juu ya yote,huko juu ya maala pa juu,Mungu mzima asiye kosekana muda wowote,mshindi aliye juu.*

*41. Mungu alitangulia kuenea bila mwanzo wala mwisho sababu ya kupatikana na fahamu ya ajabu isiye shindwa*

*42. Na baada ya utangulizi wake,akatokeza viumbe vyote kwa njia ya mapenzi yake.*

*43. Kwa sababu hakufanyike jambo kinyume na idhni yake,hutakika uzima upatikane kwa ulimwengu kutimilika.*

*44. Kuona kama Mungu pekee ndio mwenyi uzima,ndio maana yeye peke yake ndio mwenyi uwezo wa kuumba.*

*45. Ametokeza kwa rafla kiumbe ambacho hakikuwaka popote ulimwenguni.*

*46. Mungu haonekaniake viumbe ajili ya kutokurubiana naye katika fahamu.*

*47. Mungu ni Mjuzi,lakini viumbe havijue.*

*48. Viumbe hufikiri tafauti na kujua,walio na pumzi; na hupitiwa wasio kuwa na pumzi.*

*49. Mola mtukufu ni muweza bila msaidizi wala muchoko, mu miliki wa ulinzi na karama.*

*50. Shuudieni Mwenyenzi Mungu,uzima ushindaye,Mola wa mashariki na magharibi ,mamlaka katika yote pahali pote ulimwenguni.*

*51. Hakika ujuzi ndio ukamilifu ambae ni uzima kadiri ya umungu.*

*52. Ni muujiza wa maajabu ambae hupatikanisha kila kitu,wala hakuna cha faida mfano wake,wala utasi kinyume naye.*

*53. Mola atulizaye tatizo kwa hudumu lake,msemeleaji wa viumbe.*

*54. Aliye umba mbingu angani kama vile tungi ,ambae huzagaa na nuru.*

*55. Na akaumba dunia ukiwani kama ganda yenyi kujaa giza.*

*56. Hakika Mungu ndio mwenyi kuwako imara na daima*

*ulimwenguni,wa milele aliye juu.*

*57. Haiwezekane viumbe ambae havijue vipatikane na Muumba ajuaye akosekane.*

*58. Hakiwe kiumbe ila kilicho umbika na Muumba.*

*59. Tumieni maamrisho ya Mungu ili Mwenyenzi akuamrishe kuishi milele.*

*60. Na atumiaye makatazo hufupisha umri wake,na pia hujiangamiza mwenyewe.*

*61. Kama utatenda mabaya usizani kama unam'buguzi Mungu,hakika umejizulumu mwenyewe.*

*62. Mungu sio mfano wa kiumbe ambae hutaabika na kasirani,uzaifu kama huo haum'kurubie kamwe.*

*63.Anaye chukizika,hulia;na anaye furahi,hucheka .Mtukufu aliye juu,hujitenga mbali sana na uzaifu huo wa kulia na kucheka.*

*64. Mola wa ulimwengu sio mvuguvugu katika hali yake,hapungukake wala haongezekake,kwa maana yeye ni Mkamilifu.*

*65. Mungu ni mwenyi uhuru,baba wa salama aliye Salama,hafikiwake na yale asiyo yataka.*

*66. Hali yake Mungu ya uhuru haimziwilie kuongoza viumbe vyake na kuwawekea maamzi, namna ya kutenganisha adili na batili.*

*67. Na humlipa mtenda mema baraka na mtenda zambi laana,hali ya kua mubora wa mahakimu.*

*68. Na kama Mungu aliwawekeeni sheria,sio ajili ya usalama wake bali ajili ya usalama wenu.*

*69. Watu wengine hawamkubali Mungu ajili ya kutomuona na macho ya miili zao,wamezani kama amefanana na viumbe.*

*70. Na wengine hawamuamini sababu ya ugumu wa neno lake,na hali roho huangazia akili ya watu urakibuni.*

*71. Neno ni ngumu kimwili uatiduni, ajili ya kukumbwa na giza.*

*72. Na ni mwepesi kuheleweka urakibuni katika roho ajili ya nuru.*

*73. Mungu hasemi ila kijuzi,ispokua viumbe ndio husema kifikara.*

*74. Kuona kama Mungu ni Mjuzi,matendo yake ni ya kijuzi vilevile,namna ya muujiza,namna ya maajabu.*

*75. Kwa kufahamu neno la Mjuzi ni lazima kutimilika kikafara;yaani kua na akili.*

*76. Neno la Mungu hufanyika kifikara kadiri ya kusema kwa watu ili wapate kulisikia.*

*77. Na ndio maana hakika ya kadiri yake haikadiriwe ispokua katika mifano.*

*78. Neno lake ndio nuru inayo angazia watu, hufanya wamzingatie mwenyi uzima ulimwenguni.*

*79. Hakuna wala hakukua,wala hakutakua mola mwengine badala yake ,sababu hakuna kabla wala baada ya umungu.*

*80. Hutukuka jina lake ulimwenguni,Mola mkamilifu katika yote,mlezi wa viumbe.*

*81. Umungu ni mamlaka ya ajabu,utukufu wa namna yote,katika yote,pahali pote ulimwenguni.*

*82. Anaye tawanisha hewa katikati ya ulimwengu kadiri ya idhni yake,ndiye Mola wa arshi tukufu.*

*83. Hakuna kilicho kurubia uwezo wa Mungu ambae mchoko haumguse,ambae hukadiriana vipimo ajili ya kujua yaliyo mbele yao na yaliyo nyuma yao.*

*84. Na akataaye kipimo cha Mwenyenzi Mungu na kutarajia tamaa ya nafsi yake ndio mzalili,umbo ya hadezeni.*

*85. Mola wa Anga na Ukiwa hatendake kadiri mutu anavyo tendaka,lakini hutenganisha nuru na giza bila kudanganyika wala kusambisha.*

*86. Aliumba mutu katika umbile la katikati juu yake pumzi na chini yake mwili.*

*87. Na silaha ya utetezi kifuani mwake,ili asiangamie ajili ya uziwi na upofu.*

*88. Akili huapa kwa jina la ujuzi,na humsujudia Mola wake katika yakini.*

*89. Na muguu wake wa kuume juu ya maji,na muguu wake wa kushoto juu ya udongo na moyo wake katika hifadhio la adili.*

*90. Huamini Mungu katika yakini,na zamiri yake ndani ya mipaka ya neno la Mungu.*

*91. Na ndio maana matendo yake hubarikiwa na nuru hutiliwa ndani mwake.*

*92. Kuamini Mungu kwa yakini ndio tendo kubwa,hutimiliza nafsi yako kua roho.*

*93. Roho ni nuru,hakuna shaka ndani mwake ajili ya kuzingatia.*

*94. Uvuli wa Enzi tokea uzimani,silaha ya utetezi na dira kwa wamchao Mungu.*

*95. Ni neno la Mungu ndio huleta uhai rohoni na mauti mwilini.*

*96. Na kuamini Mungu kwa mashaka ndio tendo mbaya,huzaufisha nafsi yako kua mauti.*

*97. Kuona kama mwili ni giza,kuna mashaka ndani mwake ajili ya kutozingatia.*

*98. Mwenyenzi Mungu ni mshindi,hodari katika arshi yake,jalali ulimwenguni.*

*99. Huenea katika yote,muda wote,maala pote,mwenyi uzima,imara na daima milele na milele*

*100. Huinuka ulimwenguni ajili ya milki kamilifu,ambae ni mamlaka ya kuenea katika yote ulimwenguni.*

*101. Karama zote ni zake Mungu,ambae peke yake ndio mzima,wa pekee aliye huru kutenda kila apendalo.*

*102. Watu hawamfahamu mwenyi daraka ulimwenguni ajili ya kuvaa miili.*

*103. Hakika Mungu Mwenyenzi kudiriki vyote ulimwenguni.*

*104. Mola mtukufu asiye na doa, ambae huzagaa juu ya ulimwengu,mtawala wa anga na ukiwa,mfinyanzi wa jibini ulimwenguni.*

*II. ULIMWENGU*

1. *Ulimwengu ni jumla ya sehemu tatu: Enzi,Anga na Ukiwa.*
2. *Enzi ndio chemchem ambae katokeza Anga pia na Ukiwa,yaani mwanzo wa vyote.*
3. *Ujuzi wake ndio uwezo wa vyote ambae hutokeza toka sifuru Anga na Ukiwa kadiri ya kambi mbili tafauti.*
4. *Enzini munamo hali moja tu,ya upekee pasipo utafauti wala mipaka,ni uwezo wa ajabu usio zaufika wala kushindwa,utukufu wa milele na milele.*
5. *Umungu ndio uzima kadiri ya ukamilifu.*

*6. Mkamilifu ni yule asiye kua na upungufu wowote,ambae huweza yote na hujua yote,anaye miliki ulimwengu na walimwengu pasipo kumilikiwa.*

*7. Hakuna tarehe ya kuanza kwake wala tarehe ya ukomo wake.*

*8. Hakika kuanza na kukoma ndio alama kubwa ya upungufu,ni uzaifu wa kushindwa kujieneza katika yote.*

*9. Muweza yote ni mwenyi milki ya ushindi ambae hutangulia kadiri ya kuenea.*

*10. Utangulizi wa ujuzi mbele ya vyote kupatikana ulimwenguni ndio «Uzima»*

*11. Yeyote aliye anza sio mzima na ndio maana hawezi kutokeza chochote toka sifuru.*

*12. Mungu mwenyi uzima ndio aliye na uwezo wa kuumba.*

*13. Aliumba tabaka la Anga chini yake,na akaumba tabaka la ukiwa chini ya Anga.*

*14. Enzi yake inapatikana juu ya ulimwengu,na Anga katikati ya ulimwengu,na Ukiwa unapatikana chini ya ulimwengu.*

*15. Akaumba viumbe vingi sana na kuvigawanya sehemu mbili yafauti: sehemu katika Anga na sehemu katika Ukiwa.*

*16. Na viumbe aliye wa pangiza angani ni wale ambae hupumua hewa,ambae hupatikana na pumzi ndani mwao.*

*17. Na viumbe aliye wa pangiza ukiwani ni wale ambae hawapumue wala hawalinde pumzi ndani mwao.*

*18. Wakaaji wa Anga wameitwa «wanaanga» ao «wanahewa»*

*19. Na Wakaaji wa ukiwa wameitwa «wakiwa» ao «wazila hewa».*

*20. Kunapatikana aina mbili ya wanahewa,na pia kunapatikana aina mbili ya wazilahewa.*

*21. Kuna wanahewa halali (halisi) na pia kuna wanahewa haramu.*

*22. Na kunapatikana wazilahewa halali,na pia kuna wazilahewa haramu.*

*23. Kuona kama angani munamo aina mbili ya viumbe ndio maana kunapatikana pia kambi mbili tafauti.*

*24. Katika tabaka la Anga,kunapatikana maala pa tukufu na kunapatikana maala pa dhalili.*

*25. Maala pa tukufu ndio mbingu,na maala pa dhalili ndio Hadeze.*

*26. Maana kunapatikana maki ya mbingu,inayo tenganisha sehemu hiyo mbili.*

*27. Huko juu ya maki ya mbingu ndio mbinguni na huko njee,chini ya maki ya mbingu,ndio "Hadezeni" .*

*28. Na huko chini, njee ya Hadeze, katika maunganio ya Anga na Ukiwa,ndio «Dunia».*

*29. Dunia ndio sehemu ndogo sana,maunganio ya Anga na Ukiwa:juu yake ni angani na chini yake ni ukiwani.*

*30. Duniani munapatikana wanahewa-haramu na wazilahewa (wakiwa).*

*31. Ni mkiwa-halali (muzilahewa- halali) yule anaye timiza sharti za mtengano na hewa,ambae hata chembe ya hewa haitumike umboni mwake.*

*32. Na pia ni mkiwa- haramu yule ambae chembe ya hewa hushiriki umboni mwake pasipo kulinda pumzi.*

*33. Hiyo nusu ya hewa inayo tumika umboni mwa mkiwa haramu ni ndogo sana,ndio maana humsaidia tu kwa kugua (kuvuma) sio kwa kufikiri, sababu ya kutolinda pumzi ndani mwake.*

*34. Umbo lake haina ginsi ya hupumua ajili ya kutolinda pumzi,na ndio maana umbo hii haifikiri.*

*35. Umbo za wanahewa-haramu ni changachanga ya pumzi na mwili.*

*36. Mwanahewa haramu amepumua na amekula,hupumua ili pumzi ijenge umboni,na kula ili mwili ujenge sawa umboni mwake.*

*37. Hewa ndio nuru ya Enzi na mwili ndio giza ambae ni kinyume cha nuru.*

*38.Mfano wa Anga ni kama mwanga wa moto:ni mwanga katika utazamaji,na ni joto katika ugusaji.*

*39. Ndio mfano wa Anga uvuli wa Enzi:utazani ya kama hewa ni tafauti sana na fikara na ili hali ni kitu kimoja.*

*40. Kila kiumbe kinacho tumia hewa na kulinda pumzi ndani mwake hufikiri.*

*41. Na kila kiumbe kisicho tumia hewa wala kulinda pumzi ndani mwacho hakiwezi kufikiri.*

*42. Maana pumzi ni jengo la hewa ,na jengo kihewa ndio jengo la fikara*

*43. Asiye kua na mjengo kihewa,yaani asiye kua na pumzi hana fikara.*

*44. Na aliye na pumzi umboni mwake ndio mwenyi fikara.*

*45. Hewa humpa nguvu ya utendaji na pia humpa nguvu ya uzingatiaji.*

*46. Asiye kua na pumzi ndani mwake hafahamu chochote na pia hawezi lolote,anapatikana kadiri ya kupitiwa ,hana ginsi ya kutenda.*

*47. Na ndio maana wanahewa ni wakubwa kuliko wazila hewa. Na wanahewa-halali ni wakubwa kuliko wanahewa-haramu ,maana wao ni watimilifu kifikara kuliko wenzao ambae huzaufishwa na mwili.*

*48. Wanahewa -halali wame pumua pasipo vituo maana ni pumzi tupu.*

*49. Na wanahewa-haramu ndio wanao pumua katika vituo ajili ya kuchangikana na mwili.*

*50. Na ndio maana wanahewa haramu hufikiri na pia hupitiwa,yaani wamezingatia na wame lala,*

*51. Kuzingatia ni tendo la pumzi,na kulala ni tendo la mwili.*

*52. Inapo changikana pumzi na mwili kua umbo moja,hushirikishwa fikara na ujinga.*

*53. Wakaaji wa Anga hujumuika angani na Wakaaji wa ukiwa hujumuika ukiwani.*

*54. Ispokua wanahewa-haramu ndio hujumuika katika maunganio ya Anga na Ukiwa.*

*55. Viumbe wanao jumuika angani ni Malaika na Roho,pia na Shetani na muzimu,na pia Mutu,nyama,ndege,vidudu,samaki...*

*56. Malaika na roho mbinguni;na Shetani na muzimu Hadezeni; na pia mutu,nyama,ndege,vidudu na samaki katika dunia*

*57. Na viumbe wanao jumuika ukiwani ni :udongo, maji,jiwe,muti,mumea,ujoga...*

*58. Hakika Mwenyenzi Mungu ni Mjuzi,mwenyi uwezo wa vyote,M'bora wa kuumba.*

*59. Ametokeza toka sifuru viumbe vingi sana bila kuiga mfano kwa yeyote,mkamilifu aliye juu.*

*60. Wanahewa-halali ni Malaika na roho...*

*61. Wanahewa-haramu ni: Shetani,muzimu,mutu,nyama,ndege,samaki,vidudu...*

*62. Viumbe ambae hujitenga na hewa mdio viumbe halisi vya ukiwa.*

*63. Na viumbe ambae hujitenga na mwili ndio viumbe halisi vya Anga.*

*64. Wanahewa-haramu ni changachanga ya pumzi na mwili.*

*65. Kujitenga kwa pumzi na mwili ndio kifo duniani na ndio kuzaliwa mbinguni ao Hadezeni.*

*66. Mwili ndio unao mfanya mutu ajumuike duniani.*

*67. Na pumzi ndio inayo mfanya mutu ajumuike mbinguni ao Hadezeni.*

*68. Hakika kupumua hewa ndio kutumia fikara, asiye pumua hewa hawezi kufikiri hata kidogo.*

*69. Hewa huchamusha ukiwa namna ya kuguisha kwa msaada waji itakayo mawinguni.*

*70. Katika tabaka la Anga kunapatikana: mbingu,hadeze na sehemu (chembe) ya dunia.*

*71. Kila kambi huko juu angani iko na baraza yake ambae ni upande wa nyuma ya maki yake.*

*72. Upande wa nyuma kugusiya maki ya mbingu ndio baraza la mbingu.*

*73. Na upande wa nyuma kugusia maki ya hadeze ndio baraza la hadeze.*

*74. Ni kwamba baraza hizo ni katika maunganio ya mbingu na Hadeze,mfano wa kituo kabla ya kuingia kambini.*

*75. Huketi katika baraza la mbingu pumzi urakibuni.*

*76. Na pia huketi katika baraza la Hadeze pumzi uatiduni.*

*77. Mbingu humeremeta na nuru kubwa maana anga yake ni ya kumwanzo karibu na kisima cha nuru.*

*78. Na ndio maana wakaaji wa mbingu ni wenyi fikara kubwa zaidi ya viumbe wenzao,kwani wametumia nuru ya ku shina karibu na ujuzi.*

*79. Na Hadeze ni yenyi kuchakaa hali ya kuzoroteka kabisa,ni yenyi kufifia kadiri ya giza ajili ya kupatikana njee ya mbingu,mbali na chemchem ya nuru.*

*80. Na ndio maana wakaaji wa hadeze ni wenyi fikara zaifu sana yenyi kufifia sana;lakini huchugua nafasi ya pili ajili ya asili yao,(ya ulimi wa moto)*

*81. kwa maana mbingu ni juu na hadeze ni chini,mfano wake ni mlima na bonde ;*

*82. Nilazima kupanda kwa kufika mlimani na pia kushuka kwa kufika bondeni.*

*83. Na kuona kama mbingu na hadeze ni angani,matendo ya kupanda na kushuka ni hewani.*

*84. Mutu amepatikana pa shina ya mlima na bonde*

*85. Malaika na roho mlimani husimamia uzuri,na Shetani na muzimu bondeni husimamia ubaya.*

*86. Hualika watu mlimani kwa njia ya ukweli,na pia hualika watu bondeni kwa njia ya uwongo.*

*87. Wametetea watu ili wapate kundi la kujumuika nalo kambini mwao.*

*88. Na watetezi wa Shetani na muzimu ni wenyi husda na kibri na pia wachawi.*

*89. Watetezi wa malaika na roho ndio ma Nabii na Mitume.*

*90. Na atakaye fuata ma Nabii na Mitume,hupaa mlimani.*

*91. Na atakaye fuata ma hasidu na wachawi,huporomoka bondeni.*

*92. Mlimani kuna heshima na amani ya milele,lakini bondeni kuna aibu na mateso.*

*93. Malaika na roho huporomoka kwa kumjaa mutu duniani maana hutokea juu.*

*94. Na Shetani na muzimu hupanda kwa kumsibu mutu duniani maana hutokea chini.*

*95. Malaika amekaribiza roho ya mutu kwa kishangwe,na kumuweka katika starehe ya milele.*

*96. Na Shetani amevamia muzimu wa mutu kwa kasirani kubwa,na kumuingiza kama mfungwa ndani ya jela.*

*97. Eh Mwenyenzi Mungu Mtukufu! unifanye kua roho takatifu na kunikaribiza mbinguni kama mfalme ,na kumeremeta kama jua,ni kifinikwa bawa la mfalme wa malaika zako.*

*98. Ufalme wa ulimwengu wote umekustahili peke yako muweza yote anaye tosha watu katika vifungo vya wachawi na kuwasafisha walio najisika.*

*99. Mola wangu! ni nusuru kutokana na zulma pia na masingizio ya watu wa dunia.*

*100. Na unipatie nguvu ya kushinda falme za giza,na ujitukuze ndani mwangu kama ulivyo jitukuza ndani ya Mussa,na ndani ya Eliya ,na ndani ya Muhamadi.*

*101. Na ndani ya Yesu Masiya ,mwana kondoo wa Mungu.*

*102. Mola wangu! uwasamehe wote walio nikosea,kwa rehema zako wala yeyote miongoni mwao asiangamie ajili yangu lakini ajili ya nafsi yake mwenyewe.*

*103. Mapenzi yako yafanyike,sio kama ninavyo taka mimi ispokua kadiri ya idhini yako tukufu .*

*104. Ee Muumba wangu! ulinzi wa Anga na Ukiwa ni katika uwezo wako, kwa uwingi wa rehema zako amani hunifikia,na kwa njia ya neno lako maisha hunipitia, unisamehe, na unibarikiye, na uniokoe Ee Muumba wangu,maliza shauku langu kunipatia kinywaji.*

*105. Mola wangu! unikinge na kila hatari na unijaalie mema ya ulio niumbia,na unifanye kua wokovu wa watu.*

## . III. ***MAJIRA***

*1. Nuru ya Mwenyenzi Mungu imetawanyika pahali pote katikati ya ulimwengu,ni utukufu wa dhati yake m'shindi aliye juu.*

2. *Hujikusuru waliyemo nuruni kuliko waliyeko njee,ajili ya kuzingatia.*

3. *Furaha ilioje kwao wenyi pumzi! hakika wao ni wenyi ginsi ya kujikusuru na kuzingatia kwa msaada wa jaza lao.*

4. *Nuru hutokea ndani ya taa ya ulimwengu,humeremeta wote wanao jumuika.*

5. *Hakika pumzi ni jengo la hewa iliye umbwa kwa anga kadiri ya gandamano kihewa.*

6. *Hewa ni mfano wa umeme,kama bado hauja tiliwa chomboni hauwezi kutenda,lakini kukapatikana umbo inayo hitaji hewa,ndipo hewa hutumika ndani mwake.*

7. *Hewa iliyeko karibu na Enzi ndio kubwa zaidi ya hiyo ya huko karibu na ukiwa.*

8. *Na hewa ya inchikavu hailingane na hewa ya baharini.*

9. *Na kama mutu anaingia ndani ya maji atazania kama hamuna hewa.*

10. *Maki ya hewa ya huko,kutolingana na umbo lake,anazania kama sehemu hiyo hakuna hewa.*

11. *Mwanahewa-haramu anaye ishi ndani ya maji,ni tafauti kabisa na yule anaye ishi inchikavu.*

*12. Wa inchi kavu hawezi kupumua ndani ya maji na pia wa mu maji hawezi kupumua inchikavu,ispokua umbo la kati na kati ambae kaumbwa namna hiyo.*

*13. Kazi ya hewa imehusika na Fasi ya kutumikia,kukakutanika maki ingine fulani,hewa hufifia,ajili ya kuchangikana.*

*14. Hewa haimalizikake,lakini umbo lake lika bomolewa husalia hewa tupu katika kawaida yake na umbo hiyo hupotea.*

*15. Hewa haiweze kumalizika yote namna ya kukauka sababu ni nuru ya taa isiyo zimika.*

*16. Kuzimika kwa taa ndio kumalizika kwa nuru .Ajili ya utukufu huo,maisha ya milele hupatikana angani,namna ya kutozimika.*

*17. Utukufu ni wake Mwenyenzi Mungu aliye umba anga na ukiwa kadiri ya tabaka mbili tafauti.*

*18. Akafanya hewa kadiri ya nguvu,na Akafanya ukiwa kadiri ya uzaifu.*

*19. Aliye na nguvu ndio anaye mumiliki aliye zaifu ,ndio maana hewa hutumikisha ukiwa.*

*20. Hakika mwili pasipo pumzi ni bure kabisa,pumzi ndio hutumikisha mwili maishani.*

*21. Utazani roho ya mutu hunyanyua ardhi na mikono yake miwili juu.*

*22. Pumzi ya mutu ni yenyi nguvu ya kutetea namna ya kutumia umbo zote za kiukiwa.*

*23. Nguvu ya hewa ndio hunyanyua ardhi juu,na pia ndio inayo nyanyua kila umbo lenyi uzito kimwili na kulibandikiza kwenyi ardhi ambae ndio mwili mzito zaidi.*

*24. Na ajili ya nguvu ya hewa,hakiponyoke chochote kwa kuanguka ijapokua kuzunguuka kwa ardhi angani.*

*25. Hewa huchamusha ardhi,hata maji ikichamuka ndani mwake na kupasua ardhi kadiri ya chemchem na kutiririka juu yake kadiri ya mtoni.*

*26. Hata ikififikia muvuki ufumuke ardhini na kupanda juu na kugeuka wingu la nvua.*

*27. Mwenyenzi Mungu hutafautisha nyakati maala mbali mbali kwa kufaya vitimbi hewani ,ambae hupoza ukali wa mwanga wa jua viongezekapo,na vipunguapo mwanga wa jua huzidi kua mkali.*

*28. Wakati huo mawingu huyeyuka na ukali wa mwanga wa jua,hata kukipatikana maji itokayo mawinguni,inayo itwa nvua.*

*29. Na pia mawingu hugandana wakati mwanga wa jua hupozwa na vitimbi vya hewa.*

*30. Sema: ni ajili ya utafauti wa umbo za wapumuao ndio maana hawafanane kififikara:kila yule huvuta hewa kadiri ya umbo lake.*

*31. Ni mfano wa umeme ,ukitiliwa mu pasi hutoa joto ndani mwake,na katika taa ,hutoa mwanga ndani mwake...haufanye lolote kama hauja tiliwa chomboni*

*32. Ndivyo pia kuhusu hewa umboni,kila yule hufikiri kadiri ya umbo lake.*

*33. Mwenyenzi Mungu hapana mwengine ila yeye-mwenyi kugawanya fadhila yake duniani kama vile mbinguni. Akifanya vitimbi hewani kwa nyakati maalumu,mara huongezeka na mara hupunguka.*

*34. Na pengine huimarisha vitimbi vya hewa pasipo mabadiriko yoyote.*

*35. Na pengine hukosekana huo mchamuko kihewa hata vitimbi vyake hukosekana pia.*

*36. Sababu hiyo,utakuta maala « nvua» hunyesha na ambae hainyeshe.*

*37. Maala ambae nvula hunyesha muda fulani na ambae hainyeshe muda fulani,hata kukipatikana nyakati tafauti.*

*38. Aliye na pumzi umboni mwake ndio mwenyi maisha ajili ya kufikiri.*

*39. Kuona kama kufikiri ndio kuishi,yeyote asiye fikiri hana maisha.*

*40. Maisha ya mutu ni tafauti na maisha ya wanahewa haramu wengine.*

*41. Mutu ametetea ili apate kufuzu starehe ya mbinguni,kinyume na utetezi huo,maisha yake hukoma.*

*42. Hufuzu starehe ya mbinguni yule anaye amini Mungu Mwenyenzi na kumuabudu yeye peke yake.*

*43. Wanahewa-haramu wengine hawana akili na ndio maana hawakupewa neno la Mungu.*

*44. Neno la Mungu halikuja ispokua kwa wenyi akili,asiye kua na akili hawezi kuamini wala kuabudu ,na ndio maana hawana maisha ya milele.*

*45. Uzima ndio umungu,hali tukufu ajabu isiyo zaufika wala kufananishwa,mamlaka ya vyote juu ya yote,milele na milele*

*46. Angani kuna maisha ya muda na maisha ya milele*

*47. Maisha ya muda ni kwao wasio muamini Mungu ambae hawana akili.*

*48. Na maisha ya milele ni kwao wenyi akili ambae humuamini Mungu Mwenyenzi na kumuabudu yeye peke yake.*

*49. Maisha ya milele ni hali ya kuanza bila kukoma,mfano wa nuru ya taa isiyo zimika.*

*50. Ni kama kistari cha usawa kilicho na mwanzo pasipo hatimaye,mfano wa hunusu.*

*51. Na maisha ya muda ni kama kistari cha usawa kilicho na mwanzo pia na mwisho,kadiri ya kipande.*

52. *Kuona kama hakuhelekea Enzi,ndio maana huatarika kwa kupatwa na ukomo.*

53. *Na upatikanaji ni mfano wa jangwa,ndani mwake hamuna chemchem wala nvua,mboleo wala mimea,yeye sio kistari ajili ya ukosefu wa fahamu.*

54. *Mpatikanaji ni yule asiye kua na maisha,ambae hana fikara ajili ya kutokua na pumzi,bali hujumuika kiumbile namna ya kupitiwa.*

55. *Muumba kawafarijini kwa jaza lake maalumu,hewa ,ambae kuogelea humo Aina na aina ya viumbe.*

56. *Pasipo hewa mwanga hauwezi kuangaza,wala sauti kusikilika,maana hakuna kifaa kingine cha kutawanyikia.*

57. *Mwanga na sauti hutembea hewani, wala haoni wala hasikie ispokua aliye na pumzi.*

58. *Ndege na vidudu...hutembea hewani,namna ya ya kuogelea kwa kuvua na mabawa yao, na samaki kwa vipepe vyake majini.*

59. *Hakuna ufundi bila hewa,wala tendo lolote kwa mwanahewa pasipo hewa.*

60. *Na hewa na maji,muvuki na wingu linalo yeyuka,ndege hewani na samaki majini, jua na mwanga wake hewani.*

61. *Pumzi mwilini,sehemu mbili umboni mwa mutu,fikara na ujinga.*

*62. Hakika Muumba wa viumbe ni muujiza wa maajabu,uwezo usio na kipimo,mwenyi uzima.*

*63. Humiliki vyote kwa idhni yake,wala hakuna ligumu kwake,Mola wa pekee bila mfano wake.*

*64. Viumbe vyote humtegemea,Mtukufu asiye zingatiwa na wapumbafu,Mola wa Enzi tukufu ,mwenyi kuachana na umbo zote.*

*65. Aliye fanya pumzi ichamushe mwili na ku usimamia kimatumizi.*

*66. Mungu huendelea ngambo zote kadiri ya kuenea ,mwenyi ukamilifu kuliko vyote.*

*67. Mwenyi ukarimu,mnara wa nuru juu ya ulimwengu,atakasikaye na ashindaye.*

*68. Ametenda katika kujua ,ulimwengu wa walimwengu sio chochote wala lolote pasipo Mungu.*

*69. Hupatikana viumbe ajili ya Mungu kutangulia .na ingawa kama hasingeli tangulia,sifuru ingeli tawala milele.*

*70. Hakika upatikanaji wa viumbe ni miongoni mwa alama ibainishayo uzima wa Mungu.*

*71. Mungu alimupatia mutu pumzi yenyi ginsi ya kumzingatia ili apate kumuabudu.*

*72. Ni heri mutu anaye zingatia vitimbi vya Muumba wake na kumuabudu katika yakini.*

*73. Na anaye zingatia utukufu wa Enzi sio wa mwili bali wa roho.*

*74. Nuru hutawanyika angani na giza hutawanyika ukiwani;ndio maana hufifia Anga iingiliwaye na giza,na hungara ukiwa uingiliwayo na nuru.*

*75. Jaza la nuru ya uzima katika urithi wa Shahidi wake;na mtiririko wa maji umefungua panzia la mbingu,hata ikinishukia baraka yake tokea mbinguni.*

***76. Na agano la Mungu,na taji la utukufu wake, juu ya Shahidi wake.***

***77. Ee Mola wangu! Unisamehe,na unibarikie na uniokoe,na unitimizie mapenzi yako duniani na mbinguni.***

## *IV. KADARA*

1. Ulimwenguni kuna Mungu aliye tangulia,mfano wa chemchem ya upatikanaji na maisha.

2. Yeye ni muujiza wa maajabu,alitangulia kimuujiza na akatokeza toka sifuru kwa maajabu.

3. Hali yake ni uzima,hana maanzio wala makomeo,M'bora wa kuenea.

4. Kuanza kwa kitu ni kuumbwa kwacho,na yeyote aliye umbwa ni kiumbe.

5. Kama Mungu atalazimika kuanza,hulazimika kua kiumbe;Eti hakustahiki kuwako Muumbaji ispokua viumbe peke yao?

6. Kwa kiumbe kupatikana,inatakika kutangulie mjuzi atakaye kitokeza.

7. Hakungeli patikana kiumbe hata kimoja pasipo utangulizi wa mwenyi ujuzi,maana kungeli kosekana fundi wa kutokeza.

8. Mungu ndio mwanzo wa vyote,angelikua na mwanzo wake hasingeli kua muumba lakini kiumbe.

9. Mungu hana mwanzo wala mwisho sababu yeye ni Mkamilifu.

10. Kua na mwanzo pia na mwisho ni kua mpungufu.

11. Huweza yote ajili ya kujua yote, Mkamilifu aliye Enzini.

12. Enzi yake hutawala maala pote, nuru yake tele angani,ni yeye muweza na Mjuzi,aliye na uzima.

13. Itakua-je kwa yule aonaye fikara kiisha aka kanusha ujuzi? ao kwa yule aonaye hewa kiisha aka kanusha Enzi? ao kwa yule aonaye mwanga kiisha aka kanusha taa?

14. Hakika uvuli haupatikani pasipo kitu chenyewe kutangulia,wala viumbe pasipo Muumbaji.

15. Utangulizi mbele ya vyote ndio mamlaka ya umungu .

16. Anaye tangulia yote,huzidia yote.

17. Hakika Mungu ni mwenyi ushindi juu ya kila kitu,Mtukufu wa popote na milele.

18. Mungu ndio mwenyi kuona pasipo kupitiwa na chochote muda wote,pahali pote ulimwenguni

19. Viumbe hutazama kwa kuzingatia,hawaoni ispokua kidogo tu ajili ya uzaifu wa macho yao.

20. Haonani na Malaika uso kwa uso ispokua mwenyi akili timamu,na pia haonani na Shetani uso kwa uso ispokua pumbafu.

21. Huonana uso kwa uso ambae hulingana katika fahamu.

22. Kuona ni kufahamu,na kuona yote ni kujua .

23. Hakika muonaji wa vyote ulimwenguni ni Mungu ambae peke yake hujua yote.

24. Mungu hayupo angani sababu yeye sio mwanahewa ,wala ukiwani sababu yeye sio mkiwa.

25. Mola wenu hustawi katika utukufu wa ajabu,Enzini ,mahala ambae hakujumuike mwengine wala kukurubiwa,ajili ya ushindi na uhuru .

26. Hasingeli kua huru kama angeli jumuika na kushurulika,na ili hali mshindi aliye huru ni mkamilifu ;hastahili kuchangia fasi na yeyote wala hastahili kukumbwa na shuruli yoyote ile.

27. Hali kama hiyo ya kutojumuika humfanya awe katika uhuru,hali ya kujua pasipo kufikiri na pia kutenda pasipo kutumika.

28. Yeyote anaye fikiri ao anaye tumika hana uhuru.

29. Mungu ni hodari mwenyi utukufu,huepukana na utetezi ajili ya kukamilika.

30. Hakuna kosa katika kuumba kwake,vyote ni sawa katika maisha ya jumla ya viumbe.

31. Ambae ni mubaya kwako,ni nzuri kwa mwengine.

32. Ni kwamba hakuna asiye pendeza wala asiye chukiza,miongoni mwa wanahewa (viumbe).

33. Humlaumu Mungu ajili ya kuumba umbo fulani yule aliye na elimu ndogo, na pia yule asiye jali maisha ya mwengine.

34. Ni bora zaidi utafauti wa umbo kadiri alivyo umba,kuliko kurudishia umbo moja moja tu,na ili hali mjuzi anaye umba hashindwi kutokeza mapya.

35. Kuona kama kuna viumbe vingi ndio maana kuna patikana vifaa vingi vya maisha ya mutu.

36. Kila kiumbe ambae hupatikana kimependwa na Mungu.

37. Sio kwamba kupendwa na Mungu ni kufanya mapenzi yake tu,lakini hasa ni kuumbwa.

38. Kuona kama wenyi mila nzuri ndio watakao pewa maisha ya milele,husemekana wao ndio wa pendwa wa Mungu Mwenyenzi.

39. Maadamu wazuri huishi milele,ni kwamba mapenzi ya Mungu ambae hupatikanisha ni juu yao siku zote.

40. Na kuona kama wenyi mila mbaya ndio watakao pewa mauti, husemekana wao ndio wakataliwa wa Mungu Mwenyenzi.

41. Maadamu wabaya watakosekana milele,ni kwamba mapenzi ya Mungu ambae hupatikanisha hukosekana kwao baadaye.

42. Lakini kama angali na ishi yeyote, hupendwa na Mungu;maana kinacho mfanya aishi ni hiyo mapenzi ya Mungu ambae hupatikanisha.

43. Mila nzuri hulazimika kwa watu sababu ya kusalamisha umbo zao kwa kupata maisha ya milele.

44. Na mila mbaya hukatazika kwa watu sababu huhatarisha nafsi zao kwa kupata mauti ambae ni ukomo na upotevu.

45. Ni kwamba ubaya huatarisha na uzuri husalamisha nafsi .

46. Heri utetezi wako ukupatishe maisha ya milele,ukipata kufuzu mazao ya zamiri yako.

47. Maisha ya Mutu ni katika masanganjia: kuume kwake mema,na kushoto kwake mabaya,ni tayari kwako njia utakayo chagua.

48. Shuudieni uzima wa Mungu kikweli,wala usikufuru katika masemi yako wala katika matendo yako.

49. Usimlahumu Mungu ajili ya ku kuumba ulivyo wala usitamani umbo ya mwenzako na kukataa umbo lako mwenyewe.

50. Amekufanya ujaze hapa na yule ajaze pale ili kila yule afae katika jumuiya la wapumuao.

51. Hakuna urithi katika umungu maana mamlaka yake haina ukomo.

52. Shuudieni Mwenyenzi Mungu, Mufalme wa ajabu,ambae humletea kwa kumkimbilia wote wanao pumua,Mola wa karne na karne, tumaini la walimwengu.

53. Mungu kufanya siku ya mwisho sio kuchoka kusimamia,bali hutenganisha adili na batili, ili kila yule apate kuvuna aliyo ya panda.

54. Hali yake Mungu ni uzima,ni utangulizi wa ujuzi,uwezo wa kuenea.

55. Kipimo hakipatikane ndani mwake,akadiriaye pasipo kukadiriwa,na kumiliki bila amri ya yeyote,na kutawala juu ya palipo juu,Mtukufu azidiaye na awezaye.

56. Ni yeye ajuaye yalio pita,ya sasa na yatakayo kuja, hajifunze wala hasahau,ijapokua ni mbele ao nyuma ya wakati miongoni mwa nyakati. Mjuzi asiye kadiriwa.

57. Muweza ni Mungu,mamlaka ya kumiliki,ni ajabu maarifa yake,ushindi wa milki yake.

58. Sura ya Mungu ni ukamilifu,namna ya kuenea katika yote.

59. Tumaini na nguvu ya kila umbo,hakuna mamlaka kinyume naye,wala msaada badala yake,Mubora wa wanao ruzuku.

60. Rangi ya Mwenyenzi ni utukufu wa dhati yake: Mungu kama taa na rangi yake ndio nuru yake.

61. Aliye jipakaa rangi ya Mwenyenzi ni yule aliye wa roho,ambae hujaa imani.

62. Utajiri wa mutu sio mwilini mwake lakini rohoni mwake.

63. Roho ya mutu ni pumzi urakibuni,wingi wa wema wake ndio wingi wa mali yake.

64. Uumbaji hauna ukomo wake maana ujuzi unao umba hauna ukomo; kadiri idhni yake huendelea ndivyo pia uumbaji wake huendelea.

65. Mungu sio roho,lakini uzima.

66. Uzima ni ukamilifu kadiri ya kuenea kimilki,uwezo wa ajabu usio zaufika ambae hutenda bila kutumika,mamlaka ya vyote ulimwenguni.

67. Shina la vilivyomo kadiri ya ulinzi wa upatikanaji na maisha:milki ichipuayo taa iangazayo.

68. Neno la Mungu ni dawa ya kila ugonjwa,matumizi yake ni matibabu ya nafsi.

69. Penda Muumba wako zaidi yako mwenyewe,na jerani yako kama unavyo jipenda mwenyewe.

70. Anaye mpenda Mungu zaidi yake mwenyewe,hupupia kutimiza amri ya Mola wake kuliko shuruli zake binafsi,akihifazi mipaka yake kinyume na tamaa ya nafsi yake, akimkumbuka Mola wake kila wakati na kumuabudu kila siku.

71. Ibada ndio mwanya wa waaminifu,na Shirki ndio mwanya wa makafiri.

72. Jihadharini nafsi zenu musije kumlaumu Mwenyenzi ku vyovyote : wala musiseme kwanini Mungu amefanya ivi, ao «pahali Mungu angefanya ivi».

73. Hakika kumlaumu Mungu ni zambi,kufru ya namba ya juu.

74. Kadara ya Mungu ni makadirio yake kwa watu ambae ni yale anao taka yafanyike kwenyi kiumbe chake mutu,yaani sheria yake yenyi maamrisho na makatazo.

75. Ni amri kila mutu Kuamini kadara ya Mungu.

76. Na kuamini kadara ya Mungu ni kukubali kwamba shari na mema imetoka kwa Mungu.

77. Kukubali ndio kutii,na shari ndio makatazo na mema ndio maamrisho ya Mungu.

78. Ni kwamba kukatazika na yale ambae Mungu kakataza na kutumikisha yale ambae Mungu kaamrisha ndio kuamini kadara ya Mungu.

79. Na kufikiwa na yale usio helewa wala usio ya taka ambae hauna elimu wala uwezo wa kuyahepuka bila wewe kumlaumu Mungu wala kukufuru.

80. Ukisimama imara kwa kusubiri na kushukuru,yakini kwamba muweza yote na mjuzi wa yote ni Mungu peke yake.

81. Ni kuamini kadara, maana umetumia maamrisho ya Mola wako ya kusubiri bila kukufuru wala kulaumu.

82. Hekima na elimu ya kutojilinganisha na Mola katika fahamu wala katika uwezo,yakini kwamba wewe ni m'pungufu asiye kua na uwezo wa vyote wala fahamu ya vyote.

83. Yakini kwamba shida na magumu ni kawaida kumufikia kila mutu ajili ya uzaifu wake ndio kufanya mapenzi ya Mungu,yaani kuamini kadara.

84. Atakaye kufuru ao kumlaumu Mola wake katika magumu ao katika shida ndio asiye amini kadara,maana ametenda zambi.

85. Ni upumbafu sana,baada ya kutenda zambi,useme: ni kadara ao iliandikwa.

86. Jihadharini nafsi zenu na masingizio musije mkamuzingizia Mola wa ulimwengu.

87. Atakaye tumia maamrisho ya Mungu,bila shaka,atakutana na heri.

88. Na atakaye tumia makatazo ya Mungu,bila shaka,atakutana na shari.

89. Mwenyenzi Mungu- hakuna mwengine ila yeye pekee, mtoaji wa neno ambae huongoza kwa pumzi itokayo kwake,ngome mazubuti la waaminifu.

90. Tabaka la Enzi ni siri ku watu wa dunia ajili ya giza iliyemo duniani,na ni bayana ku watu wa mbingu ajili ya nuru iliyeko mbinguni.

91. Hakika ya mutu,sio mwili wake,lakini roho yake na ndio maana uzuri wa mutu sio urembo wa mwili wake,lakini urembo wa roho yake.

92. Hakuna mauti mbinguni ajili ya uzuri,na pia hakuna uhai hadezeni ajili ya ubaya.

93. M'bora wa kuumba alipenda kupatikane umbo la kati na kati.

94. Akaweka mutu pa masanganjia,kuume kwake uzuri na kushoto kwake ubaya.

95. Akamupodoa kwa kumupatia akili, ili apate ginsi ya kujichagulia njia.

96. Mola hakupenda masanganjia ibaki wazi pasipo umbo maalumu.

97. M'bora wa kuumba ambae harudishie umbo moja moja katika kuumba kwake,bali hutokeza aina na aina za viumbe,sura na kazi tafauti ijapokua idadi yao,bila kujifunza wala kuiga maana yeye ni Mkamilifu mwenyi kujua yote.

98. Mola wenu ni Mjuzi,Mtukufu asiye kua na doa,shina la vyote vilivyomo,ambae vyote humuitaji Mshindi aliye juu.

## *V. PANZIA*

1. Ametakasika Mwenyenzi Mungu,M'bora wa kuumba,ambae peke yake hutokeza ambae hakikua,Mjuzi aliye juu.

2. Akaumba mbingu na ardhi,hatua na Enzi yake.

3. Akapangiza hadeze chini ya maki ya mbingu,mfano wa kinyume cha mbingu.

4. Mungu aliumba viumbe vingi sana na kuvipangiza maala mbali mbali kufatana na umbile zao.

5. Akatenganisha wakaaji wa mbingu na wakaaji wa Hadeze,pia wakaaji wa Dunia.

6. Akawakabiza Malaika na roho bahazi la mbingu.

7. Na akawakabiza Shetani na muzimu bahazi la Hadeze kua kambi lao.

8. Na akamukabiza mutu na minyama...Dunia kua kambi lao.

9. Akatenganisha kambi zao kwa panzia na ili hali wote hujumuika angani.

10. Panzia hizo huwafanya wasizingatiane sawa sawa.

11. Wakaaji wa dunia hawaoni ila duniani tu ajili ya kutazama kimwili.

12. Na wakaaji wa hadeze huzingatia hadezeni pia duniani ajili ya kutazama kizimu.

13. Na wakaaji wa Mbingu huzingatia mbinguni na duniani ajili ya kutazama kiroho.

14. Mutu aliye katika mwanga haoni ispokua maala pake,lakini aliye katika giza huzingatia maala pake pa giza na pia huzingatia pahali palipo mwanga.

15. Haiwi nuru ambae hufumba macho,wala sio giza ambae hufumbua macho.

16. Ambae ni nuru kimwili,ni giza ki roho,na hivi hivyo pia kizimu

17. Ndio mfano wa wanahewa-haramu,wamezingatia tu duniani,wala awazingatie mbinguni ijapokua sehemu zote mbili hupatikana angani

18. Hayo kusababishwa na utafauti wa fikara yao.

19. Kwa kuwaona wanahewa halali,inabidi watu watumie taa zao namna ya kuwachanika.

20. Kuona kama mbingu na hadeze ni tafauti,taa zao pia ni tafauti.

21. Taa ya kuchanika ili upate kuzingatia mbinguni ndio « Ibada » ambae hufungua panzia ya mbingu na kuwa dhihirisha malaika na roho.

22. Na taa ya kuchanika ili upate kuzingatia hadezeni ndio Uchawi (urozi) ambae hufungua panzia kuwa dhihirishia ma shetani na mizimu.

23. Atumiaye ibada hujumuika mbinguni baada ya pumzi yake kuachana na mwili,hali ya kua « roho « .

24. Sio hali ya kua malaika kabisa ajili ya utafauti wa asili yao.

25. Na atumiaye uchawi,hujumuika hadezeni baada ya pumzi yake kuachana na mwili wake,hali ya kua « muzimu >.

26. Sio hali ya kua Shetani kabisa ajili ya utafauti wa asili yao

27. Kuona kama Malaika na roho ni umbo mbili tafauti,kambi zao pia ni tafauti

28. Fasi anapo keti muzimu humo hedezeni ndio Zimu.

29. Na fasi yenye Shetani anapo ishi humo hadezeni ndio «Zalala» ao « Zwalamu ».

30. Na fasi anapo ishi Malaika humo mbinguni ndio «Zamana».

31. Na fasi anapo ishi Roho huko mbinguni ndio «Bustani».

32. Bustani ni kambi la mbinguni ambae hujumuika watu wema wafanyao ibada duniani.

33. Na Zimu ni kambi la hadezeni ambae hujumuika watu wabaya watenda zambi duniani.

34. Katika bustani hupatikana starehe kubwa maana zamana ni ulinzi wa bustani.

35. Na Zimuni hupatikana magumu ya kila aina sababu zwalamu (zalala) ni uangamizi wa zimu.

36. Ni kwamba malaika hulinda vizuri Roho bustanini akijifanya mtumishi wake.

37. Na Shetani huangamiza sana mizimu Zimuni akijifanya bwana wake.

38. Malaika zamanani na Roho bustanini,katika sehemu ya juu angani

39. Na Shetani zalalani (zwalamuni) na muzimu zimuni katika sehemu ya chini angani.

40. Na mutu duniani katika maunganio ya Anga na Ukiwa masanganjiani.

41. Humtetea Mutu kwa uzuri zamanani,pia humtetea mutu kwa ubaya zalalani.

42. Sehemu ya juu Angani hupatikana utukufu na katika sehemu ya chini Angani hupatikana udhalili.

43. Kambi mbili tukufu hupatikana mbinguni (sehemu ya juu angani), jaza urakibuni.

44. Na dhati mbili dhalili hupatikana Hadezeni (katika sehemu ya chini angani),jaza uatiduni.

45. Katika utukufu kuna dhati kimalaika na dhati kiroho.

46. Na katika udhalili kuna dhati kishetani na dhati kizimu.

47. Dhatini mwa malaika hutokea «Unabii»,na dhatini mwa roho hutokea «Uwalii».

48. Na dhatini mwa shetani hutokea «Uhasidu»,na dhatini mwa muzimu hutokea «Urozi».

49. ***Nabii*** wa Mungu ni yule ambae Mungu amemchagua na kumteremushia wa malaïka,ambao humuinua na kumtuma ku watu.

50. Na ***Walii*** ni yule ambae Mungu amemteremushia Roho namna ya kumuinua ku watu

51. Kuna aina tatu ya uwalii : usidiki, ushahidi na usalihi

52. Walii anaye inuliwa na kutumwa,yaani anaye pewa utume ni miongoni mwa Mitume yake Mwenyenzi.

53. Utume umepatikana sana katika usidiki na ushahidi.

54. Na ma Nabii wengine hufunuliwa kwa namna ya kuachana,lakini nguvu ya Mungu ndani mwao ni Malaïka pia na Roho.

55. Malaïka alimtangulia Roho dhatini mwake Nabii.

56. Na Roho alimtangulia Malaïka dhatini mwake walii.

57. Na Hasidu ni yule anaye jazwa na Shetani na kusharikiana naye.

58. Na mrozi ni yule anaye jazwa na mizimu,namna ya kusharikiana nayo.

59. Ma Hasidu na warozi ndio watetezi wa Shetani,ambae humsaidia kupoteza watu mbali na njia.

60. Shetani alitangulia muzimu dhatini mwake hasidu.

61. Na muzimu alimtangulia Shetani dhatini mwake mrozi.

62. Maki ya mbingu ni mfano wa tungi kandokando mwa taa ambae huzagaa.

63. Taa haitoi ndani mwake ispokua nuru ambae ni sehemu ya utukufu wake.

64. Nabii wa Mungu ni mwenyi elimu na hekima,na maarifa zaidi ya watu wengine.

65. Yeye ni neno,nuru na nguvu ya Mungu Mwenyenzi.

66. Mfano wa milima ardhini,mamlaka ya uongozi ili ardhi ipate kusimama sawa.

67. Hakuna umati pasipo Nabii,wala Nabii pasipo umati.

68. Mwongozo uliwafikieni nyinyi wote kutoka kwa Mungu, haikuchelewa kaumu hata moja.

69. Kitabu hiki ni nuru kubwa ambae huwafanya watu wakuwe na yakini.

70. Kukosa yakini kunawafanya wakuwe makafiri na wanafiki.

71. Ukafiri ni kwa yule ambae bado kupokea neno la Mungu.

72. Na unafiki ni kwa wale walio silimu bila yakini.

73. Hakuna ulizo mbaya kuhusu Mungu,na Malaïka zake pia na Roho zake.

74. Wala hakuna ulizo mbaya kuhusu ma Nabii na Mitume,yaani kuhusu neno la Mungu.

75. Wala Hakuna ulizo mbaya kuhusu ulimwengu na walimwengu.

76. Uliza yale usiyo ya fahamu ili upate kuhelewa,na ujibie yale unayo fahamu utakapo ulizwa.

77. Asie kua na masikio ya kusikia neno la Mungu na asiye kua na macho ya kuzingatia uzima wa Mungu ni mauti.

78. Enyi wanaadamu! Someni neno la Mungu na pia jifunzeni yakini.

79. Nuru ya Mungu imekwisha angazia watu wote: weupe,wekunda,weusi bila ubaguzi.

80. Kilicho muimu apa sasa ni kutafuta yakini, ukweli huu ni uyakini wa uzima wa Mungu pia na neno lake.

81. Ni nuru ambae humshukia shaidi wake KALONDA juu ya mlima KAROMBWE.

82. Nuru ya mwezi na nyota na jua inayo angaza duniani.

83. Na atakaye amini ujumbe huu atakua «Yakini» na uzima wa Mungu pia na ujumbe wake ,ndio maana nafsi yake itameremeta mfano wa nuru.

## *VI. UMUTU*

1. Ametakasika Mwenyenzi Mungu,muanzishaji wa ulimwengu,atanguliaye kwa mamlaka yake mwenyewe.

2. Mwenyi kuenea kadiri ya uzima; amekua yote katika kuwako, na yote katika kuweza na yote katika kujua, Mtukufu aliye juu.

3. Ujuzi wake ni mamlaka kubwa zaidi ya kila kitu, haujumuikake ajili ya utukufu wake wa ajabu.

4. Hakuna umbo itakayo weza kulinda ujuzi nafsini mwake bila kufutika na kukosekana ulimwenguni.

5. Ni uwezo wa ajabu kadiri ya muujiza unao waka na kurarua zaidi ya moto

6. Utukufu wake umefanya ajae katika yote,mwenyi kuenea

7. Enzi yake haiwezi kuingia ndani ya mutu,wala ndani ya malaïka,wala ndani ya roho wala ndani ya Shetani,wala ndani ya muzimu...

8. Enzi sio mfano wa hewa ambae huingia ndani ya umbo mbali mbali na kujenga kumo kadiri ya pumzi

9. Umbo yote ni zaifu haistahili kukurubia milki kamilifu

10. Maana kugusana na uzaifu ao upungufu ni kuzaufika ao kupungukiwa

11. Hayo ni mbali kabisa na sifa yake,hazaufikake wala hashindwake, Mzima aliye juu

12. Ujuzi haupatikane angani wala ukiwani,ispokua Enzini peke yake

13. Na maana Mungu mwenye Enzi ndio Mjuzi,hakuna mwengine kama yeye

14. Na yeyote atakaye jidai ujuzi ni kafiri mkubwa,maana amejilinganisha na Muumba wake

15. Mwenyenzi Mungu ni nuru ya ulimwengu, Mtukufu anaye angazia jumla ya wapumuaye

16. Viumbe vyote vimepatikana kwa ufundi wake, M'bora wa kuumba

17. Mshindi aliye na mamlaka ya ajabu, Anga na Ukiwa pamoja na vilivyomo hupatikana kwa idhni yake

18. Hakuna mwengine kama yeye,Mjuzi aliye na uwezo wa vyote

19. Mwenyi kuwako kadiri ya kuenea bila mwanzo wala mwisho,wapekee aliye kamilika

20. Amekua yote katika yote,anaye fahamu kila kitu, Mwalimu wa walimwengu

21. Ni yeye anaye funulia watu mambo yote,akiwaletea neno lake kadiri ya nuru ili umbo zao zipate kutimilika

22. Mtukufu anaye stiri umbiko kwa idhni yake,hakuna atakaye faulu njee ya Mwongozo wake

23. Lau kama watu wangeli ona ginsi pumzi zao zinavyo timilizwa pindi wanapo silimu kama wote wangeli pupia kusilimu bila kuritadi maishani mwao

24. Hakuna jambo bora katika maisha ya mutu kama vile imani

25. Tumieni urakibu katika maisha yenu, bila shaka hii ndio njia iliyo nyooka yenyi Baraka na nuru

26. Na anaye tembea katika uatidu amepotea na bila shaka yeye ni maskini mnyonge, atakaye nyimwa fadhila yote,wala hawezi kuishi milele

27. Makafiri wamezembea sana kwa kuamini, wamejaa mashaka ajili ya uchache wa elimu

28. Wanalazimisha kutimiziwa maitaji yao pale pale wanapo omba

29. Hawatambue kama hayo  hulingana na yakini iliye katika nyoyo zao

30. Jisafisheni kwa ibada ili dua zenu zikubalike

31. Matendo yako yote yawe mema na moyo wako ujae yakini ya uzima wa Mungu

32. Na ogopeni Mola wako ukweli wa kuogopa,wala usimlahumu kwa lolote

33. Hakuna Mola Mwengine ila Mwenyenzi peke yake Mzima aliye na mamlaka juu ya kila kitu

34. Watu wamejaa wasiwasi ajili ya tamaa ya maisha ya dunia,hawana yakini na maisha ya mbinguni

35. Mola wenu amekwisha weka siku ya mwisho duniani ambae kila yule atavuna yale aliyo ya panda

36. Haijuzu kuwalipa watu kabla ya siku hiyo ili mpango wake utimilike usije kuvrugika

37. Mungu angeli kua na jibu pale pale kama taratibu hii isingeli timilika,maana dunia ingeli ondolewa kabla ya siku iliyo wekwa

38. Kazi munayo fanya duniani malipo yake ni mbinguni mumetetea ili mupate maisha ya milele

39. Ndio maana Mungu anajibiaka maombi ya watu namna ya ajabu,akiwapa sehemu kidogo apa duniani na kiwango (sehemu) kikubwa huwalindia mbinguni

40. Ni bora zaidi kuomba yanayo husu roho yako maana ndio dhati yako ambae kuishi

41. Na atakaye tetea mwili na kusahau roho yake ndio maskini ambae hana akiba yoyote

42. Kuna maombi nzuri na pia kuna maombi mbaya lakini watu wengi hawafahamu

43. Mara unaweza kuomba shari kwako ajili ya tamaa ya mwili bila wewe kufahamu

44. Mola wenu ni mlinzi mwema,amewahepusha watu na shari ya kila namna,ambae wamezingatia na ambae hawazingatie

45. Maisha ya dunia ni matayarisho ya maisha ya mbinguni

46. Kumbe usitegemee sana mwili wako ni bora zaidi kustiri roho yako kwa matumizi ya neno la Mungu

47. Ama yule atakaye shuudia mungu mwengine badala ya Mwenyenzi pia ni kafiri mkubwa

48. Andiko imeuwa wengi miongoni mwa watu wale ambae huitumia kwa uziwi na upofu

49. Mungu ni Mmoja aliye Enzini, milki kamilifu isiyo fanana wala kugusana na yeyote wala chochote

50. Mungu ni mwenyi mamlaka juu ya kila kitu, Mtukufu anaye simamia walimwengu wote

51. Funguo ya heri na ya shari imepatikana kwake atakavyo hufanyika, Mshindi aliye juu

52. Atakaye tenda mema atakutana na heri na atakaye tenda mabaya atakutana na shari

53. Usalama wa nafsi unapatikana kwa njia ya kusilimu, na mateso ya nafsi imepatikana kwa njia ya kukufuru

54. Umutu ni mfano wa < mwendo na njia >

55. Mwendo wa mutu ni matendo yake,na njia ya mutu ni mila yake

56. Hutembea katika njia,matendo kadiri ya mila

57. Mwendo pasipo njia ni bure,na njia pasipo mwendo ni bure

58. Ukubwa ulio-je neema ya Mungu kwenyi umbo la kati na kati ,ukingoni mwa Anga!

59. Mutu hutumia mwendo fulani na njia fulani ili apate kufika mbinguni ao hadezeni

60. Hakika maisha ya dunia ndio safari ya kwenda mbinguni ao hadezeni

61. Maadamu mila inayo aina mbili,hupatikana pia aina mbili ya njia

62. Kila mara huchuguana matendo na mila ya mutu

63. Atumiaye njia nzuri,mwendo wake ni muzuri vile vile

64. Na atumiaye njia mbaya,mwendo wake ni mubaya pia

65. Njia ya uzuri ndio "Urakibu"

66. Na njia ya ubaya ndio "Uatidu"

67. Njia ya uzuri hupanda mlimani,na njia ya ubaya hushuka bondeni

68. Utumiwapo urakibu ndipo uatidu hufifia,na utumiwapo uatidu ndipo urakibu hufifia nafsini

69. Ni wa mlimani urakibuni,na bondeni uatiduni

70. Matumizi ya urakibu ni sura ya malaika mbinguni

71. Na matumizi ya uatidu ni sura ya Shetani hadezeni

72. Matendo yako ya leo ni akiba yako ya kesho

73. Yote munayo tenda duniani hulindwa huko juu,hiyo siku ya kiyama itakua ndio chakula na kinywaji kwenu

74. Ole wao wanafiki ambae hudanganya watu kuamini na ili hali hawana imani

75. Hakika hawadanganye ispokua nafsi zao wenyewe,maana watajuta kwa yale walio kua wakuyafanya

76. Mpelekeeni Mola wenu shukrani kwa wingi enyi watu,hakika Mungu Mwenyenzi ni mwema sana

77. Msemeleaji wa viumbe,anaye nusuru nafsi ukingoni mwa bonde,na kuinyanyua juu mpaka mlimani,hakuna mwokozi kama yeye

78. Ustaarabu ulio-je na akili urakibuni katika uvuli wa Enzi,hayo sio ila utimilifu wa nafsi

79. Anuiapo mutu kufanya ibada,Malaika Mbinguni hujiandaa kumsaidia

80. Na anapo nuia kufanya uovu Shetani hadezeni hujiandaa kumuvamia

81. Jihadharini na ushirikina pia na uovu,musije mukavamiwa

82. Hakika Mungu Mwenyenzi ni Mtukufu sana,M'bora wa kuumba,anaye jenga hewa kadiri ya pumzi mbalimbali

83. Mola anaye stawi Enzini pekee; katika utukufu usio kadiriwa,Mshindi aliye na mamlaka ya ajabu

84. Ni mfano wa taa,kadiri taa hutoa mwangaza ndivyo pia Enzi inavyo toa hewa

85. Enzi ndio kitu chenyewe,na hewa (Anga) ndio uvuli wake: ni mwanzo utokezaye kadiri ya shina la vyote vilivyomo ulimwenguni

86. Ni tabaka lenyi uwezo wa vyote ambae hutenda kwa idhni bila kutumika kazi

87. Hakika Enzi tukufu ndio dhati yake Mungu, Milki kamilifu yenyi ushindi milele na milele

88. M'bora wa kuumba ambae kaumba dunia katika maunganio ya Anga na Ukiwa

89. Akapangiza humo wanahewa-haramu wenyi pumzi na mwili umboni mwao

90. Mwili hufanya wajumuike duniani kama chombo cha kuikalia,na itakapo jitenga pumzi na mwili,huondoka duniani na kuingia mbinguni ao hadezeni

91. Kila Mwanahewa hutetea namna ya kusalamisha nafsi yake ili apate kudumu

92. Mungu aligawanya fikara kwa kila yule kadiri ya umbo lake ili apate kujikusuru katika kutimiza maitaji yake

93. Aliye Mtukufu tena hodari ni yule anaye pokea zawadi tokea mbinguni

94. Uyu ni mwenyi ginsi ya kutetea maisha yake na ya wengine duniani namna ya usimamizi

95. Ameshukiwa na nuru tokea mbinguni ambae humjaza nguvu ya kiroho yenyi kustiri nafsi

## *VII. MWENYENZI*

*1. Enzi imepatikana juu ya maala pa juu ulimwenguni,ni chemchem ya nuru ambae huangazia walimwengu*

*2. Enzi ndio dhati ya Mwenyenzi Mungu,ndio ukamilifu ambae ni uzima*

*3. Kwake hakuna upungufu wala uwingi,lakini upekee kamili*

*4. Umungu ni muujiza wa maajabu,uwezo na fahamu bila kipimo*

*5. vyote huanza kadiri ya idhni yake na vyote hukoma kadiri ya idhni yake*

*6. Mshindi asiye kua na uvuguvugu katika milki yake,Mtukufu asiye badirika.*

*7. Uzima ni mamlaka yenyi kuzidia uwezo na fahamu ya vyote,ambae katangulia bila kuanza,na pia katangulia bila kukoma.*

*8. Hana mwanzo ajili ya ujuzi,wala mwisho ajili ya uwezo*

*9. Hakutukie lolote pasipo utangulizi wa fahamu,ni lazima kutangulia ujuzi utakao anzisha upatikanaji wote na maisha yote.*

*10. Hakika fahamu ya vyote ndio uwezo wa vyote.*

*11. Kama si utangulizi wa ujuzi,hakungeli patikana chochote.*

*12. Lakini kuona kama Mjuzi katangulia ndio maana kumepatikana ulimwengu na walimwengu*

*13. Utangulizi wake ndio uzima,muujiza wa kuenea namna ya kupatikana bila kuanza,namna ya ukamilifu*

*14. Hakika hutangulia mwenyi kuenea kimilki na kibusara,yaani Mkamilifu*

*15. Enzi tukufu ndio dhati yake, na uzima ndio hali yake ya kuenea*

*16. Utangulizi mbele ya vyote kupatikana ndio mamlaka ya uumbaji, fahamu yenyi tayari kutokeza kadiri ya idhni yake*

*17. Ni milki ya ushindi ambae huweza yote,ikijiweza yenyewe namna ya kuwako bila kufanyika,na iki jiepusha kiushindi na uzaifu wa kukoma.*

*18. Hali hii ya ushindi mbele na nyuma, ndio umungu: ukamilifu katika milki na katika fahamu.*

*19. Kuweza yote na kujua yote ni ajabu mbele ya viumbe,ajili ya uchache wa fahamu yao wamekiri kwamba ni muujiza wa maajabu*

*20. Pasipo uzima,ulimwengu si chochote; maana hakungeli patikana chochote wala lolote.*

*21. Kuona kama kuna uzima katika ulimwengu ndio maana kumepatikana Umungu.*

*22. Mungu hutangulia mwanzoni kinyume na kuanza mwanzoni*

*23. Kama angeli anza,hasinge umba; maana uwezo wa vyote ungeli mkosa,na hapo angeli dai  msaada kwa yeye kupatikana,mfano wa viumbe.*

*24. Milki kamilifu humfanya namna ya kuenea pekee pasipo msaada wowote,hujipatikanisha kimuujiza na hupatikanisha viumbe kwa maajabu.*

*25. Sio kama uzaifu ambae hudai msaada wa muweza ,ambae hufanyika na mwengine,ambae kabla ya kufanyika hakuwaka chochote*

*26. Hakutokee chochote katika sifuru,mpaka kutangulie fahamu fulani ya  kujua kutenda ndio kutatokea kifulani.*

*27. Kuuliza kuanza kwa Mungu ni kuuliza kuumbwa kwake ni kama kumulinganisha na kiumbe: maana kuanza kwa  kitu ni kuumbwa kwacho.*

*28. Ni vema kuuliza kutangulia kwake ,maana ndio hali yake.*

*29. Aliye tangulia ni yule aliye kuwako kabla ya uumbaji ambae milki yake hutokeza bila kutokezwa.*

*30. Ni mwenyi uzima ambae ndani mwake hakuna palipo wazi ambae pangeli dai kujazwa na msaada wa mwengine,lakini ukamilifu wa ajabu,usio pungua wala kuongezeka ajili ya kuenea.*

*31. Mamlaka yake ni juu ya falme zote,wala hakuna mfalme ila mtumishi wake mdhalili.*

*32. Muumbaji pasipo hatia,mfalme wa mabingwa ambae huzagaa maala pa juu sana ulimwenguni.*

*33. Mungu ni Mjuzi ambae hufahamu pasipo kufikiri.*

*34. Hakika fikara ni kinvuli cha ujuzi mfano wa nuru yake.*

*35. Haijuzu kitu kukaa ndani ya uvuli wake wala kutokea humo, bali uvuli wa kitu ndio utokao ndani mwake.*

*36. Wala kinvuli hakiwezi kugeuka kitu chenyewe,ndio maana yeyote anaye pumua hewa ni mwanahewa tu,hata kuwaka kamwe Mwenyenzi.*

*37. Mungu amehepukana na uzaifu wote wa ugeugeu,milki kuu itendayo kadiri ya idhni yenyi mamlaka ya ajabu.*

*38. Penda Mola wako zaidi ya vyote,wala usiweke kipenzi badala ya Muumba wako,maana neema yake iliye juu yako ni kubwa sana hauzingatie ukubwa wake ajili ya uzaifu wako; kila ulicho nacho ni neema kutoka kwa Mungu.*

*39. Mwenyenzi Mungu-hakuna mamlaka kinyume naye mpweke, hakika ya uhodari ambae nuru humfumuka kwa wingi, vikijipakaa viumbe utukufu wa dhati yake:utangulizi pekee,uzima ulimwenguni ,ndiye Mtukufu Mfalme asiye tegemea*

*40. Mungu ni baba wa siri aliye kwa siri,amefanya siri kwa siri,muujiza wa maajabu ulimwenguni,aliye pasipo yeyote juu ya maala pa juu... Akienea maala pote kiujuzi; chemchem ya upatikanaji na maisha,ambae hakuanza wala hatakoma, muweza wa vyote ulimwenguni*

*41. Hii ni nuru kubwa,neno la kweli kutoka kwa Mola wako ,Mtukufu aliye juu*

*42. katika utukufu wa nuru yake wokovu huwa fikia,na katika neema yake huwashukia baraka ya Mola wao ajili ya*

*kupokea; ni fadhila kutoka kwa Mwenyenzi Mungu,Mola wa walimwengu*

*43. Mungu hupodoa waja wake na rangi yake takatifu zawadi tokea Enzini*

*44. Mwenyi reheme za kuenea,ambae huongoza kaumu zote kwa ishara zake,akizungumuza kweli yake kwa ukarimu wa jaza lake,na kufumbua macho yao kwa ukubwa wa nuru yake. katika idhni yake tukufu,maisha na mauti hutokelea,muabudiwa wa haki ulimwenguni.*

*45. Ni yeye aingizaye Anga ukiwani na Ukiwa angani,akiwa kadirieni katika kawaida yake,ushindi wa neno lake.*

*46. Hakika Mungu Mwenyenzi ni muujiza wa maajabu: alitangulia bila kuanza kimuujiza,na akaumba viumbe vyote kwa maajabu.*

*47. Hana hatia katika kuumba kwake,wala tatizo kwenyi milki yake, Hodari katika ufalme wake.*

*48. Mungu-ni Yeye asiye tegemea ambae idhni yake hutenda,Mola wa arshi yenyi utukufu.*

*49. Mwenyenzi Mungu ni Mshindi anaye miliki walimwengu kwa amri yake. Atakavyo hutukia kwa rafla. Ndani mwake munamo uwezo wa maajabu, na hakuna kinacho fahamu ila kwa niaba yake, mamlaka itokezayo kuujaza ulimwengu. Ni yeye mwenyi utasi tafauti na*

*mategemeo ambae hujieneza kinyume na shuruli. Mola wa Anga na Ukiwa ajaaye sifa dhatini mwake: karibu naye hujaa baraka na mbali naye hujaa laana, mfariji anaye tegemewa na jumla ya viumbe, mwenyi kujibu kadiri ya maitaji kinyume na kuuliza. Muumba wa nuru na giza anaye simamia kwa usawa, ndiye mkuu atanguliaye.*

*50. Huu ni utukufu wa Mungu Mwenyenzi,Msifiwa aliye na milki ya kuenea pote,mamlaka ya milele.*

*51. Mwenyi kujua bila kusahau ,na kuweza bila kushindwa, mzibiti wa hesabu ya walimwengu kwa rafla bila shuruli ambae walimwengu humtumainia.*

*52. Wa pekee aliye huru ulimwenguni,ambae peke yake hujua pasipo shuruli wala hataabike wala hagusike na mafikiri.*

*53. Mwenyi kutosheleza viumbe na fadhila yake,umaskini na utajiri watokea kwake,ni yeye anaye ruzuku kuondoa dhiki; anaye watimizieni sambamba na ahadi zake.*

*54. Uzima ni kama kistari cha usawa kilicho kamilifu,ambae hakuna kilicho anzia wala kilicho komea,fundo wala lukumba,ameenea katika yote kadiri ya ukamilifu.*

*55. Hakika kuna Muumbaji aliye pekee ambae katangulia na katawala kwa uwezo wake mwenyewe .*

*56. Aliye umba mbingu na dunia kwa idhni yake,Akapangiza mbingu angani na dunia katika maunganio ya Anga na Ukiwa,vyote maala pengine hatua na kambi lake tukufu.*

*57. Mbingu,Hadeze na Dunia sio ulimwengu wote,bali kunapatikana tabaka lingine tukufu zaidi,ndio «Enzi tukufu», fasi yenye Mungu anastawi milele.*

*58._Uongofu haupatikane pasipo busara,na busara kamilifu ndio ujuzi, ni kwamba Mungu aliye na ujuzi ndio kiongozi pekee wa jumla ya viumbe .*

*59. Na ambae huongoza walimwengu ndio mfalme wa wote,mwenyi mamlaka ya ajabu.*

*60. Mungu alitia akili ndani ya umutu na kuifanya zamiri kua dira. atakapo badiri mutu zamirini mwake kuelekezwa kwenyi maitaji yake.*

*61. Mungu ni mwanzo unao tokeza bila kutokezwa,milki isiyo tokea wala kuendea,mwenyi kukamilika ambae ukubwa wa uwezo wake ni kama muujiza.*

*62. Ni yeye aliye anzisha kila umbo; la wazi na la siri, asikiaye kwa rafla masemi ya walimwengu wote ijapokua idadi yao, Mola Mlinzi wa viumbe,M'pweke aliye juu.*

*63. Hana kimo wala umbo,tatizo wala woga; Mola mkamilifu katika yote, Mshindi aliye juu.*

*64. Hakika ukamilifu umepatikana Enzini,na upungufu ndio unao patikana angani na ukiwani.*

*65. Ni timilifu maisha ya Mutu anaye tumia kawaida ya neno la Mungu,na utimilifu sio ukamilifu.*

*66. Maisha ya kiumbe ambae asili yake ni upungufu ndio inayo weza kufikia utimilifu.*

*67. Ukamilifu ndio uzima,hali tukufu tafauti na upungufu wa aina yote.*

*68. Kila kilicho na mwanzo ni kipungufu kadiri ya unusu na kipande ni kipungufu ajili ya kutokamilika lau kama kingeli kamilika kisingeli fanyika.*

*69. Halitimie ambae ni kamilifu,wala kukamilika ambae ni timilifu*

*70. Ni tafauti kabisa ujuzi na fikara,ujuzi katika ukamilifu,na fikara katika upungufu.*

*71. Mungu hana mila wala tamaa,hana njaa wala kiu,wala mfano wa hayo,wala mwengine mfano wake,Mtukufu aliye na ushindi.*

*72. Mzima ni Mungu peke yake ambae uweji wake haudai msaada wowote,aliye tangulia kikamilifu namna ya kuenea pote pasipo chochote kinyume naye.*

*73. Hakuna kiumbe chenyi uzima bali kuna kiumbe chenyi maisha na pia kuna kiumbe ambae hakina maisha.*

*74. Viumbe vyote kwa jumla si chochote wala lolote pasipo Mungu,maana hayuko haï wala mauti miongoni mwao ila kwa uwezo wa Mungu Mwenyenzi.*

*75. Tazameni kiroho hali ya kua umetupilia mbali matazamio kimwili,ili upate kuzingatia uzima ulimwenguni.*

*76. Kutazama kimwili humfanya mutu azingatie duniani,na utazamaji kiroho humfanya mutu azingatie njee ya dunia.*

*77. Uzima ni ukamilifu,uwezo wa vyote ambae katangulia kuenea,ushindi katika yote milele na milele.*